

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 30 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE – NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:**  
Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2008/2009 (*Statement of Reallocation Warrant No. 1 of 2008/2009*).

Taarifa ya Mwaka ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2008 (*The Annual Report of The National Board of Accountants and Auditors Tanzania for the year ended 30 June, 2008*).

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kwa mwaka 2007/2008 (*The Annual Report of Tanzania Revenue Authority for the year 2007/2008*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI k.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, jukumu la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbali na kuisimamia Serikali pia lakini na Taasisi nyingine zote ambazo ziko Serikalini ikiwemo Mahakama katika utendaji wa jumla.

Mahakama imekuwa ikichelewesha sana kesi za madai kiasi cha kwamba wanaodai hufika mahali mpaka wakafariki bila kupata haki zao. Lakini hata pale Mahakama inapoamua bado wadai wanasmubuka sana kupata malipo yao hasa pale wanapoidai Serikali. Kuna kesi maarufu nyingine ambazo zimefanya nje ya Mahakama kama kesi ya akina Mzee Tango ambayo naifahamu, pia ya Mama mmoja kutoka Kondoa amesumbuka sana pamoja na kwamba Mahakama imeamua lakini bado malipo hayapatikani.

Ni kwa nini Serikali ambayo inasimamia utawala bora baada ya maamuzi ya Mahakama inachelewa kuwalipa watu haki zao?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kucheleta kutolewa kwa maamuzi na utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya Mahakama kunatokana na sababu nyingi. Katika hatua ya awali ambayo pengine zinachukua muda mrefu inachangiwa na upande wa utetezi lakini vile vile na upande wa wale wanaolalamika. Kwa hiyo, ni mambo mengi ambayo yapo katika ule mchakato ambayo wakati mwengine yanapelekea kucheleta sana.

Lakini azma ya Serikali, nina hakika umeshamsikia Mheshimiwa Jaji Mkuu, mara nyingi ni kujitahidi kuwa na mfumo ambao utasaidia sana kuharakisha hizi kezi ziweze kumalizika upesi hasa kesi za madai. Ukipata hukumu ni kweli vile vile kwamba kuna mchakato ambao ni lazima uzingatiwe ili uweze kufika mwisho hukumu ile iweze kukazwa. Sasa ukishafikia hatua ile kwa kweli utekelezaji unatakiwa kuwa mwepesi kwa sababu hakuna sababu yoyote ya kuchelewesha utekelezaji wa jambo hilo. (*Makofii*)

Sasa wakati mwengine inaweza ikachelewa tu kwa sababu ya watu kutokujua sasa baada ya pale inakuwaje na wakati mwengine vyombo vinavyohusika navyo vinachelewesha, wakati mwengine madalali nao wanashiriki katika ucheleweshaji kwa namna moja au nyingine. Lakini kwa kweli mimi nasema ukimaliza kesi hakuna sababu hata kidogo kwa nini utekelezaji uchukue muda mrefu.

Sasa umetoa mfano kesi ya Mzee Tango, Mzee Tango kesi yake ni kesi ninayoifahamu muda mrefu sana na kilichofanyika pale ni kwamba Mahakama iliona itumie busara nzuri kwamba jambo hili liende likatatuliwe Serikalini kwa kuzingatia hali halisi. Sasa ni kweli kesi hiyo ni ya muda mrefu na imechukua muda mrefu sana lakini wewe ni shahidi nimejitetahidi sana sana kiasi kwamba angalau ameweza kupata kiasi cha malipo ambayo mimi nilidhani kingemsaidia katika hatua nyingine hasa kwenye afya yake.

Najua bado anatudai na nimeigiza Serikali sasa kwa kuzingatia makubaliano tuwe na timu ya pamoja, tupaite tena madai ya Mzee huyu na mimi nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba nitajitahidi kulisukuma hili chini ya Wizara ya Fedha ili Mzee huyu aweze kupata haki yake mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana kwanza kwa majibu mazuri.

Kwa kuwa haya madai yamechukua muda mrefu na kuna *accumulation* ya *interest* ya riba kwa malipo haya. Mara nyingi Serikali huwa haipendi sana kulipa riba, je, sasa si wakati muafaka kwa wale watu ambao wanaidai Serikali na hasa ukizingatia kwamba haya madai ya Serikali ni makubwa kwa mfano chukua kesi zile za wahujumu uchumi toka mwaka 2003 na wengine mpaka leo hawajalipwa. Huoni kwamba Serikali inajirundikia madeni ambayo hayana sababu na maamuzi ya kimahakama yameshapatikana kwa hiyo wangeharakisha kulipa hayo madeni ili Serikali ikaondokana na mzigo wa madeni ya ndani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kama kesi imemalizika kwa utaratibu wa kimahakama ndani ya hukumu ile huwa ndani yake vile vile yako maamuzi juu ya riba na hili huwa halina mjadala kwa mtu yeote anayetekeleza ile hukumu. Tatizo linaibuka pale ambapo suala la riba liko nje ya mfumo wa uamuvi wa mahakama. Sasa pale mnajaribu kuzungumza kati ya Serikali na mlalamikaji.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, hapo mimi ndiyo nadhani kwenye ngoma sasa maana yake kama unavyomjua Mheshimiwa Mustafa Mkulo mgumu sana kwenye jambo hili na hata aina ya riba ambayo inatakiwa itumike nayo inakuwa ni suala ambalo lazima likubaliwe.

Lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba mara nyingi tunategemea sana ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anavyotushauri sisi kama Serikali kazi yetu ni kutekeleza. Kwa hiyo, tutaendeleza hizi juhudhi ili kuhakikisha kwamba maamuzi haya hayachukui muda mrefu bila sababu za msingi. (*Makofii*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Waziri Mkuu katika nchi yetu kuna maeneo mbalimbali ya hifadhi ya wanyamapori moja ni *National Parks* ambayo tunajua kwamba hakuna matumizi ya binadamu yanayofanyika ndani ni wanyamapori tu ndiyo wako humo.

Kuna mapori ya akiba yaani *Game Reserves* na kuna makazi ya binadamu yanayofanyika humo. Lakini kuna uwindaji wa waliopeva vitalu ndani ya *Game Reserves* hizo. Kuna maeneo ya *Game Control Areas*, ambayo hii *Game Control Area* ndiyo kuna makazi ya watu, malisho ya mifugo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge swali tafadhali maana unatoa hotuba sasa!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Na ndiyo *blocks* za wawindaji, je, *Loliondo Game Control Area* ambayo tunajua iko katika *category* hiyo ambayo wananchi wako humo na malisho yanapatikana humo. Je, imekuwaje Serikali ikachukua hatua kuwahamisha wananchi katika *Game Control Area* na hiyo *Game Control Area* haina hadhi zaidi ya *Longido Control Area* ambayo kuna vitalu vya uwindaji vitano? Naomba jibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe radhi sana Mheshimiwa Michael Laizer kwamba sitaweza kulijibu swali hilo mpaka labda na mimi nipate maelezo kidogo kuhusu swali zima maana lina mambo mengi kwani kuna wananchi wamehamishwa, kuna suala la hifadhi na aina ya hifadhi yenye na kwa nini Serikali imefanya hivi. Sasa sikuwa nimelitarajia katika mfumo wa aina hiyo, pengine nikuombe radhi tu, nipe muda nimtake Waziri wa Maliasili anipe maelezo ya kina juu ya hadhi za maeneo yote mawili na kwa nini Serikali iliamua kuchukua hatua hiyo na katika kuchukua hatua hiyo ni mambo gani ambayo Serikali vile vile imeyafikiria ama kwa ajili ya wananchi inayowahamisha au kwa

ajili ya huyo ambaye tunasema anabaki katika eneo hilo. Vinginevyo nitapiga blaa blaa na mimi nisingependa kusema uongo hapa kwako wewe mtu mzima kama mimi. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba pia na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu miaka sasa inakwenda bado unyanyaswaji wa wanawake pamoja na watoto unakithiri sana na migogoro ndani ya ndoa hasa pale mwanamke anapofiya na mume wake na pale ndoa zinapovunjika watoto wananyanyaswa. Unakuta kwamba sheria inaelekeza kwamba baba atoe shilingi 100/= kwa ajili ya matumizi ya mtoto, lakini bado mwanamke mjane pia anapokuwa amefiwa ananyanyaswa kupita kiasi na hata ndoa inapovunjika manyanyaso yanakuwa ni yale yale kutokana na sheria iliyopitwa na wakati.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa Serikali italeta lini Muswada wa Sheria ya Ndoa ili tuweze kufanya marekebisho?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu dada yangu Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo, kwa maelezo yake inaonekana yako mambo matatu makubwa ambayo yanajitokeza, yaani kuna suala la Sheria ya Ndoa, lakini amegusa vile vile Sheria ya Mirathi lakini katika kujieleza nimemuelewa vile kwamba anazungumzia haki za watoto katika mazingira yoyote yale yatakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Sheria ya Watoto kwa maana ya haki za mtoto ambazo zinatakiwa kuheshimika na kila mtu hatua za Serikali zilizochukuliwa ni kubwa na mimi matarajio yangu ni kwamba chini ya usimamizi mahiri wa Mheshimiwa Mama Margaret Sitta nina hakika kabisa Sheria hiyo itaweza kuletwa Bungeni kama si Bunge lijalo basi itakuwa linalofuata kwa sababu tumeshaipitia kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Baraza la Mawaziri, kilichobaki kwa kweli ni kuchapishwa na kuletwa Bungeni. Kwa hili la watoto kwa ujumla wake nadhani hili limeshakamilika na muda si mrefu Sheria itatungwa.

Suala la Mirathi na Ndoa ni jambo ambalo sasa itabidi nilieleze kidogo ili uweze kupata ufahamu wake. Maeneo yote mawili yamekuwa yanajadiliwa Serikali na kila tunapotaka kuyasukuma mbele tunapata mawazo mengine mapya kutoka kwa jamii. Kwa hiyo, hatimaye Serikali imeamua kwamba tuandae Mheshimiwa Spika utaniwia radhi nitaongea Kiswahili na Kiingereza, tuandae *White Paper*. Imeshakamilika tayari tunatakiwa tuisambaze kwa wananchi wote na itasimiwa na utaratibu mahususi kabisa ili tuweze kupata maoni ya Watanzania wote juu ya Sheria ya Ndoa na matatizo yanayoendana na ndoa na vile vile suala la mirathi na matatizo yanayoendana na masuala ya mirathi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi hilo ndipo tutaweka pamoja na hatimaye kukamilisha sheria zote mbili. Matarajio yangu ni kwamba ifikapo mwaka kesho hivi pengine tunaweza kuwa tumeshakamilisha huo mchakato. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kumekuwa kikitolewa maoni mbalimbali na wanasiwa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa kidini na wananchi mbalimbali kuhusiana na kila kinachoitwa Ilani ya Kanisa Katoliki kuelekea uchaguzi wa 2010. Nini msimamo wa Serikali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mara zote akisimama ndugu yangu Salim Hemed Khamis huwa natetemeka kweli hapa, lakini leo *inshallah* naona ameuliza swali zuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujuu nini msimamo wa Serikali kuhusu suala hili la kile kilichoitwa Ilani ya Uchaguzi ambayo imetolewa na dhehebu la dini ya Kikatoliki, jambo ambalo limeleta mjadala mkubwa karibu sehemu nyingi hapa nchini na hata Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru nakumbuka naye alitoa mchango wake alipokuwa hapa Bungeni.

Sasa ninaloweza kusema ni nini? Mimi si mara ya kwanza kuona hizi ilani karibu kila wakati wa uchaguzi unapokaribia wamekuwa wakifanya hivyo. Lakini lazima tukubali vile vile kwamba mambo haya yanakwenda na wakati.

Mara ya kwanza sikusikia maneno juu ya jambo hili yaani katika uchaguzi ule wa kwanza lakini hata ule wa pili, lakini safari hii yamejitekeza. Kwa hiyo, ukiniuliza mimi, mimi rai yangu ingekuwa kwamba aah, dhehebu hili ambalo wametoa jambo hili wasipuuze kauli za Watanzania zinazojitekeza sasa, na mimi nadhani kubwa hapa ni kwamba je, hivi kama kila dhehebu litaamua kutoa ilani yake tutakuwa na uwezo wa kudhibiti yale yaliyomo katika hizo ilani ? Maana ndiyo wasiwasi wangu.

Kwa hiyo, upande wa Serikali ni lazima vile vige tuanze kufikiria kwamba pengine iko haja ya kuzungumza na madhehebu ya dini hata kama inabidi yatoe maelekezo fulani, pengine iko haja ya kusema hivi hamuwezi hayo mawazo yenu mkayaleta Serikalini halafu yakinaka kwa mfumo mmoja kama yana nia nzuri ili tusije tukajikuta kila dhehebu linatoa mambo yake na mengine yanaweza kuwa ni yale ambayo hatuna uhakika kama yanasaadidu kujenga umoja wa kitaifa au yanaweza yakapelekea kubomoka kwa umoja wa kitaifa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naweza tu nikasema kwamba baada ya kuyasikiliza majadiliano marefu sana nadhani na wenyewe wenzangu wa Katoliki hawa wamelisikia na mimi nasema rai yangu ni kwamba tusipuuze mengine ni majadiliano mazuri tu ya kujaribu kusema tunachohoji kina msingi fulani. Sasa upande wa Serikali tutaangalia tuone na sisi tunajipangaje na tufanye nini ili kuhakikisha umoja wa kitaifa unaendelea kuwepo maana ndiyo kazi kubwa tuliyonayo. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini nasema yanapotolewa matamko mazito kama haya ambayo yanagusa hisia za watu wengi na Serikali kuchelewa kuyatolewa maelezo kama alivyofanya kwa ujasiri mkubwa Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, huoni kama hii inakaribisha machafuko ya hali ya hewa kiasa nchini wakati imechelewa na watu wanaendelea kubishana na kubishana? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, haraka haraka nayo haina baraka, wakati mwingine si vizuri ukaharakisha kuingilia kati wakati hujapata hasa tatizo likoje. Lakini mimi nina hakika kabisa kwamba baada ya mzungumzo marefu na mabishano ambayo yalikuwa yakiendelea tuko katika nafasi nzuri zaidi kama Serikali kuona busara ipi sasa itumike katika kujaribu kuelekeza Taifa na watu wake katika masuala kama haya.

Kwa hiyo, mimi nadhani hatujakosea na wala sidhani tumeshafikia mahali ambapo sasa nafikiri mchafuko wa hali ya hewa utajitokeza kwa sababu ya jambo hili, hapana! Mimi nadhani bado yako ndani ya uwezo wetu kuweza kulisimamia vizuri. (*Makofi*)

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kiasi fulani amejibu swali langu kwa sababu halijatofautiana sana na swali la Mheshimiwa Michael Laizer wa Longido.

Lakini nilitaka tu kumuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anatafuta yaliyojiri katika kuondoa wafugaji katika maeneo ya kitalu cha *OBC* aangalie vile vile ni sheria gani ilitumika kuwaondoa watu wale kwa sababu haikuwa ni amri ya Mahakama. Naomba sana hilo lizingatiwe na ukweli watakaomsaidia wamueleze ukweli.

**SPIKA:** Huo ni ushauri tu Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeupokea!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Hivi majuzi wakati Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, akiwasilisha hotuba yake ya Bajeti alizungumzia suala zima la wanafunzi wote ambao watakuwa na vigezo vyta kuweza kuingia vyuo vikuu watapata hiyo fursa. Lakini Bodi ya Mikopo vile vile hivi karibuni imetoa barua inayoelekeza kwamba watapunguza *support* kwa wanafunzi ambao wataomba mikopo kwenda kwenye Bodi ya Mikopo kwa madhumuni mazima ya kuweza kuingiza vyuo vikuu.

Sasa kutokana na maelezo haya mawili tofauti ya Waziri mwenye dhamana ambaye anasema kila mwanafunzi ambaye ana vigezo atasoma na Bodi ya Mikopo kwamba wanapunguza idadi ya wanafunzi. Sasa ninataka nipate kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, dada yangu Halima ameuliza swali ambalo kwa ujumla wake wote linasimamiwa na sekta moja Wizara wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, sasa Bodi iko chini yake na kwa hiyo kauli yake ni kauli yake yeye mwenyewe.

Kwa hiyo, ninachoweza kumuomba Mheshimiwa Halima Mdee ni kwamba kama pengine unaona kuna mkanganyiko katika yale maelezo na ungependa pengine yangewekwa vizuri ili yaonekane yameeleweka zaidi. Ninachoweza tu kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii ni kwamba apate fursa hata kama siyo Bunge hili basi Bunge lijalo atoe kauli hapa ya Serikali itakayoliweka jambo hili vizuri ili liweze kuelewaka na Watanzania wote. Tutakuwa tumechelewa kidogo kwa maana ya udahili wa wanafunzi lakini bado nadhani ni vizuri likatolewa kauli. Lakini kama ataweza hata Bunge hili kwa umahiri wake basi mimi nitashukuru kweli! Lakini nadhani iko haja. (*Makofi*)

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu imekuwa ikitoa maamuzi mbalimbali lakini baadhi ya maamuzi yake yanakuwa hayatekelezwi kwa muda ambao umetazamiwa. Kwa mfano, mwaka jana kupitia Bajeti Serikali ilitoa tamko namna gani itaweza kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania la ATCL, mwaka ukapita. Mwaka huu kupitia Bajeti Serikali imetenga shilingi bilioni moja na kusema kwamba kuna wawekezaji watakuja, hali ya shirika hili inazidi kuwa mbaya zaidi.

Napenda kujua ni nini msimamo wa Serikali juu ya Shirika hili ambalo ni muhimu sana kwanza kwa uchumi wa nchi, lakini pili kwa kurahisisha mawasiliano kwa Watanzania hapa nchini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, yapo mambo mawili hapa moja anauliza kwa nini Serikali inapofanya maamuzi inachukua muda mrefu sana kuyatekeleza. Jibu langu kwa hili ni kwamba inategemea suala lenyewe linaloshughulikiwa, tunajitahidi sana Serikalini kutekeleza maamuzi yetu kwa haraka kwa kadri inavyowezekana na hasa pale ambapo kunakuwa hakuna vikwazo vya namna yoyote. Lakini inawezekana tukachelewa vile vile kwa sababu nyine za kitaalamu, za kifedha na kadhalika, lakini azma ya Serikali kwa kweli ni kutekeleza wajibu wake kwa kadri inavyowezekana kwa haraka sana.

Lakini lipo hili sasa ambalo ni mahususi kuhusiana na shirika, ninachowea kumwambia tu ni kwamba tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunalipa kila aina ya nguvu ili kuhakikisha kwamba linafanya vizuri pamoja na matatizo yote ya kifedha yaliyopo na matatizo mengine lakini bado tunao wajibu mkubwa wa kuhakikisha chombo hiki kinafanya kaziyake vizuri.

Kwa hiyo, nataka nimuhakikishie tu Mheshimiwa Chegeni kwamba tutafanya kila juhudhi na kwa kushirikiana na Wabunge naamini kabisa tutaweza kusaidia sana kwenye chombo hiki.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilivyosema maamuzi mbalimbali ya Serikali ni pamoja na watu kukaimu nafasi, kwa sababu unakuta mtu anakaimu nafasi kwa muda mrefu sana...

**SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni wewe unajua hilo ni swali jipya kabisa sasa.

**MHE. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu *ATCL* sasa hivi kiongozi anakaimu.

**SPIKA:** Basi lenga kwenye *ATCL*.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa *ATCL* amehamishwa na nafasi yake inakaimiwa na mtu mwingine, na bado shirika hili lina matatizo mengi sana.

Ni lini uamuzi wa Serikali utablegemeza shirika hili ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi na kufanya maamuzi yasiyokuwa ya kukaimu kaimu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala la *ATCL* wala tusilitazame tu kwa maana ya matatizo ya *management*, maana hata huu uamuzi unaouona umefanywa na Serikali na unaona mpaka sasa hatujafika mahali tukafanya uamuzi wa kusema tuwe na Mtendaji Mkuu ambaye ameteuliwa, ni kwa sababu kuna mambo mengi pale ambayo Serikali bado inayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga vizuri sana kufufua kampuni hii na nina hakika tutaweza. Katika mchakato ule ndiyo mambo yote yamezingatiwa Bodi pamoja na

*Management* vyote viko pamoja ikiwa ni pamoja na suala zima la fedha. Kwa hiyo, dhamira ipo na mimi naamini tulipofika siyo pabaya hata kidogo tutalikamilisha na utaona matokeo yake. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nimuulize Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2006 wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge wakati wa mjadala kwa wakati huo aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Edward Lowassa, wakati anahitimisha mjadala wa Bunge la Bajeti alitutajia Kamati ndogo ambayo itashughulikia suala la mfuko wa uwezeshaji maarufu kama JK. Baada ya kuundwa Kamati hiyo nilichokuwa nataka njue kwanza Kamati hiyo iko wapi? Na kama ipo imefanya kazi gani? Na naomba njue mafanikio yake hadi hivi sasa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala analoliulizia Mheshimiwa Juma Killimbah najua lina hisia kali kwa sababu zilizowazi. Fedha ambayo Mheshimiwa Rais aliamua kwamba itolewe na Serikali kwa ajili ya kusaidia kuwezesha jamii yetu hasa Watanzania, wakati kauli ile imetoka ilitoa matumaini makubwa mno, kwa sababu ukisema bilioni moja kwa kila mkoa unaona kama vile pengine italeta mabadiliko makubwa sana katika Mkoa unaohusika. Lakini ukweli unabaki pale pale kwamba fedha ile ilikuwa ni chachu tu lengo ilikuwa ni kuanzisha mfumo wa kuwa na mfuko wa mzunguko ambao utakuwa unakuwa mwaka hadi mwaka na hivyo kuongeza idadi ya watu wanaoweza kunufaika. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba ndugu yangu, Mheshimiwa Edward Lowassa wakati ule aliahidi kwamba ataunda Kamati. Ilikuwa ni Kamati ya kiutendaji ndani ya Serikali, Kamati ambayo imekuwa ikisaidia kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango mzima wa fedha ile ya JK. (*Makofi*)

Sasa awamu ya kwanza imepita, tulitoa taarifa, tumeonyesha ni vikundi kiasi gani vimenufaika na watu kiasi gani wamenufaika na mpango ule. Vikundi pamoja na vyama mbalimbali vya SACCOS karibu 50,000 wameweza kufikia fedha zile na kuzipata katika viwango tofauti tofauti. Lakini bado unaona fedha ile *impact* yake hatujaiona na nadhani ndiyo maana Watanzania wengi wanahoji na wangependa kuona fedha ile iko wapi. Hatujalikatia tamaa, tumekwenda awamu ya pili na katika awamu hiyo tunesema zile Wilaya zote ambazo mara ya kwanza hazikupata fedha, awamu ya pili lazima zilengwe na zipate zile fedha kutumia vikundi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nadhani tuendelee na jitihada hizi, najua haziwezi kuzaa matunda ndani ya mwaka mmoja au miwili kwa maana ya kuongeza wigo, lakini kadri muda unavyokwenda, nina hakika kabisa wengi zaidi watanufaika na ule mpango kwa kadri itakavyowezekana. Na sisi tutaendelea kufuatilia na kuona kama kuna haja ya kuboresha mfumo mzima wa namna ya kuzitoa zile fedha. (*Makofi*)

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi, nimuulize swali moja dogo tu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mfumo ambao tunao sasa ni wa Serikali mbili; Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Humu Bungeni tunaambiwa kwamba kuna mambo au kuna Wizara zinahusu Muungano na kuna mambo ambayo hayahuusu Muungano. Kwa mfano, Miundombinu, Afya na Elimu.

Sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu liko hapa, ambalo mimi linanitatiza, haya mambo ambayo si ya Muungano yanasisamamiwa na Serikali gani? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, niliamini leo nimepona, lakini naona niko pale pale. Ni kweli kabisa kwamba kwa mfumo wa Muungano wetu ulivyo yapo masuala ambayo yako chini ya Jedwali ambalo linagusa masuala ya Muungano na yako mambo ambayo tulikubaliana kwamba hayatakuwa chini ya Muungano. Sasa kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, yale mambo ambayo si ya Muungano yanasmamiwa moja kwa moja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa upande wa Bara au Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yale mambo ambayo hayapo chini ya mfumo wa masuala ya Muungano, masuala haya kwa makubaliano yatasimamiwa na Serikali hiyo hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa inawezekana unaona kuna utata na kwa kweli ukiniuliza mimi ningesema njia rahisi ilikuwa ni kufika mahali siku moja *Inshallah* Mungu akijalia, mnakuwa na Serikali moja na nchi moja, hiyo ndiyo ingetupa suluhu hiyo. Kwa sasa ni lazima tuendelee na mfumo huo ambao tumekubaliana. Kwa hiyo, sisi upande wa Jamhuri, tutakuwa tunashughulika na masuala ya Muungano, lakini kwa yale ambayo yamebaki si ya Muungano, Wizara zile zitaendelea kusimamia, lakini chini ya kofia ile ile ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi/kicheko*)

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa majibu hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mambo ambayo si ya Muungano lakini yanasmamiwa na Serikali ya Muungano, utakubaliana nami kwamba kwa mfumo huo Serikali ya Tanganyika imezama ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ningetumia lugha ya Mtume Issa, ningesema; “umenena”. Kwa hiyo, ninachotaka kusema tu ni kwamba hivyo ndivyo tulivyokubaliana kwamba kwa upande huu baada ya kukubaliana kwamba Tanganyika haitakuwepo tena, tutakuwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi yale masuala yote ambayo yalikuwa ya Kitanganyika Tanganyika, unaweza ukageuza ukatumia lugha unayoitumia, lakini bado msingi wake utakuwa ni ule ule wa Kikatiba kwamba hayo yanasmamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwishapita. Namshukuru sana na tena tukumbuke kwa Mkutano huu wa Kumi na Sita, hicho ndicho kilikuwa kipindi cha mwisho cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunamshukuru kwa yote aliyoyafanya katika kipindi kizima na tunamtakia afya njema aweze kuendelea na shughuli zake kama tunavyomtazamia. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 309

### Vituo vya Polisi Mipakani

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa bado kuna wimbi kubwa la ujambazi na biashara zisizo rasmi katika maeneo ya mipakani; na kwa kuwa hali hii huhujumu uchumi wetu na kutishia usalama wa raia na mali zao ikizingatiwa kuwa vituo vya polisi katika maeneo hayo ni vichache:-

Je, Serikali ina mikakati gani kabambe ya kujenga vituo vya kutosha vyenye watalaam wa vitengo vya Uhamiaji, *TRA* na polisi mipakani?

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum - Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanaishi kwa amani na utulivu. Aidha, wale wote wanaostahili kulipa kodi kwa shughuli wanazozifanya wanafanya hivyo, na wageni waliopo hapa nchini wanaishi kihalali.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali inahakikisha kwamba katika kila mipaka rasmi ya nchi yetu kunakuwepo na taasisi zote muhimu za Serikali ambazo ni Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Polisi na Idara ya Forodha (*TRA*) na hata maafisa wanaoshughulikia mazao na maliasili.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kujenga vituo zaidi na kuendelea kuimarisha vituo vilivyopo mipakani kwa kupeleka watumishi wa kutosha wenyewe ujuzi sambamba na vitendea kazi muhimu. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu itaanza ujenzi wa vituo vya polisi katika Kata za Kegonga mkoani Mara, Muhukuru mkoani Ruvuma, Horohoro mkoani Tanga na Mtambaswala mkoani Mtwara .

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imeanzisha vitengo maalum kikiwemo cha *Border Management and Operations* katika idara ya Uhamiaji na Kitengo cha Kupambana na Kuzuia Wahamiaji haramu na Biashara haramu ya Binadamu chini ya Jeshi la Polisi. Vitengo hivi vinashirikiana kufanya misako na *Operations* hapa nchini ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wale wote wanaojihusisha na uhalifu wa jinai. Kwa upande wa maeneo ya mipakani misako hiyo pia huhusisha watendaji wa *TRA* kwa lengo la kudhibiti wale wanaokwepa kodi. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba sasa ana mkakati wa kupeleka watumishi pamoja na vitendea kazi kwenye vituo vyetu vya mipakani pamoja na kujenga vituo vipyaa, je, katika kupeleka watumishi kwenye vituo hivyo vya mipakani, itakuwa ni pamoja na kukarabati vituo hivyo ambavyo havina hadhi kabisa ukilinganisha na vituo vya nchi jirani pamoja na kupeleka doria kwenye maeneo ya wazi huko mipakani ambayo ni marefu, ili kuendelea kudhibiti wahalifu pamoja na wafanyabiashara haramu katika mipaka yetu ambayo kuna njia zinaitwa njia za panya?

Swali la pili, kwa kuwa hawa wageni wanaoingia nchini wengi wao wanafikia kwenye nyumba za kulala wageni na wengine wanapokelewa na wananchi wetu, je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa agiza kali kwamba kila wahudumu katika nyumba za kulala wageni pale wanapowapokea wageni pamoja na kuandikisha maelezo yote iwe ni pamoja na kuonesha vitambulisho vya mkazi ama *passport* na vingine vinavyoonesha uraia wa mtu ametokea wapi, pamoja na wananchi wetu kutangaziwa kwamba, anapopokea mgeni ni lazima atoe taarifa kwenye maeneo husika ya Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili

ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala yake ni maswali lakini pia yana ushauri ndani yake, niseme kuwa ushauri kwa kweli ni mzuri na tunaupokea. Lakini niseme kwamba kuhusu suala la kwanza kukarabati vituo, nikiri kwamba hii ni changamoto ambayo tunayo lakini ni matatizo kama nilivyokuwa nasema hapo siku za nyuma kidogo kwamba matatizo tuliyonayo katika mipaka yetu mbali na kwamba mipaka ni mirefu kwa hiyo inatoa changamoto ya vitendea kazi kuweza kutizama hiyo mipaka jinsi tutakavyoweza kuitizama na kuchukua hatua zinazostahili kuchukuliwa.

Lakini niseme kwamba ni matatizo ambayo yamekuwa ya muda mrefu na kutokana na matatizo tuliyonayo katika Bajeti, tunajitahidi hatua kwa hatua kuona jinsi gani tutakwenda katika kutatua matatizo hayo lakini hiyo ya kukarabati vituo tunayo na tunaichukulia kama ni changamoto na nakiri kabisa kwamba baadhi ya vituo kwa kweli vimechakaa sana. Lakini sasa ndiyo tunajikuta tuna changamoto ya kutaka vituo vipyaa katika maeneo ambayo ni mapya ama ambayo yanataka vituo lakini katika baadhi ya maeneo ambayo vituo viro, vile vituo vimechakaa, ni vya muda mrefu kwa hivyo vinatakiwa kukarabatiwa kwa hiyo, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili tumekwishatoa maagizo kwa Jeshi la Polisi, kwamba watakuwa wanapita katika hizi nyumba za wageni ambazo tunaita *Guest house* na watakuwa wanashirikiana na watu wa uhamiaji na madhumuni ni katika hiyo hiyo, wasiwasi mkubwa tulionao wa wahamiaji haramu amba wanakuja kwa nia mbaya katika nchi yetu. Kwa hiyo, hilo linatekelezwa lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tutaliwekea nguvu zaidi kuona kwamba linatekelezwa kwa umakini na kwa nguvu zinazostahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi wanaopokea wageni wanaokuja nchini, changamoto tuliyonayo ni kweli tumekuwa tunajaribu kuwaambia wananchi kwamba wajaribu kufichua baadhi ya watu, maana yake Polisi Shirikishi au Polisi Jamii inataka ushirikiano wa wananchi kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nataka kukuhakikisha kwamba tutalifanya na tutatoa matangazo zaidi kuhakikisha kwamba Polisi na Uhamiaji wanakuwa na ushirika zaidi na wananchi ili tuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama. (*Makofii*)

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kiini cha swalii ni hoja ya ujambazi mipakani na vile vile Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu anasema mipaka yetu mingi ina uwanda mrefu sana, mmoja wa mipaka hiyo uko *Lake Tanganyika* na kwa bahati mbaya zaidi mpaka ule una ujambazi hasa wa kiharamia wa watu wanaotoka nchi jirani kuja kupora zana za uvuvi za wananchi wetu ni mkubwa, je, Serikali inasema nini kuhusu kuongeza doria na kufuatilia wale wanaokuja kuwapora watu wetu mali zao na kuwashafisha kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Manju Msambya, Mbuge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania mipaka yake ni mirefu na ni majirani na takribani nchi tisa kwa hiyo, unaona changamoto kubwa tuliokuwa nayo. Kuhusu uharamia na ujambazi katika eneo la *Lake Tanganyika*, hili ni suala ambalo Mheshimiwa Peter Serukamba, tumezungumza naye mara nyingi ni suala ambalo

Mheshimiwa Kabwe Zitto tumezungumza naye mara nyingi na amekuwa na *concerns* kubwa hata na wewe pia. (*Makofî*)

Lakini Mheshimiwa Mbunge, utakubaliana na mimi kuwa jitihada kubwa zinafanyika, tuna uhaba wa vitendea kazi lakini pia tuna jukumu la kuhakikisha kwamba tunalinda raia na mali zao na kwa kweli ukitazama ujambazi uliokuwepo miaka ya nyuma kidogo na sasa hivi, utaona kwa kweli jitihada zinafanyika na tunazidi kupiga hatua ingawa kweli changamoto bado zipo, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba tunakabiliana na hali hiyo. (*Makofî*)

Na 310

### **Vitambulisho vya Uraia**

**MHE. PONSIAONO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshindwa kutoa ufumbuzi wa suala la kutoa vitambulisho vya uraia kwa Watanzania:-

- (a) Je, ni lini hatma ya jambo hili ikiwa ni pamoja na usalama wa Tanzania kwa sasa na kwa siku zijazo?
- (b) Je, kutokana na ucheleweshaji wa kutoa vitambulisho, Serikali ina uhakika gani kuwa itakapoanza kutoa vitambulisho itawapatia raia wa kweli?
- (c) Je, vitambulisho hivyo vitatolewa vya aina ngapi kutegemeana na tofauti za uraia uliopo kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na pia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haijashindwa kutoa ufumbuzi wa suala la kutoa vitambulisho vya Taifa. Serikali inayo nia thabiti ya kuhakikisha kuwa raia wake na wageni waishio nchini kihalali wanakuwa na vitambulisho vya Kitaifa. Kutokana na umuhimu wa mradi huu, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Aidha, inakamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi atakayeunganisha mfumo mzima wa utunzaji wa kumbukumbu (*Database*) ambapo kwa sasa makampuni matano kati ya makampuni 54 yaliyoomba zabuni yamekwishapita katika hatua ya mchujo wa awali na hatua nyingine za kukamilisha taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa kutoa vitambulisho hautaathiri utambuzi wa raia halali wa Tanzania. Ili kuhakikisha kuwa vitambulisho hivi vinatolewa kwa raia halali wa Tanzania na wageni waishio nchini kihalali, Serikali inakusudia kwamba zoezi hili litaanzia katika ngazi ya vitongoji kwa kuwa huko ndiko watu wanafahamiana vizuri zaidi. Wizara yangu pia kupitia Idara ya Uhamiaji, imekwishaanza kuorodhesha wageni katika daftari maalum ambalo litatunza taarifa zote za wakazi katika kitongoji husika. Aidha, mchakato

mzima wa kutambua raia halali wa Tanzania na wageni wakiwemo wakimbizi, utashirikisha TAMISEMI na RITA.

(c ) Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina madaraja (*grades*) ya raia. Hivyo basi vitambulisho vitakavyotolewa vitakuwa vya aina mbili tu. Aina ya kwanza ni kwa raia wote wa Tanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kundi la pili ni kwa wageni wote waishio nchini kihalali.

**MHE. PONСIAONO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ni miaka mingi sasa imepita na hakuna dalili ya kuweza kufanikiwa kutolewa kwa vitambulisho, ni mchakato, mchakato kila siku, lakini Zanzibar tayari wana vitambulisho vya uraia, sasa swali langu hapa ni kwamba ni uwezo gani, maarifa, pamoja na mbinu gani ambazo zimewfanya Wazanzibar waweze lakini Tanzania bado inasuasua? Na vitambulisho vya Zanzibar ni hivi hapa.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionesha vitambulisho alivyodai ni vya Uraia wa Zanzibar )*

**MHE. PONСIANO D. NYAMI:** Swali la pili, kwa kuwa nchi nyingi ambazo zimekuwa zikitoa vitambulisho huwa zinatoa vitambulisho vya aina tofauti tatu au nne, vitambulisho vya raia wa kuzaliwa, raia wa kuandikishwa au tajinisi, raia wa kurithi au raia wa nchi mbili kama wapo na vinakuwa na rangi tofauti, je, Tanzania hatuwezi tukaandaa hivyo ili kutambua ma-group? Nashukuru!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Zanzibar ni sehemu, ama tuseme katika huu Muungano wetu tuna Zanzibar na tuna Tanzania Bara ambayo ndiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kusema kuwa Zanzibar wana vitambulisho vya uraia, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo si sahihi! Zanzibar wana vitambulisho vya ukazi siyo uraia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la uraia ni tofauti na ndiyo maana mchakato ni tofauti. Lakini nikiri kwamba Mheshimiwa Nyami anaposema kwamba mchakato umechukua muda mrefu, ni kweli umechukua muda mrefu, sasa hivi tunavyozungumza ni takribani miaka 30 lakini tumefika mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kwa ridhaa yako kwa sababu tarehe 8 Julai, 2009 takribani siku 23 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alilizungumzia suala hili kwa urefu sana ndani ya Bunge lako Tukufu na hata kabla ya hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alilizungumzia, kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Nyami uwe na amani kwamba tunakwenda vizuri na mahali tulipofika na kwa kweli sina mapya ambayo naweza nikazungumza sasa lakini nimhakikishie kwamba tunakwenda vizuri na tutafika mahali vitambulisho vya Utaifa vitatoka kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili, kama tulivyosema vitambulisho vya Uraia vitakuwa vya aina mbili, itakuwa ni kwa wale ambao ni Watanzania na wale ambao sio

Watanzania lakini wanaishi hapa nchini kihalali, ni aina hizo mbili tu. Sasa kama kutakuwa na mambo mengine ndani mle ya kusema huyu ni Mtanzania kwa vipi? Hayo ni mambo mengine lakini katika mtazamo mkubwa itakuwa ni sehemu hizo mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Sheria ya Vitambulisho vya Uraia ilipitishwa mwaka 1987, na kwa kuwa gharama za vitambulisho hivi zinaonekana kupanda kila siku; na kwa kuwa Zanzibar pamoja na kwamba ni vitambulisho vya Ukaazi lakini wameweza kuonesha kwamba wao walitumia Dola za Marekani Milioni Tatu ( \$ 3,000,000) kwa watu laki tano. Bajeti ya Serikali hapa inaonekana kwamba vitambulisho hivi vitatumia wastani wa Dola za Marekani milioni 221 (\$ 221,000,000) huoni kwamba wangetumia utaalamu ambaulishajengeka pale Zanzibar ili kupunguza mzigo huu wa gharama unaotaka kuwabambika Watanzania bila sababu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Hamad Rashid kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuitia Wizara yangu kwamba popote inapowezekana kupunguza matumizi, kubana matumizi, kutumia fedha ambazo zinatosheleza mradi ambaulisho unafanyika kwa gharama ndogo, hilo ndilo lengo letu kuu. Sasa hili ni wazo lakini pia niseme kwamba teknolojia ambayo inazungumziwa katika kutengeneza vitambulisho hivi ni teknolojia ambayo ni ya kisasa, na ni tofauti sana na hiyo ambayo kwa mujibu wa taarifa tunayo. Lakini bado nikuhakikishie kabisa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwamba bado mlango haujafungwa maana yake bado tumo katika suala hili la zoezi na pale ambapo itaonekana kweli ipo haja na ikathibitika tunaweza tukabana matumizi, tukatumia fedha kiasi kidogo ili kufikia hilo lengo letu ambalo tunalitarajia, sioni kwa nini pawepo na matatizo. Mimi nikutoe wasiwasi kwamba kumekuwa na hisia nyingi katika mradi huu na ni kweli kabisa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, lakini nia ni nzuri tu kwamba tutakapoona ipo haja ya kupunguza matumizi hayo tutafanya hivyo na ushauri wako tutauzingatia. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Ningependa kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, vitambulisho hivyo vitatolewa bure kwa Watanzania au vitauzwa? Kama vitauzwa, vitauzwa kwa bei gani, na je, kwa wale ambaulisho hawana uwezo wa kununua itakuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Kimaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali analouliza Mheshimiwa Kimaro ni sahihi lakini niseme kwamba tunajaribu kila njia kuona kwamba Mtanzania haingii katika gharama kubwa ama gharama ambayo hawesi kuimudu katika shughuli hii na ndiyo maana kwa sasa hivi siwezi nikakupa jibu ambalo liko sahihi, kwa sababu nikikwambia kwamba hivyo vitambulisho vitawekwa gharama ambayo itatoka kwa mpata vitambulisho, suala litakalofuata litakua ni gharama gani na kiasi gani? Na huko bado hatujafika kwa sababu bado tunatazama suala zima la vitambulisho vitakavyotengenezwa na wapi tutakapopata hizo fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba suala la Mheshimiwa Mbunge tunalizingatia na limo katika utaratibu lakini mpaka sasa hivi niseme kwamba hatuna jibu ambalo tunaweza tukampa Mheshimiwa Mbunge, vinginevyo sitaki niseme uongo kwamba tutafanya hivi , halafu tukaja tukafanya vingine na Mheshimiwa Mbunge akaja akasema mlipokuwa mnajibu swali hili mlajibu vile. Kwa hiyo, naomba tu atupe muda tunalitizama kama masuala mengine yoyote na tutakapokuwa na uhakika kabisa tutakuja hapa Bungeni tutasema kwamba njia na utaratibu utakuwa kama ifuatavyo. Ahsante! (*Makofi*)

Na. 311

### **Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini**

#### **MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepata mafanikio makubwa kutokana na mradi wa usambazaji umeme vijijini uliofanywa kwa lengo la kuibua uchumi kwa wanavijiji; miradi iliyopangwa kutekelezwa mwaka 2007/2008 katika wilaya ya Rorya haijaanza:-

- (a) Je, miradi mingapi ambayo mchakato wa utekelezaji wake umekwishaanza?
- (b) Je, ni miradi mingapi ambayo utekelezaji wake haujaanza na lini utaanza?

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Philemon Mikol Sarungi, Mbunge wa Rorya lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rorya ni Wilaya mpya yenyewe Tarafa nne, Kata 21 na vijiji 98 na inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 270,000. Mpaka sasa vijiji 19 tayari vimeshapatiwa umeme na vijiji saba visto katika orodha ya vijiji vinavyoombewa fedha kutoka katika mfuko wa umeme vijijini (*REA*). Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya umeme wa vijiji vya Rorya ziliombwa toka Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), lakinii hazikupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 zilitengwa fedha shilingi milioni 250 kwa ajili ya miradi ya umeme Rorya. Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka njia ya msongo wa kilovolti 33 iliyopo katika barabara ya Tarime na kupeleka umeme Nyanchabakenye yenyewe umbali wa kilomita 9.5 na kijiji cha Marasibona na uwekaji wa transfoma tatu kwa gharama ya shilingi kama milioni 462.2

Kwa upande wa vijiji vya Nyarombo, umeme utatokea katika njia ya msongo wa kilovolti 33 ya Shirati umbali wa kilomita 9 na kutawekwa transfoma moja kwa gharama ya shilingi milioni 463.5. Kijiji cha Masonga kitapatiwa umeme kutoka njia ya Shirati umbali wa kilomita 5.5.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mchakato wa utekelezaji wa miradi mitatu ya kupeleka umeme Marasibora na Nyanchabakenye, Nyarombo na Masonga katika Wilaya ya Ranya umekwishaanza, ambapo maandalizi ya zabuni kama tulivyosema juzi wakati wa kuhitimisha Makadirio ya Wizara kumpata mkandarasi yamekamilika na inatarajiwaa kutangazwa mwishoni mwa mwezi wa Julai, 2009 au mwanzo mwa mwezi ujao.

(b) Mheshimiwa Spika, miradi ambayo mchakato wake haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha ni miradi saba nayo ni kupeleka umeme Luagar, Bukama, *Sota Ferry, Changuge Health Centre*, Kisumu Ranya, Mwita wa Bachira, Kowak Sayi, Kibuyi, Ingrichini, vijiji hivyo saba. Punde fedha zitakopatikana, utekelezaji wa miradi hii utaanza kwa sababu utafiti umeishafanywa.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kijana wangu Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima, kwa majibu yake yenyeye matumaini makubwa na wananchi wa Ranya wamenipigia simu kwamba awafikishie pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wake na viongozi wote kwa kazi nzuri walioifanya kuwezesha miradi hii itekelezwe, nina swali moja tu la nyongeza.

Katika (b) wamesema punde fedha zitakopatikana, hizo fedha ni za ndani ama nje na zitapatikana lini? Naomba majibu yenyeye matumaini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, labda niseme kama tulivyosema juzi miradi ya *REA* ni mingi na inatofautiana kwa ukubwa. Kuna maeneo ambayo miradi yenyewe ambayo inatarajia *REA* itumbukize fedha ni shilingi bilioni 3 au 4 sehemu zingine ni milioni 250, 400 lakini miradi yenyewe ni mingi. Sasa tulichofanya kwanza kabisa kwa miradi ya Ranya ni kuvitambua hivi vijiji saba halafu pili, Serikali imejiwekea mikakati ambayo kusema kweli ni Bunge hili ambalo litaridhia huo uwezo mkubwa zaidi wa Ranya kutokana na ukusanyaji mkubwa zaidi wa mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa tukiweka tozo kwenye umeme, petroli vitu vyote hivi vikalenga kuingia kwenye mfuko wa *REA* ili kuipa uwezo zaidi mahitaji ya *REA* ni makubwa sana kulingana na mfuko wake. Kwa hiyo, mimi naomba nimhakikishie Mzee Mheshimiwa Sarungi kwamba miradi imefanyiwa kazi, tathmini kwa wakati huu wa mwaka huu 2009/2010 gharama inaeleweka na kwa hiyo, kulingana na upatikanaji wa fedha kwa ukusanyaji wa humu ndani na misaada mbalimbali ambayo tunatarajia kupata kwa wahisani utekelezaji wa miradi hii na miradi mingine ya *REA* tunatarajia itapata utekelezaji wa ufanisi.

Na. 312

### **Kuweka Lami Barabara ya Njombe - Makete**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Njombe hadi Makete kuititia Igori haipitiki; na kwa kuwa *TANROADS* iliahidi kujenga kilometra mbili kila mwaka katika kiwango cha lami:-

- (a) Je, mipango hiyo itaanza lini?
- (b) Je, gharama za ujenzi huo wa barabara kutoka Njombe hadi Makete ni shilingi ngapi?

## **WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe - Makete yeny urefu wa kilometra 110 ni barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Makete na mji wa Njombe kwenye barabara kuu ya Songea – Makambako. Barabara hii inahudumiwa na Wizara yangu kwa kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kilometra tano kwenye barabara hii kwa kiwango cha lami umeanza kuanzia Makete kuelekea Njombe. Mkandarasi yupo kwenye eneo la kazi na amekwishakamilisha maandalizi ya vifaa pamoja na mitambo muhimu kwa ajili ya kuanza ujenzi kulingana na mkataba.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Njombe – Makete kwa kiwango cha lami unakisiwa kugharimu shilingi bilioni 88 kwa wastani wa shilingi milioni 800 kwa kilometra moja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri kidogo yamenishtua sana, kwa sababu barabara hii ya kutoka Njombe kwenda Makete ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Makete na Njombe.

Sasa swal, kwa kuwa ushauri wa kitaalamu wa *TANROADS* ilikuwa barabara hii ianzie kujengwa Njombe kwenda Makete ikimaanisha kwamba lami inayojengwa Makete haitawasaidia wananchi wanaoishi Makete kama hapa katikati pana ukorofi kwa mfano maeneo ya Makoga, Ulembwe, Iyagala na mpaka sasa hivi sielewi ni kigezo gani cha kitaalamu kilichotumika kuanzia Makete wakati barabara hii inatakiwa ianzie Njombe kwenda Makete.

Swali lingine la pili ni kwa kuwa takriban miaka 22 ndiyo itakapokamilika kujengwa hii barabara ya lami kutoka Njombe kwenda Makete. Sasa kwa nini isiwe ni busara lile eneo korofi lianzie kujengwa kwa sababu gharama zinafahamika kwa lami ni shilingi milioni 800 kila kilometra moja, kwa nini isiwe busara kujenga maeneo ya Makoga ambako korofi au Lembwe au sehemu za Mang'oto au zile sehemu ambazo ni korofi kuliko kuanzia ambako wananchi hawatafaidika. Kwa sababu uamuvi wa busara ni kuanzia mwanzo kwenda mwisho, kuliko kuanzia mwisho kwenda mwanzo.

**SPIKA:** Hatima yake ni hiyo hiyo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa sababu barabara ile ya Makete - Njombe cha muhimu ni kwamba Serikali imeweka msisitizo kuhakikisha kwamba barabara hiyo yeny umuhimu mkubwa kiuchumi inajengwa na inajengwa kwa wakati muafaka ili kuondoa tatizo kubwa la usafiri katika eneo hilo. Kwa hivyo, busara zimeonyesha kwamba tuanzie Makete kwa Makao Makuu ya Wilaya ile ili kurahisisha usafiri kuanzia kule Makete.

Lakini ni kwamba hii barabara haitoishia kule Makete tu tumepanga kilometra tano za mkandarasi wa hivi sasa ambaye anajenga lakini tayari katika kasma ya mwaka huu wa fedha 2009/2010 tena Serikali imepanga kujenga kilometra tano za ziada kwa kasma ya shilingi 1,500,000,000/= ambazo zimetengwa ili tuweze kuipeleka kwa haraka iwezekanavyo. Azma

kubwa ni kuipeleka hii barabara kwa kasi ili tuweze kuimaliza mapema sio miaka hiyo 22 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anavyokisia. Sasa pamoja na ujenzi huu wa lami maeneo yote korofi fedha za ukarabati katika maeneo korofi zitaendelea kutengwa na TANROADS Mkoa itahakikisha kwamba maeneo korofi yote yanashughulikiwa ili barabara hii iendelee kupitwa wakati ujenzi wa lami unaendelea kutekelezwa.

Na. 313

**Utengenezaji wa Barabara za Nzega – Mpanda na  
Ipole – Rungwa – Itigi - Kigoma**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Nzega - Tabora – Ipole - Mpanda, Ipole - Rungwa na ile ya Itigi - Tabora - Kaliua na Kigoma ndizo zinazotegemewa na wananchi wa Mikoa ya Magharibi katika maendeleo ya kiuchumi ya mikoa hiyo; na kwa kuwa ahadi ya kuzitengeneza barabara hizo imeendelea kutolewa bila kutekelezwa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga barabara hizo ili ziwe za kudumu?
- (b) Je, Serikali inafahamu kuwa mikoa hiyo ya Magharibi inaweza kuendelea kubaki nyuma kiuchumi kwa kukosa miundombinu imara hasa ya barabara?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa miundombinu imara ni kichocheo cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kutokana na umuhimu huo ndiyo maana Serikali inafanya kila linalowezekana ili kujenga barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ahadi yake ya kuzijenga barabara zilizotajwa kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa ahadi hii upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Nzega – Tabora (km 115): usanifu wa kina wa barabara hii unaendelea na utakamilika mwezi Desemba, 2009. Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010 imetenga fedha shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

(ii) Barabara ya Tabora – Sikonge – Ipole – Koga – Mpanda (km 359): katika mwaka wa fedha 2009/2010, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 400 fedha za ndani kwa ajili ya kuifanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa lengo la kujenga kwa kiwango cha lami.

(iii) Barabara ya Ipole – Rungwa (km 192): barabara hii inaendelea kuimarishwa kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika muda wote wakati Serikali ikitafuta fedha za kujenga kwa kiwango cha lami.

(iv) Barabara ya Tabora – Urambo – Kaliua (km 126): upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hii kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2007. Mazungumzo na Serikali ya Kuwait kuhusu fedha za kugharamia ujenzi wa sehemu hii yanaendelea.

(v) Barabara ya Kaliua – Malagarasi – Ilunde (km 156): maandalizi ya ujenzi wa daraja la Malagarasi na barabara zake za maingilio zenye jumla ya urefu wa kilometra 48 yanaendelea chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea. Serikali pia inafanya mazungumzo na Serikali ya Saud Arabia ili kupata fedha za kugharamia kilomita 108 zilizobaki.

(vi) Ilunde –Uvinza – Kidahwe (km 104): mazungumzo na Serikali ya Abu Dhabi kupitia *Abu Dhabi Fund* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa barabara hii yamekamilika. Mkataba wa mkopo wa masharti nafuu unatarajiwa kusainiwa mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha 2009/2010.

(vii) Barabara ya Kidahwe – kigoma (km 35.7): ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unaendelea na unatarajiwa kukamilika Januari 2010.

(viii) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 270): Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, Serikali ilitenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa kuzingatia kuwa gharama za ujenzi wa barabara yote ni kubwa na uwezo wa Serikali ni mdogo, juhudzi zilielekezwa katika kutafuta msaada ama mkopo kutoka nje. Aidha, Serikali ilianzisha mchakato wa kuitisha zabuni za ujenzi wa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya baada ya kutiliana saini Hati ya Maelewano ama *Memorandum of Understanding* kati ya Serikali ya Iran na Serikali ya Tanzania mwezi Desemba 2008.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2009/2010, Serikali imetenga fedha jumla ya shilingi bilioni 9.76 kuendeleza azma ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutokea Manyoni kuelekea Tabora.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mkoa wa Tabora ndio mkoa pekee ambao haujaunganishwa kwa barabara za kiwango cha lami kama ilivyo mikoa mingine, je, kwa nini Serikali kwa makusudi isiweze kuusaidia mkoa huu kwa kuanzia kujenga barabara alizozitaja hasa zile za Manyoni, Itigi - Tabora, Tabora - Ipole – Koga - Mpanda zikajengwa kutoka Tabora kwa kiwango hicho cha lami?

La pili, kwa kuwa kwenye majibu yake Mheshimiwa Waziri kwenye barabara ile ya Ipole - Rungwa ya kilometra 192 wameonyesha kwamba barabara hii itaendelea kuimarishwa tu kwa kiwango cha changarawe bila hata zile hatua za awali za upembuzi yakinifu na usanifu kuonyeshwa katika utekelezaji. Napenda nimwulize Mheshimiwa Waziri kwa kiwango hiki ambacho anakieleza hapa azma ile ya Serikali ya kwamba ifikapo mwaka 2012 barabara zote kuu zitajengwa kwa kiwango cha lami itatimizwa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, swali lake moja kuhusu umuhimu wa barabara za mkoa. Hilo Serikali inalitambua na linalipa umuhimu mkubwa kuhakikisha kwamba mkoaa huu wa Tabora unaunganishwa na barabara za lami na mikoa mingine nchini Tanzania. Ni azma ya Serikali kuhakikisha Makao Makuu yote ya mikoa iwe

imeunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017 nina uhakika kwamba kazi hii kwa mkoa wa Tabora tutahakikisha tunaifanya kabla ya muda huo. Ndani ya mwaka huu wa fedha 2009/2010 nia madhubuti imefanywa kwa ajili ya kuunganisha kujenga barabara ya Tabora - Nzega na pia kujenga barabara ya Tabora - Kaliua ambayo tayari tutaanza na kilometra zile 16 za kutoka Tabora mpaka Tumbi lakini pia tuna mchakato wa kuunganisha Tabora na Manyoni kwa hivyo tutatarajia kwamba katika mwaka huu wa fedha tuweze kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua kwamba kwa upande wa barabara ambayo inaunganisha Tabora na Mkoa wa Mbeya kwa maana ya Tabora – Ipole - Rungwa hadi Mbeya kuna kipande cha Ipole ambacho hakijafanyiwa usanifu, hiki mwaka huu wa fedha tumeshindwa kukitengea fedha. Lakini kwa ujumla barabara hiyo tayari kazi imeshaanza Mbeya kwa kazi ambayo imefanywa Mbeya, Mbeya - Luhanjilo, Luhanjilo - Chunya na Chunya - Makongorosi ambazo kandarasi zake zimeshatoka kwa hivyo barabara hiyo nayo iko mbioni katika ujenzi wa kiwango cha lami tunatarajia kwamba ufuatilaji wa kazi hiyo utaiunganisha hasa Tabora na Mkoa wa Mbeya bila ya kusita na pengine kwa kipindi kifupi. (*Makofi*)

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kunipatia nafasi hii. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa utendaji wake mahiri sana ambao umezidi kuudhihirisha pale siku ya Jumapili iliyopita kuweza kuitembelea ile barabara Mheshimiwa Rais aliahidi kule mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Hai, Kwa Sadala - Masama, na kwa kuwa sasa upembuzi yakinifu na sanifu umeshakamilika kwenye hii barabara ya Kwa Sadala – Masama, je, Mheshimiwa Waziri ni lini hii kazi itaweza kuanzia ili kutumiza ile ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kwa pongozi. Jumapili iliyopita tu tulikuwa na ufunguzi wa barabara kule mkoani Kilimanjaro na nimetumia nafasi hiyo kuikagua barabara ya Kwa Sadala mpaka Masama. Tunaazimia katika mwaka huu wa fedha kuanza ujenzi katika barabara hiyo. Natambua kwamba tuna upungufu wa fedha katika Bajeti yetu ya mwaka 2009/2010 lakini nia iko pale pale na tumehakikishia tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wa Hai kwamba tutaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hiyo ndani ya mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimeona Mheshimiwa Selelii umehangaika sana sana, hebu tumalizie basi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa jicho lako zuri la kuniona.

Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri ile sehemu ya nne ya barabara ya Tabora – Urambo - Kaliua ameeleza kuna mazungumzo ya *Kuwait Fund*, lakini hakutamka kabisa juu ya makubaliano ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Tabora kwenda Tumbi kilometra 15. Je, mazungumzo haya ya *Kuwait Fund* yatakamilika lini na ujenzi huo wa kiwango cha lami kwa fedha za ndani unaanza lini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nimetaja barabara ya Tabora - Urambo hadi Kaliua yenyeye urefu wa kilometra 126 ikiwa inajengwa kwa ufadhilli wa nchi ya Kuwait. Mazungumzo haya ni ya uhakika tunaendelea nayo lakini kama nilivyo eleza wakati nawasilisha Bajeti yangu na hoja ambazo zilikuwa zimetolewa juu ya suala la Tabora hadi Tumbi urefu wa kilometra 16. Nilijibu kwamba ujenzi huo utaanza mwaka huu wa fedha kwa fedha za ndani ikiwa ni maandalizi ya kutegemea kwamba Kuwait itatupatia fedha za kuendelea na kazi hii kwenye barabara hiyo hiyo. Kwa hivyo, ni uhakika

kwamba barabara ya Tabora kuelekea Urambo hadi pale Tumbi itajengwa ndani ya mwaka huu wa fedha kwa kiwango cha lami kwa fedha za ndani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimwa Wabunge nadhani hapo ni pazuri kuishia kuhusu maswali. Muda wa maswali umepita. Matangazo tukianza na wageni.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo amba ni viongozi 22 wa Wizara ya Fedha na Uchumi wakiongozwa na Bwana Ramadhani Khija, Katibu Mkuu wa Wizara. Ahsante sana, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ni kama ifuatavyo, Profesa Beno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Yule pale, karibu sana Gavana tumefurahi kukuona, Bwana A. Kihwele, Mtendaji Mkuu Benki ya Posta Tanzania, yule pale na Bwana Njau Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa Dar es Salaam, yule pale. Sikupewa majina zaidi tangazo linasema tu wageni 13 wa Wizara ya Fedha na Uchumi amba ni Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Naomba kwa pamoja tafadhalii wasimame wale amba Wakuu mbalimbali wa Taasisi. Ahsante sana. Nitashangaa kama *TRA* hawapo, lakini kwa sababu ndio moja ya Taasisi muhimu sana za Wizara hii. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela amba ni wanafunzi sita kutoka Chuo cha Mahakama Lushoto amba wanaongozwa na Ndugu Nuhu Selemani, Rais wa wanafunzi. Wale pale ahsante sana, ahsante sana. Tunawataki mema katika mafunzo yenu tunawahitaji sana tuna upungufu mkubwa sana wa Mahakimu kila mahali katika nchi yetu. Kwa hiyo Ndugu Tesha, Ndugu Boniface Alpha, Ndugu Rehema Brayson, Ndugu Ester Injinji na Elmes Mtatina. Karibuni sana tunafurahi kuwaona. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Waheshimwa Wabunge Margaret Mkanga na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir na Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji amba ni waratibu wa Chama cha Wasioona Tanzania. Ndugu Michael Mkanjiwa pamoja na Ndugu Ruvuva Omari Ruvuva. Wale pale, ahsante sana. Ndugu John Tongoo na Ndugu Gordon Milangasi. Karibuni sana. Tunafurahi sana kukukaribisheni Bungeni na Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita liko imara kutetea maslahi ya wenzetu wenye matatizo ya ulemavu. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa William Kusilla na Mheshimiwa Mariam Mfaki ni Madiwani 29 wa Wilaya ya Bahi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Hussein Kamau na Mheshimiwa Nollo M. Mzanjila, Makamu Mwenyekiti, wale ndio Madiwani kutoka Wilaya ya Bahi. Tunashukuru sana kuwakaribisha Waheshimiwa Madiwani kutoka Bahi, jirani zetu hapo na karibuni sana kuendelea kuangalia shughuli za Bunge.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tume ya Mipango, Balozi Charles K. Mutalemwa naye yupo hapa, yule pale ahsante sana nashukuru sana karibu sana Bungeni. Yupo Bwana Carl Fox, Mkuu wa Masuala ya Siasa na Uchumi kutoka Ubalozi wa Marekani.

*From the American Embassy in Tanzania Mr. Carl Fox, you are warmly welcome to Parliament. It is always a pleasure for us to see in these chamber representatives of countries that have excellent relations in Tanzania. Thank you very much. (Applause)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Omar Kwaangw' amba ni Gabriel Sagday, Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Wilaya ya Babati. Yule pale amefuatana na Ndugu Hiiti Qambalali na Ndugu Stephano Salaho wale pale. Karibuni sana, karibuni sana. Wageni wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwanza ni Mkaguzi Mkuu Msaidizi ambaye ni

Bwana G. Teu. Yule pale karibu sana *Mr. Teu*. Mkuu wa Kitengo cha Mipango Ndugu Malima Mkilijiwando, yule pale, Mkaguzi Mkazi *RAS* Dodoma Martin Jidasaka na Ndugu Fortunatus Donge Mkaguzi Mkazi Bunge. Yule pale, ahsante sana karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dorah Mushi nao ni Elizabeth Aroma ni Missionari Shirika la *World Trumpet Ministry* Uganda, karibu sana. Yupo Bwana Twazihirwa Loshiro kutoka Taasisi ya *Cross Discipleship Ministry*, Mererani Mkoa wa Manyara. Wale pale ahsante sana karibu sana. Wako wageni 51 wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ni wanafunzi kutoka Chuo cha *UDOM* na *St. John's* wakiongozwa na Bwana Edson T. Mulyowa kutoka *St. John's University*. Sijui wako wapi aahh, wale pale, ndio. Nina hakika hawa kwa sababu ni wageni wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed watakuwa ni wanachama wa kile chama cha *CUF*. Basi muendeleze mjadala huko ni vizuri tu jamii yote imo katika vyama mbalimbali vya siasa ni jambo la afya tu kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Manju Msambya ambaye ni Bibi Mwani Msambya, mke wake. Yule pale ahsante sana. Naona mzee ni *Alhaj* na mama ni *Hajjat* basi mambo yamekaa vizuri tu na majina haya mume anaitwa Manju na mke anaitwa Mwani. Vizuri sana basi ni dalili ya kupendana hiyo. Wageni wa Mheshimiwa Pascal Degera kutoka Kondoa Kusini ni Ali Kilala Mwenyekiti wa Kijiji cha Mrijo Chini. Yule pale na Bwana Shabani Matereka Mwenyekiti wa CCM Kata ya Dalai. Ahsanteni sana karibuni sana kutoka Kondoa Kusini. Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o wakiongozwa na Paul Luchemba kutoka *Future Group International*. Yule pale karibu sana. Bwana Majula Mahendeka kutoka Taasisi hiyo hiyo na Bwana Justin Nyamoga. Ahsanteni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Janet Kahama ambaa ni kutoka Ujerumani wamekuja kujitolea kulea watoto yatima katika kijiji cha Matumaini Dodoma ni Ndugu Hannah Neuman, yule pale Mama Hannah Neumann na Andreas Otiker anayewasindikiza ni mjukuu wa Mheshimiwa Kahama ambaye anaitwa Anna Sayi Makwaiya. *We are happy to see our guests from Germany, it is a pleasure that we are coming for good course for Tanzania, keep up the good work please.* (*Applause*)

Wapo wanafunzi 40 na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Ufundji Hijra Dodoma, sio hao tena labda wapo kwenye ukumbi mwengine. Wapo wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Ualimu cha Donbosco Salesian Seminari Dodoma. Wale pale na Masista na viongozi, karibuni sana tunatumaini mnafanya kazi kwa bidii katika masomo kwa sababu nchi itaendelea kuhitaji wasomi wazuri lakini pia wenye nidhamu na uaminifu. Karibuni sana. Wako wanafunzi 20 na walimu wao kutoka Shule ya Menonite wakiongozwa na Mchungaji Musa Manwa, nadhani wamekosa nafasi pengine wako ukumbi mwengine. (*Makofi*)

Mheshimia Naibu Waziri wa Nishati na Madini anao wageni wake ambaa ni Ndugu Jaffer King'ande ambaye ni mtoto wa dada yake na anasoma Liverpool, Uingereza. Yule pale pamoja na mtoto wa kaka yake anaitwa Abdulfatah Ramadhani Dau. Karibuni sana tunawataki mema katika masomo na wewe ulie nje usije ukawaabisha wazazi wako na nchi yetu, kuna mambo ya ovyo ovyo huko. (*Makofi*)

Sasa matangazo ya kazi, leo Kamati zote zinakutana. Sijui humu Bungeni tutabaki wangapi? Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba saa saba mchana Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji wakutane Ukumbi namba 227. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje anaomba naye saa saba katika ukumbi namba 219 Wajumbe wote wa Kamati yake wahudhurie Kikao kifupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anaomba leo saa tano asubuhi hii Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane katika ukumbi namba 219. Hawa wote nimewapa ruhusa wafanye hivyo kwa sababu kuna masuala ya kuzingatia ambayo yatakuja kwenye *order paper* kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anaomba saa tano asubuhi katika ukumbi namba 133, wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, m Ulinzi na Usalama mkutane kwa Kikao namba 133 jengo la utawala. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane leo saa saba mchana ukumbi namba 231. (*Makofi*)

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mwenyekiti wa Kikundi cha Umoja wa Wabunge Maskauti anaomba wajumbe wote wa kikundi hicho wakutane leo saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Katibu wa Bunge anatangaza kwamba yapo maonesho ya *video* juu ya hali ya uchumi ya mwaka 2008 na viashiria vya umaskini kutokana na utafiti wa mapato na matumizi wa mwaka 2007 kwenye eneo letu la maonesho. Ni fursa nzuri ya kuona jinsi ambavyo masuala ya umaskini katika nchi yetu yanavyoshughulikiwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa pale kwenye eneo la maonesho ambayo yataendelea leo na kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba leo baada ya kuahirishwa Bunge pale jioni tukutane kwa ajili ya *briefing* kuhusu mfuko wa kuchochi maendeleo ya Jimbo (*CDCF*). Ni vizuri tukakaa pamoja kwa sababu kuna mambo mmekuwa ninyi wenye mkiulizauliza. Si ya wale Wanaharakati ambao! Ukiwa msomi unatakiwa kwanza ulielewe jambo ndiyo ulihoji. Hawa wetu wa siku hizi wengine wanashangaza sana. Muswada huu ni tofauti kabisa na jinsi wanavyajaribu kuueleza kwa wananchi na hatuelewi shabaha yao ni nini. Lakini sisi tukatulie tuelenze vizuri ili utakapokuja Bungeni tuweze kupitisha bila matatizo. Lingine ni kwamba kesho jioni na hii ni kwa kujipangia ratiba kesho baada ya kuahirishwa Bunge tutafanya ile tafrija yetu ya kawaida ya kufunga na mnajua Jumamosi ndiyo mwisho wengine watapenda kuondoka. Kwa hiyo, kesho Kamati yetu ya Tafrija chini ya Uenyekiti shupavu wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, wameandaa mambo mazito kweli kweli kesho. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nakuombeni sana muweze kuhudhuria ili tuweze kupongezana kwa kazi kubwa. Wale waliokosoana basi wasameheane. Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Sasa kuna uamuzi wa Spika.

**UAMUZI WA SPIKA (SPEAKER'S RULING) KUHUSU SUALA LA  
MHESHIMIWA SHOKA KHAMIS JUMA, LILILOJITOKEZA  
TAREHE 12 JUNI 2009**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, chimbuko la madai. Tarehe 12 Juni, 2009 Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, wakati akiuliza swali la nyongeza kuhusu mwitikio mdogo wa kupiga kura kwenye Uchaguzi Mdogo, alieleza kwamba: "Kuna Chama kimoja kikubwa

nchini (baadaye akakitaja Chama cha Mapinduzi) kina tabia ya kununua shahada za wapiga kura” na kumtaka Waziri mhusika atoe maelezo. Kabla ya kumruhusu Waziri atoe majibu. *Presiding Officer* wa siku hiyo Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika alimtaka Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, atoe ushahidi kama kweli kura ziliibiwa.

Baada ya Mheshimiwa Shoka kufafanua kuwa yeye hakusema kuwa kura ziliibiwa, bali kuna tabia ya kununua shahada za wapiga kura, Mheshimiwa Naibu Spika alimtaka athibitishe na hilo pia la ununuzi wa shahada za wapigakura.

Baada ya kipindi cha maswali kukamilika, Mheshimiwa Naibu Spika alimtaka Mheshimiwa Shoka Khamis Juma ifikapo tarehe 18 Juni, 2009 atoe uthibitisho wa kauli yake kuwa “Kuna Chama kimoja kikubwa sana hapa Tanzania kina tabia ya kununua shahada za wapiga kura, hususan wale kinaowaona hawakiungi mkono.”

Waheshimiwa Wabunge, ufanuzi, mapema mnamo mwezi huu, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, aliwasilisha kwa Spika ushahidi wake kuthibitisha kauli yake Bungeni. Baada ya kupitia vielelezo vyta Mheshimiwa Shoka alivyowasilisha ambavyo kwa kiasi kikubwa ni nakala ya magazeti yaliyoripoti mwenendo wa Uchaguzi Mdogo Jimbo la Busanda na kwingineko, na kwa kuwa hadi sasa hakuna shauri lolote lililoamuliwa Mahakamani wala na Tume ya Uchaguzi kuhusu ununuzi wa shahada za uchaguzi, madai ya Mheshimiwa Shoka hayajathibitika. (*Makofi*)

Kwa mujibu wa Kanuni 63(2) magazeti yanatambulika kuwa vyanzo rasmi vyta habari ambavyo vinaweza kutumiwa na Mbunge anapokuwa anazungumza Bungeni. Hata hivyo, maamuzi ya Spika katika Bunge hayawezi kufanyika kwa kutegemea magazeti peke yake. (*Makofi*)

Pili, shahada ya kupigia kura ni kitambulisho cha kupiga kura ambacho hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, ambayo imezuia mtu ye yeyote kuuza, kununua au kuhamisha umiliki wake kwa mtu mwagine. Hivyo, kuuza na kununua shahada ni kosa la jinai ambapo mahakama ikithibitisha, muuzaji na mnunuzi wanawenza kutiwa hatiani kwa mujibu wa sheria za nchi. Lakini Kukusanya takwimu ili kuhakiki wapigakura waliojandikisha si kuiba wala kununua shahada. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wa Spika ni kuwa kuto kana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa madai ya Mheshimiwa Shoka, bado ni tu huma (*allegations*) tu, kama yalivyo malalamiko mengine yanayowasilishwa na vyama vyta siasa juu ya ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi na ambayo bado hayajawahi kuthibitishwa na Mahakama.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia kuwa Bunge haliwezi kufanya maamuzi dhidi ya tu huma ambazo hazijathibitishwa katika Mahakama, na kwa kuwa yaliyoandikwa kwenye magazeti si ushahidi unaotosheleza kuthibitisha alichokitamka Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Bungeni, matamshi yake kwamba: “Chama kimoja kikubwa sana hapa Tanzania kina tabia ya kununua shahada za Wapiga Kura, hususan wale kinaowaon hawakiungi mkono” hakuyathibitishwa kwa kiwango kinachohitajika na ya Kanuni ya 63(6). (*Makofi*)

Hivyo basi, kwa kuwa Mheshimiwa Shoka alitakiwa kuthibitisha kauli yake Bungeni, hawezu kulindwa na Kanuni ya 63(2) na kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1) namwagiza Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, afute kauli yake niliyoinukuu hapo juu kabla ya mwisho wa Mkutano huu wa 16 wa Bunge. Uamuzi huu nimeutoa leo tarehe 30 Julai, 2009. (*Makofi*)

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza huo ndiyo uamuzi na tukizungumzia magazeti leo gazeti moja ambalo linatumwiwa na watu ambao hawanipendi kabisa eti linasema Spika ameingia njama za kuchoma Ofisi za Bunge ili afiche ushahidi wa matumizi yake. Kama kweli ningehitaji kuficha ushahidi wa matumizi, nani ataninyima *file* la Bunge hapa? Si naliondoa *file* tu. Eti niingie njama nikae na watu hebu nifikirieni mtu mzima kama mimi nikae nafanya mkutano wa njama. (*Makofi*)

Lakini niwaambieni tu kwa sababu lisirudie rudie sana hili. Wale maadui zangu wamechagua magazeti manne. Mojawapo linaitwa Tazama, lingine linaitwa Tanzania Daima na mengine mtakuwa mnayaona. Wanatunga vitu wanapeleka kwenye *internet* kwanza wala si watumishi wa Bunge. Ni kundi limekaa Dar es Salaam hata hivi sasa lipo kazini linaniangalia. (*Kicheko/Makofi*)

Wanatunga, wakishatunga wanaweza kwenye *internet* halafu magazeti yao yanaichukua hiyo kuwa ni habari. Ni mambo ya ajabu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi naomba ulinzi zaidi. Hii vita ni kubwa sana sasa. Ulinzi mnaonipa ni dhahiri hautoshi. Kama watu wanaweza wakafikia kufanya uhuni namna hii ndani ya nchi na kutumia fedha nyingi sana wala sisemi zile fedha wanazopeleka Jimboni. Nazo zile wanasaidia kupunguza umaskini Urambo wala hawatashinda. (*Makofi/Kicheko*)

Wananchi wa Urambo wanaelewa ninachokifanya kwa hiyo waendelee kupokea hiyo neema inayotujia ya mapikipiki na nini. Lakini tutashinda uchaguzi na Mungu akiniweka hai nitaendelea kuwa Spika katika kipindi kijacho cha miaka mitano. (*Makofi*)

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Majadiliano ya Kukuza Vitega Uchumi Kati ya Serikali ya Tanzania na Canada**

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kama itakavyokumbukwa tarehe 24 Juni, 2009. Wakati wa kikao cha kumi na mbili cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tarehe 9 Julai, 2009 kwenye kipindi cha Maswali ya Papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini aliuliza swali kufuatia taarifa za kwenye mtandao za majadiliano yanayofanywa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Canada kuhusu mkataba wa kukuza na kulinda vitega uchumi yaani *Foreign Investment Promotion Agreement*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Kabwe Zitto pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa majadiliano baina ya Serikali ya Tanzania na Canada kuhusu Mkataba wa kukuza na kulinda vitega uchumi hayakuanza mwezi Machi, 2008 bali mchakato wa mawasiliano kati ya Serikali hizi mbili yalianza mwanzoni mwa mwaka 2004 na kufuatiwa na majadiliano yasiyokuwa rasmi (*informal consultations*) tarehe 5 -6 Novemba 2007 yaliyofanyika Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majadiliano rasmi ya awamu ya kwanza yaani *formal consultations* yalifanyika Ottawa, Canada tarehe 11 – 14 Machi 2008 na kufuatiwa na awamu ya pili yaliyofanyika Dar es Salaam tarehe 5 -8 Mei, 2008. Majadiliano ya awamu ya tatu yalifanyika tena Ottawa, Canada tarehe 15 -19 Septemba, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi kumalizika kwa majadiliano ya awamu ya tatu, pande zote mbili bado hazijakubaliana kwenye vipengele vingi vya rasimu ya Mkataba na hivi sasa Kamati ya majadiliano inapitia mapendekezo mapya yaliyowasilisha na Serikali ya Canada kuhusu rasimu ya Mkataba husika kabla ya kuanza tena majadiliano ya awamu ya nne. Kwa kuzingatia maelezo hayo, suala la Tanzania kukubali kuharakisha mazungumzo halina msingi na wala halihusiani na mchakato wa Tume ya Jaji Bomani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chimbuko la majadiliano ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi. Tanzania imeridhia mikataba ilioanzisha *Multilateral Investment Guarantee Agency* au kwa kifupi *MIGA* pamoja ya ile ya *International Centre for Settlement Investment Dispute* zote zikiwa ni Taasisi zilizo chini ya Benki ya Dunia ambayo Tanzania na Canada ni wanachama. Malengo Makuu ya Taasisi hizi ni kuhakikisha kuwa vitega uchumi vya wawekezaji wa kutoka nchi moja hadi nyine vinalindwa ipasavyo pamoja na kuhakikisha kuwa migogoro inayotokana na vitega uchumi vilivyoewekezwa na wawekezaji kutoka nchi moja kwenda nchi nyine inasuruhihwa kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na kukubaliwa kimataifa.

Mikataba ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi yaani *Foreign Investment Promotion Agreement* au *Bilateral Investment Treaties* sio migeni na wala si mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa na majadiliano ya Mikataba ya aina hii. Tanzania ina mikataba ya aina hii na tayari inatekelezwa baina yetu na nchi za Uingereza, Sweden, Denmark, Finland, Italia, Uhlanzi, Uswis Afrika Kusini na Mauritius.

Mheshimiwa Spika, sambamba na majadiliano ya Serikali ya Canada, Tanzania inaendelea kufanya majadiliano ya Mikataba hii na Serikali za nchi mbalimbali zikiwemo za India, Jordan, Urusi, Malawi, Zimbabwe, Qatar, Algeria, Libya, Falme za Kiarabu, Iran, Uturuki, Oman, China, Slovakia pamoja na *OPEC Fund*. Masuala muhimu yanayojadiliwa kwenye mikataba ya *FIPA*. Vipengele muhimu vilivyozingatiwa katika makubaliano na nchi mbalimbali kuhusu Mikataba ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi ni pamoja na uendelezaji wa uwekezaji rasilimali, ulinzi wa vitega uchumi (*Investment Protection*, utoaji wa vivutio, utaifishaji wa rasilimali, fidia wakati wa matukio yasiyokuwa ya kawaida kama vile vita na machafuko, uhamishaji mali na faida, usuluhisho wa migogoro na utaratibu wa muda wa kuanza utekelezaji wa makubaliano.

Mheshimiwa Spika, haya yanaratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi na yanahusisha wadau kutoka Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali majadiliano ya kukuza na kulinda vitega uchumi kati ya Serikali za Tanzania na Canada yalianza mwanzoni mwa mwaka 2004 na bado yanaendelea. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa maslahi ya taifa yanalindwa kama ambavyo mikataba ya aina hii imefikiwa na inaendelea kutekelezwa baina yetu na nchi mbalimbali nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, dhana kwamba Serikali inafanya makubaliano na Canada ili kuingia Mkataba wa kulinda Makampuni ya Canada yaliyowekeza Tanzania kama ilivyoeleza kwenye baadhi ya vyombo vya habari vilivyonukuu Mheshimiwa Kabwe Zitto ni ya kupotosha ukweli. Mikataba ya aina hii inalenga kuwajengea imani na uhakika kwa wawekezaji kutoka nje kwamba vitega uchumi vyao vitakuwa salama nchini Tanzania kama Sera yetu ya kukuza uwekezaji ya mwaka 1996 inavyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 Wizara ya Fedha na Uchumi**

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu kwako mwenyewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge, kwa kuendesha majadiliano ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ustadi na umakini tangu yalipoanza hadi sasa. Aidha, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchambua mapendekezo ya Bajeti za Wizara, Idara na Mikoa na hatimaye kutoa maoni na ushauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyyoyatoa kwa Wizara. Nachukua fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujadili hoja mbalimbali kwa kina na umahiri na kutoa mapendekezo yanayochangia katika kuboresha utendaji wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee, kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika maandalizi ya Bajeti hii. (*Makofi*)

Aidha, ninawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, chini ya Katibu Mkuu Bwana Ramadhani M. Khijjah, na Naibu Makatibu Wakuu Bwana John M. Haule, Bwana Laston T. Msongole na Dr. Philip I. Mpango. Ninaomba ushirikiano walionipa uendelee ili tuweze kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ukamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara ya Fedha na Uchumi inasimamia utekelezaji wa majukumu muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea; kupunguza umaskini wa wananchi kwa namna iliyodhahiri; kujenga uwezo wa kugharamia bidhaa tunazoagiza toka nje zinazohitajika kusukuma maendeleo yetu; kuendelea kuimarisha Sekta ya Fedha ili iweze kukabili ipasavyo changamoto ya huduma na kukua kwa uchumi wa Taifa; kupunguza tofauti kubwa kati ya riba za amana na mikopo; kujenga mazingira mazuri ya kuziwezesha benki na asasi nyingine za kifedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake; na kuhakikisha kuwa wanaostaafu katika utumishi wa Serikali na taasisi zake wanalipwa mafao yao bila usumbufu na kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, mafanikio mengi yamepatikana yakiwemo yafuatayo:-

Wizara ilisimamia utekelezaji wa Mkakati wa Uboreshaji Makusanyo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuhakikisha uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji ili kupanua wigo wa kodi pamoja na kusajili walipa kodi wapya kama nilivyoeleza katika hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010. Hatua hizi zimesaidia katika kuongeza mapato ya ndani. Aidha, utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania na Mkakati wa Kusimamia Madeni, umeendelea kuboresha uhusiano na washirika wetu wa maendeleo na kuhakikisha upatikanaji wa misaada na mikopo yenyenye masharti nafuu kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usimamizi wa matumizi ya Serikali, Wizara iliendelea kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa wa kuandaa, kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma. Vile vile, Wizara ilichangia katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi kuititia Serikali za Mitaa (*D by D*), na kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi kwa kuhakikisha shughuli zote zinazohamishiwa kwenye Halmashauri zinapewa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza umaskini, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambao umeonyesha mafanikio katika maeneo mengi hasa katika kuongeza Pato la Taifa kutoka shilingi bilioni 20,948.4 mwaka 2007 hadi shilingi bilioni 24,781.7 mwaka 2008. Mapitio na marekebisho ya Sheria za Fedha ikiwemo Sheria ya Benki Kuu yameendelea kuimarisha sekta ya fedha ili iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, Sheria mpya zilitungwa zikiwemo Sheria ya Bima ya mwaka 2009 (*The Insurance Act, 2009*) ili kuboresha utaratibu wa kusimamia na kuimarisha shughuli za bima nchini; na Sheria ya Mikopo ya Karadha ya mwaka 2008 (*Finance Leasing Act, 2008*) ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya vifaa vya uzalishaji mali kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza tofauti iliyopo kati ya riba za amana na mikopo, mchakato wa kuondoa fedha za Serikali kutoka kwenye mabenki ya biashara na kuzihamishia Benki Kuu unaendelea. Aidha, Serikali imeendelea kupunguza mikopo yake kutoka kwenye mabenki ya biashara. Hatua hizi zinalenga katika kuboresha riba za akiba hivyo kuwashamasisha wananchi kuweka fedha zao katika akaunti za akiba. Vile vile, ili kuwashamasisha utoaji huduma ya mikopo yenyenye masharti nafuu kwa wanawake, Wizara imewezesha kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake kwa kutoa mtaji wa shilingi bilioni 2.1 kuititia Bajeti ya Wizara husika katika mwaka wa fedha 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Taifa linakuwa na fedha za kigeni zinazotosheleza uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje, hadi Juni, 2009 akiba ya fedha za kigeni iliongezekwa kufikia Dola za Kimarekani milioni 2,918.6. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji bidhaa kutoka nje kwa miezi 4.6.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa mafao yao bila usumbufu wala kucheleweshwa, Wizara imefanya uamuvi wa kuwashamasisha watumishi 54,996 waliostaafu kabla ya Julai, 2004 kwenye Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma (*PPF*) na wale waliostaafu baada ya Julai, 2004 kuwashamasisha kwenye Mfuko wa Pensheni ya watumishi wa Umma (*PSPF*). Kutokana na uamuvi huo, Serikali pia imeweza kuwalipa wastaafu kuititia akaunti zao binafsi kuanzia Julai, 2008. Wastaafu wanaolipwa kuititia akaunti zao ni wale tu waliohakikiwa na kuwasilisha taarifa za akaunti zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009 na malengo ya mwaka 2009/2010: Katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutekeleza majukumu yafuatayo; kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje pamoja na matumizi ya Serikali; usimamizi wa mali za Serikali; kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA; kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya uwezeshaji kiuchumi; kupanga mipango ya maendeleo; kuandaa na kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za Uhasibu, ukaguzi wa ndani Serikalini na Ununuzi wa Umma; na Kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Wakala za Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yamegawanywa katika mafungu manne ya Kibajeti kwa lengo la kuhakikisha kuwa yanatekelezwa ipasavyo na kwa ufanisi. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi; Fungu 21 - Hazina; Fungu 22-- Deni la Taifa; na Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (Fungu - 45) ambayo inajitegemea, inaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Mpango Mkakati ulioandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, MKUKUTA na Malengo ya Milenia, sambamba na kutekeleza Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) 2007/2008 – 2009/2010. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, mwenendo wa Bajeti na utekelezaji wa majukumu ya Wizara yalikuwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani mwaka 2008/2009: Katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Wizara iliendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Marekebisho ya hatua za mapato kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2008 yaliandaliwa na kukamilishwa, hivyo kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 kufanyika; kusimamia utekelezaji wa maboresho ya Mfumo wa Kodi; kuendelea kurekebisha na kupanua wigo wa kodi kwa kudahili walipa kodi wapya; na kuendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo: katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara iliendelea kuratibu na kuboresha upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka nje ya nchi. Katika kipindi hicho, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 1,988.11 ambazo ni asilimia 87 ya makadirio ya misaada kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza MPAMITA kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa misaada na mikopo kutoka nje. Mambo muhimu yaliyotekelawa katika kipindi cha mwaka 2008/2009 ni kuratibu mchakato wa kuandaa Sera ya Misaada ya Kiufundi (*Technical Assistance Policy*); kukamilisha mfumo mpya wa majadiliano kati ya Serikali na washirika wetu wa maendeleo kwa lengo la kupunguza gharama za ushirikiano baina yetu; na Kukamilisha mgawanyo wa ushiriki wa washirika wetu wa maendeleo katika sekta mbalimbali za uchumi wetu. Mbali na juhudi za ndani, Wizara pia ilishiriki katika mikutano ya kimataifa iliyofanyika New York, Accra na Doha kuzungumzia haja na mbinu za kuboresha ufanisi wa misaada kulingana na misingi ya Azimio la Paris la mwaka 2005 kuhusu misaada na mikopo kwa nchi maskini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara pia iliratibu maandalizi na uendeshaji wa mkutano wa kila mwaka wa mapitio ya utekelezaji malengo ya

misaada ya Kibajeti (*General Budget Support Annual Review*). Mkutano huo ambao baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kushiriki, ulifanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Novemba mwaka 2008. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwekwa sahihi kwa mikataba ya misaada na mikopo ya wafadhili mbalimbali kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za kuchangia Bajeti ya Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Serikali inategemea kupokea shilingi trillioni 3.18 kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo ikiwa ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Kati ya fedha hizi, shilingi trillioni 1.19 ni misaada ya Kibajeti, shilingi bilioni 572.92 ni mifuko ya pamoja na shilingi trillioni 1.42 ni kwa ajili ya miradi katika sekta mbalimbali. Kiasi hiki ni ongezeko la shilingi bilioni 722.41, sawa na asilimia 30 ya kiwango cha misaada katika Bajeti iliyopita. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi kwa mwaka 2008/2009: kulingana na taarifa za hesabu za matumizi ya Serikali hadi Juni 30, 2009, mwenendo wa matumizi katika mafungu yote matano (Fungu 50, 21, 22, 23 na 45 ) yaliyoombewa fedha na Wizara ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 50- Wizara ya Fedha na Uchumi: Kwa mwaka wa fedha 2008/09, Bajeti ya Fungu 50 kwa Matumizi ya Kawaida ilikuwa shilingi bilioni 36.30. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.52 zilikuwa ni mishahara, shilingi bilioni 21.14 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya idara zilizo chini ya fungu hilo, na shilingi bilioni 12.64 zilikuwa ni kwa ajili ya vyuo na taasisi zilizo chini ya Wizara. Bajeti kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 78.78. Kati ya hizo, shilingi bilioni 6.03 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 72.75 ni fedha za nje. Hadi Juni 30, 2009 Fungu hili lilipokea na kutumia shilingi bilioni 35.58 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 19.84 kwa matumizi ya maendeleo, kati ya hizo shilingi bilioni 3.99 ni za ndani na shilingi bilioni 15.85 ni fedha za nje. Upungufu katika matumizi ya maendeleo ulisababishwa hasa na kuchelewa kwa utekelezaji katika baadhi ya miradi ya *MCA-T* kutokana na taratibu za *MCC* kuchukua muda mrefu wa uchambuzi na mashauriano yanayojumuisha wataalam mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 - Hazina: Bajeti ya Fungu 21 kwa matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 736.71. Kati ya hizo, shilingi bilioni 1.11, ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 353.41 ilikuwa ni kwa ajili ya marekebisho na malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Serikali ya miezi sita, shilingi bilioni 126.77 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya *TRA*, shilingi bilioni 24 ilikuwa nyongeza ya mtaji wa *TIB*, shilingi bilioni 155.64 ni matumizi maalum na shilingi bilioni 75.78 kwa ajili ya matumizi ya fungu hilo. Makadirio kwa ajili ya fedha za matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 30.08. Kati ya hizo, shilingi bilioni 11.29 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 18.79 ni fedha za nje. Hadi Juni 30, 2009 matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 715.04 ambapo matumizi ya fedha za maendeleo yalifikia shilingi bilioni 20.81 kati ya hizo shilingi bilioni 9.58 ni za ndani na shilingi bilioni 11.23 ni fedha za nje. Upungufu wa matumizi ya maendeleo ultokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa: Bajeti ya Fungu 22 ilikuwa shilingi bilioni 684.57. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni 2009 matumizi yalifikia shilingi bilioni 682.23.

Mheshimiwa Spika, Fungu 23-Mhasibu Mkuu wa Serikali: Bajeti ya fungu 23 kwa matumizi ya kawaida ilikuwa shillingi bilioni 109.03. Bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi

bilioni 8.23 kati ya hizo, shilingi bilioni 1.77 zikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 6.46 fedha za nje. Hadi Juni, 30 2009 matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 106.63 na matumizi ya fedha za maendeleo yalifikia shilingi bilioni 1.39 kwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2.71 kwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Fungu 45: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Bajeti ya Fungu 45 kwa matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 13.30. Bajeti ya maendeleo kwa Fungu hili ilikuwa shilingi bilioni 6.23, kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 2.80 na fedha za nje zikiwa ni shilingi bilioni 3.43. Hadi mwezi Juni, 2009 matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 12.85 na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 3.93, kati ya hizo fedha za nje ni shilingi bilioni 2.65 na shilingi bilioni 1.2 ni fedha za ndani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kusimamia na kuendeleza uchumi: katika jukumu la kusimamia na kuendeleza uchumi, yaliyofanyika ni pamoja na: kutathmini maoteo ya takwimu za kiuchumi na matokeo yake kutumika katika kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2008 na maoteo ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010; kufanya uchambuzi wa Uhimili wa Deni la Taifa kwa lengo la kuangalia athari zake endapo Serikali itaamua kukopa kutoka soko la mitaji la kimataifa pamoja na kuangalia uhimili wa deni la taifa baada ya kutekeleza Mpango wa Nchi na Taasisi za Kimataifa wa Kusamehe Madeni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara kuitia Benki Kuu iliendelea kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha (*monetary policy instruments*) katika kudhibiti ukuaji wa ujazi wa fedha. Nyenzo hizo ni kama vile kuuza na kununua dhamana za Serikali za muda mfupi na muda mrefu, pamoja na kuuza na kununua fedha za kigeni. Aidha, Benki Kuu iliendelea kuweka uwiano mzuri zaidi katika mauzo ya dhamana za Serikali na fedha za kigeni katika utekelezaji wa sera za fedha kwa lengo la kuwa na utulivu katika viwango vya riba, pamoja na kuhakikisha kwamba gharama za utekelezaji wa sera ya fedha zinakuwa katika viwango vilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuchambua na kubuni sera, kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi; kuandaa sera na mikakati inayolenga kuongeza mapato ya ndani hadi kufikia lengo la asilimia 16.4 ya Pato la Taifa au wastani wa shilingi bilioni 394 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji rasilimali: katika mwaka 2008/2009 Wizara ilisimamia ukuzaji wa rasilimali za Taifa kutoka shilingi bilioni 6,209.7 mwaka wa fedha 2007/2008 hadi shilingi bilioni 7,381.3 mwaka wa fedha 2008/2009, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Ukuaji huu ilitokana na Uwekezaji katika ujenzi wa majengo; uagizaji wa vifaa vya uwekezaji mitaji; kuongezeka kwa uendelezaji ardhi, barabara na madaraja. Kwa ujumla, uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 29.7 ikilinganishwa na asilimia 29.6 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa: katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kusimamia uratibu na ulipwaji wa Deni la Taifa. Hadi mwishoni mwa Desemba 2008, Deni la Taifa lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 6,329 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 5,891.9 mwishoni mwa Desemba 2007. Kati ya Deni hilo, Dola za Kimarekani milioni 4,822.0 ni la nje na Dola za Kimarekani milioni 1,507.0 ni la ndani. Aidha, Deni la Taifa liliongezeka kutoka asilimia 31.8 ya Pato la Taifa mwaka 2007 hadi asilimia 32.6 mwaka 2008 ambapo deni la nje liliongezeka kwa asilimia 14.3. Ongezeko hilo lilitokana na malimbikizo ya deni hasa la nchi ambazo si wanachama wa *Paris Club*, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania pamoja na ongezeko la mikopo. Hata hivyo, Taifa bado linao uwezo

wa kuhimili deni hili. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kulipa riba na madeni yote yatakayoiva kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, uandaaji, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali: katika uandaaji, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuendelea kujenga uwezo wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuboresha uandaaji wa mipango na Bajeti pamoja na utumiaji wa mifumo ya kompyuta katika utoaji taarifa za utekelezaji; kurekebisha Mfumo wa Takwimu za Kifedha za Serikali (*GFS classification*) ili uendane na mabadiliko ya Kimataifa yaliyofanywa kwa lengo la kuwezesha kufanyika kwa uchambuzi wa kiuchumi na upimaji wa matokeo ya Bajeti katika uchumi; na kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu mfumo huo ambao umetumika katika kuandaa mipango na Bajeti kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara iliendelea na ukaguzi wa miradi inayotekelawa na Serikali kupitia Wizara mbalimbali, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali. Lengo ni kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa zinatumika kwa shughuli zilizopangwa. Wizara ilifanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kiufundi katika miradi mikubwa ya maendeleo 45 inayotekelawa ikiwemo miradi ya Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*). (*Makofi*)

Aidha, miradi mingine 258 ilikaguliwa ikiwemo ya kilimo, maji, umwagiliaji, elimu, viwanja vya ndege na barabara katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. Matokeo ya jumla ya ukaguzi huo yalionyesha kuwa, pamoja na miradi mbingi kutekelezwa vyema bado kuna changamoto nyingi, hususan katika kufuata ratiba za utekelezaji na uzingatiaji wa Bajeti zilizopangwa. Kwa mwaka 2009/2010 Wizara itaendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya Bajeti kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na kuendelea kuzijengea uwezo katika utoaji taarifa za utekelezaji na kufanya ukaguzi wa kitaalamu (*Technical Audit*) kwa miradi inayotekelawa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuondoa umaskini na uwezeshaji wananchi kiuchumi: katika jukumu la kuondoa umaskini na uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA na Mpango wa Ufuatiliaji (*MKUKUTA Monitoring Master Plan*) ili kupima mafanikio na changamoto zilizopo na kuiwezesha Serikali kuchukua hatua za kuondoa upungufu na kuboresha utekelezaji. Mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha kukua kwa pato halisi la Taifa kutoka asilimia 7.1 mwaka 2007 hadi asilimia 7.4 mwaka 2008; idadi ya Watanzania wasiojitosheleza kwa mahitaji ya lazima imeshuka kutoka asilimia 35.6 mwaka 2001 hadi 33.4 mwaka 2007 na wasiojitosheleza kwa chakula imepungua kutoka asilimia 18.7 mwaka 2001 hadi asilimia 16.5 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilikamilisha utayarishaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Kinga ya Jamii (*National Social Protection Framework*) ambao upo katika mchakato wa kupata idhini ya Serikali. Lengo la mfumo huu ni kusimamia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa sera na mikakati inayolenga kuboresha hali ya maisha ya makundi yaliyo katika hali ya umaskini uliokithiri pamoja na makundi tete kama vile watu wenye ulemavu; wajane na wazee maskini; watoto yatima wasio na msaada na wale waishio kwenye mazingira hatarishi. Malengo mengine ya mfumo huu ni pamoja na: kubuni mikakati na programu/miradi mipyä inayolenga makundi haya; kuboresha utekelezaji wa MKUKUTA na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji kwa kuwawezesha kiuchumi ili makundi haya yaweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji, kujipatia ajira na kujiongezea kipato na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi wa Taifa; na kukusanya rasilimali za kusaidia juhudzi za

Serikali kutoka kwa wadau wa maendeleo, wakiwemo sekta binafsi, washirika wa maendeleo na jamii kwa jumla kwa lengo la kuleta matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya uwezeshaji, Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi umekamilishwa na upo katika hatua ya kuchapishwa ili usambazwe kwa wadau mbalimbali kwa utekelezaji. Aidha, tathmini ya mafunzo ya elimu ya ujasiriamali ilifanyika katika mikoa ya Kagera, Dodoma, Singida, Rukwa, Shinyanga, Pwani na Morogoro. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa ujasiriamali, hivyo Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa elimu hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu midahalo ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa. Mdahalo wa Kitaifa ulifanyika Dar es Salaam tarehe 4 Desemba, 2008 chini ya uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Lengo la mdahalo huo lilikuwa ni kuainisha fursa na juhudzi za uwezeshaji kiuchumi zilizopo. Katika mdahalo huo yalitolewa maazimio na majukumu ya kila mdau katika ngazi zote ambayo ni pamoja na kutaka kila mkoa uwe na mpango mkakati endelevu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuwepo na dawati la uwezeshaji katika ngazi ya wilaya, mkoa hadi Wizara; kuweko vigezo vya kupima maadili ya utendaji bora kwenye makampuni, Mashirika, Wizara, Idara na Wakala za Serikali ili kuimarisha, ushiriki, uwazi na uwajibikaji; kufanya mabadiliko ya haraka ya sheria ili biashara ndogo zimilikiwe na Watanzania; biashara za jumla ziwe kwa ubia kati ya Watanzania na wageni; kuzifanya marekebisho sheria za madini ili leseni za uchimbaji ziwe ni kwa ubia na Watanzania; Serikali itoe upendeleo maalumu kwa makampuni ya Kitanzania na yale yanayosaidia uwezeshaji wa Watanzania kiuchumi hasa kwenye sera ya manunuzi; kuharakisha kupunguza gharama za kufanya biashara katika ngazi ya wilaya, mkoa na Taifa; na Wizara zote zishirikiane kikamilifu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili lifanye kazi yake ya uratibu na ufuatiliaji kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo; kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasisikini (MKUKUTA II); kusimamia mfumo unaotoa takwimu na kupima mafanikio ya MKUKUTA na Malengo ya Maendeleo ya Milenia; na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na udhibiti wa fedha: katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea na usimamizi na udhibiti wa fedha kwa kutekeleza yafuatayo; kutoa miongozo mbalimbali ya usimamizi wa fedha; kusimamia matumizi ya fedha za Serikali; kuunganisha Hazina Ndogo na Makao Makuu ya Wizara ili kuweza kurahisisha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha za Umma; kuendelea kufanya malipo ya Serikali ndani ya saa 24 baada ya kupokea hati za malipo zisizokuwa na matatizo; na Wizara iliandaa hesabu za Serikali za mwaka 2007/2008 kwa kutumia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji katika taarifa za hesabu za Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelizwa ni kama ifuatavyo; kuboresha muunganiko na usalama wa mtandao wa Malipo ya Serikali; kuandaa majumuisho ya maoteo ya taarifa ya mtiririko wa fedha kila mwezi; kukusanya taarifa za akaunti maalumu za Serikali kwa lengo la kuzifunga. Kufikia Mei 2009, akaunti 10,000 kati ya 24,000 za Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*PEDP*) zilifungwa; na kuboresha kitengo cha *Cash Management* kwa kutoa mafunzo ikishirikiana na wataalamu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kusimamia matumizi ya Serikali kupitia mtandao wa malipo ikiwa ni pamoja na kutayarisha majumuisho ya hesabu za Wizara, Mikoa na Idara zote za Serikali; na Kuboresha Kitengo cha *Cash Management* ili kiweze kusaidia katika usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamiaji na uratibu wa mifumo ya teknolojia ya habari; katika usimamiaji na uratibu wa mifumo ya teknolojia ya habari, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuandaa mfumo wa kutoa mishahara na kutunza kumbukumbu za wafanyakazi na mchakato wa kuuboresha na kuusambaza unaendelea; kuandaa mfumo wa kiteknolojia wa kuwezesha taarifa za wastaifu kuhamishiwa kwenye mifuko ya akiba; kuweka mfumo wa kuhifadhi na kuangalia mwenendo wa kesi zihuuzo kodi na unatumika katika ofisi za Rufaa za Kodi; kuhuisha mfumo wa mawasiliano wa Wizara. Aidha, mfumo wa malipo na utunzaji wa kumbukumbu za wastaifu wa Serikali ambao hawakuhamishiwa katika mifuko ya pensheni unaandalila. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu mifumo ya teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma, Wizara imefanya yafuatayo; malimbikizo ya nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi wa Serikali ya Januari – Juni, 2008 yalilipwa kuanzia mwezi Agosti, 2008; utaratibu wa kutoa nyaraka za kulipa mishahara kila tarehe 20 ya mwezi umeboreshwa na hivyo kuwezesha mishahara kuendelea kulipwa kabla au tarehe 23 ya kila mwezi kama ilivyo ahadi ya Serikali; kukamilisha ukaguzi wa nyaraka za malipo katika mikoa minne na Halmashauri zake ili kubaini watumishi waliostaifu, waliofariki na walioacha au kuachishwa kazi kwa lengo la kuondoa majina husika kwenye orodha ya mishahara. Katika zoezi hilo, kiasi cha shilingi milioni 248.28 ziliokolewa na kurejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha taratibu za ulipaji wa mishahara, uhakiki ulifanyika kwenye hospitali teule 84 za Wilaya, hiari na za mashirika ya kidini zinazopata ruzuku ya mishahara kutoka Serikalini, pia uhakiki huo ulifanyika kwenye Taasisi na Wakala za Serikali 29 zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Aidha, Wizara imeendelea kuhakiki malipo ya waajiriwa wapya, marekebisho ya kumbukumbu na mishahara ya wafanyakazi yanafanyika kwa usahihi. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kusimamia ulipaji wa mishahara kwa wakati kwa watumishi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma kwa wastaifu na warithi, katika juhudzi za kuboresha huduma inayotolewa kwa wastaifu, katika mwaka 2007/2008, Serikali iliamua kwamba huduma ya wastaifu inayotolewa na Hazina ihamishiwe kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Katika kutekeleza uamuza huo, Wizara iliwaelekeza wastaifu wote walioko kwenye daftari la pensheni la Hazina kufungua akaunti binafsi katika benki ili zitumike kuwalipa pensheni badala ya utaratibu wa zamani kulipwa fedha taslimu kupitia benki. Zoezi hili lilifanyika Tanzania Bara na Zanzibar sambamba na uhakiki wa Daftari la Wastaifu ili Wastaifu halali waendelee kulipwa pensheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na zoezi hili kufanyika kwa ufanisi utaratibu wa kulipa wastaifu kupitia akaunti zao binafsi ulianza Julai, 2008. Wastaifu wanaolipwa kupitia akaunti zao ni wale tu waliohakikiwa na kuwasilisha taarifa za akaunti zao. Wastaifu 54,996 walihakikiwa na kuhamishiwa kwenye Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) kutoka kwenye daftari la pensheni la Hazina. Wizara kupitia *PPF* inafanya uhakiki wa akaunti za wastaifu kila baada ya miezi sita ili kuhakikisha kuwa daftari la pensheni lina

orodha ya wastaaful halali. Katika mwaka 2008/2009, zoezi hili lilifanyika mwezi Novemba, 2008 na Juni, 2009. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010, kiwango cha chini cha pensheni kimeongezwa kutoka shilingi 21,601 hadi shilingi 50,114 kwa mwezi, sawa na ongezeko la asilimia 132. Serikali itaendelea kuboresha viwango nya pensheni pale ambapo hali ya mapato ya Serikali inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mirathi bado ni tatizo linalotakiwa kushughulikiwa kwa kushirikiana na Wadau wengine kwani linahusisha wadau mbalimbali. Mwezi Novemba na Desemba, 2008, Wizara ilifanya semina za kikanda kwa maafisa wa Wizara, Idara na Mikoa wanaoshughulikia huduma ya mafao ya wastaaful na warithi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Mahakama inaangalia uwezekano wa kuendesha semina kwa watendaji wa Mahakama na Hazina Ndogo ili kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa mali za Serikali, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara iliendelea kusimamia mali za Serikali kulingana na taratibu na kanuni zilizopo kwa kuhakiki bohari 350 za Serikali na kutoa ushauri kwa Maafisa Masuuli kuhusu upokeaji, utunzaji, utumiaji wa mali za Serikali na uondoshaji wa mali zisizohitajika pamoja na kuthamini mali za Serikali katika Wizara na Idara za Serikali 20; mali zenye thamani ya shilingi bilioni 51.17 zilithaminiwa; mali chakavu zenye thamani ya shilingi milioni 68.71 zilipata kibali cha kufutwa na kuondoshwa kwenye daftari. Shilingi milioni 528.82 zilipatikana kutokana na mauzo ya mali chakavu kwa njia ya minada ya hadhara; mali potevu zenye thamani ya shilingi milioni 8.48 zilizofutwa kwa kibali cha Bunge; Wizara ilichambua na kushughulikia madai mbalimbali yaliyowasilishwa dhidi ya Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.48 zililipwa kama fidia na kifuta machozi kwa makampuni na watu binafsi waliokuwa na madai mbalimbali dhidi ya Serikali. Aidha, Serikali ilifidiwa jumla ya shilingi milioni 110.25 kutoka kwa makampuni na watu binafsi walioisababishia hasara. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuandaa taarifa mbalimbali za usimamizi wa mali za Serikali na kuboresha uingizaji wa taarifa hizo kwenye daftari la mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi, ushauri na uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, katika mwaka wa fedha 2008/2009, jukumu la ushauri, uratibu na usimamizi wa shughuli za Wizara liliendelea kutekelezwa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Mpango Mkakati wa Wizara 2009/2010 - 2011/2012 ambao umetumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010; na kuhakiki na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi zake. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kusimamia na kufutilia utekelezaji wa Mpango Mkakati wake na kuandaa programu ya mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati wa kutekeleza Awamu ya Tatu ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP III*) ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2008. Mkakati huu unalenga kuongeza ufanisi katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kwa kuongeza rasilimali fedha kwenye maeneo yafuatayo; usimamizi wa Bajeti ya Serikali; mfumo wa matumizi; ukaguzi wa hesabu za umma; ununuzi wa bidhaa na huduma; na kuimarisha uwezo wa Kamati za Bunge katika utendaji wa kazi zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, kazi zilizofanyika ni pamoja na Mpango Mkakati wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP III*) ulikamilishwa ambao umewezesha kueneza programu kwa Wizara nyingine sita za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii, TAMISEMI, Afya na Ustawi

wa Jamii, Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Miundombinu; uanzishwaji wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani inayojitegemea; huduma za kitaalamu kwa Serikali za Mitaa kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma na matumizi ya kompyuta zilitolewa kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI; na uboreshaji wa usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma itajielekeza katika kuimarishe mtandao wa malipo ya Serikali (*IFMS*); ukaguzi wa ndani; usuluhisho wa taarifa za hesabu za benki, uimarishaji wa kutumia fedha halisi katika kutekeleza Bajeti ya Serikali (*cash budget management*); taratibu za ukusanyaji wa mapato; utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; ununuvi wa umma; ukaguzi wa hesabu na uwajibikaji kwa Bunge. Aidha, programu hii itaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto za usimamizi wa fedha za umma kadri zitakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara na Taasisi, katika kutekeleza majukumu ya kutoa ushauri wa kisheria, kuandaa nyaraka mbalimbali za kisheria, kusimamia maandalizi ya Miswada ya Sheria za Fedha na kushughulikia kesi na madai yanayohusu Serikali, Wizara ilifanya kazi zifuatazo; kukamilisha Muswada wa Sheria ya Bima wa mwaka 2009 ambao ulipitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2009 na kuwa sheria; kuandaa na kukamilisha Kanuni za Sheria ya Ukaguzi wa Umma (*Public Audit Regulations, 2008*); na kuandaa na kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ununuvi wa Umma Sura 410 ambayo tayari Serikali imeshatolea maamuzi; na kuandaa Sheria ya Nyongeza ya Bajeti ya mwaka 2009 (*Supplementary Appropriation Act, 2009*) kuhusu makadirio ya matumizi ya nyongeza ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009 iliyopitishwa na Bunge mwezi Februari, 2009. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuititia sheria za fedha na ununuvi na kutoa ushauri ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuvi wa umma, Wizara imeendelea kuimarishe shughuli za ununuvi wa umma kwa kuanzisha Kitengo cha Sera ya Ununuvi wa Umma. Kitengo hiki kimepewa jukumu la kusimamia, kubuni, kuendeleza na kupendekeza marekebisho ya Sera, Sheria, Kanuni, Nyaraka na Miongozo ya Ununuvi wa Umma ikiwa ni pamoja na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Ununuvi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Huduma ya Ununuvi Serikalini (*Government Procurement Services Agency*) pamoja na Bodi ya Wataalamu wa Ununuvi na Ugavi (*Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board - PSPB*) ambazo zilikuwa chini ya Wizara ya Miundombinu, kuanzia mwaka 2009/2010 zitakuwa chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Hatua hii ni kutekeleza ahadi ya Serikali Bungeni mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara kuititia Wakala wa Huduma ya Ununuvi wa Serikali katika kutekeleza Sera na kukamilisha mipango yake utafanya yafuatayo; kuanzisha utaratibu utakaoziwezesha Wizara, Idara na Halmashauri kununua vifaa na huduma zitumikazo mara kwa mara kwa pamoja kwa lengo la kupunguza gharama za ununuvi Serikalini; kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini iwapo ununuvi wa mafuta ya magari ya Serikali unaweza kufanywa kwa kutumia *Smart Card* ambapo kila gari la Serikali litapewa kadi kwa ajili ya ununuvi wa mafuta kwenye vituo vya *GPSA*; na kukamilisha ukarabati na kupanua uwezo wa visima vya mafuta Kurasini na Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuvi wa Umma (*PPRA*). Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara kuititia Mamlaka ya Ununuvi wa Umma ilifanya

yafuatayo; kuandaa mkakati wa kuzuia rushwa kwenye ununuzi wa umma ambao uliiwezesha mamlaka kusimamia, kufuatilia na kupima ukubwa wa tatizo la rushwa katika ununuzi wa umma kwa kutumia viashiria rushwa vilivyoainishwa katika mkakati huo; kuandaa mfumo wa kompyuta unaosaidia usimamizi wa ununuzi wa umma nchini (*procurement management information system*) kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za zabuni. Taasisi zaidi ya 100 kati ya 364 zimeunganishwa katika mfumo huu na mafunzo ya mfumo huu kwa taasisi zote za umma yanaendelea; kukamilisha Rasimu ya Kanuni za maadili ya Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2008; na kufanya ukaguzi wa ununuzi katika Taasisi 65 za umma ambapo ilibainika kuwa kiwango cha uzingatiaji wa Sheria kimeongezeka kutoka wastani wa asilimia 40 hadi asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inatarajia kufanya yafuatayo; kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mkakati wa kuzuia rushwa kwenye ununuzi wa umma; kuendelea na mchakato wa kumpata mtalaam mwelekezi atakayefanya utafiti wa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao (*e-Procurement*); kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, kanuni na taratibu zake; na kufanya ukaguzi wa ununuzi katika taasisi za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (*PPAA*), katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ilipokea jumla ya rufaa 25 ikiwa ni ongezeko la asilimia 127 ikilinganishwa na rufaa 11 mwaka wa fedha 2007/2008. Kufikia Juni, 2009 jumla ya rufaa 22 zilikuwa zimesikilizwa na kutolewa maamuzi wakati rufaa tatu zilikuwa zinaendelea kushughulikiwa na Mamlaka. Aidha, mamlaka ilitoa elimu kwa umma juu ya taratibu za uwasilishaji rufaa na malalamiko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Mamlaka inatarajia kupokea na kutoa maamuzi ya rufaa 30 zinazohusu ununuzi wa umma na kuzishughulikia katika muda uliowekwa kisheria. Aidha, mamlaka itaendelea na juhudhi za kuelimisha wadau juu ya haki zao na utaratibu wa uwasilishaji malalamiko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari, elimu na mawasiliano, katika kutekeleza jukumu la kuratibu habari, elimu na mawasiliano, Wizara imetua elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, machapisho na kushiriki katika maonesho mbalimbali kwa lengo la kuelezea majukumu yake. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha tovuti yake ikiwa ni pamoja na kuhuisha taarifa mbalimbali, pia imeratibu ushiriki wa vyombo vya habari katika mikutano na shughuli mbalimbali za Wizara. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu utendaji wake na utaratibu wa malipo kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa ndani, Wizara imeendelea kuimarishe kada ya ukaguzi wa ndani Serikalini kwa kusimamia ajira ya watumishi wa kada hiyo na kuboresha vitendea kazi; na kazi za kada ya Ukaguzi wa Ndani, kwa kutoa mafunzo na kufanya ukaguzi maalumu katika maeneo tofauti, ili kuimarishe usimamizi wa matumizi ya Serikali. Aidha, Wizara iko katika hatua za mwisho za kuanzisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani inayojitegemea katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), katika mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka ya Mapato Tanzania iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wake wa tatu kwa kusimamia na kutekeleza mfumo wa kodi pamoja na hatua za marekebisho ya kodi zilizopendekezwa ikiwemo kupanua wigo kwa kusajili walipa kodi wapya, kuendelea kutoa elimu ya biashara na ukokotoaji kodi kwa wafanyabiashara pamoja na kujijengea uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, *TRA* itaimarisha matumizi ya mtandao wa kompyuta. Hii itahusisha, uandikishwaji wa walipa kodi wapya, ulipaji wa kodi na uwasilishaji wa nyaraka za kiforodha kwa njia ya mtandao wa kompyuta (*Asycan*) pamoja na usimamizi madhubuti wa misamaha ya kodi kwa njia za kisasa ikiwa ni pamoja na kuboresha matumizi ya mtandao wa kompyuta wa *ASYCUDA++* ili uweze kutumika kwa kutumia intaneti. Aidha, katika kupanua wigo wa kodi, *TRA* itaendelea kusajili walipa kodi wapya kwa msingi wa Vitalu vya Walipa kodi (*Block Management System*), na utaratibu wa Taarifa ya Jiografia za Maeneo. *TRA* itadhibiti ukwepaji kodi kwa kuzingatia viashiria hatarishi na kuboresha usimamiaji wa mapato ya kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rufaa za kodi, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Bodi ya Rufaa za Kodi ilipokea, kusikiliza na kuzitolea maamuzi rufaa 72 kutoka kwa walipa kodi dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Aidha, Baraza la Rufani za Kodi lilipokea rufaa 17, zilizotokana na maamuzi ya Bodi ya Rufaa za Kodi, limesikiliza na kutolea maamuzi rufaa 15.

Mheshimiwa Spika, Bodi na Baraza wametoa elimu kwa walipa kodi katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Morogoro na Dar es Salaam kuhusu sheria za kodi na jinsi ya kutatua migogoro ya kodi na taratibu za kukata rufaa. Bodi na Baraza wamekamilisha maandalizi ya *Tanzania Tax Law Reports* ambazo zinajumuisha mwenendo na maamuzi ya rufaa zote zilizotolewa na taasisi hizo kuanzia mwaka 2002 hadi 2004. Ripoti hizo zinatarajiwa kutumika kama rejea kwa wanasheria, wasimamizi wa kodi, washauri wa kodi na taasisi za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Bodi na Baraza la Rufaa za Kodi wataendelea kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi ya Rufaa kwa wakati. Ili kuhakikisha migogoro ya kodi inaanuliwa kwa ufanisi, Bodi na Baraza wataendelea kutoa elimu kwa wajumbe wake na wadau kuhusu taratibu za kukata rufaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma, mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusudia kukusanya kiasi cha shillingi bilioni 90.27 ikiwa ni maduhuli. Hata hivyo, katika kipindi hicho Ofisi iliweza kukusanya maduhuli yapatayo kiasi cha shillingi bilioni 74.16 ikiwa ni pungufu ya makadirio kwa asilimia 17.8. Upungufu huo ni matokeo ya kutopatikana kwa Shillingi bilioni 15 za mauzo ya asilimia 5 ya hisa zilizotengwa kwa ajili ya wafanyakazi wa NMB. Fedha hizo zitakusanywa mwaka 2009/2010 baada ya wafanyakazi kulipia hisa zao. Aidha, hisa hizo zinaendelea kutunzwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuchambua Miundo na Kanuni za Utumishi, Kanuni za Fedha na Mifumo ya Mishahara ya Mashirika na Taasisi ambapo hadi kufikia Juni, 2009 miundo ya utumishi ya mashirika 35 ilikwisha chambuliwa, uchambuzi wa kanuni za utumishi kwa Taasisi 28 umekamilika na uchambuzi wa Kanuni za Fedha kwa Mashirika na Taasisi 28 umekamilika. Aidha, makadirio ya Ikama na Taasisi za Serikali 103 yalichambuliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya malipo ya mishahara na ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi za Umma zinawajibika kisheria kuwasilisha Mikataba ya hiari kwa idhini ya Msajili wa Hazina kabla ya kuanza kutumika. Mikataba ya hiari ikiwasilishwa kwa Msajili wa Hazina, inachambuliwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba Shirika lina uwezo wa kulipia makubaliano yao yote bila kuibebesha Serikali mzigo wa madeni pindi taasisi zinaposhindwa kutekeleza makubaliano ya Mikataba ya Hiari. Katika

mwaka 2008/09, uchambuzi wa mikataba saba ulikamilishwa na uchambuzi wa mikataba mitatu ya taasisi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura 257, uteuzi wa wajumbe wa bodi za mashirika ya umma unapaswa kuzingatia sifa mbalimbali zikiwemo elimu, uzoefu na maadili ya kikazi. Aidha, kifungu cha 12 cha Sheria hii kinatamka bayana kwamba mtu mmoja atateuliwa kuwa mjumbe wa Bodi zisizozidi tatu. Vile vile kifungu hiki kinampa mamlaka Msajili wa Hazina kuridhia uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma ili kuhakikisha matakwa ya Sheria hii yanazingatiwa ipasavyo. Aidha, katika kuimarisha usimamizi na menejimenti ya Mashirika na Taasisi za Umma, Wizara ilikamilisha marekebisho ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, utendaji katika Idara ya Msajili wa Hazina unakabiliwa na changamoto nydingi. Maeneo ambayo yanachangia ni pamoja na muundo wa Idara kuwa ndani ya Wizara; sheria ya Msajili wa Hazina inayokinanza na majukumu yake pamoja na sheria mbalimbali zilizoanzisha mashirika yanayosimamiwa na msajili; na idadi ndogo na taaluma ya watumishi waliopo ikilinganishwa na majukumu ya Msajili. Wizara kwa kutambua changamoto hizo, ilimteua mshauri mwelekezi ili afanye uchambuzi wa kina wa sheria zote zinazohusiana na utekelezaji wa majukumu ya Msajili wa Hazina na hatimaye kutoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Mshauri mwelekezi tayari amekamilisha kazi yake na kuikabidhi Wizarani. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itapitia taarifa hiyo ili iweze kuiwasilisha katika ngazi za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri zote za Wilaya na Miji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma pamoja na miradi inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia ina jukumu la kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali ambazo hesabu zake zinakaguliwa na ofisi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2008/2009, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilitekeleza yafuatayo; likagua hesabu za mafungu yote 49 ya Wizara na Idara za Serikali, Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, Halmashauri 133 za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Mashirika ya Umma 125, Balozi zote 32 za Tanzania zilizoko nje ya nchi na Wakala 33 za Serikali; kitengo cha ukaguzi wa ufanisi kiliimariswa kwa njia ya mafunzo na kukipatia vitendea kazi zaidi na ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi (*Value for Money Audit*) zilikamilishwa na ripoti mbili zipo katika hatua za mwisho kukamilika; kitengo cha ukaguzi wa kiutambuzi (*Forensic Audit*) kilianzishwa; ukaguzi kwa kutumia mifumo ya kompyuta katika Wizara 10 na Mikoa mitatu ulifanyika; ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa ya Singida na Mbeya ulikamilika, na ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa ya Lindi na Morogoro ulianza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Ofisi itatekeleza yafuatayo; kukagua hesabu za mafungu 49 ya Wizara na Idara zote za Serikali, Mikoa 21 ya Tanzania bara, Halmashauri 133 za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Balozi 32 za Tanzania zilizopo nje, Wakala 33 za Serikali, na Mashirika ya Umma 170; kukamilisha mchakato wa muundo mpya wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kukidhi mahitaji ya sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma (*Public Audit Act 2008*); kuandaa na kufanya ukaguzi wa ufanisi (*Value for Money Audit*)

katika maeneo manne pamoja na kukamilisha kaguzi mbili zilizokwishaanza; kuimarisha kitengo cha Ukaruzi wa kiutambuzi na kuongeza wigo wa ukaruzi wa kiutambuzi (*Forensic Audit*); na kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa ya Lindi na Morogoro pamoja na kuanza ujenzi katika mikoa mingine miwili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa biashara ya fedha haramu, kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu kimetekeleza yafuatayo; kuratibu shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu wa Fedha Haramu, Wizara iliratibu maandalizi ya Mkutano wa 17 wa Maafisa Waandamizi wakiwemo Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha, Sheria na Mambo ya Ndani wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika za Udhibiti wa Fedha Haramu na Ugaidi. Mkutano huu ulifanyika mnamo tarehe 31 Machi hadi 3 Aprili, 2009 mjini Arusha; kitengo kimeweka mfumo wa kompyuta katika ofisi zake ambao ni mahususi kwa uchambuzi wa masuala ya fedha katika kubaini fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi; kutoa miongozo mitatu kwa taasisi za fedha ambayo ni *Guideline for verification of customer identities, Anti-Money Laundering Guidelines to Banking Institutions, na Anti-Money Laundering Guidelines to Bank of Tanzania*. Aidha, katika mwezi Februari 2009, Wataalamu kutoka Umoja wa Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu kwa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika *The Eastern and Southern Africa Anti-Money Laundering (ESAAMLG) walifanya tathmini (Mutual Evaluation)* kwa nchi ya Tanzania kuhusu hatua za kisheria na za kisera zilizochukuliwa na Tanzania katika udhibiti wa biashara ya fedha haramu na ufadhilli wa ugaidi. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuboresha Kitengo ili kiweze kutoa huduma kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, katika mwaka wa 2008/2009, Tume ilifanya uchambuzi wa ripoti kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Taarifa ya uchambuzi huo imewasilishwa Serikalini ambapo Serikali kwa kutumia wataalamu wake mbalimbali imeifanyia uchambuzi ripoti hiyo na kutoa mapendekezo ambayo yatawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa hatua zaidi. Aidha, Tume imekamilisha uchambuzi wa uhusiano katika Sera za Bajeti na Fedha baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, na uchambuzi wa vyanzo vya mapato ya Muungano na Mfumo wa Takwimu. Vile vile, Tume imeanza kuandaa mwongozo wa uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na kutafiti Mfumo wa Bajeti na Kodi utakaokubalika kwa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Tume inalenga kufanya yafuatayo; kuendelea kukusanya na kuchambua taarifa za fedha zinazohusu mambo ya Muungano; kukamilisha uchambuzi wa deni la Taifa linalohusu serikali mbili (SMT na SMZ); kuweka mfumo utakaowezesha kufuatalilia mwenendo wa kiuchumi wa Serikali mbili; kukamilisha uchambuzi na kuandaa ripoti kuhusu Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja, Mfumo wa Bajeti na Kodi utakaokubalika kwa pande mbili za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifuko ya pensheni, katika kuhakikisha kuwa wastaifu wanapata mafao yao kutoka mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kutumia vigezo vinavyofanana, kusimamia uwekezaji wa fedha za wanachama ili kuhakikisha mafao ya wastaifu yanalipwa kwa mujibu wa sheria, Bunge lilipitisha Sheria ya Usimamizi wa Mifuko ya Jamii 2008 (*National Social Security Regulatory Authority Act, 2008*). Sheria hii inayosimamizi na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana itawezesha kuwa na msimamizi mmoja wa mifuko ya pensheni na mfumo mmoja katika kuwahudumia wastaifu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*), katika mwaka 2008/2009, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma uliendelea kutekeleza

majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Hadi Juni, 2009 mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 259.44, kati ya hizo Shilingi bilioni 215.63 ni michango ya wanachama na Shilingi bilioni 41.09 ni mapato yatokanayo na vitega uchumi. Aidha, mfuko ulifungua ofisi katika mikoa ya Tanga, Pwani, Ruvuma, Dodoma, Singida, Kilimanjaro na Morogoro ili kusogezza huduma karibu zaidi na watumishi na kufanya jumla ya ofisi za mikoani kufikia 14. Jumla ya Shilingi bilioni 115.75 zilitumika kulipa mafao ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi. Jumla ya Wanachama 3,033 walistaafu mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 384.80. Kati ya hizo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 295.27 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 89.53. Mfuko utaendelea kufadhili ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, makazi ya Askari Polisi na nyumba za gharama nafuu. Mfuko unatarajia kulipa mafao, kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi ya kiasi cha shilingi bilioni 209.99. Ifikapo Juni 2010, thamani ya Mfuko unatarajiwa kuwa shilingi bilioni 895.07 sawa na ongezeko la asilimia 18.52 kutoka shilingi bilioni 755.19 mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (*GEPF*), katika mwaka wa fedha 2008/2009, uliendelea kutekeleza majukumu ya kuboresha huduma kwa wanachama, kukusanya michango kutoka kwa wanachama, kulipa mafao kwa wastaafu na kuwekeza fedha za wanachama katika vitega uchumi vilivyo salama. Katika kipindi hicho Mfuko ulizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja na tovuti yake ili kuboresha huduma na kurahisisha mawasiliano. Hadi kufikia mwezi Juni, 2009 Mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 47.63 sawa na asilimia 101 ya malengo ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, *GEPF* itaendelea na zoezi la kupanua wigo wa wanachama wake kwa kuwafikia waajiri wengi zaidi kutoka waajiri 32 waliopo sasa. Mfuko unategemea kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 58.02 kutokana na michango ya wanachama na vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*, katika mwaka 2008, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma ulilipa mafao ya shilingi bilioni 36.9 kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 24.84 zilizolipwa mwaka 2007. Thamani ya mfuko katika mwaka 2008 ilikuwa shilingi bilioni 498.1 ikilinganishwa na thamani ya shilingi bilioni 391.3 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009, Mfuko unategemea kusajili wanachama wapya 35,000 kutoka sekta binafsi, mashirika ya Umma na sekta isiyo rasmi. Aidha, Mfuko utaendelea kufadhili ujenzi wa baadhi ya majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Hoteli mkoani Mwanza. Inategemewa kwamba Mfuko huo utakuwa na thamani ya shilingi bilioni 573.2 ifikapo Desemba, 2009. Mfuko unategemea kulipa mafao ya jumla ya shilingi bilioni 39.1 ifikapo Desemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za kibenki, Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Benki Kuu ilitekeleza yafuatayo; ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2), uliongezeka kwa asilimia 18.4 kwa mwaka ulioishia Mei, 2009 ikilinganishwa na lengo la asilimia 22.4; ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3), ilikua kwa asilimia 15.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 22.0 kwa mwaka; mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa shilingi bilioni 1,142.1 sawa na ukuaji wa asilimia 32.2; na akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa dola za kimarekani milioni 253.7 na kufikia dola milioni 2,918.6, kiasi hicho kinatosheleza uagizaji bidhaa kutoka nje kwa miezi 4.6.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Benki Kuu inatarajia kutekeleza yafuatayo; kudhibiti kasi ya upandaji wa bei na kuhakikisha inakuwa asilimia 6.0 ifikapo Juni, 2010; ukuaji wa mikopo kwa sekta ya binafsi isiyopungua asilimia 28.7 kwa mwaka; akiba ya fedha za kigeni ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne; kusimamia mabadiliko muhimu katika sekta ya fedha; kusimamia utulivu wa sekta ya fedha; na kuhakikisha uendelevu wa uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*), katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea kutekeleza azma yake ya kukuza mtaji wa *TIB* kwa kuipatia shilingi bilioni 18 zikiwemo shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kuanzisha dirisha la mikopo ya kilimo. Katika kipindi hicho, benki iliendelea kutoa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu. Mikopo iliyotolewa iliongezeka kutoka shilingi bilioni 40.46 mwaka 2007 hadi kufikia shilingi bilioni 71.58 mwaka 2008. Aidha, katika kipindi hicho amana za wateja ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 69.79 hadi shilingi bilioni 76.68.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Benki ya Rasilimali Tanzania itaendelea kufanyiwa marekebisho ili iweze kutekeleza jukumu lake jipya la Benki ya Maendeleo ya Taifa. Wizara imetenga shilingi bilioni 26 kwa madhumuni ya kuiongezea mtaji zikijumuisha shilingi bilioni 20 kwa ajili ya dirisha la mikopo ya kilimo ikiwa ni hatua ya mwanzo ya mchakato wa kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta Tanzania (*TPB*), katika mwaka 2008, Benki ya Posta iliendelea kutoa huduma za kibenki katika matawi yake ambapo matawi mawili zaidi yalifunguliwa na kufikisha idadi ya matawi 27. Amana za wateja ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 79.6 kutoka shilingi bilioni 73.8 mwaka 2007 likiwa ni ongezeko la asilimia 7.9. Aidha, utoaji wa mikopo umeendelea kukua mwaka hadi mwaka ambapo katika kipindi hicho, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 45.6 ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 36.4 zilizotolewa katika mwaka 2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.4.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Benki ya Posta italenga kufanya yafuatayo: kuboresha na kuhamasisha wananchi kijiwekea akiba; kuendelea kupanua wigo wa huduma za mikopo; kuendelea kutoa huduma ya *Western Union Money Transfer* kwa kuimarisha mawakala waliopo; kukuza matumizi ya mtandao wa kompyuta kwa kuanzisha huduma ya kutuma ujumbe mfupi kwa wenye simu za mikononi na benki mtandao (*Internet Banking*); na kufanya ukarabati matawi mbalimbali ya Benki. Aidha, Wizara imetenga shilingi bilioni moja ili kuongeza mtaji wa benki hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Twiga Bancorp Limited*, katika mwaka 2008, *Twiga Bancorp Limited* iliendelea kukusanya amana na kutoa mikopo kwa wateja mbalimbali. Hadi kufikia Desemba 2008, amana za wateja zilifikia shilingi bilioni 32.53 kutoka shilingi bilioni 27.73 mwezi Desemba, 2007 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 4.80 sawa na asilimia 17. Aidha, katika kipindi hicho benki iliweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 24.16 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.87 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2007 sawa na ongezeko la asilimia 122. Kutokana na utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, Benki ilikusanya mapato ya shilingi bilioni 6.16 na kupata faida ya shilingi milioni 254.8.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, *Twiga Bancorp Limited* imepanga kutekeleza yafuatayo: kutoa huduma kwa kutumia Mashine za kuchukulia Pesa (*ATMs*); kufunga matawi zaidi ya kibiashara katika miji ya Dodoma na Dar es Salaam; kuendelea kutoa mikopo kwa sekta ya viwanda na biashara ndogo na kati na mikopo ya

kulipia bima za wateja; na kuandikisha na kulea vikundi mbalimbali vyatuzalishaji mali chini ya *Village Community Bank (VICOBA)*. Aidha, Taasisi hii itaongezewa mtaji wa shilingi bilioni moja ili kuendeleza mchakato wa kuifanya kuwa benki kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Consolidated Holdings Corporation (CHC)*, katika mwaka 2008/2009, *Consolidated Holdings Corporation* ilitekeleza kazi zifuatazo: kukusanya madeni chechefu ya iliyokuwa *NBC* ambapo katika kipindi hicho shilingi bilioni 1.20 zilikusanywa; kuuza majengo na viwanja ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.12 zilipatikana; kushughulikia kesi 542 na kufanikiwa kumaliza kesi 85; kupokea mashirika 34 kutoka iliyokuwa *PSRC* na mashirika 28 yaliyokuwa yamesalia kutoka *Loan and Advances Realization Trust (LART)*. Katika kipindi hicho *CHC* ilikamilisha uuzaji wa hisa za Serikali katika *NMB Ltd* na Hoteli ya Embassy pamoja na kuuza mali za iliyokuwa *Plant and Equipment Hire Co. Ltd (PEHCOL)* na kukamilisha ufilisi wa mashirika saba kati ya tisa yaliyokuwa kwenye mchakato wa ufilisi.

Mheshimiwa Spika, *CHC* imefuatilia na kutathmini utendaji wa kampuni 55 kati ya mashirika yaliyobinafsishwa ili kujiridhisha kwamba kampuni husika zinafanya kazi kama ilivyokubaliwa kwenye mikataba ya ubinafsishaji. Aidha, Shirika limeendelea na jukumu la kusimamia hisa za Serikali katika *NBC Ltd*. na kupata gawio la shilingi bilioni 3.25. Shirika lilipata ziada ya shilingi bilioni 4.74 kutokana na shughuli lilizofanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za bima, idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (*Insurance Supervisory Department- ISD*), katika mwaka 2008/2009, sekta ya bima chini ya Idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima iliendelea kukua ambapo pato la bima lilifikia shilingi bilioni 181.1 mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na shilingi bilioni 150.3 mwaka 2007/2008 sambamba na kukua kwa pato la bima, idadi ya Makampuni ya bima, Madalali na Mawakala wa bima nayo iliongezeka. Idadi ya Makampuni ya bima iliongezeka kutoka 18 mwaka 2007/2008 hadi kufikia 20 mwaka 2008/2009, Madalali wa bima, kutoka 57 hadi 62, Mawakala wa bima kutoka 430 hadi 459. Madai ya bima yaliyolipwa yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 30.3 mwaka 2007/2008 hadi kufikia shilingi bilioni 51.2 mwaka 2008/2009, sawa na ongezeko la asilimia 69.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa (*NIC*), katika mwaka 2008, *NIC* imeendelea na biashara ya bima ambapo hadi Desemba 2008, makusanyo ya ada za bima yalifikia shilingi bilioni 25.2 na mapato mengineyo shilingi bilioni 14.4. Madai ya bima hadi kufikia Desemba 2008 yalikuwa shilingi bilioni 28.03. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Machi 2009, makusanyo ya ada za bima yalikuwa shilingi bilioni 5.0 na mapato mengine shilingi milioni 719 na madai yaliyolipwa yalifikia shilingi bilioni 1.14.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuza wa Serikali wa kulirekebisha Shirika la Bima la Taifa kabla ya kulibinafsisha kwa kuuza hisa kwa wananchi na wawekezaji mahiri, yafuatayo yamefanyika; kupunguza wafanyakazi na kubakia na idadi ndogo kulingana na biashara iliyopo; kuunda Bodi mpya inayosimamia urekebishiwa wa Shirika; kutayarisha muundo mpya na kutangaza nafasi za kazi zinazokidhi muundo huo; kuweka mtandao mpya wa kompyuta utakaorahisisha utendaji; pamoja na kutathmini majengo na viwanja visivyoendana na biashara na kuwasilisha taarifa Serikalini. Katika mwaka 2009, Shirika litaendelea kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusu njia bora ya kuliboresha na kuendelea na matayarisho ya Mpango wa Biashara ambao utatumika kama dira ya kuliongoza katika kipindi cha miaka mitatu ya marekebisho, na kuhakikisha madai ya wateja yanahakikiwa na kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya mitaji na dhamana, katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*) imeendelea kusimamia masoko ya mitaji na dhamana kwa kuidhinisha yafuatayo: uuzaji wa hisa za benki ya *CRDB* na *NMB* kwa umma; uuzaji wa Hatifungani za Kampuni ya *Aluminium Afica (ALAF)*; uuzaji wa vipande vyta mifuko miwili ya uwekezaji vyta *Unit Trust of Tanzania (UTT)* kwa wananchi; na kuorodhesha hisa za *Kenya Commercial Bank* katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, Mamlaka iliendelea kuridhia kuorodhesha kwa Hatifungani za Serikali za miaka miwili, mitano, na kumi katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya uanzishwaji wa Soko la Kukuza Makampuni (*Enterprises Growth Market (EGM)*) yanaendelea ambapo soko hilo linategemewa kuanza kazi mwezi Oktoba, 2009 chini ya Soko la Hisa la Dar es Salaam. Soko hili litawezesha Kampuni ndogo, za kati, na mpya kupata mtaji kwa kuuza hisa. Kufuatia uanzishwaji wa Soko hili, mafunzo kwa wadau mbalimbali na makampuni yanayotarajiwa kuorodhesha yatapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa sera za uanzishwaji wa soko la Hatifungani za Manispaa (*Municipal Bonds*) unaendelea. Utafiti huo utakamilishwa mwaka huu ili kuwezesha kuanza mchakato wa kuweka sheria na taratibu zitakazotumika katika kuanzia soko hili. Aidha, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka inaendelea na utafiti wa kuboresha shughuli zake ikiwa ni pamoja na kuboresha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya Mwaka 1994. Maboresho haya yatalenga katika ukuaji na usimamizi wa masoko endelevu ya mitaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*), katika mwaka wa fedha 2008/2009, Soko la Hisa la Dar Es Salaam liliorodhesha uuzaji wa hisa za *National Microfinance Bank (NMB)*, *CRDB Plc* na *Kenya Commercial Bank (KCB)*. Aidha, *DSE* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana (*CMSA*) ilifanikiwa kutoa elimu kwa umma kuhusu kuwekeza katika masoko ya mitaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Shinyanga, Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Soko la Hisa la Dar Es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*) litaendelea kuelimisha na kushawishi Kampuni mbalimbali kuorodhesha hisa zake katika soko la Dar es Salaam. Matarajio ni kuorodhesha Makampuni matatu ili ifikapo Juni, 2010 *DSE* iwe na jumla ya Makampuni 18.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (*UTT*), katika mwaka 2008/2009 *UTT* ilianzisha Mifuko miwili mipyä ambayo ni Mfuko wa Watoto na Mfuko wa Jikimu, na kufanya idadi ya mifuko kuwa minne hadi sasa. Mfuko wa watoto unaelekeza nguvu katika kumpa mwekezaji uwezo wa kupanga maendeleo ya elimu ya watoto wake, wakati Mfuko wa Jikimu unatoa fursa kwa mwananchi kujivekea akiba yake na kupokea mapato ya mara kwa mara. Aidha, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imeimarisha mfumo wa kompyuta wa kuhudumia wawekezaji kwa kuuboresha kutoka mfumo wa zamani kwenda katika mfumo mipyä ambao utaiwezesha *UTT* kuwa na uwezo wa kuwashudumia wawekezaji wake katika Mifuko minne iliyopo sasa na mifuko mingine itakayoanzishwa baadaye. Vile vile, *UTT* imeendelea kuimarisha mfumo wa pili wa dharura nje ya ofisi ambao utaiwezesha kurudisha huduma zake haraka wakati wa majanga iwapo yatatokea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, *UTT* inatarajia kupanua huduma kwa wateja kwa kufungua ofisi katika kanda tano nchini. Katika kufikia azma hiyo ya kuwa na

ofisi za kanda, *UTT* inakusudia kuingia makubaliano na Shirika la Posta ili kutumia majengo ya Shirika hilo kufungua ofisi zake. Katika kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, *UTT* inalenga kuanzisha Mfuko mpya wa uwekezaji utakaojulikana kama *Vision Tanzania Fund*. Mfuko huo unatarajiwa kutoa mitaji kwa wajasiriamali wadogo katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji, ufgaji, uvuvi na usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taasisi nyinginezo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*NBS*), katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea na kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa na takwimu za kiuchumi na kijamii zikiwemo, takwimu za Pato la Taifa kwa kila nusu mwaka kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2008 na takwimu za Mfumuko wa Bei kwa kila mwezi. Aidha, ripoti za tafiti zihusianazo na Mapato na Matumizi ya Kaya (*Household Budget Survey – HBS*), Viashiria Ukimwi (*HIV/AIDS Indicator Survey*) na Watu Wenye Ulemavu (*Disability Survey*) zimetolewa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Kazi ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika mfumo wa takwimu za kijiografia (*Geographical Information System - GIS*) umekamilika kwa asilimia 20 katika mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Morogoro, Dodoma na Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea na kazi ya kutenga maeneo kwa ajili ya matayarisho ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2012, kuendelea kutayarisha takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa ajili ya kufuutilia mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Katika jitihada za kuboresha takwimu nchini, *NBS* itaendelea na mchakato wa kuandaa Mpango Kamambe wa Kuimarisha Takwimu Tanzania (*Tanzania Statistical Master Plan*). Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kukamilisha ukarabati wa jengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (*NEEC*), katika mwaka wa 2008/2009, Baraza liliratibu utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ambapo hadi Juni 2009, mikopo yenyenye masharti nafuu ya shilingi 42.48 ilitolewa ikilinganishwa na shilingi bilioni 31.5 zilizokadiriwa hapo awali; Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi na mradi wa kuhudumia biashara ndogo (*SELF*) kwa pamoja ilitoa mikopo yenyenye thamani ya shilingi bilioni 68.58 kwa wajasiriamali 131,640 kupitia *SACCOS* 210 na vikundi 86. Kati ya wajasiriamali hao, wanawake ni 58,907 na wanaume 72,633. Aidha, mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa watendaji 1,889 kutoka *SACCOS* na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Pia uhamasishaji wa wajasiriamali kujiunga katika *SACCOS* ulifanyika na kufanikiwa kuongezeka kwa idadi ya *SACCOS* kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi 4,780 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Baraza litafanya yafuatayo; kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu na elimu ya ujasiriamali chini ya Mpango wa Serikali wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; kuendelea kutekeleza majukumu ya Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (*Mwananchi Empowerment Fund*); kutekeleza maazimio ya mdahalo wa Kitaifa wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi; kufanya tafiti kwa lengo la kubaini maeneo yenyenye fursa zinazoweza kuleta matokeo ya haraka katika uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuainisha sheria zinazokinzana na sheria ya uwezeshaji na kuzihuisha; kushirikiana na wadau husika kuainisha aina za biashara zinazostahili kufanywa na Watanzania pekee na zile zinazoweza kufanywa kwa ubia na wageni; na kuendesha warsha za viongozi katika ngazi za mikoa na wilaya kwa ajili ya kueneza, kuelimisha na kuhamasisha wadau mbalimbali juu ya Sera na Sheria ya Uwezeshaji Kiuchumi katika mikoa 14. Aidha, Wizara imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji wa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (*NBAA*) ilitekeleza yafuatayo: kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Utaalamu wa Uhasibu kilichopo Bunju wilayani Kinondoni; kudahili jumla ya wataalamu 3,599 katika ngazi mbalimbali za taaluma ya Uhasibu, na jumla ya makampuni 146 ya Wakaguzi wa hesabu; kukamilisha mpango wa kuboresha na kutenganisha majukumu ya Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi na yale ya usimamizi wa huduma kwa wanachama wake na hivyo kuwa na vyombo viwili vya kitaalamu yaani Taasisi inayojitegemea na Mamlaka inayosimamia sera na uendeshaji shughuli zote za kihasibu na ukaguzi wa fedha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 *NBAA* itahuisha mpango wake wa Maendeleo utakaonza kutekelezwa Julai, 2010. Katika mpango huo *NBAA* kwa kushirikiana na Wizara, itapitia na kuimarisha sheria zote zinazohusu uhasibu na ukaguzi wa fedha Tanzania; miongozo rahisi itatengenezwa kuziwezesha taasisi ndogo za kifedha (*MFIs*) na biashara ndogo na za kati (*SMEs*) kutayarisha taarifa za kifedha. Aidha, Bodi itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Utaalamu wa Uhasibu kilichopo Bunju wilayani Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (*GBT*) ndiyo msimamizi wa biashara ya michezo ya kubahatisha hapa nchini. Katika mwaka 2008/2009, Bodi iliridhia mkataba wa kuanzishwa kwa huduma ya uwekaji wa mfumo wa kompyuta (*Central Electronic Monitoring Systems*) katika *Slot Machines*. Madhumuni ya mfumo huu ni kurahisisha usimamizi wa mashine hizi pamoja na kuwezesha kutoza kodi kutohana na mapato ya kila mashine badala ya utaratibu wa sasa ambapo kodi hutozwa kwa idadi ya mashine. Bodi inatarajiwu kusaini mkataba huo mwaka huu wa fedha. Awamu ya kwanza ya mfumo huo utafungwa mara baada ya kusaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, bodi vilevile imekamilisha uandaaji wa kanuni mpya za *40-Machine Sites* ambazo zimekwishardhiwa na kwamba zinasubiri kuchapishwa rasmi katika Gazeti la Serikali ili ziweze kuanza kutumika. Leseni zitaanza kutolewa mara baada ya kanuni kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali. Uanzishwaji wa leseni mpya za uendeshaji wa *40-Machine Sites* ni aina mpya ya leseni ambapo muendeshaji atatakiwa kuwa na mashine arobaini katika eneo lake (*gaming hall*). Utaratibu huu ni mpya na una maudhui ya kasino ndogo isipokuwa hautakuwa na michezo mingine inayopatikana katika kasino. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Bodi inatarajia kukusanya kodi ya shilingi bilioni 5.7 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 4.11 kilichokusanya mwaka wa 2008/2009. Ongezeko hili litatokana na uanzishwaji wa *Televised Bingo* na *40-Machine Sites*, na kutoza kodi ya uendeshaji wa *slot machines* kwa asilimia ya mapato badala ya kodi ya *flat rate* hasa kutohana na kuwekwa kwa mitambo ya *Central Electronic Monitoring System*; na kuanzishwa kwa michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa (*National Lottery*). Mchakato wa kumpata mwendeshaji wa michezo wa Bahati Nasibu ya Taifa unaendelea na matarajio ni kuwa michezo huu utaanza rasmi mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa *Millenium Challenge Account- Tanzania*. Kitengo cha *Millenium Challenge Account – Tanzania (MCA-T)* kinawajibu wa kusimamia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la *Millennium Challenge Corporation (MCC)*. Miradi hiyo inahusisha miradi ya ujenzi wa barabara, Kiwanja cha ndege cha Mafia, usambazaji wa umeme na huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, *MCA-T* ilitekeleza yafuatayo: kusainiwa kwa makubaliano ya jumla ya utekelezaji wa miradi; kukamilisha masharti yote ya

makubaliano yaliyotakiwa ili kuweza kuanza rasmi kwa miradi; mikataba nane ya utekelezaji wa miradi iliwekewa sahihi kati ya *MCA - T* na taasisi mbali mbali; na kuwekwa sahihi kwa mikataba ya washauri waelekezi. Kwa wakati huu *MCA-T* iko katika hatua za kutoa zabuni za ujenzi kwa miradi inayohusika na hivyo shughuli za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa 2009 na mapema mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 kazi zilizopangwa ni kukamilisha mapitio ya makabrasha ya usanifu na mipango ya fidia katika maeneo ya barabara za Namtumbo – Songea, Peramiho – Mbinga, Tunduma – Sumbawanga na Barabara za Vijiini – Pemba. Kazi nyingine ni kuomba na kupata vibali vya hifadhi ya mazingira (*Environmental Certificates*) na kukamilisha uchambuzi wa wahandisi wasimamizi, makandarasi na hatimaye kuweka sahihi mikataba ya ujenzi. Aidha, usanifu na michoro ya kiwanja cha ndege cha Mafia na barabara ya Kilindoni – Utende unakamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya nishati, kazi zilizopangwa kwa mwaka 2009/2010 ni kukamilisha usanifu, michoro ya kihandisi, ripoti ya mazingira na fidia, kulipa fidia katika maeneo yote ya mradi na kupata makandarasi. Kazi za ujenzi wa Mradi wa Uwekaji Miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar zimepangwa kuanza Machi 2010. Vile vile, mikataba wa ujenzi wa Mradi wa Ukarabati na Usambazaji wa Miundombinu ya Umeme kwa Mikoa sita ya Tanzania Bara unatarajiwa kuwekwa sahihi Machi, 2010. Mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme na kujenga mtandao wa kusambaza Umeme Kigoma imepangwa kuwekwa sahihi Februari, 2010.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekeliza katika miradi ya maji kwa mwaka 2009/2010 ni kukamilisha mapitio ya michoro; kuandaa ripoti ya mazingira ya makabrasha ya zabuni kwa kazi ya ujenzi; kuwapata makandarasi wa ujenzi kwa ajili ya upanuzi wa machujo ya maji Ruvu Chini na ukarabati wa machujo ya maji kwa ajili ya mtambo wa maji mjini Morogoro. Kazi nyingine ni pamoja na kukamilisha makabrasha ya mikataba ya kitendaji (*Performance Based Contracts*) kwa mradi wa kupunguza maji yasiyolipiwa, kuendelea na utekelezaji wa programu ya kuzijengea uwezo *DAWASA/DAWASCO* ili ziongeze ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asasi za mafunzo kwa Taasisi ya Uhasibu Arusha (*IAA*), katika mwaka wa fedha 2008/2009 ilitekeleza yafuatayo: kudahili wanafunzi 2,871 ikilinganishwa na wanafunzi 991 mwaka 2007/2008, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 1,880. Aidha, Taasisi iliendelea na ujenzi wa maktaba.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhasibu Tanzania (*TIA*), katika mwaka wa fedha 2008/2009, Taasisi iliendelea na utoaji wa mafunzo katika fani za Uhasibu na Ununuzi kwa kutekeleza yafuatayo: kudahili jumla ya wanafunzi 1,802; kuajiri walimu wapya sita na kuwapatia mafunzo Walimu 10 katika ngazi ya shahada ya uzamili. Kazi nyingine zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya jengo la utawala; ununuzi wa kompyuta 100, vitabu elfu mbili vya masomo mbalimbali na software kwa ajili ya usimamizi wa wanafunzi na maktaba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Taasisi ya Uhasibu itakamilisha ujenzi wa Maktaba ya kisasa. Aidha, katika mwaka 2009/2010 taasisi itaaniszha kozi mpya saba za shahada ya kwanza na kozi mbili za shahada ya uzamili na inategemea kuongeza usajili wa wanafunzi kufikia 3,500 na inatarajia kuongeza jengo la ofisi na madarasa katika kampasi ya Mbeya ili kuongeza uwezo wa kuendesha kozi nyingi zaidi. Taasisi inatarajia kudahili

wanafunzi ngazi ya shahada katika fani za Uhasibu na Ununuvi. Aidha, Taasisi itaanza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala ambalo litakuwa na ofisi ya wafanyakazi, maktaba na chumba cha mafunzo ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), katika mwaka wa fedha 2008/2009, Chuo kilitekeleza yafuatayo: Mitaala ya shahada katika fani ya Uhasibu, Benki na Fedha, Bima na Hifadhi ya Jamii, Kodi na Teknolojia ya Habari na Sayansi ya Kompyuta ilitayarishwa na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Tanzania na kuanza kutumika; kuendelea kutoa mafunzo ya shahada ya uzamili kwa kushirikiana na Taasisi ya Biashara za Kimataifa ya India, Chuo Kikuu cha Strathclyde (Scotland), pamoja na Chuo Kikuu cha Avinashilingam kilichopo India. Aidha, katika kuongeza umahiri wa wahadhiri katika Chuo, wahadhiri 27 walidhaminiwa katika Shahada ya Uzamivu kati yao watatu walihitimu; wahadhiri 22 Shahada ya Uzamili kati yao 13 walihitimu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza uwezo, Chuo kimepata eneo la ekari 300 Msata wilayani Bagamoyo kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya pili ambayo ikitakilika itakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi zaidi ya 10,000, na hivyo kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Chuo kitaandaa mpango mpya kwa kipindi kingine cha miaka mitano cha 2009-2014. Aidha, katika kuongeza mapato na kuinua kiwango cha taaluma, Chuo kinakusidia kuboresha shughuli za utafiti na ushauri. Kwa upande wa mitaala Chuo kitaanza kutoa mafunzo ngazi ya Diploma katika fani zote. Hata hivyo, stashahada za juu zinaendelea kutolewa hadi hapo wanafunzi waliosajiliwa katika mafunzo hayo watakapohitimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – (*IRDP*), katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kiliendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri kwa wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo halmashauri za wilaya, miji na majiji, wizara, sekta binafsi na mashirika ya kidini. Vile vile, utekelezaji wa shughuli za uboreshaji wa miundombinu na kujenga uwezo wa utendaji wa watumishi wa chuo uliendelea. Matokeo yalikuwa ni kuongeza udahili kutoka wanafunzi 1,070 mwaka wa masomo 2007/2008 hadi wanafunzi 1,359 mwaka wa masomo 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa yaliyolenga kuongeza stadi za kuboresha usimamizi wa shughuli za maendeleo kwa ufanisi. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na: utawala bora, uongozi na utungamanishaji (*mainstreaming*) wa mfumo wa uandaaji wa mipango kwa kutumia fursa na vikwazo kwa maendeleo; pamoja na mafunzo ya uchambuzi wa sera ya kuondoa umaskini kwa taasisi za kiraia. Mafanikio mengine ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kwanza la taaluma na kuanza kutumika. Ujenzi wa ukumbi wa matumizi mbalimbali umefikia asilimia 80, matarajio ni kulikamilisha ifikapo mwezi Novemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo kitaanza ujenzi wa jengo la pili la taaluma, pia kitakamilisha ujenzi wa jengo la ukumbi na kutafuta eneo la hekta 17 kwa ajili ya upanuzi wa Chuo. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi, viongozi wa Halmashauri na Wajasiriamali ili kutoa huduma bora katika programu ya uboreshaji wa utendaji wa Serikali za Mitaa hususan katika kutekeleza Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi kuititia Serikali za Mitaa (*Decentralization by Devolution (D by D)*). Vile vile,

Chuo kitajenga uwezo wa kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu zitakazotumika katika utayarishaji wa mipango ya maendeleo vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (*EASTC*), katika mwaka 2008/2009, kilisajili wanafunzi wa cheti na stashahada 141, kiliendesha mafunzo kwa wafanyakazi 16 wa Bima ya Afya ili kuwajengea uwezo wa uchambuzi wa takwimu za Afya na Bima za Afya na kozi ya mbinu za utafiti wa kitakwimu kwa washiriki 9 kutoka nchi mbalimbali. Kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), chuo kiliendesha warsha ya mfumo wa kulinganisha bei (*PPPs*) chini ya mradi wa *EASTC-ICP* Afrika. Aidha, Chuo kilianza mchakato wa kuanzisha shahada ya Takwimu kukidhi mahitaji ya soko la nje na ndani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo kilitekeleza yafuatayo: kukamilisha jengo la maktaba na maabara ya kompyuta; kuanza ujenzi wa jengo moja la madarasa; kufanya ununuvi wa samani za ofisi, maktaba, maabara; na kuweka Mfumo wa Mawasiliano ya Kompyuta kwenye maktaba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo kitatoa mafunzo ya Shahada ya Takwimu. Pia kitaendelea kutoa mafunzo ya Cheti na Stashahada ya Takwimu kwa wateja mbalimbali, kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya uchambuzi wa takwimu kwa Idara za Serikali, Mashirika ya umma na watu binafsi. Chuo kitaendesha tafiti za kitakwimu, na kufanya ushauri elekezi kwenye maeneo ya takwimu. Aidha, Chuo kitashirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Kilimo inayoendelea nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, changamoto na hatua ilizochukuliwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Fedha na Uchumi ilikabiliwa na changamoto zikiwemo zifuatazo:

Mheshimiwa Spika, msukosuko wa fedha na uchumi duniani umeanza kuathiri uchumi na Bajeti ya Serikali. Sekta zilizoathirika ni kilimo, viwanda, utalii na madini (isipokuwa dhahabu). Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuunusuru uchumi kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 10/6/2009 na maeleo yangu kwenye hotuba ya Bajeti ya Serikali 2009/2010. Hatua zilizochukuliwa hadi sasa ni pamoja na zifuatazo; Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuongeza bei ya pamba kutoka shilingi 360 iliyotangazwa awali hadi kufikia shilingi 440 kwa kilo. Hatua hii itawasaidia wakulima kuuza pamba na vilevile kuwashamasisha kuendelea na kilimo cha zao hilo katika msimu ujao.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kufidia vyama vya ushirika na vyombo vingine vya fedha vilivyoathirika na msukosuko umeanza kutekelezwa ili kuviwezesha kuendelea na ununuvi wa mazao kwa msimu huu. Tayari Benki Kuu imekamilisha uchambuzi wa vyama vya ushirika vilivyoathirika na msukosuko huu pamoja na viwango vya fidia itakayotolewa. Kilichobaki ni kukamilisha taratibu za kufanikisha hili. Aidha, mifuko ya *Export Credit Guarantee Schemes (ECGS)* na *Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme (SMECGS)* itaongezewa mitaji ili iweze kuendelea kukopesha wahusika. Sehemu ya fedha kwa mifuko hii zitaanza kutolewa kuanzia robo ya kwanza ya mwaka mpya wa fedha. Vile vile, Wizara imekwshawasiliana na Benki Kuu kuhamishia Wizarani albaki ya fedha za *EPA* ili zitumike kuongeza mtaji wa *TIB* katika dirisha la mikopo kwa ajili ya sekta ya kilimo. Hatua nyingine za kukabiliana na msukosuko zitaendelea kutekelezwa kadri maandalizi yatakavyokamilika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokufikiwa kwa lengo la mapato kwa mwaka 2008/2009, makusanyo ya mapato kwa mwaka 2008/2009 hayakufikia lengo. Hali hii imechangiwa na msukosuko wa kiuchumi duniani. Wizara, katika mwaka 2009/2010, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa kodi kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti kubwa kati ya riba kwenye amana na mikopo imeendelea kuwa kubwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine hasa Benki Kuu na Benki za Biashara nchini, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kurekebisha hali hiyo ikiwa ni pamoja na Serikali kuendelea kupunguza mikopo yake kutoka vyombo vya fedha vya ndani ili vyombo hivyo viweze kukopesha zaidi sekta binafsi kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi, upungufu wa wafanyakazi umesababisha baadhi ya shughuli zilizopangwa kutokutekelezwa kwa wakati au kutumia watumishi wachache waliopo kufanya kazi kwa saa nyingi zaidi ya zilizopangwa kisheria. Aidha, upungufu wa ofisi na vitendea kazi umeathiri utendaji ikiwa ni pamoja na kufuutilia utekelezaji wa miradi. Ili kuondoa upungufu huu, Wizara imedhamiria kujenga ofisi mpya, kuongeza vitendea kazi, kuendelea kuajiri wataalam wa fani mbalimbali ili kujaza mapengo yaliyopo na kujenga uwezo wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani kutoka Mashirika ya Umma Sheria mbalimbali zilizoanzisha Mashirika ya Umma, Wakala na Mamlaka za Serikali, zilikuwa haziwezesi Serikali kupata mapato ya ziada kutoka Mashirika hayo. Hali hii ilikosesha Serikali mapato ya ziada kutoka kwenye Mashirika ya Umma, Wakala na Mamlaka za Serikali. Katika kurekebisha hali hiyo, Wizara ilikamilisha mwongozo unaolekeza Mashirika ya Umma, Wakala na Mamlaka za Serikali kuwasilisha sehemu ya mapato ya ziada kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (*PMG*). Wizara imesambaza Waraka Na. 8 wa Hazina wa mwaka 2009 mwezi huu wa Julai 2009 ambao unayataka Mashirika, Wakala na Mamlaka za Serikali yawasilishe sehemu ya mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2009/2010, maombi ya fedha ili kutekeleza majukumu ya Wizara na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu inaomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha fedha kama ifuatavyo:- Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi kiasi cha shilingi milioni 97,015.221 (bilioni 97.02) kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya hizo mishahara ni shilingi milioni 2,805.442 (bilioni 2.81) na matumizi mengineyo shilingi milioni 94,209.778 (bilioni 94.21). Kiasi cha shilingi milioni 188,166.40 (bilioni 188.2) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo fedha za ndani - shilingi milioni 6,000.0 (bilioni 6.0), fedha za nje - shilingi milioni 182,166.402 (bilioni 182.2).

Fungu 21 – Hazina, kiasi cha shilingi milioni 597,612.40 (bilioni 597.61) kwa ajili ya matumizi ya kawaida Kati ya hizo shilingi milioni 1,135.50 (bilioni 1.14) ni mishahara, shilingi milioni 68,519.28 (bilioni 68.52) ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara ya kitaifa. Shilingi milioni 365,793.99 (bilioni 365.79) ni kwa ajili ya matumizi maalum ikiwa ni pamoja na dharura, shilingi milioni 126,383.13 (bilioni 126.38) ni kwa ajili ya *TRA* na shilingi milioni 35,780.50 (bilioni 35.78) ni kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara, michango ya Kimataifa na matumizi ya idara zilizo chini ya fungu hilo. Kiasi cha shilingi milioni 73,996.32 (bilioni 73.99) kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya hizo fedha za ndani - shilingi milioni 10,217.73 (bilioni 10.22), fedha za nje - shilingi milioni 63,778.59 (bilioni 63.77).

Fungu 22 - Deni la Taifa, Deni la shilingi Taifa shilingi milioni 1,515,794.54 (trilioni 1.52) Kati ya hizo: Deni la ndani ni shilingi milioni 1,408,940.00 (trilioni 1.41) na Deni la nje ni shilingi milioni 106,854.54 (bilioni 106.85).

Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali, matumizi ya kawaida - shilingi milioni 97,623.68 (bilioni 97.62) kati ya hizo mishahara shilingi milioni 2,772.4 (bilioni 2.77) na matumizi mengineyo shilingi milioni 94,851.2 (bilioni 94.85). Miradi ya Maendeleo - shilingi milioni 2,050.76 (bilioni 12.05), kati ya hizo fedha za ndani - shilingi milioni 6,000.0 (bilioni 6.0), fedha za nje shilingi milioni 6,050.0 (bilioni 6.05).

Fungu 45: Ofisi ya Taifa ya Ulagazi, Matumizi ya Kawaida - shilingi milioni 17,280.63 (bilioni 17.28), kati ya hizo mishahara ni shilingi milioni 3,230.63 (bilioni 3.23) na Matumizi mengineyo ni shilingi milioni 14,050.0 (bilioni 14.05). Miradi ya Maendeleo - shilingi milioni 8,290.63 (bilioni 8.3), kati ya hizo: Fedha za ndani- Shilingi milioni 2,800.0 (bilioni 2.8), Fedha za Nje - shilingi milioni 5,490.63 (bilioni 5.5)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua washirika wetu wote wa maendeleo kwa misaada yao ambayo imechangia mafanikio yetu katika sekta mbalimbali za uchumi wetu. Naomba niwataje mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo, Belgium, Canada, China, Denmark, United Kingdom, Finland, France, Germany, India, Ireland, Italy, Japan, South Korea, Kuwait, The Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Switzerland, United States of America, *African Development Bank, BADEA, European Union, Global Fund, Opec Fund, Saudi Fund, United Nations Agencies* na *the World Bank*. Tunawashukuru sana hawa wote kwa misaada yao.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu ilikuwa ndefu, lakini kwa sababu ya muda, mengine sikuyasema, lakini tuliomba kwamba hotuba nzima iingie kwenye *Hansard*, kwa hiyo, hata yale ambayo sikuweza kuyasoma, ni imani yangu kwamba yote pamoja nah ii ambayo ni summary, lakini haya yote ambayo yako kwenye kitabu yataingia kwenye *Hansard*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Nikuhakikishie kabisa kwamba hotuba yote itatoka katika *Hansard* kama ilivyo. Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mwenyekiti au mwakilishi wa Mwenyekiti. Anakuja mwenyewe Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa Taarifa ya Kamati. (*Makofî*)

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, nachukua nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Wizara kuhusu Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Maoni ya Kamati kuhusu Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 21 Julai, 2009, na kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka 2008/2009 na Mpango wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010. Kamati inampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa husika. Kamati ilijikita zaidi katika kuiongelea taarifa ya Wizara ili kuepuka tatizo la kujadili Bajeti ya Wizara kama vile, kinachojadiliwa ni Bajeti ya Serikali ya Taifa. Lengo ni kuishauri Wizara kutekeleza majumu yake ipasavyo. Nawashukuru kwa dhati wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa

kuijadili kwa kina na ufasaha hoja iliyowasilishwa na wote napenda kuutambua mchango wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo, Mheshimiwa Abdallah Kigoda –Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha –Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence Liamba, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omary Nibuka Mzeru, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyojadiliwa na Kamati. Kamati imeishauri Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na masuala mengi ya kitaalamu inayoyatekeleza ipo haja ya kuhakikisha kuwa mengi ya maeneo ambayo yalijadiliwa na kukubalika katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010 yanayowalenga na kuwanufaisha wananchi wengi wa kipato cha chini, utekelezaji wake uwe wa tija na ufanisi. Maeneo hayo ni pamoja na malipo ya pensheni kwa wastaafu. Wastaafu wengi wamefarijika na uamuzi wa Serikali wa kuongeza viwango vya malipo ya pensheni kutoka sh. 21,000/= hadi sh. 50,000/=.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni lile la uvezeshaji wa wananchi walio wengi. Uendelezaji wa *SACCOs* na mifuko mbali mbali ya kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini uimarishwe na upatiwe raslimali za kutosha. Mfumo wa Kitaifa wa Kinga ya Jamii (*National Social Protection Framework*) uliokamilika mwaka 2008/2009 ni vyema ukaelezwu vizuri ili ueleweke na wananchi wengi, hasa ikizingatiwa kuwa mfumo huu ni wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera na mikakati inayolenga kuboresha hali ya maisha ya makundi yaliyo katika hali ya umaskini uliokithiri pamoja na makundi tete kama vile watu wenye ulemavu, wajane na wazee maskini, watoto yatima wasio na msaada na wale waishio kwenye mazingira hatarishi ili kuongeza kasi ya kuinua hali ya maisha ya makundi hayo.

Eneo lingine ni lile la kurekebisha mishahara ya watumishi wa umma na kulipa malimbikizo, hususan yale ya walimu. Wizara imeshauriwa kuboresha hali ya maisha ya askari na Jeshi kwa kuwajengea nyumba bora na vitendea kazi. Aidha, Kamati imeishauri Wizara kutenga fedha haraka kwa Benki ya Raslimali zitakazohudumia dirisha la kilimo. Hili ni eneo litakalotengeneza ajira na kuongeza mapato ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Wizara kushughulikia kwa makini tatizo la Deni la Ndani linalogusa mishahara ya waalimu, malipo ya makandarasi, malipo ya askari Jeshi na Polisi pamoja na lile la malipo ya Wazabuni hususan wanaotoa huduma ya chakula mashulenii. Wengi wa Wazabuni hawa wanatishia kutokutoa huduma zao, hata kufanya shule nyingine kufungwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Wizara kuondokana na tatizo la ufinyu wa Bajeti katika yale maeneo yanayoiingizia gharama kubwa zisizo za lazima Wizara inatumia fedha nyingi kwa kupangisha majengo kuhudumia ofisi zake. Kamati imeishauri Wizara kuangalia uwezekano wa kuchukua majengo kwa mfano ya Shirika la Bima na kadhalika. Hali hii itapunguza gharama kubwa za pango kwa Wizara. Aidha, miradi ya kukarabati

baadhi ya majengo ikamilike haraka kwa mfano Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Chuo cha Mipango Dodoma na kadhalika. Zipo Idara na taasisi nyingi za Wizara, kwa mfano *CHC, Tanzania Postal Bank* ambazo zinapangisha majengo badala ya kuwa na Ofisi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeipongeza Wizara kwa kubuni utaratibu wa kupunguza Kodi ya Thamani (*VAT*) kutoka asilimia 20 hadi asilimia 18. Hata hivyo imebainika kuwa tozo la *VAT* katika pango limeanza kuwaathiri wananchi wenyе vipato vya chini. Kamati imeishauri Wizara kuliangalia eneo hili na hatimaye kulitolea maamuzi. Kamati vile vile imetoe angalizo ili Wizara ione nini athari (*impact*) ya punguzo hilo kwa ujumla wake katika ukusanyaji wa mapato unaofanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara, moja ya jukumu lake kubwa ni kukusanya mapato, vile vile inawajibika moja kwa moja kuhakikisha kuwa raslimali fedha inayokusanywa inatumika vizuri. Fedha inayotumika inatakiwa ilingane na matokeo (*value for money*). Kamati imeishauri Wizara kufanya kila jitihada ya kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili zijenge uwemo (*capacity building*) wa uwajibikaji, usimamizi, ufuutiliaji na menejimenti ya raslimali nyingi ziendazo kwenye Halmashauri hizi. Wizara isaidiane na TAMISEMI kurekebisha na kuboresha mtiririko na mstari wa mamlaka (*line of authority*) katika usimamizi wa fedha. Kamati imegusia migongano inayojitokeza katika usimamizi wa fedha kwenye halmashauri baina ya Wahasibu, Wakaguzi, Waweka Hazina na mara nyingine hata Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya. Mgongano huu hauleti tija katika usimamizi na menejimenti ya fedha zinazotarajiwa kusaidia maendeleo ya wananchi. Kwa nini Serikali isianzishe nafasi ya Mhasibu Mkuu (*Accountant General*) wa TAMISEMI. Kamati imeuliza swali hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeonyesha wasiwasi wake juu ya kiwango kikubwa cha utegemezi wa fedha za wahisani katika kuchangia maendeleo yetu. Takwimu zimeonyesha kuwa pamoja na utegemezi mkubwa wa fedha za kigeni, mafungu ya fedha yanayotengwa, upangaji wa fedha kwenye kasma ya maendeleo ni ndogo, ikilinganishwa na kasma ya matumizi ya kawaida na hususan matumizi mengineyo. Kama hali hii ni dhahiri, utegemezi huu unatia wasiwasi. Ama sivyo inawezekana tatizo likawa ni utaratibu wa kuandika vitabu vya Bajeti na kupanga fedha husika katika kasma mbali mbali. Inawezekana fedha ambazo zitagharimia miradi ya maendeleo zinaonyeshwa kwenye kasma za matumizi ya kawaida. Hali hii haionyeshi picha halisi ya gharama zetu za maendeleo katika uchumi wetu. Kamati imeelezwa kwa mfano fedha za *TIB*, fedha za *SGR* zimewekwa kwenye Bajeti ya matumizi ya kawaida, utaratibu ambao hauionyeshi picha sahihi ya gharama za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Wizara iwe makini katika kufuatilia fedha za wahisani hasa katika upatikanaji wa mapema wa fedha hizo. Hili ni zingatio muhimu kwani hata Wizara imekiri kuwa imetokea upungufu mkubwa katika matumizi ya fedha za maendeleo uliotakana na fedha za wahisani kutokelewa kwa wakati kama ilivyotarajiwa, katika kipindi cha mwaka 2008/2009. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Wizara kuendelea kuangalia mikakati ya kuongeza makusanyo ya mapato kutoka Wizara mbalimbali, yaani mapato yasiyo ya kodi (*Non tax revenue*). Wizara ya Fedha imeweka lengo la kukusanya shilingi trilioni 5.1 mwaka 2009/2010. Shilingi Trilioni 4.84 zitakusanywa na *TRA* kutokelewa kwa wakati kama ilivyotarajiwa, 254.9 zitakutoka na mapato yasiyo ya kodi (*non tax revenue*). Hiki ni kiwango kidogo hasa tukizingatia fursa zilizopo katika maeneo ya uwindaji, utalii, uvuvi, mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeisisitiza Wizara kuwa makini katika eneo la kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma ili kusaidia kuleta maendeleo ya nchi. Matumizi yasiyo ya lazima yaachwe na maeneo yanayohamasisha matumizi mabaya ya fedha yafutwe pamoja na kuziba mianya ya matumizi mbaya. Kwenye eneo la usimamizi na udhibiti wa fedha, Kamati imeipongeza Wizara kwa kufunga akaunti 10,000 za *PEDP*. Serikali imekuwa na akaunti nyingi sana wakati Halmashauri nyingine zina akaunti zaidi 3000. Wingi wa akaunti hizi kwanza unadhoofisha uwajibikaji na unachochea matumizi mabaya na yasiyo ya lazima ya fedha. Kamati inajiliza hivi sasa zimebakia akaunti ngapi na kwa nini zisizohitajika zinacheleweshwa kufungwa, kwa madhumuni ya kuboresha menejimenti nzuri ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile imehoji eneo la manunuzi ya umma. Hali halisi ilivyo sasa sera na Sheria hii si rafiki wa wanaozitumia (*not user friendly*). Kwa kufuata utaratibu wa Sheria hii kumeletea Mashirika mengi kutumia fedha nyingi, zaidi ya bei za vitu au vifaa vinavyotakiwa kununuliwa. Iko haja ya kurejea mara kwa mara; (*constant review*) utaratibu huu na *PPRA* wabaini mapungufu na hatimae sheria hii iletwe Bungeni kwa marekebisho ili iwerafiki na wadau (*user friendly*). Muda mrefu unatumika katika mchakato wa manunuzi hivyo kuongeza gharama zisizo za lazima na hata mara nyingine kuchelewesha utekelezaji wa miradi muhimu. Wizara iangalile eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeiuliza Wizara pamoja na Serikali kuwa na mashirika mengi inayomiliki hisa zake ni kwanini gawio (*dividend*), kuanzia Julai, 2008 hadi Aprili 2009, kwenda Serikalini ni shilingi bilioni 21.9 tu. Kwa nini mashirika hayo yanatoa gawio dogo Serikalini wakati Serikali ni mwekezaji hisa mkubwa. Swali ni kuwa je Serikali iendelee kuyabeba mashirika hayo au la? Kamati imeishauri Wizara kuharakisha mchakato wa kuuza hisa kwa wananchi walio wengi ili kwanza kupunguza gharama za hisa kwa Serikali, pili kuongeza mapato yake ambayo yangeweza kuelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu na tatu kuwashirikisha wananchi katika uchumi na kuongeza vipato vyao. Aidha, Kamati imeishauri Wizara kuwasiliana na Taasisi ya Soko la Mtaji na Hisa kungalia upya na kurejea masharti ya kuingia katika soko la Hisa ambayo kwa sasa ni magumu na yenye gharama kubwa (*not cost effective*). Hii itawezesha wananchi wengi na wafanyabiashara wengi hata wadogo kujinga na soko hili. Hii ndiyo dhana nzima ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ili kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika na hisa inayowekeza, Kamati inaishauri Wizara kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kifedha, usimamizi na menejimenti. Mkakati wa kufanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa huru (*independent*) utasaidia na ni vizuri ikafuata mwenendo wa *Private Public Partnership*. Suala muhimu ni Utekelezaji wa haraka wa mkakati huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhika na kasi ya Serikali ya kuziimarisha Benki zake mbili *Twiga Bancorp* na *Tanzania Postal Bank*. Kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuongeza mitaji *Twiga Bancorp* na Benki ya Posta, ili zifanye kazi kwa ufanisi. Utaratibu huu utasaidia kuzalisha faida katika Benki hizi za kwenda kwa *exchequer*, lakini hatimaye kuongeza kiwango cha gawio kwenda Serikalini kama njia ya kuongeza mapato. Kwa sababu Benki Kuu imetoa sharti la kuongeza mitaji ya mabenki, Serikali ichukue hatua hii haraka, kuititia Wizara. Benki ya Posta ni mfano mzuri wa Benki ya Wanyonge na inahitaji kuendelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kupata maelezo kuhusu vyanzo vya fedha za mikopo ya ndani na matumizi yake. Kamati imetahadharisha kuwa *deficit financing* kutoka Benki Kuu kama chanzo cha fedha hizi mara nyingi huchochea mfumko wa bei. Ni vipi

Serikali inaweza kuzuia mfumko huo. Kamati imeshauri Wizara kuwa fedha hizi zitumike kwenye ujenzi wa miundombinu, kwani hatua hii itasaidia kuujenga uchumi wetu, pamoja na Kamati kutambua kuwa uchumi wowote hauwezi kukua bila mfumko wa bei, unaohimilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile imeshauri Wizara kuja na mfumo bayana wa kuonyesha matumizi ya sh. 1.7 triliuni ya kunusuru uchumi, matumizi ya kukarabati Reli ya Kati kwani sh. 48.6 bilioni zilizotengwa kwa Msajili wa Hazina ni chache na katika fungu la deni la Taifa fedha zilizotengwa zimeonyeshwa kama vile ni za kugharamia utawala, badala ya kugharamia malipo ya deni husika (*debt servicing*). Kamati imeshauri hili lirekebishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kufikisha kwenye chombo husika taarifa ya uchambuzi wa ripoti ya Tume kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano ili kupata maamuzi. Kamati imeleza kuwa licha ya uchambuzi huo kufanyika na Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint finance Commission*), na taarifa hiyo kuwasilishwa Serikalini takriban miaka mitatu iliyopita, kasi ya kutoa maamuzi ni ndogo na hivyo kuleta malalamiko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mipango Dodoma hivi sasa kinahitajika zaidi kuliko mwanzoni, hasa tukizingatia utaratibu wa *D by D* ulioanzishwa nchini. Kama mipango ya uchumi jumla itatekelezwa vizuri ni lazima iende sambamba na upangaji mzuri wa mipango ya ngazi za Kata na Wilaya (*micro level*). Chuo hiki kina kila taaluma ya mipango kwa ngazi mbalimbali. Wizara inapaswa itoe fedha za kutosha ili kuboresha na kukamilisha miundombinu inayohitajika katika Chuo cha Mipango. Mafanikio hayawezi kupatikana bila ya mipango. Aidha, imefika wakati sasa kwa Serikali kuwatambua wahitimu wa tuzo ya vyeti na stashahada kutoka Chuo cha Mipango. Hivi sasa havitambuliki na Kamati inaiuliza Serikali kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile ilipenda kujuu utendaji kazi wa Wizara na Ushirikiano wake na Tume ya Mipango. Eneo hili inabidi liangaliwe vyema kwani Kamati bado inaona upo upungufu katika mfumo wa Tume ya Mipango na hivyo kuleta wasiwasi kwa Taifa letu kukosa utekelezaji wa dhana nzima ya Tume ya Mipango kuwa *think tank* ya mipango nchini. Aidha, kwa mfumo wa sasa uwezekano wa taaluma ya mipango kubanwa na uchumi au kuwa *fused* kwenye uchumi ni mkubwa sana. Hali hii itadhoofisha uandaaji wa mipango ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho kwa niaba ya wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Nawashukuru Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu Bwana Ramadhan Khijjah na wataalam wote wa taasisi na Wizara waliotusaidia katika kuchambua hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Ndugu Anselm Mrema, Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Michael Kadebe, kwa kazi nzuri ya kuandaa maoni ya Kamati kwa wakati unaotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwishowe niwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Handeni kwa msaada na kuniunga mkono kwa hali ya juu. Bado ujumbe wangu kwao ni ule ule, mambo mazuri hayataki haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Abdalah Kigoda, sasa ni wakati wa kumuuta Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Fedha na Uchumi na nimearifiwa kwamba kwa niaba yake atakuwa ni Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji. Mheshimiwa Fatma, tafadhali

**MHE . FATMA ABDULHABIB FEREJI k.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7) toleo la mwaka 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao mkubwa, wakiongozwa na Mheshimiwa Dr.Willibrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Upinzani waliofanikisha hadi kuniwezesha kusimama mbele yenu kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kukushukuru wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na watendaji wa Ofisi yako, wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah kwa utendaji wao wa viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru sana wapigakura na wananchi wote wa Jimbo la Mji Mkongwe kwa kuendelea kuniunga mkono kwa muda wote ninapokuwa katika kazi za kibunge na nje ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru familia yangu hasa watoto wangu na mume wangu mpenzi Bwana Mohamed Break kwa kuendelea kunisaida katika shughuli zangu, lakini zaidi kwa kunivumilia kwa wakati wote ninapokuwa mbali nao nikilitumikia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pamoja na wakuu wa vitengo na asasi zilizo chini yao kwa maandalizi ya Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ni kwa mratibu mshauri wetu ambaye tunamlipa wenyeve Ndugu Oliver Mwikila, Katibu Muhtasi Mama Salvina Mahundu na Mhudumu Grace Samuel kwa mchango wao mkubwa wa kuisaidia Kambi yetu kutimiza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti yetu mbadala tulionyesha maeneo mengi ambayo Serikali ingeliongeza wigo wa mapato, ni matumaini yetu kuwa Serikali itazingatia ushauri wetu, kama alivyoahidi Waziri wakati wa majumuisho ya hoja yake, hata hivyo, naomba nimuongezee Waziri maeneo ambayo anakusanya kodi lakini hayakusanyi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, migodi mikubwa ya dhahabu huzalisha madini kadhaa wakati wakisafirisha dhahabu na kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano mgodi wa Bulyanhulu umezalisha toka mwaka 2004 hadi 2008 ili kuwa dhahabu (*130739.77 Troy ounce*) sawa na 40.53 Mt, shaba (*38694145.79 Pounds*) sawa na 17567.12 Mt na fedha (*Silver*) (*1001586.97 Troy Ounce*) sawa na 31.01Mt. Kwa mrahaba wa asilimia tatu kila aina ya madini kwa bei za leo mapato yangalikuwa kwa madini ya shaba (*copper*) kwa mrahaba wa 3% ni *USD 3,952,602.*, madini ya fedha (*silver*) mapato ya mrahaba wa 3% yangalikuwa ni *USD 6,977.25*. Jumla ya mapato ni *USD 3,959,579.25*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka minne madini haya ya shaba na fedha Serikali imekosa mrahaba wa shilingi za Kitanzania 4,751,495,100/=. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atuambie kwa kipindi hicho chote mapato yaliyokusanywa ni shilingi ngapi kama mrahaba wa madini hayo toka Mgodi huo wa Bulyanhulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madini haya yote ni wenye mali ndio hutuambia walichopta baada ya kupeleka mchanga nje na kuusafisha. Bei ya dunia ya shaba ni wastani *wa USD7,500 Mt.* hivyo hivyo kwa madini ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vito wanaofaidi ni wageni kwa mfano katika machimbo ya vito vya *Ruby Gem, caret* moja hufika *USD 30,000* lakini thamani yanayotiwa wakati wa kusafirishwa ni *USD 150* tu hivyo kuikosesha mapato halali Serikali.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa ni kwa Serikali kushirikiana na wachimbaji wadogo wadogo ili kujifunza namna bora ya kukadiria thamani ili Mtanzania afaidike na Serikali ifaidike. Vinginevyo tutaendelea kutoa sadaka rasilimali za nchi na kuwaachia vizazi vyetu mashimo na kemikali za sumu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara. Wizara hii ndiyo msimamizi na mtekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini unalenga kufanikisha kufikia malengo ya milenia. Hata hivyo utekelezaji wa MKUKUTA umesuasua kwa sababu gharama za mkakati hazikukadirwa mapema. Ukadiriaji wa gharama za MKUKUTA katika baadhi ya sekta muhimu ulikamilika mwishoni mwa mwaka 2006 na gharama zake zikabainika kuwa ni kubwa mno kuliko uwezo wa serikali kwa hiyo MKUKUTA hautekelezeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano gharama za kutekeleza MKUKUTA katika sekta ya nishati ilikadirwa kuwa wastani wa dola milioni 911 kwa mwaka kati ya 2006/2007 mpaka 2009/2010. Sekta ya kilimo ilikuwa inahitaji wastani wa dola milioni 300 kwa mwaka. Sekta ya afya ilihitaji wastani wa dola milioni 476 kwa mwaka. Sekta ya barabara ilihitaji wastani wa dola milioni 922 kwa mwaka. Sekta nne za nishati, kilimo, afya na barabara zilikadirwa kuhitaji wastani wa dola milioni 2609 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mahitaji haya ya sekta nne ni zaidi ya asilimia 70 ya matumizi yote ya Serikali ya mwaka 2006/2007. MKUKUTA haukutekelezwa kama ipasavyo kwa sababu gharama za mpango hazikukadirwa mapema, na ukadiriaji ulipomalizika gharama zilikuwa kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa Bajeti ni wa mwisho wa utekelezaji wa MKUKUTA. Waziri kaeleza kwamba Serikali inaanadaa MKUKUTA namba II. MKUKUTA wa kwanza haujafanyiwa tathmini ya kina ili kujifunza kutoka mapungufu yaliyojitekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ni wazi MKUKUTA wa pili hautakamilika na kuanza kutekelezwa mwaka wa bajeti wa 2010/11. Ikiwa serikali ina lengo thabiti la kuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaotekelzeza inastahili kujipa muda kutathmini MKUKUTA

na kushirikisha wadau wote katika kuandaa mpango mbadala wa kukuza uchumi kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Serikali kushirikiana na vyama vya upinzani, taasisi zisizokuwa za kiserikali na wananchi kwa ujumla kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo na MKUKUTA namba II ili kuibua dira mpya ya maendeleo na mpango wa muda mrefu unaotekelzeza utakaoongoza mipango na bajeti ya serikali. Kambi ya upinzani inashauri kuwa MKUKUTA mpya usianze mpaka Uchaguzi Mkuu utakapokwisha ili kuondoa mashaka kuwa moja ya chama cha siasa kinatumia MKUKUTA kama ilani yake ya uchaguzi na hivyo kuzuia mawazo huru yenye kuweza kuchangia Dira ya Taifa baada ya mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. MKUKUTA mpya uanze mwaka 2011 na upitishwe na Bunge la Kumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kupitia kwa makini takwimu zilizomo kwenye sura ya Bajeti na vitabu vyote vya matumizi ya kawaida na maendeleo inasikitika kwamba pesa zote zinazokusanywa toka kwa walipa kodi wa nchi hii lengo/kazi yake ni kuziwezesha Wizara kuwepo na si kwa ajili ya kuwaletaa maendeleo. Kwani maendeleo yao yanapatikana na fadhila za wahisani. Hivyo basi, inaitaka Wizara hii iliangalie jambo hili kwa makini kwa kupanga vipaumbele vyenye umuhimu kwa watanzania nasio vinginevyo. Kwa mfano Kasma 229900 ushauri wa kitaalam, ushauri uelekezi utatumia shilingi 1,888,000,000/= karibu 1.9 bilioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mradi mkubwa wa vitambulisho vya Taifa, japokuwa hatujui hatma ya mchakato unaoendelea, Kambi ya Upinzani imefanya utafiti na kugundua kuwa gharama zinazungumziwa ni kubwa mno bila ya sababu, kwani vitambulisho vya aina hii vimewahi kutengenezwa Uhlanzi, *South Africa*, Nepal na Peru, lakini hata ndani ya nchi yetu, SMZ imetengeneza vitambulisho 500,000 kwa gharama ya dola za kimarekani 3milioni tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kama gharama hizo za Zanzibar zingeziidhwa mara 40, vitambulisho hivyo visingezi *USD 120* milioni sawa na sh.15.6 bilioni ambapo katika kipindi hiki cha msukosuko wa kiuchumi, hali ya ukame na kuwa kuwa na Bajeti tegemezi haiingii akilini, ni kwa nini Serikali imepanga kutumia zaidi ya bilioni mia mbili za ishirini (shs.120bilioni)? Kambi ya Upinzani naomba majibu kwa matumizi haya yanayotisha.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa maoni kuhusiana na deni la Taifa (Fungu 22) naomba kuangalia kwanza Bajeti ya matumizi ya kawaida iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya fungu hili ya shilingi bilioni 684.572/= na hadi mwezi mei 2009 matumizi yalikuwa shilingi billioni 542.237/= Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa hasa watumishi wa idara hii wanafanya kazi gani hadi kupewa kipaumbele na kupangiwa Bajeti ambayo ni kubwa

mara 5 kuliko Bajeti iliyopitishwa mwaka huo ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya shilingi billioni 133.704/=. Tunataka maelezo kuhusiana na hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhamini wa Serikali, kuna utaratibu ambao umekuwa sugu sana kwa Serikali kutoa dhamana kwa makampuni binafsi na mwisho wake makampuni hayo yanashindwa kulipa au kukataa kwa makusudi na hivyo kusababisha deni hilo kurudi Serikalini na huo kuwa ni msalaba kwa walipa kodi, mfano ni Mkopo wa NSSF kwa kampuni za *M/S Kiwira Coal* na *M/S Power CO.Ltd, Kagera Sugar, Standard Chartered Bank* kwa kiwanda cha Nyama cha *SAAFI* na kadhalika. Pia Chama cha Ushirika cha Nyanza kilipata dhamana ya shilingi 530,000,000 bila ya kuwepo idhini ya wala mkataba kati ya pande hizi mbili na kutoa wajibu wa kila mhusika jinsi ya urejeshaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona haya ni mambo ambayo Watanzania wanatakiwa kupata majibu sahihi. Sambamba na hili Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini pale Serikali inapotoa dhamana hizo haiweki utaratibu wa pale mdhaminiwa akishindwa kurejesha fedha hizo basi iwe ni kwa Serikali kununua hisa za Kampuni husika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya sh.1,676,891,328/= kama adhabu ya kuchelewa kulipa mikopo ya Serikali, hii ni hasara kubwa na wahusika wapo wanaendelea na kazi, Kambi ya Upinzani inauliza ni lini mtindo huu wa kutokuwajibika (*responsible*) na fedha za walipa kodi utakwisha? Je, wanasababisha hasara hiyo kuna hatua zozote za kinidhamu wamechukuliwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutoa udhamini wa madeni ambayo wakopaji kwa sababu ya msukosuko wa uchumi wa dunia wanapata matatizo kulipa kwa wakati. Madeni hayo yanafikia shilingi 270 bilioni. Kuna hatari ya Serikali kujiingiza katika kudhamini madeni ambayo hatimaye yatabidi yalipwe na Serikali. Serikali inajiongezea mzigo wa madeni yanayoweza kutokea (*Contingent Liabilities*).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona hii itatoa mwanya kwa wanaodhaminiwa madeni wachangie kwenye kampeni na baada ya uchaguzi mzigo wa madeni ubebwe na Serikali. Kuna hatari ya *EPA* nyiningine kuzinduliwa. Ukaguzi wa kina wa mahesabu ya makampuni husika ufanywe na *CAG* kwa gharama za mabenki yaliyokopesha kabla ya Serikali kuyadhamini makampuni haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu msajili wa hisa za Hazina (*Treasure Registrar*), katika kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma au yale ambayo Serikali ina hisa, Serikali inatakiwa kufuatilia kwa ukaribu utendaji mzima wa mipango yake ya maendeleo kwa niaba ya watanzania wote. Kambi ya Upinzani inakumbushia ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwamba ofisi ya Msajili wa Hazina iimarishwe kwa kuibadili na kuunda ofisi ya Mashirika ya Umma ili kusimamia vema mashirika na mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, Waziri wakati anawasilisha Bajeti ya Taifa alieleza kuwa Serikali itaikopesha fedha *Artumas* ili waweze kuendelea kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa mikoa hiyo. Hata hivyo fedha za kuwakopesha *Artumas* hazimo ndani ya Bajeti. Kwa nini Serikali ilikopesha *Artumas*? Kama Serikali ina fedha kwa nini isiingie ubia na kununua hisa za kampuni hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikataa kuyapa ruzuku mashirika ya umma hatu yaliyokuwa yakifanya vizuri, na hatimaye kuyaiza kwa bei chee, je, sasa inakuwa bora kuzipa sadaka kampuni binafsi kwa kisingizio cha hali mbaya ya uchumi duniani?

Mheshimiwa Spika, aidha mashirika ya umma ambayo yamebinafishwa yanawajibika kisheria kuwasilisha mikataba ya hiari kwa idhini ya msajili wa Hazina kabla ya kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani mwaka 2008/2009 ililetu kilio cha waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero waliopunguzwa kazi mwaka 2000. Kambi ya Upinzani inauliza hivi kwa nini mkataba wao wa hiari Na. 4 walioingia na mwekezaji wamelipwa wachache tu na wengi bado hadi leo hawajalipwa? Aidha kifungu Na. 9.5 (a) – (c) havikutekelezwa badala yake mafao yao yalitumika kulipia gharama za *redundancy*, tunaomba ufanuzi wa suala hili ambalo linazidisha deni la Taifa pasipo sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa Msajili wa Hazina ndiye anayeridhia na kuidhinisha uteuzi wa wajumbe wa Bodi mbalimbali za mashirika, taasisi na wakala za Serikali. Hivyo basi, tunataka kujuwa toka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atoe ushauri wa kuwaondoa Wabunge au wanasiasa katika ujumbe wa bodi za asasi za Serikali, hadi sasa utekelezaji wa hilo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi. Waziri wa Fedha akiwasilisha Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2009/2010 ukurasa wa 47 alieleza kuwa misamaha ya kodi ilikuwa ni wastani wa asilimia 30 ya mapato ya kodi au asilimia 3.5 ya Pato la Taifa, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Ikiwa misamaha ya kodi itapunguzwa mpaka kufikia asilimia 0.5 ya Pato la Taifa, ukusanyaji wa kodi utafikia asilimia 20 ya Pato la Taifa. Misamaha hii inapunguza uwezo wa Serikali kutoa huduma za msingi kwa walipa kodi, na huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali yetu. Ni ukweli kuwa misamaha mingi hutolewa kwa misingi ya kujuana na si kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonyesha kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 misamaha ya kodi ilikuwa ni shillingi 754,316,200,000/= sawa na 21.2% ya makusanyo yote. Kwa mpango huu hata kama *TRA* itakusanya mapato mengi kiasi gani itakuwa ni sawa na kazi bure kwa misamaha nayo itazidi kuwa mingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Bajeti wa 2008/2009, Serikali iliendeleza sera ya kutokukopa kutoka vyombo vya fedha kugharamia Bajeti yake hasa matumizi ya kawaida. Hata hivyo riba ya Hawala za Hazina (*treasury bills*) za siku 91 mwishoni wa Desemba, 2008 ilikuwa asilimia 11.2.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) umebaini kuwa mabenki ya nje yaliyomo Tanzania yanakula njama kuhakikisha kuwa wanapata faida kubwa kwa kununua Hawala za Hazina. Kuongezeka kwa ukopaji na mapungufu yaliyopo katika kusimamia soko la Hawala za Hazina kutaongeza gharama za riba kwa Serikali. Wakati Serikali inaongeza kukopa na riba inapanda juu Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ameeleza kwamba; “Serikali itayakopesha mabenki fedha kwa riba nafuu ya asilimia 2 ili na wao wawakopeshe wafanyabiashara fedha za mitaji ya uendeshaji kwa riba nafuu.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itakopa na kulipa riba ya asilimia 11 na kuyakopesha mabenki kwa riba ya asilimia 2. Benki Kuu haina mamlaka ya kupanga riba kwa wateja wa Benki za Biashara. Mikopo ya Serikali itawaongezea mapato wenye mabenki bila kuwasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kwani mabenki bado inawaona kuwa hawakopesheki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki Kuu ya Tanzania katika taarifa ya mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2007/2008 ambayo imewasilishwa Bungeni, imeonekana kuwa Serikali imetoa dhamana ya *EPA* ya shilingi 65 bilioni. Wakati Rais alipohutubia Bunge mwaka 2008 alisema malipo ya *EPA* yamesimama, Serikali bado imetoa “*special EPA stock*” yenye thamani ya fedha hizo. Mara kwa mara Serikali imekuwa ikirudia kusema kuwa malipo ya *EPA* yamefungwa, vile vile Benki Kuu kuitia kamati mbalimbali za Bunge imesema hivyo hivyo, kumbe hali ni tofauti. Kambi ya Upinzani inapata mashaka zaidi kwamba malipo haya mapya ya *EPA* yanafanyika kipindi kinachokaribia Uchaguzi Mkuu 2010. Katika mazingira ya sasa ambapo nchi haina sheria ya kuthibiti matumizi ya fedha katika kampeni, na kwamba *CAG* hajaanza kukagua vyama vya siasa ili kujua vyanzo vya mapato, ni dhahiri *EPA* hii maalumu in kiwingu. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kuhusu *special EPA stock*.

Mheshimiwa Spika, taairfa hiyo ya Benki Kuu inaonesha kuwa Benki Kuu imepata hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 91 ukilinganisha na faida ya shilingi bilioni 96 mwaka uliopita. Hasara hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na *loss of foreign exchange* ambayo kwa mwaka unaoishia Juni, 2008 imefikia takribani shilingi bilioni 100. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa maelezo ya kina ya hesabu hizi yatatolewa katika Kamati ya Bunge ya *POAC* chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Kabwe Zitto, hata hivyo kwa maslahi ya Taifa tunapenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu hasara hii ya Benki Kuu kwani vikao vya kamati za *oversight* ni vya faragha. Umma wa Watanzania unapenda kufahamu Benki yao inavyoendeshwa na ni kwa nini ipate hasara kubwa kiasi hicho fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Wizara hii bado ina mambo mengi sana ambayo kama yatafanyiwa kazi kama inavyostahili basi uchumi wetu unaweza kukua kwa kasi ya ajabu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na mwakani 2010 ni uchaguzi mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ule wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni kwa kuwa na uchaguzi ulio huru, haki na wazi tu ndio tunawenza tukawa na Serikali inayowajibika ipasavyo kwa wananchi walioichagua na hivyo Serikali hiyo huwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ni imani yetu kuwa chaguzi zetu zote zitaheshimu maamuzi ya wapiga kura. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, mazingira ya uandikishaji wapiga kura Zanzibar kunakowanyima hasa vijana wenye umri wa miaka 18 na kuendelea wasiopungua 120,000 hakuashirii kuwa na uchaguzi uliohuru, haki na wazi hivyo viashiria vya kuvunjika kwa amani kama ilivyotokea mwaka 2001 kuna nukia sana. Nayasema haya kwa kuzingatia kuwa hakuna maendeleo endelevu kama Serikali iliyoko madarakani haikupata ridhaa ya wazi kwa wananchi wake. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo naomba kurejea wito wangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumkumbusha aliyojasema Rais Benjamin Mkapa hapa Bungeni, mwaka 2003 na nanukuu; “Yaliyotokea Zanzibar yameitia doa nchi yetu, ni vyema tukayaepuka yasiye yakajirudia tena.” Kupeleka kwako vikosi vya ulinzi kwa idadi kubwa Pemba (JWTZ, Polisi, KMKM, JVZ, JKU, Zimamoto na kadhalika wasiopungua 2500)

wakati huu wa kuandikisha kura ni ishara kuwa unataka yaliotokea mwaka 2001 yatokee tena vinginevyo ungelikwisha chukua hatua baada ya kukupatia taarifa nyingi juu ya uvunjwaji wa Katiba na Sheria ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hala hala na jicho, mti una hoho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Fatma Fereji, kwa kuwasilisha hoja hiyo kwa ufasaha kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ya wachangiaji kama kawaida tangu tumeanza imekuwa ni ndefu mno kupita uwezo wetu. Kuna mmoja hajachangia ambaye ni Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, lakini yeye ameomba awe wa pili katika kuchangia, kwa hiyo nitaridhia ombi lake. Wapo Wabunge watano waliochangia mara moja ambaao ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh na Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tungemalizia hapo ilikuwa inatosha kabisa kwa sababu bado tuna Muswada wa *Appropriation* ambaao ingefaa tuupitishe leo kwa sababu kesho na kesho kutwa tuna mambo mengi zaidi. Hata hivyo tutaanza na Mheshimiwa Job Ndugai atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma ajiandaye. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba nzuri aliyoitoa humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wa Kongwa kwa fursa walionipa ya kuwawakilisha hapa Bungeni, nafanya kazi hii kwa moyo nikiamini kabisa kwamba tupo pamoja na kwa hatua hii nimshukuru sana Mkuu wetu wa Wilaya Ndugu Lembrus Kipuyo ambaye amefanya kazi kubwa akishirikiana nasi katika kuisogezza Wilaya ya Kongwa katika ramani ya maendeleo ya nchi yetu. Tumejenga sekondari, zahanati, barabara na huduma nyingi za kiuchumi tumerekebisha na tunaendelea kufanya vizuri katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulipopata uhuru viongozi wetu wa awamu ya kwanza walituambia kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne ambayo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mambo ya msingi kabisa tangu wakati ule waliposema viongozi wetu waasisi mpaka leo na mimi leo ningeongeza katika manne hayo ili tuendelee tunahitaji jambo la tano nalo kwa maoni yangu tungeliita fedha na uchumi. Ukishakuwa na yale manne ukiongeza na fedha na uchumi hapo inakaa sawa sawa. Maana unaweza ukawa na rasilimali nyingi lakini mwisho wa siku usiwe na maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Afrika tuna nchi ya Nigeria ambayo ni nchi yenye watu wengi naamini kuliko nchi zote hapa Afrika na ina rasilimali nyingi hasa za mafuta, hesabu za kawaida wanazopiga wao toka wamepata uhuru mpaka sasa, fedha ambazo wameshapata kutokana na mafuta zinakaribia trilioni 400, Bajeti yetu ipo kwenye trilioni 9 unaweza ukafikiria inaingia mara ngapi. Mapato ya mafuta ya Nigeria ya siku kumi na tano ndiyo uchumi wa Tanzania kwa mwaka mzima, lakini hakuna kitu cha maana kuna wizi usio wa kawaida, watu wengi sana wako katika umaskini mkubwa sana, watu wachache ni matajiri kupita kiasi. Kwa hivyo unaweza ukawa na rasilimali nyingi lakini usiweze kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna rasilimali za kutosha kwa hiyo lazima tuhakikishe kwamba makosa waliyoyafanya wenzetu hatuyarudii makosa yale, kwamba tutumie rasilimali zetu vizuri ili tuweze kuendelea zaidi. Katika hilo tunawategemea sana Wizara ya Fedha na Uchumi kutusaidia na kutuwekea misingi ya mipango imara na utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa tupo katika cha Bajeti, pamoja na mambo mengine ni mgawanyo wa makusanyo ya Serikali, Serikali inatueleza imekusanya nini na mwisho wa siku kwa mwaka mzima itagawa nini ili angalau sehemu kubwa ya wananchi maisha yao yaweze kuboreka.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete anapita kwenye kampeni za mwaka 2005 hata baada ya kuchaguliwa kwa kishindo, jambo moja alilirudia mara kwa mara na Mheshimiwa Rais ni mchumi alisema kwamba Serikali ya awamu ya tatu ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa ilijenga misingi mikubwa ya uchumi, Serikali ya awamu ya nne moja ya madhumuni yake ni kuhakikisha kwamba uchumi huu unatafsiriwa vizuri na kuwafikia wananchi, itajishughulisha sana na *micro-economy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mkubwa katika madini na sekta zinazokua kwa haraka ambazo kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni pamoja na sekta ya madini japo haikui kwa haraka lakini inakuwa na ina mwekezaji mkubwa, sekta ya mawasiliano, sekta ya ujenzi, sekta ya huduma, sekta ya fedha na sekta ya kilimo. Ni namna gani wakulima wetu wanawenza wakafaidika na uwekezaji wa sekta ya madini uliopo.

Mheshimiwa Spika, tukisha-*link* haya mambo mawili faida itaonekana kwa wananchi wa kawaida, katika sekta ya huduma kwa mfano kwenye utalii, ni namna gani ujenzi wa hoteli za kitalii na ujio wa watalii walio wengi unaweza ukawafanya wananchi wetu wanaolima nyanya, vitunguu, kabichi na kadhalika wakaweza kuuza katika hoteli wakapata fedha na kipato chao kikaongezeka, namna yaku-*link* uwekezaji na uchumi wa kawaida unaotokana na uzalishaji wa wananchi wetu ili mwisho wa siku wananchi wetu ili mwisho wa siku wananchi wetu waweze kuwa na fedha. Ni namna gani nyama ya ng'ombe wetu wa Tanzania itakuwa-*packed* vizuri, inaweza ikauzwa katika hoteli zetu za kitalii, inaweza ikauzwa katika migodi yetu ya madini na kwa maana hiyo fedha ile ambayo inaagiza nyama *South Africa*, Kenya na mahali pengine inaweza ikaingia katika uchumi wetu mwisho wa siku wananchi wetu wakawa na maisha bora zaidi kama tulivyowaahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo kazi ambayo tulikuwa tumejiwekea katika awamu hii, kujaribu kuhakikisha kwamba faida kubwa za uwekezaji zinaonekana miongoni mwa wananchi wetu. Ningependa kusema tumeifanya kazi hiyo lakini bado inahitaji kufanyika kwa umakini na inataka mipango mizuri na imara iliyowekwa mapema na kuendana na sheria fulani fulani. Mfano tunawaambia ni marufuku kuagiza nyama toka nje ya Tanzania, marufuku ile inakuwa ni sera nzuri itakayosaidia kuchagiza uchumi wetu kuweza kukua, na maeneo mengine yakatazamwa kwa mtazamo huo itatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafuta ya kupikia; katika Mkoa wa Dodoma tuna uwezo wa kuzalisha alizeti nyingi, karanga nyingi na hata ufuta mwingu. Ukituhakikishia soko kwamba walaji wakubwa wa mafuta watatumia mazao yetu hapa tunahakika ya kuweza kuzalisha mafuta ya kuwezesha nchi hii isiweze kuingiza mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulizungumzia suala hili kipekee kabisa kwamba tujaribu ku-*link* uchumi huu mkubwa na uchumi wa kawaida wa wananchi wetu, pili tumekaa hapa mwezi mzima tunaangalia Bajeti ya nchi, hii ni Bajeti ya Serikali. Ningependa

kuzungumza na wananchi wa kawaida kule Kongwa na mahali pengine, katika maendeleo kuna maendeleo yanayoletwa na uwekezaji mkubwa na maendeleo haya hufanywa na Serikali, *public goods*, mambo ya barabara kubwa hizi za lami na kadhalika, ugawanyaji wa umeme, miradi mikubwa ya maji, haya lazima Serikali ndiyo ifanye kumtegemea mwananchi mmoja mmoja ni vigumu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo ambayo mwananchi mmoja mmoja ni lazima ufanye, yale ya jumla ya Serikali yakichanganyika na ya mwananchi mmoja mmoja ndiyo mwisho wa siku tunasema tumepata maendeleo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia haya ya kawaida ya mwananchi mmoja mmoja, itakuwa ni vigumu sana kupata Serikali itakayomjengea kila mwananchi nyumba ya kuishi. Ni lazima mwananchi naye afanye kazi kwa juhudi, ajenge nyumba yake, Serikali haitawenza kununUlia watu nguo, ikapangwa Bajeti ya Serikali ya kununulia watu nguo nchi nzima, Watanzania wote wanunuliwe viatu au watu wanunuliwe sabuni za kuoga na hata kufulia haiwezekani. Kwa hiyo, yapo mambo ya Serikali hayo yanaitwa *public goods* na yapo mambo ya mtu mmoja mmoja, utamkuta mtu yupo kijijini anailaumu Serikali kwamba haimletei maendeleo, ye ye mwenyewe kachakaa pale alipo, hafanyi kazi, swali ni kwamba huu uchumi wa kwako na wewe umeushughulikiaje. Tuilaumu Serikali kwa ajili ya barabara ina mashimo lakini yapo mambo ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tufike mahali tuambiane kwamba tukutane katikati, Serikali ije na ya kwake na sisi wananchi tufanye yale ya mmoja mmoja, ili mke wako apendeze ni lazima umnunulie nguo wewe mwenyewe. Ukitegemea Serikali itagawa khanga na vitenge, mimi sidhani kama hata jamaa zangu wa upinzani wakiingia watayaweza haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Fedha na Uchumi kwa namna mmoja ama nyingine ndiyo pia inawezesha Bunge kukutana, mimi nina tatizo kwamba Wizara imekuwa inaminyi Bajeti ya Bunge, tukitakiwa tukae hapa Dodoma tunakaa wiki mbili, hivi wiki mmoja kweli kwa unyeti wa shughuli za Bunge zimekosekana fedha za wiki mmoja ya Bunge ili kutimiza zile wiki tatu? Tulitakiwa tukae hapa mpaka mwezi wa nane katikati, kweli maelezo yametolewa na tukaelewa. Lakini kweli kwa mbanano huu mwisho wa siku tunawenza tukasema tija imepatikana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano Wizara ya Afya jana, ilikuwa na wachangiaji 50 waliochangia hata robo hawakufika, Wizara ya Elimu, hizi ndizo Wizara za Ubunge Wizara zenye mambo yanayogusa wananchi unaweka siku moja, hivi kweli tunawatendea haki wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa muda wote ambao tumekaa anachangia mara moja aliyechangia sana ni mara nne. Jambo hili tulitazame sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi umekuwa ni mtindo kwamba kila kikao cha Bunge kinapunguziwa Bajeti, mimi naomba tufike mahali tupeane asilimia za uhakika kutokana na Bajeti nzima. Bunge liwe na asilimia yake kama ilivyo kwa Kenya na Uganda na sisi tuwe hivyo hivyo. Mahakama wawe na asilimia yao ili tusilaumiane, tupange asilimia yetu vizuri tujue tunafanyaje na Bunge lijalo wataongezeka Wabunge karibu hamsini hapa, sijui wanakuja kufanya nini kwa sababu muda wa kuchangia haupo, hapa imeshakuwa ni mkutano wa hadhara kusema ni vigumu, ukisema mara moja wanaandika kwenye daftari umeshasema wewe, sasa utawakilisha wananchi wako saa ngapi kwa utaratibu huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii itazame jambo hili Bunge lina nafasi yake kwani ni mhimili, mnamuweka mahali pagumu sana Mheshimiwa Spika, tutafika mahali tutamlaumu lakini kumbe ni kwa sababu ya mazingira ambayo ni magumu sana. Bajeti ya Bunge itazamwe kipekee ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kuweza kutoa michango ya uwakilishi wao kwa uhakika kama ambavyo Katiba inataka na wananchi walivyotutuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuzungumzia mwenendo wa bei, bei zetu bao ni kubwa hasa vifaa vya ujenzi kama mbao hata hapo nyuma niliwahi kueleza kwamba VAT ambayo inatozwa mara mbili mbili kule *Sao Hill* na mashamba mengine ya miti inasababisha bei ya mbao zetu kuwa juu. VAT inatozwa mara mbili, kwenye nguzo za umeme, inasababisha nguzo za umeme za Tanzania kuwa na bei ya juu zaidi kuliko nguzo za umeme za *South Africa*. Mti unaponunuliwa unapigwa VAT, unapokuwa *processed* kabla ya kuuzwa VAT tena kwa mara ya pili. Hapo hapo kuna kitu kinaitwa *LMDA, royalty*, hapo hapo kuna *cess* na mlolongo mwengine wa kodi ndogondogo ambazo zipo kwenye idara ya misitu, inafanya bei za vitu hivyo viwe juu sana, inaturudisha nyuma sana kimaendeleo. Bei ya simenti, bei ya nondo, bei ya bati, bei ya misumari, katika eneo zima la ujenzi zipo juu sana. Naomba Wizara hii ikae chini iangalie eneo hili kwani ni muhimu sana. Pale ambapo kuna kodi mbili mbili zitazamwe na zirekebishwe, hatutarajji matatizo haya kwenye bajeti ijayo yatokee tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama mkija kwenye Bajeti ijayo na matatizo haya yanayojirudia na ambayo tunayasema kila siku tutafika mahali hututalewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Mtambile kwa ushirikiano wao, busara zao, hekima zao na dua zao kwangu katika kufanya kazi zangu kwa ufanisi ndani ya Bunge au nje ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aliyyasema Mheshimiwa Job Ndugai mwisho kwamba muda ni mdogo ni kweli, mimi binafsi niliomba kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini sikupata nafasi na leo hii ndiyo inakuwa mara yangu ya kwanza, ni vema hili likazingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi wangu wakuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*) Profesa Ibrahim Haruna Lipumba - Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Machano Khamis Ali na Katibu Mkuu Maalim Seif Sharif Hamad kwa busara zao na hekima zao katika kuendeleza chama chetu, Mungu awabariki na *Inshallah* tupo pamoja nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri aliongelea sana suala la wastaifu nami nataka nianzie hapo. Kila mfanyakazi ni mstaifu mtarajiwa, hali za wastaifu wetu ni mbaya sana, bei za bidhaa zimekuwa zikipanda siku hadi siku na inaonekana bado Serikali haijaka ikapanga mipango madhubuti ya kuwaenzi na kuwaendeleza wastaifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la *pension* ya wastaafu wa kima cha chini ambacho kilitangazwa Juni na leo hii, kwamba Serikali imepandisha kima cha chini cha *pension* cha wastaafu kutoka shilingi 21,601 hadi shilingi 50,114 wastani wa shilingi 1,670 kwa siku, kwa hiki ni kima kidogo sana, ni lazima Serikali iangalie utarabu mwingine.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba wakati Waziri akitangaza kima hiki cha chini cha *pension* nadhani alikuwa hajaangalia jambo lingine, kuna tangazo la Serikali GN. 89 ambalo lilikwishatangaza rasmi kima cha chini cha *pension* kitaondoka kutoka shilingi 21,601 hadi shilingi 36,000. Ni GN. 89 la tarehe 21 Julai, 2006 ndani ya awamu hii ya nne.

Mheshimiwa Spika, anapokuja Mheshimiwa Waziri akasema sasa tunaondoka kwenye shilingi 21,601 tunakwenda kwenye shilingi 50,000 je, ile GN. ambayo imetolewa kwenye kipindi hicho yeeye alikuwa haelewi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu GN. hiyo Na. 89 ili Waziri baadae wakati akijumuisha anieleze na awaeleze Watanzania GN. hiyo ilikuwaje. Naomba kunukuu; “*Subsidiary Legislation to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 29 Vol. 87 dated 21<sup>st</sup> July, 2006 Printed by the Government Printer, Dar es Salaam, by Order of Government. GN. No 89 Published on 21<sup>st</sup> July 2006 The Public Services Retirement Benefits Act Cap. 371 Order made under Sec 30 of The Public Services Retirement Benefit Minimum Pensions Amendment Order 2006:*

1. *This Order may be cited as The Public Services Retirement Benefit Minimum Pensions Amendment Order 2006 and shall be reads as one with The Public Services Retirement Benefits Minimum Pensions Order 2003 referred here in the Principal Order and shall be deemed to have come into Operation on the 1<sup>st</sup> day of, 2002.*

2. *The Schedule to the Principal Order here by deleted and Substituted for it with a fallen new schedule rate percent from 7.79 % from 21,601/= Monthly to 36,000/= is the same annually from 129,606/= to 216,000/=.*

Mheshimiwa Spika, hapa inaonekana kwamba wastaafu katika kipindi hiki walitakikana waondoke kutoka katika shilingi 21,601/= hadi shilingi 36,000/= kwa kipindi cha muda wa miezi sita. Mstaafu ambaye alikuwa akipata shilingi 129,606/= alitakikana apate shilingi 216,000/=. Tena basi shughuli hii ilikuwa ianze kuanzia Julai, 2004. kwa muda wote hivi sasa ni miezi sitini sasa kwa hiyo, kwa kila kipindi cha muda wa miezi sita, kila mstaafu wa kima cha chini cha pensheni anaidai Serikali shilingi 87,000/= kila muda wa miezi sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni miezi sitini kwa hivyo kila mstaafu anaidai Serikali shilingi 870,000/= ninayo hapa na baadae nafikiria kwa utaratibu inaweza ikafika kwako, Mheshimiwa Waziri atueleze ilikuwaje, mkatoa jambo zuri hili la Serikali mliloliandaa na vielelezvo vyote lakini hadi leo hakuna utekelezaji. Je, hamuoni mnawadhulumu wastaafu wa kima cha chini cha pensheni haki yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni haki yao na ni matarajio yangu kuwa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho nafikiri atatueleza na ataeleza wastaafu wa Tanzania wote haki yao hii ya msingi. Hilo ilikuwa ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na hilo vile vile baya zaidi kwa kipindi hiki toka Julai, 2004, wastaafu walikuwa wakipewa *pension slip* zao lakini sasa zimeondoshwa, kipindi hicho zimeondoshwa na hasi sasa hawapatiwi. Hasa kumekuwa na mkanganyiko mkubwa hawaelewii malipo yao halali ni yapi! Unapowaondolea *pension slips* zao hawaelewii. Nafikiria ni vyema Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho na hili nalo alitolee ufanuzi juu ya ni sababu zipi za msingi ambazo zilifanya waondoe *pension slips* za wastaafu hawa tangu mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika hilo mimi nina ombi maalum, pale ambapo mstaafu mme au mke atakapofariki mmojawapo atakayebakia basi pensheni ile aendelee kupewa mmoja wapo kwa sababu mambo mengi yanamuelemea, aendelee kupewa pensheni ile mpaka na yeze atakapofariki. Nafikiria hili litawenza angalau kumfariji huyo mmoja aliyebakia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata mafao yao unachukua muda na imebainika kwenye ripoti mbalimbali na kwa mujibu wa ripoti inayoonekana mara nyingi basi kumekuwa na malalamiko mengi, lakini hata hivyo wastaafu wanadhuluiwa, wastaafu wengi inapofika wakati wa kupata mafao yao wanadhuluiwa na kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2007 imebainika kuna mapungufu makubwa katika ukokotoaji. Ripoti hii inabainisha kwamba katika majalada 7,014 ambayo yalikaguliwa imegundulika majalada 514 yangelipwa wastani wa pungufu wastani wa shilingi milioni 416, huu ni msiba mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inaonekana sisi hatuna watalamu wa kutosha ndani ya maeneo haya, inakuwaje unakokotoa unawapunja wastaafu? Mbona mara nyingi huwaongezei, kwa nini uwapunje kila wakati tu, si uwaongezee? Uwaongezee fedha ndiyo utaonekana umekokotoa vizuri ati! Lakini mimi najiuliza, hivi shughuli kama hii ya kukokotoa ambayo inahitaji watalamu, ni kweli hatuna watalamu wa kutosha? Hivi hao wanakokotoa na wao wakati ukifika watajipunja? Kweli hilo!

Mheshimiwa Spika, ningombaa Mheshimiwa Waziri eneo hili nalo aliangalie. Lakini si ripoti hii tu, hata ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2008 vile vile nako kuna matatizo makubwa na hapo kuna matatizo makubwa imegundulika kwamba katika majalada 5,313 ya wastaafu majalada ya wastaafu 142 yangelipwa pungufu shilingi 288,320,408/= huu ni msiba mkubwa! Sasa mimi najiuliza jamani, Mheshimiwa Waziri hivi huko Wizarani huko jamani kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nalo ni vema Waziri akaliangalia ili lipatiwe ufumbuzi, mwaka jana nilisema kwamba haipendezi hata kidogo inafika wakati mstaafu ameshafariki ndiyo mnaandaa risala kwamba ulikuwa unamuenzi na unampenda, lakini alipokuwa hai hukufanya lolote na hukumpa mafao yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa haraka haraka; midhamu ya matumizi ya fedha Serikali; naipongeza sana *TRA* kwa kukusanya fedha nyingi, karibu bilioni 350 kwa mwezi ni jambo zuri. Lakini inaonekana pamoja na jitihada kubwa ambazo zinafanywa na *TRA* inaonekana kuna ubadhifuru mkubwa wa fedha za Serikali. Inaonekana kwamba kipindi cha mwaka 2002 mpaka 2006 kuna jumla ya upotevu wa fedha, ufisadi na ubadhilifu wa shilingi bilioni nne milioni mia nne na tatu na Serikali ilishtaki kesi 321 Mahakamani, lakini kwa bahati mbaya sana, Serikali ilishinda kesi 14 tu. Ni Serikali ambayo ilishtaki kesi mahakamani 321 ikashinda kesi 14 tu mahakamani, hii ni aibu kubwa. Serikali ina vielelezoo vya kuitetea Serikali lakini Serikali baadaye katika majibu ambayo yameletwa hapa Bungeni

kwa *Hansard* ya tarehe 31 Julai na 31 Agosti, 2008 imeeleza wazi kwamba, ushahidi umekosekana Mahakamani na baadhi ya wahusika wametoroka.

Mheshimiwa Spika, Serikali yenyewe ndiyo iliyoshtaki ina watalaamu wa kutosha, wamekwenda mahakamani halafu mnapojobu wananchi fedha zao za umma walipakodi maskini mnasema baadhi ya wahusika wametoroka au hakuna ushahidi wa kutosha, kwa kweli haiingii akilini hata kidogo, ningeiomba Serikali ikae kwa umakini sana kuona fedha hizo za mlipa kodi maskini basi kwa vyovyyote iwayyo basi virejeshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa haraka haraka; kuna vichekesho vingine ukiangalia ripoti ya *CAG* ukurasa wa 141 naomba ninukuu kwa haraka haraka, taarifa za upotevu inaonesha kuwa hasara kwa Serikali imeongezeka kutoka shilingi bilioni mbili milioni mia tatu na sabini laki sita na themanini na nane katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi shilingi bilioni tatu milioni mia tano tisini na nne mia mbili na tisa elfu katika mwaka 2007/2008 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni moja milioni mia mbili ishirini na tatu mia tano ishirini na moja elfu sawa na hamsini na mbili huu ni msiba mwingine mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila siku fedha zinapotea, namna ya kudhibiti hakuna, ahadi zimekuwa nyingi tutaendelea kupanga mikakati kabambe kuwadhibiti wabadhilifu na ufisadi, walipa kodi maskini wanaendelea kuchangishwa fedha zao lakini hali imekuwa ni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, tumekuwa na kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo kwanza, lakini naangalia nadharia nzima hii kwamba ni jinsi gani wakulima wetu wananzaika na mazao ambayo bei ya mauzo ya nje yakipanda, ukiangalia kitabu cha hali ya uchumi ukurasa wa 48, utakuta kwamba mauzo ya nje ynaongezeka kwa baadhi ya mazao lakini ndani ya nchi hapa mazao bei yake inapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano nikichukua sasa zao moja la karafuu nasema vile vile wastani wa bei katika soko la dunia uliongezeka kutoka dola 3577.5 kwa tani kutoka mwaka 2008 kutoka dola 2968.3 mwaka 2007 sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Hii inaonyesha kwamba bei ya karafuu inaonekana ukikokotoa kwa taarifa hii inaonekana kwamba angalau kwa kilo ingelikuwa shilingi 4200. Lakini mkulima wa karafuu wa Pemba, Unguja, Tanga na Morogoro bei ya karafuu hapa kwa kipindi hiki ilishuka. Mwanzo wakulima wa karafuu walikuwa wakilipwa shilingi 3500. Basi baadaye ikaja ikateremshwa kutoka 3500 mpaka 2500 hivi najiuliza je, kwenye soko la dunia ikiongezeka nchi kwetu tunateremsha? Huo ndiyo mpango wa uchumi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kengele ya pili. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud Salim kwa kuongea kwa dhati. Sasa sijui kama uliyoyasema ni sahihi lakini ndiyo mchango hivyo.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu. Baada ya hapo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii muhimu ya Wizara ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuchelea yale ambayo yalinikuta nilipochangia Wizara ya Katiba na Sheria ambapo nilijiandaa sana lakini hatimaye yake nikapata maeneo machache mawili tu na basi na leo nimechagua maeneo machache ya kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza mchango wangu unakwenda katika Benki ya Posta, hii ni benki ya Watanzania. Mheshimiwa Waziri ameita benki ya umma, imeundwa chini ya Sheria namba 11 ya mwaka 1991. Kwa ujumla inajitahidi sana kufanyakazi zake. Tunaona, Wabunge tunakopeshwa lakini inakabiliwa na matatizo mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 48 amezungumza Benki hii na amesema mpaka sasa ina matawi 27 tu Tanzania nzima. Matawi 27 kwa Mikoa 26 na katika matawi hayo 8 yapo Dar es Salaam basi wazi ni kuwa haikuenea. Haikuenea kimikoa na kwa maana hiyo haimo katika Wilaya zote za Tanzania. Hilo ni moja katika tatizo lake. Mtandao wake ni mdogo sana. Sisi kule Zanzibar tunayo Mjini Unguja tu, Pemba haiko na katika Mikoa mingine yote haimo. Aidha, kwa utafiti wangu hapa Tanzania Bara Mkoa wa Singida haiko Benki ya Posta. Kwa hiyo, Mikoa hiyo hamna lakini katika Wilaya zote Tanzania, Benki hii haimo. Lakini ni benki ya umma na ni Benki ya Serikali. (*Makofi*)

Aidha, benki hii inakabiliwa na matatizo ya majengo. Katika taarifa ambazo ninazo ni kuwa majengo yake yote wanakodi yaani siyo yao. Kwa maana hiyo, wanapoteza fedha nydingi sana za kulipa na pale inapofika wakati wa kukarabati basi wanakarabati. Lakini kubwa kuliko yote ni ndogo mno kintaji haina mtaji wa kujitosheleza. Kwa maana hiyo haikui, inaendelea kudidimia. Haitoi huduma muhimu za Kiserikali kutokana mtandao wake na mtaji wake. Haitoi mishahara kwa wafanyakazi, haitoi malipo ya pensheni, na kwa maana hiyo basi ni benki butu yaani benki ambayo ina upungufu mkubwa sana katika kuhudumia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10 alisema maneno yafuatayo naomba kunukuu; “Baada ya kuimarisha mtaji wa benki hii, kwa maana kuhusu pia *TIB*, Serikali itaelekeza nguvu katika Benki ya Posta ambayo pia ni benki ya umma.” Hayo ndio maneno ambayo yamesemwa mwaka jana. Lakini jibu ambalo mara hii anatupa juu ya *commitment* yake hiyo basi ni kuwa ameipatia Benki hii shilingi bilioni moja katika kitabu chake ambacho leo ametusomea Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 48 namba 91 mstari wa mwisho anasema; “aidha Wizara imetenga shilingi bilioni moja ili kuongeza mtaji wa benki hii.”

Mimi nadhani bado amefanya mchezo tena mchezo wa kweli kweli kwa sababu ameilingansiha kwenye ukurasa wa 49 sawa sawa na *Village Community Bank* ambapo nayo ameipa bilioni moja vile ambavyo tunaita *vicoba*. Kwa hiyo, Benki ya Posta katika umuhimu wake lakini unailinganisha sawa sawa na *vicoba*, mimi nadhani Mheshimiwa Waziri bora atutake radhi kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Wizara haijawa *serious* katika kuisaidia benki hii. Ni benki muhimu, benki yetu lakini Serikali haijaisaidia. Uwezo wake katika baadhi ya mabenki kwa uzoefu wangu ukiacha hapa Dodoma ambapo napatumia sana ninapoondoka hapa ninapo kwenda pale Zanzibar basi kwa heshima yangu ndio nakubaliwa nichukue milioni mbili. Lakini ninapomtuma mke wangu au mtu mwengine yoyote basi hapewi milioni mbili, anapewa chini ya hiyo au afanye *order* ya muda mrefu ndio anaweza akapewa milioni mbili. Ni benki ndogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba zaidi Mheshimiwa Waziri aitazame ili iweze kukua nayo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Unaweza ukahamishia fedha kwenye Benki ya Wanawake. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nadhani baada ya kumaliza kikao hiki na mimi nitakwenda kujunga ndani ya benki hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mada yangu ya pili ni Chuo cha Mipango. Chuo cha Mipango kina umuhimu wake katika nchi yetu. Kinatoa watalaam wazuri, wanatusaidia lakini nacho kina *challenge* nyingi sana. Kwa bahati nzuri Waziri naye ameizungumza vizuri mwisho wa kitabu chake ya kuisaidia ili ikue kwa hiyo, ninamuunga mkono kwa hili la kukisaidia Chuo cha Mipango ili nacho kikue. Lakini katika sura yake ya sasa basi nacho hakukukaa vizuri, kimejitawanya sana siyo kwa maana ya ufanisi lakini kwa maana ya ufinyu wa ile *infrastructure* yake. Ukienda *Furaha hostel* hapo ina sehemu kidogo, *CCT* pale Kanisani ina sehemu kidogo, *Area D*, ina sehemu kidogo, Miiji huko *main campus* nako ina sehemu kidogo. Lakini nashukuru amesema kuwa ataisaidia, nadhani imeshapata eka 17 ili hapo baadaye iweze kuja. Lakini ni maneno tu ambayo amesema hasa hajasema amekipa chuo hiki kiasi gani ili kiweze kuondoka katika sura kama hiyo. Kwa hiyo, nacho ni chuo muhimu kinakabiliwa na matatizo mengi lakini bado hakijapata uwezeshaji wa kutosha nacho kikakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kama nilivyosema sina mengi umuhimu wa Wizara hii katika mambo ya Muungano. Unapozungumza na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar basi wanasesma Wizara hii ndio inayongoza kwa kero za Muungano na ni kweli. Lakini Waziri wa Wizara hii ndiyo mtoro kabisa wa vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni mtoro *number one*, katika Mawaziri ambapo hawaendi katika vikao vya kufanikisha utatuzi wa hayo matatizo. Sasa sina uhakika lakini naamini walioniambi ni viongozi Mawaziri, sasa kama si kweli basi atatuambia kuwa si kweli basi lakini kama kweli apunguze utoro ili tufike kwenye muafaka wa vikao vyetu hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo kama nilivyosema sina mengi naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kwa kweli kwa kunipatia nafasi hii walau na mimi kuweza kutoa mawazo yangu machache kwa muda huu wa dakika kumi na tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi maskini, ni moja kati ya nchi ambazo ziko katika umaskini uliokithiri. Nchi yetu kutokana na hali hiyo imekuwa ikijitahidi sana kwa vipindi mbalimbali kuweza kuhakikisha kwamba inajaribu kutoondoka kutoka pale tulipo ili walau kutusogezza na sisi tuweze kuwa katika hali iliyobora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo ambayo imesababisha hata viongozi wa siasa na hususan chama chetu kuja na kauli mbiu ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, yote hii ni katika kuhakikisha kwamba tunaboresha hali za kiuchumi kwa wananchi wetu ili waweze kuwa na maisha bora hapa Tanzania. Lakini ingawa nchi yetu ni maskini, nchi yoyote maskini inakuwa na changamoto nyingi sana na kutokana na changamoto hizo inabidi hata

vipaumbele vyake vinakuwa ni vitu ambavyo mtu unaweza ukakaa kila kitu unakiona na kipaumbele kwa sababu afya za watu zinakuwa ziko katika hali ngumu kwa hiyo unajitahidi walau uboreshe afya, chakula kuna uhaba wa chakula, elimu, elimu ni duni kwa hiyo kila kitu unakiona ni kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninachotaka kusema ingawa nchi yetu ni maskini lazima viongozi wa Tanzania tuwe na vipaumbele. Nasema hayo kwa sababu hata siku moja huwezi mtu ukasema, wazungu wanasesma *if all roads take you there, no road will lead you there, au if all road takes you there, you will never get lost*. Kwa sababu kama wewe unasesma barabara hii itanifikisha ninakokwenda huwezi kupotea kwa sababu hatimaye utafika sehemu. Lakini suala linakuja kwamba unafika wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto kubwa sana katika hii nchi lakini mimi tatizo kubwa ambalo nalionia ni mipango mingi bila utekelezaji usiokuwa madhubuti na ambaa unajali muda muafaka. Nasema hivyo kwa sababu yako mambo mengi sana ambayo Serikali inayapanga na yako mambo mengi sana ambayo Serikali inayafanya kwa mustakabali wa Taifa letu. Lakini hivi tukikaa hapa hata hawa Wabunge tukikaa tukijuliza kwamba tangu tumekuja mwaka 2005 baada ya kuchanguliwa tumekuja hapa Bunge kuanzia mwaka 2006 mpaka leo, ni kitu gani kikubwa ambacho unaweza kusema kwamba hiki walau tumetoka kuanzia kule tuliko kimetufikisha asilimia 90. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nawashauri viongozi tusiwe na ile tabia ya kugusa hapa unagusa kidogo, hapa unagusa kidogo hatuwezi kufika popote na hii inatusababisha kwamba unakuta kwenye elimu tunagusa kidogo, unakuta kuna madarasa tumejenga, imefika wakati walimu hakuna, tunagusa kwenye kilimo tumekwenda kidogo tunafika mahali tunakwama, tunakuta pia kwenye barabara tumekwenda kidogo tumekwenda mambo hayaendi, hivi tatizo ni nini? Mimi naona kwamba tatizo lililopo hapa sijui ni uvivu wa watu kufikiri au sijui ni ile kuona kwamba nchi yetu ni maskini basi kila mtu anafanya kivyake vyake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia pia katika hili suala zima la *coordination* kati ya Wizara na Wizara. Hili ni tatizo kubwa sana mimi naona kwamba hakuna *coordination* ya kutosha kati ya Wizara moja na Wizara nyingine na hii mfano mzuri tumeona hata jana, tunazungumzia kuondoa umaskini, lakini Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imepitisha kwamba magunia ya Tanzania yasitumike. Sasa unashangaa, watu wengine wanasesma ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya tujitahidi kuondoka kwenye umaskini lakini vile vile anakuja mtu mwingine huku, hawa wataalam wengine wanakuja na mawazo ambayo ni tofauti. (*Makofi*)

Sasa namna hii inaonesha kwamba hakuna *coordination* kati ya Wizara na Wizara na pia mfano mwingine, tunapozungumzia kwamba kauli mbiu ya sasa kwamba Kilimo Kwanza, hivi je, katika Wizara hizi wamejitahidi kwa kiwango gani kuhakikisha kwamba kweli hiki kilimo kinatutoa kule tulikokuwa kutufikisha katika hali nzuri. Nasema hivyo kwa sababu ukiaangalia kwenye kilimo, kilimo ni sekta moja, lakini katika kuinua uchumi ni sekta ambayo ni kubwa sana yaani ni sekta tegemezi kwa kweli. Lakini ukiangalia hapa kilimo hapa peke yake kuna nishati inahusika hapo kwa sababu kuna masuala ya umwagiliaji inatakiwa kuwe na *pump*, kuwe na umeme, kuna maji yanatakiwa hapo. Kuna vitu vingi sana kuna viwanda, kuna biashara, kuna masoko kuna vitu vingi. Lakini je, hivi kweli hizi Wizara zinasaidia kweli hii kauli mbiu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekaa hapa tumejadili mambo mengi sana. Mimi huwa wakati mwingine nashangaa, Tanzania ni nchi ambayo ina maziwa mengi sana. Tumeshawahi

kusema Tanzania ni nchi ambayo ina maziwa mengi sana, tumeshawahi kusema Tanzania ni nchi ambayo imebarikiwa ina rasilimali nyingine sana, lakini tunazitumiaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitolee tu mfano nchi ya Egypt mvua inanyesha siku 18 lakini inauza mchele Iraq, Turkey. Tuangalia nchi Cyprus asilimia 40 ya Pato la Taifa linatoka katika matunda wao wanauza miembe, wanauza dola milioni 100. Hivi tatizo letu sisi ni nini yaani ukiangalia unaona kwamba ni watalaam wengi sana huwa wanapenda kuja huko juu wanajaa sana lakini hivi tatizo letu inakuwa ni nini mbona hatuwezi kukaa tukasema basi tuamue kuingia katika kitu kimoja ambacho tutakifanya kazi ili tuweze kukitoa katika hali hii tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiangalia katika hilo hilo nizungumzie suala zima la *recue plan* kwa kweli katika hili napenda kumpongeza sana Gavana wa Benki Kuu. Mtu huyu anafanyakazi kubwa sana. Lakini watu huwa wanasema hivi *good person in bad system* na wewe pia unakuwa mbaya kwa sababu inabidi kwa kweli tufikie wakati tuachane na haya mambo ya kuchanganya siasa na uchumi. Tukiweza kufikia hapo tutaweza kwa kweli kuondoa Taifa letu kutoka katika umaskini huu uliokithiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani, kwa sababu hii *rescue plan* imekuja, lakini bila kuondoa urasimu uliopo huku Serikalini hakuna kitu ambacho kitakwenda. Itakuwa ni kila siku tunakaa huko Hazina mambo yanakwenda anachukua huyu faili anapeleka faili anapeleka huyu *process* ya kutoa shilingi 10,000 Serikali ni ile ile ya kutoa shilingi bilioni moja. Sasa ifike wakati tuangalie kwamba kama kweli tumeamua kuliondoa Taifa letu katika huu umaskini uliopo hivi sasa kuboresha nchi yetu na walau kuinua hali za maisha za Watanzania mimi naomba kwamba ile mipango ambayo watu walau wanakuja na mawazo mazuri ya kuweza kuhakikisha kwamba tunaboresha walau iandane na hali halisi ya utendaji kazi. (*Makofi*)

Katika hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu nilichangia nilisema hivi kwamba uozo huu wa kulindana lindana uishe. Ninapozungumzia suala la uchumi sitasita kuendelea kusisitiza hilo. Haya mambo ya kulindana kwamba huyu jamani ni mwenzetu, huyu ni mtu ambaye tuko naye pamoja, huyu tumuache acha acae kwanza, kwanza ni mtu mzima mzee karibu anastaifu, tukiendelea na utaratibu huo hii nchi itakuwa inakwenda chini, chini kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kufanya hivyo itakuwa tunachanganya siasa na uchumi. Hakuna nchi duniani ambayo imeweza kuendelea kwa kuchanganya siasa na uchumi. Wenzetu huko Ulaya na Marekani ingawa ni mifano ambayo kwa kweli tumetofautiana kwa hali nyingi lakini mimi huwa napenda kutolea wale hawana dhahabu, wale hawana maziwa makubwa kwamba sijui kuna samaki wengi, lakini ni akili tu. Sasa hizi akili ambazo wenzetu wanazitumia kila siku kuamua kila siku wanakuja na mipango mipy ya kuwainua watu wao sisi tukiwa na hawa watalaam na tukawa tunamezena wale watu ambaa wanafanya vibaya tutaendelea kuwa chini na chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine la biashara. Nizungumze kuhusu hili suala la sekta isiyo rasmi Tanzania. Kuna watu ambaa tunaita kwamba ni wajasiriamali, tunawaita wafanyabiashara ndogo ndogo. Hii ni sekta isiyo rasmi, ingawa tunaita kwamba ni sekta isiyo rasmi lakini asilimia 30 mpaka 40 ya sekta rasmi inategemea sekta isiyo rasmi. Katika uchumi wa Tanzania tuangalie je, tutawezaje kuhakikisha kwamba tunaisaidia hii sekta isiyo rasmi kuweza kuhakikisha kwamba inaijiinua na kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani, kwa sababu katika hawa wafanyabiashara wadogo hakuna mtu ambaye huwa anakaa akaibuka tu, mtu yeoyote anakuja kwa kuanzia huku chini lakini hawa wafanyabiashara ndogo ndogo ni watu amba wanakwamishwa kwa kiwango kikubwa sana. Ili mtu uweze kufanya biashara Serikali na viongozi wakubwa wote wamekuwa wakihimiza kwamba jamani jitahidini mkope ili muweze kufanya biashara. Lakini hivi haya masuala ya Serikali kuwanyamazia kimya hizi taasisi ambazo zinakopesha watu, taasisi za *Bayport*, taasisi za *BRELA* mnakaa mnawanyamazia kimya, wafanyabiashara wanashindwa kukopa kutokana na masharti makubwa, riba zimekuwa ni kubwa kupita kiasi, walimu wajitahidi walau waweze kuendesha maisha ya familia zao wanashindwa. (*Makofi*)

Mimi naomba Serikali *BoT* wamekuja na mpango huu wa kuhakikisha kwamba hizi taasisi za kibiashara wanazitoa kule kwenye Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko kuja kwao, lakini mimi naomba wahakikishe kwamba wanalfanya hili jambo kwa haraka sana huu urasimu amba unaendelea kuwepo kila siku ndiyo urasimu amba utaendelea kutunyamazisha sisi na kutufanya Watanzania wale amba ni maskini waendelee kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama mtu unakaa unasema mimi leo hii nataka nifanye biashara, labda nifanye biashara pengine biashara ambayo ni ndogo ndogo sheria mipango miji hainitambui, sheria za taasisi za mikopo, mikopo ni mikubwa hivi tutafika kweli? Hawa wafanyabiashara amba wako amba ni wafanyabiashara wadogo hatuwezi kuwasaidia na kuondokana na umaskini ikiwa kama hatutakuja na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba hii mipango mingine yote ambayo tunazungumzia kwamba tuwainue kiuchumi kama hatutahakikisha kwamba tunaiboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka nikizungumzie ni kuhusu hili suala la *second generation financial reform*. Mimi nilikuwa naomba kuulizia hivi hii imefika wapi kwa sababu hali ya uchumi ni mbaya. Kama nilivyoelezea hizi *coordination* kati ya Wizara na Wizara zimekuwa katika hali ambayo kwa kweli hairidhishi. Mimi naomba sana *BoT* waweze kuhakikisha kwamba hii *second generation financial reform* waweze kuileta kwa haraka hili ilitawezekana ikiwa kwamba tutasaidia. (*Makofi*)

Wizara nyingine zitasaidia kuhakikisha kwamba yale maeneo mengine yenye urasimu yanaondoka kwa sababu hii ndio itakuwa suluhisho la mkopaji, hii ndiyo suluhisho la hizi taasisi ambazo zinakopesha ili walau kuweza kuangalia suala zima la riba na kila kitu. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iweze kuangalia na kuhakikisha kwamba kunakuwa na mpango madhubuti wa kuweza kuhakikisha kwamba hata hii *second generation financial reform* inafanyika kwa wakati. Kwa sababu sasa tunazungumzia kwamba hali yetu ya uchumi rescue plan bila kwenda sambamba na hii *second generation financial reform* tutakuwa hatujafanya kitu kwa sababu malalamiko mengi sana ambayo yanatolew ana wananchi wetu, malalamiko mengi sana ambayo yanaletwa katika hii sekta ya fedha yanabashwa na mipango mibaya iliyopo na matatizo ambayo ka kweli ni matatizo makubwa ya kwamba mtunga sera ni mwagine na mtekelezaji ni mwagine. Unakuta kwamba mabenki na taasisi nyingine za fedha wanakuambia kwamba *BoT* wanashughulika na benki, hizi taasisi za fedha wao wanakuwa *registered BRELA* kama makampuni wakienda kule kuwa *registered* kama makampuni *BoT* wanakuambia sisi hatuna uwezo wa kuweza kuwazuia hawa watu, hatuwezi kuwa na usimamizi wa moja kwa moja kwenye hizi taasisi hizi ziko *BRELA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tukiendelea kufanya namna hii mimi wakati huwa nashangaa kwamba hivi hawa watalaan amba huwa wanakaa chini wanafikiria vitu kama hivi huwa

wanawaza nini, maana yake wakati mwingine inakuwa kama mtu anakaa chini anafikiria kitu cha kuangalia kwamba hiki ninafanya lakini anaangalia hapa tu. Lakini kila siku tunazungumzia kwamba ni lazima tuwe na mipango ambayo itakuwa ni *long term* na *short term program*. Lakini unakuta kwamba mipango mingine inakwenda inakuwa ni kama *short term* unashindwa kuelewa kwamba watu wanajua, kwa sababu hata hawa watalaam wakati ule wanakuwa wanapanga mipango walikuwa wanajua kabisa kabisa kwamba Tanzania ni nchi maskini siyo kwamba ilikuwa tajiri sasa hivi ndiyo tunaharibikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa mchango wako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunakaribia kufika muda wa kusitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu. Nirejee kusema kwamba wachangiaji wangu wawili wa jioni na baada ya hapo nitaanza kuwaita Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri. Ni Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh na nimeandikiwa barua na Mheshimiwa Kabwe Zitto amejitoa kwa hiyo, imekuwa bahati sasa kwa Mheshimiwa Maulidah Anna Komu kwa hiyo hawa wawili wakishamaliza basi tutaingia katika kusikiliza majumuisho ya hoja kutoka kwa Serikali. Kama nilivyosema lengo ni kwamba Muswada wa *Appropriation* nao tuuzungumze leo kama ulivyopangwa ili tuweze kukamilisha hiyo kazi kwa siku ya leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nakumbusha tena ni muhimu sana saa mbili jioni hii usiku kuna *briefing* fupi tu kuhusu *CDCF* imepotoshwa kiasi ambacho lazima na sisi wenyewe tukae pamoa tuweze kupata msimamo mzuri. Kwa hiyo, si kikao kirefu ni kifupi sana nitaongoza nadhani tutakwenda vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.57 Mchana Bunge lilahirishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 Jioni Bungelilirudia*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

(*Majadiliano Yanaendelea*)

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima na jioni hii kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kutoa na mimi mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa fedha. (*Makofi*)

Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Magomeni ambao wao ndiyo walioniwezesha kunipa kura nyingi na kuwa Mbunge wao kuwawakilisha katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na nahaidi kwamba ntaendelea kuwatumikia kwa moyo wa dhati kabisa na kuwatetea wao na wananchi wa Zanzibar kwa jumla kwa madhumuni ya kutafuta mstakabali wa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kiutamaduni na maendeleo kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka leo nichangie katika suala zima la *TRA*, kama tunavyojua *TRA* ni chombo cha Muungano, kinafanya kazi zake pande zote mbili za

Muungano. *TRA* ni tatizo sugu kwa upande wetu wa pili wa Zanzibar na suala hili tumepega kelele kila siku, mimi nakumbuka toka wakati naingia katika Bunge hili, kila mwaka wakati wa Bajeti nazungumzia suala hili. Lakini inapotokea kuona kwamba wenzetu wanaona kwamba kelele za mlango hazimkeri mwenye nyumba. Lakini sisi kwa kweli suala la *TRA* ni tatizo sugu na ukweli nakuambieni ni kikwazo au ni sababu kubwa sana inayoleta huu mkanganyiko wa hizi kero zinazo lipuka kila siku za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar *Alhamdulillah* hatuna matatizo ya umeme raha tupu, kila kijiji kina umeme, barabara nzuri, maji yanapatikana kwa kiasi sio nchi nzima ila sehemu kubwa sana matatizo hayo si makubwa, tatizo la Unguja sasa hivi ni uchumi wa watu mtu mmoja mmoja na uchumi wa Zanzibar upo katika nyanja ya kibashara, hiyo inaeleweka si jana, si leo ni jambo la historia kwamba Zanzibar uchumi wake uko kwenye biashara si kitu kingine. Tatizo letu ni kwamba Zanzibar ofisi za *TRA* ambazo zinafanya kazi kwa muongozo wa makao makuu ambayo yako Dar es Salaam kitu kile ambacho kwa mfano muagizaji kaagiza bidhaa kutoka nje ambayo anakuwa anapeleka *documents* zake *TRA* anaandikiwa bei na kodi ambayo anatakiwa alipe na analipa kufuatana na maelekezo au kufuatana na muongozo wa *TRA* na bei hizo sio zinabuniwa pale Zanzibar, zinabunia makao makuu kwenye *database* ya *escudo+*. Kinachoshangaza bidhaa zile baada ya kuzilipia Zanzibar kodi anakuja nazo Dar es Salaam anaambiwa weka pale zinafanyiwa *reverification* anaambiwa alipe tena *excess duty*, hiki kitu kinakuaje, hili jambo linatunyanyasa vibaya sana natumepiga kelele si jana si leo si juzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni kitu ambacho kinasababisha ukosefu wa imani wa watu wengi sana kwamba jamani na ndiyo inapofika sasa hivi mkisikia watu wanlipuka kwa maneno tu ambao wanaona kwamba inashiria Muungano ni kweli, hawana nia ya kuvunja Muungano mimi naamini kabisa watu wa Zanzibar wana nia kabisa ya Muungano, lakini inafika wakati wanasema potelea mbali, maana yake tukiwaambia kwa taratibu hawa watu hawasikii, hebu tufanye hivi jambo ambalo utaona kwamba linaleta maudhi, lakini na kweli na sisi tunaudhika sana kwa sababu haiwezekani kabisa ikiwa mtu amelipa gari yake kule Zanzibar, kwa mfano ameagiza gari akawekewa kiasi fulani kama Dola 1200 au 2500 gari ile ile kama Dar es Salaam inachajiwani *the same price* lakini ye ye akija nayo huku anaambiwa alipe ushuru zaidi nyongeza ya tofauti ya bei wakati bei ile haikutolewa pale Zanzibar imetolewa kwenye mtando ule ule ambao upo makao makuu ya *TRA*. Hii kitu kiko vipi? Lakini bei kama ile ambayo imelipwa labda Horohoro kule Tanga, ikiingia wanasema haina matatizo, ikitokea Tanga ikija Dar es Salaam haina matatizo, *why Zanzibar?* Kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi kule tunapata taabu sana kwa sababu hatuelewi mambo haya yako vipi na tunapiga kelele kila siku, kila siku ya Mungu; kwa mfano hivi juzi imetokea *system* mpya muagizaji anaagiza gari kutoka nje ameleta Zanzibar imefika anakwenda *kulodge document* inachukua mwezi mzima, siku 30, siku 30 na hajua hata ile *document* yake ifuatilie wapi na hii imefanyiwa makusudi kwa sababu siku za nyuma ilikuwa ukipeleka *document* yako siku moja, ya pili yake gari unatoa na sio kama unatoa kwa sababu ya bei ambayo inafanyiwa *favor* hapana, bei inatoka kutoka Dar es Salaam kwenye huo mtando wa *escodo* + + unalipia lakini kwa sababu ile *timing* iko haraka haraka tunafanya sisi kuwa tunafanya kazi, hakuna urasimu wakaona hata hao tuwakate hapa, tuwazue siku 30 hii *importation* ya kupitia Zanzibar isiweipo ili tu ili sisi tuumie, tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu haya ndiyo yalijitokeza juzi juzi zikatoka kauli kule watu kung'ang'ania mafuta kwa sababu tulishaona sasa hivi kwa biashara hakuna, kwa mtaji huu jamani hawa wenzetu hawataki hebu tupigeni kelele kwenye mafuta potelea mbali linalo

kuwa naliwe. Inakuja hivyo, na sio kwa nia ya kuvunja Muungano hatuna nia hiyo na hakuna hata mtu mmoja Zanzibar anayo nia ya kuvunja Muungano sisi tulijitolea kuungana na ninyi kwanza kihistoria na tunaendelea nao lakini mtutizame hali yetu tukoje? inafika wakati mtu anakwenda zake kulpia mzigo wake Bandarini Zanzibar anaambiwa tulia *lodging, documents* zako zinapelekwa Dar es Salaam zinafika, unalipia, yaani ukifika Dar es Salaam unapigwa tena siku 3, 4, 5 ili mradi *frustration uwe frustrated usiagize* tena mzigo kutoka Zanzibat ulete moja kwa moja. Sisi tutakula nini? Ndugu zangu mimi nafikiri hili suala tukae tulitafakari sana kwa sababu bila ya kuona umuhimu wa suala hili na tunazungumza kila siku, kwa nini tuzungumze kila siku? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka huu ni mchango wangu wa mara ya nne suala nalizungumza hili hili, inatosha. Sasa unakuja huu mchakato wa hii Tume ya Pamoja ya Fedha, hili swalii kila siku ya Mungu utasikia mchakato, unaendelea, mchakato unaendelea, kinachakatwa nini? (*Makofi*)

Mimi nafikiri jina la mchakato tunalitumia vibaya kwa sababu kuchakata vitu ni kukikatakata kitu kilichokua kizima unakichakata mwisho wake kiishie, hakuna kitu mwisho wake mtuambie hakuna kitu mlishakichakata, mchakato ukiisha hakuna kitu hapo. Mchakato, mchakato, mchakato mpaka lini? Tuzungumze kitu kiishe. Mwaka jana hapa nilisema sio wakati tena wa kuwa maneno tu, kila siku maneno hebu tupumzikeni, tufanyeni vitendo, nikatoa mfano kwamba sasa hivi kuna mabadiliko hata hii *music* yetu sasa, zamani *music* taarabu mtu anakaa kitini anaagalia vinanda sasa hakuna vinanda kuna kucheza haswa, tuchezeni vinanda hakuna tena, hii mchakato tuachane nao tumalizeni jambo tuishe. Ndugu zangu Zanzibar hatuna *mortaha*, watu wa Zanzibar hawana *mortaha* na kesho kutwa ramadhanii inakuja sijui watu watakuwa wageni wa nani.

Mheshimiwa Spika, watu hawana pesa mfukoni na bila ya *transaction* ya biashara harakati za kibiashara nenda rudi, nenda rudi ndiyo watu wanavyo *survive* kule mimi nawaaambieni kila siku kule hakuna ardhi ya kulima nyanya, hakuna ardhi ya kulima mchele na halafu cha ajabu nawashanga kwa sababu Wanzazibari wote wanategemea bidhaa kutoka huku, zile fedha zikipatikana kule anafaidika mkulima wa huku, hazibaki kule sisi kule *profession* yetu ni biashara ndugu zangu, kwa sababu hatuna mahali pa kulima, mtu akishapita amepata matuta yake matano ya viazi vitamu anajisifu mimi nina matuta matano nitakula futari huo ni ukulima kweli?

Mheshimiwa Spika, Wanzazibari sio wavivu bwana na nyie mnajua kazi yetu, mnajua kabisa na nyie mnajua kwamba huku kwa biashara ndiyo tunaongoza kibiashara, Dar es Salaam pale popote, hiyo ni *profession* yetu kila mmoja ana kazi yake na hayo matuta 5, 6 kule wapo ndugu zetu wa Kinyamwezi, Kisukuma ndiyo wanatulimia, lakini sisi fani yetu ni biashara tuna mgawanyo wa kazi, sio uvivu, ninyi fanyeni hivi, sisi tunafanya hivi. Ndio mgawanyo wa kazi kwa hiyo, mimi nawaomba ndugu zangu, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala la *TRA*, *TRA* ni tatizo kubwa sana. *TRA* Zanzibar, maana yake tumefika afadhali sisi tukaona kwamba ile ofisi kule haina kazi ni bora kuacha ikafungwa waache bidhaa ziingie Zanzibar, zikitoka Zanzibar zikija huku zichajiwe ushuru unaohitajika 100%. Kuna sababu gani kule zilipiwe halafu huku nako zilipiwe, maana yake nini? Hamna maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikachangia, nataka niendeleze pale pale pa ndugu yangu, ndugu Chomboh. Kuna Tume ya Pamoja ya Fedha, Tume hii ilikabidhi ripoti katika vitabu vyetu

tunaambiwa mwaka 2006 ripoti ya mchanganuo wa mapato na matumizi ya shughuli za Muungano zote mbili ilikabidiwa, tukasema sasa *Alhamdullillah* sasa cha kushangaza kimya kirefu kilivyopita leo tena tunaambiwa hivi kwamba kile kitabu kinarudishwa tena kwenye mchanganuo wa mwaka 2008/2009 eti ule mchanganuo unarudishwa tena ukapembuliwe tena ndiyo huo huo mchakato anaouzungumza ndugu Chomboh, halafu ndo irudishwe. (*Makofi*)

Sasa swalilangu linakuja pamoja je, Serikali hizo mbili zilirudisha huo mchanganuo huko kwa Tume ili zirudie tena kuchanganua au zirudie tena kulikuwa na makosa, mimi kwa hili ningeomba tu leo ndugu zangu hawa wa hii Wizara ya muhimu ya kulinda fedha yetu waniambie huu mchanganuo ulikuaje tena ukarudi nyuma mwaka 2006 tuliambiwa uko tayari? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa ukurasa wa 74 wa hotuba ya Waziri kwenye Fungu la Hazina kwa kweli ni kitu ambacho kimenishangaza sana. Kwanza nitaendelea kusema yale yale kila siku ninayozungumza kwamba hapa kinachoonekana kwamba mapato yanayokusanywa kwenye migongo ya ndugu zetu tunasema tunalipa ushuru, tunafanya hiki kukusanya mapato ili tuendele, mapato yale yanachoonekana ni kuwiweka Wizara zibaki pale, kwa sababu kinachoonekana ni nini? Ni mishahara, ni chai, ni magari, ni kile, ni hiki. Lakini kwenye pesa za maendeleo ukiangalia kila ukiangalia kipengele Wizara zote ukiangalia percent kubwa ya pesa za maendeleo tunasubiri kutoka kwa ndugu zetu tusaidiwe au tupate mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi tutaendelea hivyo mpaka lini? Na hii yote inakuja hapa ni mfano mzuri tu kuna mamilioni ya fedha ambayo ni bilioni 365 ni kwa ajili ya matumizi maalumu ikiwa ni pamoja na dharura. Sasa hizi pesa za dharura ndugu zangu wa Wizara za Fedha kama dharura haijatokea huwa zinakwenda wapi mwisho wa siku? Kwa sababu mimi sidhani kwamba miaka yote kunakuwa na dharura, kuna wakati amba dharura haipo, kama ilitokea dharura sidhani kama pesa yote iliyopangwa inatumika, kwa hiyo lazima kuna kitu ambacho kinarudi na hicho ndio huwa nasema na ninaunga mkono na wenzangu wote waliotangulia kusema kwamba muda wa kuchanganua na muda kupitia Bajeti yetu hata kama iweje ni ndogo, kama tulipanga hizi pesa mwaka 2008/2009 irudi tena kwetu tuambiwe kwamba zile tulizopanga 2008/2009 zimetumika kadha, zimebaki kadha au hazikutosha tumekopa mahala kadha. Hakuna hicho kitu, kila siku kilio changu ni hicho hicho tunaletewa majitabu yameshachapwa kwa hiyo sisi ni *rubber stamp* tu tunapitisha tu ndiyo, ndiyo, ndiyo mpaka mwisho wa siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hizi pesa za kawaida hizi za dharura mimi naomba hapa tu shemeji hapa, tutashikana na vifungu ila mshahara wa Waziri siutaki kwa sababu mdogo atapata shida lakini hizi pesa za dharura hizi nizijue hizi dharura za mwaka jana dharura imebaki imekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Julai, 2009 niliuliza swalilangu mimi hapa Bungeni kuhusu mikopo ambayo Serikali imeniambia *BOT* iwe inaweka dhamana mashirika ya watu binafsi na mengineyo na wawe wanapata hiyo mikopo, na mimi ushawishi wangu mkubwa ulikuja kwamba nataka kujua haya masharti ambayo wanapewa hawa, kabla hawajapewa hii mikopo ni masharti gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niliambiwa wao wenyewe mabenki yanakopesha. Lakini tatizo haliko kwa mkopaji, tatizo liko kwako wewe unaeweka dhamana kwa sababu mkopaji akishindwa kulipa wewe ndiyo utalipa wewe ndiyo dhamana. Lakini tuelewe kwamba tunaposema kwamba Serikali ndiyo italipa mzigo huo unarudi kwa yule yule mwananchi

anaelia kila siku, mzigo ule unarudi kwake. Kile kile kidogo ambacho ndo hicho kinaangalia Wizara na pia hakitoshi kinarudi tena hicho hicho kidogo tena kichukuliwe ilipwe ile mikopo. Haya masharti ni masharti gani? Tuelezwe hapa hata kama ni hizo benki ndio zinaweka masharti lakini ninyi ndiyo dhamana, huwezi mimi nikaja kwako nikakuambia nataka nikope halafu eti wewe unaniwekea dhamani wewe hujui mimi nimepewa masharti gani wewe unaweka dhamana. Mimi sidhani kama hicho ni kitu ambacho kina mantiki hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tuna uwezo wa kukopa kumbe tuna uwezo wa kukopa tunaambiya kwamba hapa pesa zilikopwa ambazo zilizokopeshwa mwaka jana ni shilingi bilioni 290,682,000,000 na miradi midogo bilioni 3,054,000,000 hii si pesa kidogo, kumbe kama tunaweza kuchukua dhamana tukawakopesha wengine wakashindwa kulipa mwananchi akalipa, kwa nini tusiweke hii dhamana tukakopa tukaokoa *TRA* yetu? Kwa nini tumuachie muhindi anaboronga? Kumbe sisi tuna watu ambao wapo wanasema tununue hisa kila siku, wapo hapa Watanzania wanenanua hisa ili tuweze kujiendeleza basi tuwachukulie dhamana hawa hii *TRA* irudi mikononi kwetu tuichukulie dhamana iendelee muda si mkubwa deni tutalipana Serikali itafaidika na barabara zetu zitanusurika kwa malori mazito yanayopita kwenye hizo barabra ambayo ni gharama nyininge mpya, kama tunaweza kukopa basi tukope tuinue Bandari zetu hizi, ambapo tukiinua Bandari tutapata pia faida. Nchi jirani watarudi kwetu tena kama kawaida tutaweza kujiendeleza, deni litarudi kwa haraka na Mtanzania atafaidi na pato litaongezeka la Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini leo kweli tunaenda kuwakopea wengine wafaidike washindwe kulipa tuletewe madeni hapa tuambiwe huyu alishindwa kulipa kwa hiyo tufute deni, huyu alishidwa kulipa tufute deni kama tupo hai tunabaki hapa kweli mimi nitakuwa mmoja kufanya kampeni tusikubali kufuta hilo deni au hapa tuambiwe hapa masharti gani ambayo wanapanewa ya kuweka haya madeni ili yalipwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa john Magufuli alifanya kazi tukakamata meli hapa, mimi kuna wakati nilichangia hapa nikasema bado kuna mapato mengine Mwenyezi Mungu alivyotupenda Watanzania tuna njia nydingi sana za kupata pesa bado hatujatumia rasilimali hizo na mfano Mwenyezi Mungu katuletea wazi hivi ikakamatwa meli ina rasilimali ya masamaki yaliojaa ndani ya meli hiyo ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mungu alitaka kuja katuonesha Watanzania mmelala, wenzenu wanachota huko, sisi tumelala sasa hayo madeni, tukope basi na sisi hizo meli na sisi si Mungu katuletea hapa machoni tumeona kwamba inawezekana kumbe Bahari ikatuletea mapesa, tulishangilia kweli ooh, tumekamata meli, masamaki tele, lelelee, sasa hiyo meli tuliiakamata, ngapi ziliondoka? Tumekamata mwaka huu, mwaka juzi, mwaka juzi na mwaka juzi ngapi ziliondoka? Sisi tumekaa tu, tukope basi na sisi hizo meli watoto wetu watapata ajira, masamaki hayo na sisi tutayachukua halafu na samaki tukiiza tutapata mapesa na deni litalipwa kwa haraka hakuna, vitu vingi sana vinafanyika humu na juzi hapa Mheshimiwa Richard Ndassa alisema, hizi pesa ambazo tunawakopesha hawa wanazifanyia vituko vya ajabu, wanakwenda kukarabati nyumba kwa shilingi milioni chungu nzima halafu wanauziana kwa milioni chache tu; mambo ya ajabu yanafanyika kwenye nchi hii lakini sie tumelemaa. (*Makofi*)

Ndugu zangu mimi nakuombeni Mungu mtaona maana yake kama niliambiwa siwezi kupata nafasi niliandika nakuombeni Mungu akupeni njia ya kuweza kuwaokoa Watanzania walio maskini lakini hatujafanya kazi bado, bado hatujafanya kazi, tupo tu tunajisifu

tumepandisha uchumi kwa rasilimali, tumepandisha uchumi kwa *percent*, hakuna uchumi unaopanda hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu kuna kampeni ilifanyika nzuri tu hicho nakishukuru sana. Watanzania walio wengi sasa hivi wanapeleka pesa zao benki, Watanzania walio wengi sasa hivi mishahara inapitia benki, lakini kuna kilio kikubwa cha Watanzania hawa. Mshahara wa Mtanzania walio wengi ni shilingi 80,000 *net salary*, inapitia benki; yeze kutoka nyumbani kwake mpaka afate ule mshahara anatumia angalau 500 nauli, akifika pale kachukua zile pesa anakatwa *charges* shilingi 400 akisema aharakaishe achukue tena shilingi 1,300 inaondoka, lakini ukiangalia hizo benki faida wanayopata ni kubwa sana lakini Mtanzania huyo faida haijui iko wapi na ni pesa hizo hizo. Ukiti unakwenda kukopa kila siku tunazungumza hapa ndani *percent 18* unakatwa kwa mkopo unaokopa katika mabenki yetu, *percent 18* hizo sio kwamba ni mapesa yale waliyokuja nao wazungu, ni mapesa yetu ambayo tunaweka pale katika akaunti zetu pia ndizo hizo hizo tunazokopeshana. Basi kama ndiyo hizo tunazokopeshana faida na sisi tuione na ndiyo kilio hicho Watanzania wanalia, wanasema aah, wanatwambia tu uchumi umepanda, lakini mifuko mitupu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilikuwa naangalia TV, wanasema mifuko mitupu haina kitu, sasa hiyo *percent* inayopanda iko wapi? Mtanzania anataka kuona akiweka mkono mfukoni, akitoa hivi anatoa shilingi, ndiyo anasema aah, uchumi umepanda na ndiyo maana tukamuita bwana ruksa, leo hivi bwana ruksa akirudi na kusema nataka kurudi, tutampa kwa sababu tulikuwa tukitia mkono mfukoni tunatoka na chochote, leo unaniambia uchumi umepanda nikitia mkono mfukoni kula moja inanishinda, uniambie uchumi umepanda! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa basi kwenye hesabu hizo mnazoweka kwenye benki wakati tunakopeshana faida nione, iingie kwenye mfuko wangu na nione hii ndiyo faida. Lakini leo aah, yale yale ya simu tunapeana shilingi milioni tano, hundi kwenye magazeti, kwenye ma-TV tumetoa msaada milioni tano tunashangilia eeh wanatusaidia! Wao shilingi milioni tano wamekupa wewe, wao wana milioni ngapi ndani?

Mheshimiwa Spika, tukae kitako jamani, tukae na hao tulio wapa ruhusa ya kufungua mabenki kwenye nchi yetu na sisi faida tuione, hapo ndiyo tutasema kweli kuna faida nzuri inayoingia katuika nchi na tunafaidika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hiki hiki kitabu. Nakirudia hiki hiki kitabu, hayo hayo madeni mimi hiki kitabu sijakipenda leo, kizuri kimepambwa na mabendera lakini mimi kimenipa taabu sana ikiwa hiyo Hazina, Idara moja tu kwenye Wizara inapata karibu shilingi bilioni 597 hata hivyo Kilimo Kwanza Bajeti yake haijafikia huku! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumza na tutaendelea kuzungumza kwa sababu Mwenyezi Mungu akituweka hai watakaojaliwa kurudi katika Bunge hili watarudi, watakaojaliwa wasirudi ndiyo majaliwa hayo, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mohammed Chomboh tumeshazungumza sana, tumeongea sana nafasi hazitatosha humu ndani, nafasi zinaendelea kutosha lakini kama hatujageuza mwelekeo wa njia, tusielekee njia ile tuliyokuwa tunaelekeea haifai, tugeuze sasa njia twende kwingine. Mheshimiwa Chomboh anasema taarabu zamani ilikuwa watu hukaa kwenye vitu waka-swing namna hii, siku hizi kuna kurusha roho si taarabu tena, watu wanacheza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tubadilishe leo tunafunga Bajeti Mwenyezi Mungu atuweke hai mwakani tuwepo lakini tubadilishe matumizi yapungue ili na maendeleo tuisubiri Wazungu,

maana yake ulimwengu unabadilika Wazungu wanahamia Afrika sasa. Sasa kama Waafrika tuataendelea kuwategemea Wazungu na wao wanasesma wanakuja huku, tutaanza kuuza shanga kama bibi zetu walivyoanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi lakini nikiri kabisa kwamba, nilikuwa nimekata tamaa kwamba inawezekana nisipate nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nitachangia katika maeneo machache kama ifuatavyo, lakini pia niseme bahati nzuri baada ya kuona kwamba, nisingepata nafasi nilipeleka mchango wangu wa maandishi kwa Waziri na nina hakika haya mengine inawezekana sikuyapeleka kwenye mchango wangu wa maandishi, nitapata nafasi ya kuyazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, wataalam wote wa Wizara ya Fedha na wale wote ambao walihusika katika kuandaa hotuba hii ambayo tunajadili leo hapa Bungeni. (*Makofi*)

Baada ya hayo ninaomba niseme jambo moja ambalo mimi llinigusa sana juu ya maagizo ambayo yanatolewa na wakuu wa nchi. Mwaka 2007 wakuu wa nchi zinazounda Umoja wa Afrika (*AU*) walikutana pale Addis Ababa na kutoa azimio au *declaration* kwamba pesa zitengwe ziende kwenye shughuli za utafiti na waliazimia kwamba kila Serikali itenge asilimia moja (1%) ya pato lake la Taifa kwenda kwenye utafiti ili tuweke juhudii zaidi kwenye masuala ya utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunavyojua shughuli za utafiti zikipewa kipaumbele zinaweza zikasaidia sana nchi kupiga hatua katika shughuli ya maendeleo kwa ujumla. Tamko hili liliwekwa mwaka 2007 kama nilivyosema, lakini mwaka jana 2008/2009 hakuna pesa iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010 hapa ndipo kuna matatizo kidogo na ningependa Mheshimiwa Waziri atoe maelezo na pia nataka niseme kwamba mimi niko kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu ambayo moja ya Wizara tunayoishughulikia ni Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Tulimhoji Mheshimiwa Waziri kwamba hizi fedha asilimia moja (1%) ambazo Mheshimiwa Rais aliagiza ziko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Profesa Msolla alisema pesa hizi hazipo hazikutengwa. Lakini siku moja kabla hatujakaa kule Dar es Salaam kwenye Vikao vya Kamati kwenye vyombo vya Habari Waziri alikaririwa akisema kwamba zimetengwa shilingi bilioni 70 ambazo zitaenda kwenye shughuli za utafiti. Hilo jambo lilitupa faraja ingawa pia Mheshimiwa Waziri alisema kwamba hizi pesa zitawekwa kwenye chombo kinachoitwa Baraza la Uwekezaji la Taifa au *National Economic Empowerment Council* na Waziri alikaririwa akisema kwamba chombo hiki ndicho kilichoteuliwa sasa kuratibu shughuli za utafiti nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili lilitupa taabu kidogo tukamwomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie na Waziri mwenzake wazungumze watueleze nini hasa kinachoendelea. Kwa sababu hatuwezi kuwa na vyombo viwili ambavyo vinaratibu shughuli za utafiti katika nchi. Tayari tuna Tume ya Sayansi au *COSTECH* ambayo ndiyo iliyopewa jukumu la kuratibu shughuli za uratibu katika nchi hii kuitia Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 na Ibara ya 5 ndiyo

hiyo inayoainisha maeneo yote ambayo yanapaswa kufanya shughuli za uratibu wa shughuli za utafiti katika nchi. Lakini hata baada ya kumwambia Waziri aende kwa Waziri mwenzake bado mpaka leo hatujaambiwa linalooleweka. Lakini wiki iliyopita itakumbukwa kwamba niliuliza swali hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri akasema kwamba zipo shilingi bilioni 70 tayari kwenye Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimepitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri cha Bajeti kwa makini sana na nimesoma sehemu ya Baraza hili alipoandika kwenye kitabu hiki, sijaona Mheshimiwa Waziri akizungumzia hata kitu kimoja kuhusu hiyo asilimia moja ambayo yeye ameiita asilimia moja ya Bajeti ingawa pia ukiweka asilimia moja zinakuja bilioni zaidi ya 311 na ingawa yeye alisema zimetengwa shilingi bilioni 70. (*Makofii*)

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri atusaidie ili vyombo vyta utafiti au taasisi zinazohusika na utafiti zijue kwamba pesa zipo. Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake na kwa sababu hili suala nilileta mapema basi atueleze kwamba hizi pesa shilingi bilioni 70 ziko wapi. Lakini zaidi ni kweli alitamka maneno haya kwamba chombo hiki cha *National Economic Empowerment Council*, ndicho kilichopewa jukumu la kuratibu shughuli za utafiti, na kama hivyo madaraka hayo yametoka wapi na ile Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 ambayo ndiyo iliyopewa jukumu la utafiti kazi yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba nizungumzie suala la malipo ya pensheni kwa wastaifu. Kwanza niishukuru Serikali kwamba walau imeongeza pesa kwa ajili ya wastaifu wetu, siyo jambo dogo. Si haba kutoka shilingi karibu 21,000 kwenda zaidi ya shilingi zaidi 50,000, tunaipongeza sana Serikali. Tunaipongeza sana Serikali pamoja na kwamba wenzetu na wao wanaweza wakaona kwamba hii ni hatua ndogo, mimi naiona ni hatua kubwa ambayo katika hili lazima tuipongeze Serikali kwamba tumetoka hatua moja tumekwenda hatua nyingine. La msingi hapa nakuomba Mheshimiwa Spika, kila mwaka Serikali iwe na tabia ya kuwakumbuka wastaifu kwa sababu maisha yanabadilika, hali ya uchumi inakua, basi tuwakumbuke wastaifu wetu kila mwaka. (*Makofii*)

Lakini pamoja na kuongeza tuondoe ile kero ya hawa watumishi kuchelewa kupata malipo yao. Kwa sababu kuongeza ni jambo lingine, lakini kuwalipa kwa wakati ni jambo lingine. Tunaiomba Serikali isiwashumbue wastaifu, walipwe mafao yao kwa mujibu wa taratibu zilizopo ili waone kwamba Serikali yao inawajali hasa baada ya kutumika vizuri katika kipindi chao cha utumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Bima zilizoiva kwa wale ambao walikuwa wanachama. Tumekuwa na tatizo kubwa sana katika nchi kuhusu Bima zilizoiva. Kuna wanachama wengi ambao Bima zao zimeiva kuanzia mwaka 2005 mpaka leo. Lakini hawajalipwa haki zao. Mimi kuna watu wamekuja kwangu ni bahati nzuri wengine baada ya mimi kufuatilia Bima wamelipwa kwa sababu nimefuatilia. Lakini wengine ambao pengine wamekosa msaada, wanazungushwa siku hadi siku. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ratiba ya namna gani wadai wa bima watalipwa mafao yao. Najua bima inaenda leo mabadiliko makubwa, lakini wakati mnafanya mabadiliko tafuteni pesa hawa watu walipwe kwa sababu waliweka hela zao, kulikuwa na mikataba ambayo imevunjwa na mimi sidhani kama itakuwa busara kwa watu ambao wanaidai Serikali waanze kwenda Mahakamani wakati walikuwa wanafikiria kwamba ikifika kipindi fulani wangeweza kurejeshewa fedha zao, na kwa kufanya hivi kwa kweli tumeviruga mipango ya watu kwa sehemu kubwa sana. Nafikiri pia Mheshimiwa Waziri atawaambia wale ambao walipeleka hela zao katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala ambalo nadhani wenzangu wamelizungumza. Mwaka jana nilizungumza riba kubwa kwa Taasisi binafsi au *NGO's* ambazo zinakopesha. Nilitoa mfano wa *Bayport Financial Services* nikatoa mfano wa Taasisi ingawa nilisemea *Bayport Financial Services* kwa sehemu kubwa. Lakini zipo taasisi nyingine, kuna *Bruva National Services*, kuna *Pride*, kuna *Finca* na nyingine nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taasisi hizi, mimi nilitumia maneno haya, kwa kweli zinawanyonya wananchi kwa sehemu kubwa, kwa sababu huwezi kuwa na taasisi ambayo riba yake ni kati ya asilimia 50 mpaka asilimia 200 kwa wakati mwengine. Hatuwezi kwenda hivi Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilihoji pia Serikali kwenye Bunge lako nikasema hivi Serikali inachukua hatua gani. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Fedha alijibu akasema siyo jukumu la Benki Kuu kuweka riba kwa ajili ya hizi taasisi na mimi nikashangaa. Ninavyoolewa kwa elimu yangu ndogo ya biashara kwamba Benki Kuu ndiyo inayo-regulate taasisi nyingine zote za fedha katika nchi. Sasa iweje hawa watu muwaacie hivi wafanye biashara wanavyotaka wao wenyewe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyovypote vile hili haliwezi kuvumilika na taasisi hizi bahati sana zinakwenda na lugha ya ulaghai kwa wananchi na hasa *Bayport Financial Services* imekwenda kwa lugha tamu sana kwa wananchi. Hawakuwapa wananchi wasome masharti yao vizuri, wananchi hasa walimu, na watu ambao wapo kwenye sekta wamejitumbukiza mle, walipokuja kwenye makato mtu umekopa shilingi milioni mbili unatakiwa ulipe shilingi milioni nne kama sio unyonyaji huu ni nini Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, tunarudia kuiomba Serikali, walisema kwamba Benki Kuu itafuatilia, hebu Mheshimiwa Waziri atupe taarifa Benki Kuu imefuatilia na kubaini nini na Benki Kuu inachukua hatua gani sasa ili tuisinufaishe taasisi kwa migongo ya watumishi wetu kwa migongo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo la mwisho. Jambo la mwisho ni suala la riba ambayo mabenki yanatosha kwa amana. Kwanza, Benki nazo nyingi za Biashara naweza nikasema haziwasaidii sana wananchi wa kawaida wa Tanzania, haziwasaidii sana. Unapokopa riba yake ni kubwa kati ya asilimia 10 mpaka 20 ndiyo riba ya mabenki hapa nchini. Kati ya asilimia 10 mpaka 20 nadhani mengine yanaweka asilimia mpaka 25. Lakini wewe ukiweka pesa zako benki pesa unayopewa faida unayopata sidhani kama inazidi asilimia 3 sina hakika. Sasa huu ni unyonyaji, kwa nini unaponikopesha unichaji riba kubwa lakini nikiweka hela yangu benki unanipa faida ndogo sana? Hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameandika kwenye kitabu chake nimesoma anaeleza mambo mazuri, tunaomba utaratibu wa benki katika ku-regulate haya mambo ifanywe kwa haraka ili wananchi wasiumie. Hakuna maana ya kuwa na Benki nyingi katika nchi ambayo wananchi hawawezi kufaidika nayo. Hakuna maana hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yake tukiwa na mabenki mengi wanaoweza kukopa ni wananchi wa kawaida. Lakini wananchi wangu wa kule Mbozi, wa kule Nabinzo, Nyimbili, Igamba, Itaka hawawezi kupata mikopo hii. Tutakuwa hatuwasaidii Watanzania. Mkopo wa Serikali wa JKT na mikopo mingine yoyote bado ni kidogo sana ambayo haiwatoshelezi Watanzania ndiyo sababu Wabunge hapa ndani tunasimama tunasema mikopo, mikopo. Mikopo hii ni kiasi kidogo sana. Ni kuitia kwenye mabenki tu, wananchi wengi wangeweza

kupata pesa nyingi na kwa maana hiyo wakaingiza kwenye shughuli zao za kiuchumi na kwa kweli tungeweza kuondokana na umaskini kwa sehemu kubwa sana. Lakini kwa *trend* ya sasa wananchi wetu wataendelea kubaki maskini kwa sababu taasisi zenyewe za fedha *NGO's* ndizo zinanyonya wananchi, na wananchi wengi sasa hawataona maana ya kuingia huku. Mabenki tuliyonayo hayana faida kubwa kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tufike mahali kwamba Benki Kuu ifanye kazi yake yaku-*regulate* hizi taasisi za fedha pamoja na mabenki ili wananchi waone faida ya kuwa na taasisi katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, nikisha kusema hivyo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba Mheshimiwa Spika, ukiona inafaa yale ambayo yanawahu sana wananchi basi yatolewe ufanuzi atakapokuwa anajibu hoja zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey Zambi. Sasa mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara yetu hii ya mwisho ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Fedha na Uchumi ndiyo uchumi, ni roho ya nchi yetu. Mategemeo makubwa sana kwa Wizara zote ni kutokana na Wizara hii. Sasa kama Wizara hii ndiyo tegemeo kubwa la Watanzania katika nchi yetu, naomba nitoe ushauri ufuatao kabla siaendelea kwenye jambo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii sasa ione umuhimu wa kuhakikisha kwamba pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, *cash budget* naungana naye kabisa, tukizingatia tukiitumia vizuri *cash budget* hata maendeleo yetu yataenda kwa kasi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unapopokea hii, unapokusanya pesa zako za ndani kwa kutumia pesa za ndani kwa kutumia *cash budget* basi naomba uzingatie kuhakikisha kwamba unaangalia Wizara nyeti ambazo zinaenda moja kwa moja katika kukuwekea mazingira mazuri wewe kukusanya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushauri Mheshimiwa Waziri basi Wizara zifuatazo uone kipaumbele zaidi kuhakikisha kwamba unapopata ile *cash budget* kuzipelekea fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Miundombuni na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na nyinginezo zitafuatia, kama Mheshimiwa Waziri atazingatia hili kwa kuhakikisha kwamba atakapopata hiyo *cash budget* akatumia miezi mitatu, mitatu kupeleka kwenye Wizara hizo tutasonga mbele kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri wangu huo wa mwanzoni, naomba nichukue nafasi hii sasa kuzungumzia suala la mamlaka yetu ya mapato. Kila mwaka nimekuwa nikutumia muda wangu mrefu sana kuwapongeza *TRA* kwa kazi nzuri wanazofanya na bado wanaendelea na Tanzania tunawategemea sana Mamlaka hii kukusanya mapato ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mamlaka haya sasa yameanza kuingiwa na mdudu fulani ambaye labda ni ajira labda ya vijana ambao wanakuja na uchu wa utajiri wa haraka haraka sasa wanataka kuichafua mamlaka hii. Nimwombe sana ndugu yangu Kitilya, ajira zako za vijana wanaokuja na tabia hii hebu jaribu kuangalia maana yake sasa sifa ya mamlaka inaanza kupungua baada ya kuona kwamba kuna ukwepeshaji kwa kuchukua kodi kwa walipaji kwa kuwatumia wataalam wako. Hivyo nikuombe Mheshimiwa Kitilya angalia maeneo nyeti ambayo ndiyo yanatuingizia fedha katika nchi yetu kwa walipa kodi, labda ujaribu kuweka Watendaji ambao wako karibu kustaafulu, hawawezi kufanya vitu kama hivyo watakuwa wanalinda mafao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kulipongeza sana Shirika la *PPF*. *PPF* wamewekeza pale Mkoani kwetu Mwanza. Naomba nichukue nafasi hii kwamba maamuzi yao yalikuwa mazuri, mji wa Mwanza sasa umechangamka vizuri baada ya kuwekeza pale Mkoani Mwanza. Niombe sasa ndugu zangu wa *PPF* bado tuwaombe kwenye mikoa mingine. Lakini hata Mwanza bado kama mtahitaji maeneo mengine mnawenza mkapatiwa. Nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie suala la Chuo cha Uhasibu (*IFM*). Kumekuwa na matatizo, pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba wameandaa maeneo ya ekari 500 ili waweze kupanua Chuo chao. Lakini nimejaribu kuongea na Mheshimiwa Waziri mpaka nimemwandikia barua, hebu tuone umuhimu zaidi. Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*) ndiyo kinaandaa wataalam wa kuhakikisha kwamba hesabu zetu za nchi yetu zinakaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha na Benki Kuu ni ofisi ambayo iko chini ya Wizara yako, ingawa inajitegemea kwa mambo mengine, lakini Benki Kuu nayo ingetusaidia kama Chuo cha Usimamizi wa Fedha, kuna jengo ambalo liko kwenye *plot No. 28/11* ni jengo ambalo hawalitumii. Ni kwa nini sasa Benki Kuu wanashindwa kuwasaidia Chuo cha Usimamizi wa Fedha wakawasaidia lile jengo liwasaidie kuweka angalau hosteli kwa ajili ya wanafunzi ili tuweze kupata watalaam wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu na Serikali ni moja, kama ni majengo ya Serikali na lile jengo hawalitumii, sasa kuna tatizo gani, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho anisaidie ni kikwazo gani Benki Kuu wenzetu na wale ni jirani zao na kama ofisi wanazo wamejenga jengo zuri tu la kwao. Tunaomba hilo gorofa jamani ndugu zangu mliachie watu wa Benki Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na Chuo cha Mipango pale, upanuzi wa Chuo cha Mipango kwa kweli naipongeza Serikali na eneo lile sasa hivi linaonyesha kama kweli tunatoa mabwana mipango pale. Lakini bado ninamwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kutenga fedha kwa ajili ya Chuo hiki ili kiendelee kujipanua zaidi ili tuweze kupata Maafisa Mipango wanaotoka katika Chuo chetu hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi kwa kweli kwa sababu umenishtukiza, lakini naomba nisisitize mambo yafuatayo, naomba sasa kwa sababu mafao ya wastaafulu imekuwa ni wimbo kila siku humu ndani, Mheshimiwa Waziri jipange vizuri angalau basi hawa wastaafulu tuwape haki zao. Lakini nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, ahakikishe kwamba ile *Revolving Fund* ya wachimbaji wadogo wadogo. Fedha hizi ujitalidi sana Mheshimiwa Waziri, uzitenge ziende katika Wizara ya

Nishati na Madini ili ziwafikie walengwa hawa wachimbaji wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kuchimba kwa kutumia zana za kisasa.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu kama utaweza Waziri wetu kuutenga utakuwa umewasaidia sana wachimbaji wadogo wadogo, kwa hiyo Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Wizara hii naitakia kila la kheri, lakini naomba Wizara hii baada ya kutoa fedha kwenye Wizara naomba ufuatilaji uendelee wa kuhakikisha kwamba matumizi mazuri ya fedha mnazotoa zinatekelezeka na zinatumika vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii finyu. Namshukuru Mwenyezi Mungu nimeweza kutoa ya kwangu haya niliyokuwanayo. Nawatakieni kila la kheri. Ahsante sana. Naunga mkono asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyawazwa kwa utayari wako. Inaelekea mambo haya ulikuwa unayo ndiyo maana umeweza kusema hata kwa muda huo. (*Makofî*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. OMARI S. KWAANGW'**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Manaibu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayofanya hasa ya kusimamia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi; kwa sasa mkazo ni "Kilimo Kwanza", kauli mbiu hii maana yake ni tukusanye rasilimali zote ili tuwekeza kwenye kilimo kadri itakavyowezekana. Pamoja na misamaha ya kodi kwenye pembejeo na vitendea kazi kama trekta, naona tumeacha jambo muhimu sana, nalo ni kuendelea kutoza VAT kwenye vipuri/spea za trekta kama jembe, sahani na spea zote za trekta. Hili ni kikwazo kikubwa sana kwa Kilimo Kwanza, naomba VAT iondolewe kwenye spea/vipuri.

Mheshimiwa Spika, pili, bado tunatoza kodi kwenye trela la trekta wakati tumesamehe *Motor Vehicle Licence* ya trekta ambayo ilikuwa Sh.150,000/=. Trela ndio chombo cha kusomba mazao, hivyo mwaka huu wakulima wengi hasa Babati walipata tabu sana kusomba mazao yao baada ya kukamatwa kwa trela za trekta zao. Hii imeleta usumbufu kwani hata mazao hasa mahindi yameharibikia mashambani. Wakulima wengi walidhani trela ni sehemu ya trekta kwa *Motor Vehicle Licence* na hivyo imesamehewa. Ni muhimu jambo hili likasamehewa na sidhani fedha zinazotokana na tozo hii ya trela za trekta ni nyingi kiasi cha kuathiri mapato ya Serikali. Pia naomba tusichanganye leseni ya trela na trekta na trela la magari makubwa yenye tela labda ndio utata ulipojitokeza.

Mheshimiwa Spika, ukadiriaji wa fedha za miradi na muda wa miradi, ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Mfano Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara mwaka 2008/2009, ulipewa shilingi bilioni mbili pamoja na kuwa sina hakika na kiasi gani kimetumika kuishia Juni, 2009. Kwa mwaka 2009/10, zimepangwa tena shilingi bilioni mbili. Sasa sina hakika, kama sasa tunasema tumetoa shilingi bilioni nne kwa mradi huu au ni shilingi bilioni mbili wakati kwenye *site* sijaona kama mradi umeanza na wananchi wanaauliza kila wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba Kamishna wa Bajeti mwaka 2010/2011, atenye fedha zaidi kama shilingi bilioni 10 na kuendelea ili mradi huu uwe na muda maalum wa kumalizika kwa sababu kwa utaratibu wa shilingi bilioni mbili kila mwaka itachukua miaka mingi na gharama kubwa hadi mradi huu muhimu kwa maisha ya wananchi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kazi njema.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb) pamoja na Manaibu Waziri wake na watendaji wote, kwa shughuli za kila siku za kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kutoa ajira za moja kwa moja kwa wanafunzi wa Uhasibu wanaomaliza mafunzo ili waweze kuziba matatizo ya uhaba wa watumishi wa fani hizo kwenye Halmashauri zetu kama ilivyo kwa Walimu.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa madeni kwa wazabuni wetu kwa shule za Sekondari, unawenza kuleta athari kubwa sana kwa elimu ya watoto wetu. Ni vema hatua za haraka kumaliza jambo hili zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, hivi ni lini Idara ya Msajili wa Hazina itaanza kujitegemea kama Idara badala ya kuwa chini ya Wizara?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uhasibu Tanzania (*TIA*) hakina mazingira mazuri ya kujifunzia na kusomea hasa kwa Vyuo vya Mtwara, Mbeya na Singida. Tawi la Mtwara ni majengo ya Sabasaba, kwa nini isijenge chuo (tawi) lake lenyewe? Zipo taarifa kuwa chuo kina kiwanja mjini Mtwara, jitihada gani zinafanywa ili kujenga kiwanja hicho na lini?

Mheshimiwa Spika, mji wa Mtwara unakuwa sana hasa kwa kuanzia mwakani ambapo *ST. Augustine University*, inapofungua tawi lake na hivyo kuhitaji sana nyumba. Kwa nini mfuko kama *PSPF*, *GEPF* na *PPF* isishirikiane kuwekeza kwa eneo la ujenzi wa nyumba Mtwara?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Mawaziri, Watendaji wa Wizara na Taasisi zote za Fedha chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya, kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufanuzi na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, malipo ya Wapiganaji Vita Kuu ya Dunia. Malipo yaliyowahi kulipwa kwa Wapiganaji wa Vita Kuu ya Dunia, yalisitishwa kutokana na migogoro ndani ya Chama cha Wapiganaji hao miaka michache iliyopita. Kwa kuwa baadhi ya wapiganaji hao bado wapo hai na wanaendelea kuulizia hatma ya kuendelezwa kwa malipo hayo. Ni vema Mheshimiwa Waziri wa Fedha akatoa ufanuzi juu ya hatma ya malipo hayo na iwapo nchi husika kama Uingereza imesitisha malipo hayo na kama Serikali ya Tanzania, inasema nini juu ya jukumu la malipo ya wapiganaji hao?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupunguza fedha za bajeti za Wizara. Wizara ya Fedha na Uchumi, ndio msimamizi wa makusanyo ya mapato na utoaji wa fedha kwa utekelezaji wa bajeti za Wizara kama zilivyopitishwa na Bunge. Mara kadhaa Wizara zimetakiwa kupunguza bajeti zao kutokana na Wizara ya Fedha kuona dalili za kupungua kwa makusanyo ya mapato kwa mwaka husika. Kwa kuwa bajeti hizo zinakuwa zimepitishwa na

Bunge, Wizara ya Fedha inapaswa kiliarifu Bunge inapobidi kupunguza fedha katika bajeti za Wizara. Tunapenda kupata maelezo juu ya utaratibu sahihi wa utekelezaji na utoaji wa taarifa pale inapobidi kufanyika punguzo la bajeti za Wizara.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni (*Bureau de Change*). Ipo haja kwa Wizara kuimarisha udhibiti wa maduka ya kubadilisha na kutoa fedha za kigeni. Rekodi ya mapokezi na malipo ya fedha haziwekwi sahihi na mara nyingi risiti hazitolewi. Hii inachangiwa pia na wateja hasa wanaokwenda kubadilisha fedha za kigeni kupata shilingi za fedha za Tanzania kutojali kudai risiti kwa kiasi cha fedha wanazotoa. Ipo haja ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi katika maduka hayo.

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya madai ya mafao na madeni ya wafanyakazi wa mashamba ya Mkonge. Iliyokuwa *PSRC*, imeacha majukumu yake kwa chombo maalum ndani ya Wizara ya Fedha. Wizara kuitia chombo hicho, inawajibika kufahamu kwamba bado yapo madai makubwa ya wafanyakazi wa Mashamba ya Mkonge yaliyokuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania na sasa Bodi ya Mkonge Tanzania. Kwa mfano, madai ya wafanyakzi wa Mashamba ya Muheza, Mikumbi na Kitisa, shamba la Mkonge la Kibaranga, shamba la Mkonge la Lewa, Shamba la Mkonge la Kwagungo na Shamba la Mkonge la Bwembwera. Ni vema utataribu wa madai hayo ufanyike ili Wizara ya Fedha na Uchumi iweze kujiandaa kwa kutenga fungu maalum kwa madai yanayojiteza kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, madeni ya *ATCL* na maagizo ya viongozi wakuu, ili kuiwezesha Kampuni ya Ndege *ATCL* kuruka, Wizara ya Fedha na Uchumi imekubali kusaidia ulipaji wa madeni ya mafuta ya ndege ya Kampuni ya *BP (T) Ltd.* ili *ATCL* iweze kupata mafuta bila pingamizi na kuwezesha ndege zake kufanya safari. Bila ya utekelezaji wa ahadi hiyo, Kampuni ya *BP (T) Ltd.* atarejesha hatua ya kusitisha kuipatia *ATCL* mafuta ya ndege au kuitaka kulipia mafuta hayo kwa fedha taslimu na kukatwa kiasi cha fedha hizo kufidia deni na hivyo kupata kiasi kidogo cha mafuta!

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo yanayoagizwa na Mheshimiwa Rais. Mfano, agizo la Posta kulipwa lililotolewa Februari, 2009, halikuwa limelipwa mapema na hivyo kujenga hisia za Wizara ya Fedha na Uchumi kutozingatia maagizo ya viongozi wakuu kama Rais anapoagiza malipo yafanyike mara moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa na harakati za kuanzishwa kwa matawi ya *CRDB* na *NMB* Kisiwani Unguja (Tanzania Visiwani) na mwaka jana kama sikosei, Mheshimiwa Waziri katika kujibu maswali; aliyoulizwa kuhusiana na kuanzishwa kwa matawi ya benki hizo Kisiwani huko, Waziri alisema kuwa *CRDB* tayari ilikuwa imepata ofisi kwa ajili ya uanzishwaji wa huduma zake na akisema kuwa huduma hiyo ingeanza baada ya siku chache hapo mwaka jana (2008).

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kuwa hakuna tawi la *CRDB* na *NMB* lililoanza kutoa huduma kwa upande wa Unguja. Sasa ninalotaka kujua, ni sababu zipi *CRDB* ilishindwa kuanza kutoa huduma huko na ni lini huduma hiyo itatolewa na benki hizo?

Mheshimiwa Spika, inasemekana kuwa *CRDB* ina hisa ilizonunua kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*), hisa hizo ni za asilimia ngapi na je kuna benki nyingine yenye hisa kwenye benki ya *PBZ* ukiachilia *CRDB* na ni ya asilimia gani?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa huduma ya *ATM* hasa kwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*), kwa vile mara nyingi huwa hazifanyi kazi ama kwa kutokuwa na fedha au kuwa mbovu kwa muda. Jambo la kusikitisha zaidi ni pale ofisi inapokuwa wazi wakati *ATM* ikiwa haina fedha, kitu ambacho husababisha msongamano kwenye ofisi pasipo ulazima. Je, fedha kuwekwa kwenye *ATM* ni lazima ziwekwe Afrika ya Kusini ambako inasemekana ndiko mtandao mzima wa huduma za *NBC* ulikounganishwa?

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka huu huko Unguja, hapakuwa na huduma ya ama *ATM* au ndani ya Ofisi ya Tawi la Benki hiyo, ya upatikanaji wa fedha kwa takriban siku tatu na sababu kubwa ilikuwa ni kukosekana kwa mawasiliano ya *internet* kati ya tawi la *NBC Zanzibar* na Makao Makuu (Afrika Kusini).

Mheshimiwa Spika, kama ni kweli mfumo ulipo ni ule wa Afrika ya Kusini, kudhibiti mitandao ya Benki ya NBC nchini, ni vema Serikali ikamtaka mkuu huyo kuweka taratibu mpya ambazo hazitamfanya mdau kumpatisha usumbufu wa kupata fedha zake mwenyewe ambazo ni stahili yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na usumbufu huo, wadau/wateja wengi wameamua kuachana na *NBC* kutokana na huduma zake mbaya. Ni vema Wizara ya Fedha na Uchumi, ikafuatilia jambo hili ili kubaini na kuchukua maamuzi yanayofaa ili sisi wateja tunayoipenda *NBC*, tukaendelea kupata huduma nzuri kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, suala la utafiti ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote. Najua kuna taasisi ndani ya Wizara ambazo hujihusisha na tafiti mbalimbali katika sekta tofauti, hata hivyo, fedha zinazotengwa ni chache sana na hata Serikali imeshindwa kuzibaini ni kiasi gani kwa mwaka huu zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, aliliarifu Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa Kumi na Sita kuwa Serikali ilikuwa imepanga shilingi bilioni 70 kwa ajili ya tafiti kwa taasisi husika, hata hivyo, baada ya Kamati ya Miundombinu kumwagiza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuzichambua kwa kila Wizara yenye kitengo au taasisi inayoshughulikia tafiti ili kubaini ni kiasi gani kilichotengwa kwa vitengo hivyo, hakuweza kubaini fedha hizo isipokuwa zile za *COSTECH* ambazo ni Sh.200,000,000 ambazo zimepangwa kutumika kwa Tume hiyo katika mwaka huu. Aidha, katika kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Waziri mwenye dhaman,a alisema kuwa fedha hizo ni Sh.900,000,000 na siyo zilioandikwa kwenye Kitabu cha IV cha matumizi kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17/2/2009, Serikali iliamua kutenga asilimia moja (1%) ya pato la Taifa sawa na Sh.311 bilioni (kwa mwaka huu) kwa ajili ya Tafiti na Maendeleo (*Research and Development*) ambazo Wizara iliainisha maeneo matano ya kipaumbele ya fedha hizo, (Uk 16 na 17) wa Kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia)

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu wa fedha uliopo, lakini bila kuwa na fedha angalau 0.3% ya pato la Taifa, zingetengwa katika Taasisi zetu za Tafiti, ingekuwa ni jambo la maana sana kwa vile matokeo ya tafiti hizi yangeweza kuendelezwa na mengine kugunduliwa na baadaye nahisi nchi yetu ingekuza uchumi wake kutokana na tafiti hizo.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, jambo hili hajalizungumza kwenye hotuba yake pamoja na ahadi za Wizara hii kuahidi kuwa

fedha za tafiti zingezungumzwa kwenye hotuba ya bajeti yake. Fedha hizo ziko wapi na kama hazipo, nini mkakati wa Serikali wa kutenga asilimia moja (1%) ya pato la Taifa itatekelezwa na kuanza kutumika baada ya Serikali kuamua kinadharia tarehe 17/2/2009?

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wa Wizara hii, kwa kazi zao za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaendelea kukua pamoja na kukabiliana na changamoto za kuyumba kwa hali ya uchumi duaniani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote waliotayarisha hotuba ya bajeti hii ambayo ni nzuri na inakidhi haja.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kazi nzuri mnayoifanya hasa kwa kutuwezesha kuanzisha Benki ya Wanawake. Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ushauri na mapendekezo. Singapore wanategemea Bandari katika uchumi wao wote. Napendekeza tuboreshe utendaji wa Bandari yetu ambayo inategemewa na nchi saba jirani. Uchumi utainuka na ajira nyingi zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, tufanye maboresho ya Shirika la Ndege ATCL, Shirika la Ndege la Taifa litatangaza uthalii na litaleta watalii wengi. Kenya inapata watalii wengi sababu mojawapo ni ndege yao ya *KQ* inayoenda ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Spika, tuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili tulishe majirani zetu Kenya, Kongo, Bundundi na Rwanda amba wana uhaba wa chakula.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima, *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze wewe binafsi, Naibu wako pamoja na Wenyeviti wako wote kwa imani yenu kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii iliyombele yetu, ni Wizara mama katika nchi yetu. Kutokana na umuhimu wa Wizara hii, iko haja tutimize ile kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza". Mtikisiko wa uchumi duniani, ni changamoto kubwa hapa nchini. Ili kuinusuru nchi yetu, ni vema Wizara ijitegemeze katika kusimamia kilimo. Jambo hili ni muhimu ili tujipatie uchumi katika nchi yetu hali tukujua ardhi tunayo kubwa ambayo tumekirimwi na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, elimu ya uchumi tumeletewa mikononi katika nchi yetu tena na wageni. La kusikitisha, Wizara haijataka kutumia elimu hiyo na kusema Watanzania maskini. Huu ni ugonjwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ni karibu miezi sita nyuma, Wizara ya Uvuvi ikiongozwa na Mheshimiwa Magufuli, iliwakamata wavuvi wa kigeni katika bahari yetu wakiwa na meli yao iliyojaa shehena ya samaki. Thamani ya samaki hao ilikuwa kubwa sana. Tumesoma nini katika kitendo hiki? Ni jambo gani kubwa ambalo linaifanya Wizara ya Fedha kushindwa kutafuta vifaa vya uvuvi, tukaweza kuvua samaki ndani ya bahari yetu, amba wataweza kukuza uchumi wa nchi yetu? Hivyo tunaweza kujikomboa kupitia kodi katika migodi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Fedha ya Pamoja. Kuna harufu mbaya ndani ya Serikali ya Muungano kutokana na mgao wa Sh.45 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*), imekabidhi ripoti yake inayohusu mgawanyo na jinsi ya kuchangia gharama za Muungano kwa STM na SMZ kutokea Agosti 2006 hadi hii leo kimya. Je, Wizara inasema nini kuhusiana na ripoti hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya pensheni kwa wastaafu. Naipongeza sana Wizara kwa imani yake juu ya wastaafu wetu kwa kuweza kuwaongeza malipo ya pensheni kutoka Sh.21,000 hadi Sh.50,000/=, hili ni jambo jema na niseme hongereni Mawaziri. Ninaiomba Wizara ifanikishe azma yake njema kwa wastaafu wetu ili kuwapatia haki yao hiyo kwa wakati uliopangwa ili kuwawezesha katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mustafa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Omari Yusufu, Naibu Waziri Mheshimiwa Sumari, kwa pamoja napenda kuwapongeza kwa jitihada zao, kuinusuru nchi katika dimbwi la umaskini. Mungu awape uwezo, Amin.

**MHE. KHADIJA S. ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kunijaalia nikawa mzima wa afya na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, kwa jinsi ulivyonongoza Bunge hili pamoja na Naibu na Wenyejiti wako wote kwa *speed and standard*.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza Waziri, Manaibu wake pamoja na watendaji wake wote, kwa hotuba yao nzuri, Mwenyezi Mungu awasadie ili waweze kuitekeleza, amin.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kwa masikitiko makubwa kwa jinsi Serikali yenye mipango mizuri, lakini tatizo lake kubwa ni kutoa maamuzi, kwa mfano, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) imekabidhi ripoti inayohusu mgawanyo na jinsi ya kuchangia gharama za Muungano kwa STM na SMZ tokea Agosti, 2006, bado kimya kimetawala. Kutokana na hali hii, Serikali inasababisha manung'uniko makubwa ambayo si ya lazima. Naiomba Serikali itoe maamuzi kwa haraka kwa mambo muhimu ili iepushe matatizo.

Mheshimiwa Spika, bado wananchi wa Zanzibar tunapata taabu sana ukisha-lodge document basi urasimu unaanza, inaweza kuchukua siku 28 – 30 na hujui wapi ufuatilie. Vile vile wanaweka bei bila ya kuwa na vigezo kama ukinunua gari \$2000 wao wanaweka \$5000 sijui wanapata wapi bei hizo. Kutokana na matatizo hayo, watu wengi wanashindwa kutoa magari yao bandarini na kusababishia hasara kubwa kwa wananchi. Badala ya kuwaletea maisha bora kwa kila Mtanzania, basi Serikali inaletea maisha magumu kwa kila Mtanzania, ukizingatia gari hizo watu wanazinunua mnadani, naiomba Serikali iliangalie jambo hili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, bado gari kutoka Zanzibar zinaendelea kuwa na usumbufu wa kulipa *difference* kubwa. Kulikoni Serikali moja, nchi moja, gari ikifika upande wa pili ilipiwe tena? Tunaiomba Serikali itoe ufanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi tumeyazungumza kwenye bajeti ya Serikali, nakushurukuru sana.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, huduma ya Benki Jimboni Songwe – Chunya. Kero ya kutokuwa na huduma za kibenki Jimboni Songwe, ni kubwa sana. Tawi moja la karibu la benki ya *NMB*, liko umbali wa zaidi ya km. 270 ambako mtumishi Mwalimu, Afisa Ugani na watendaji, hulazimika kuifluata huduma hiyo. Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, aliahidi kuja Jimboni Songwe, kuangalia jinsi anavyowenza kusaidia kuanzisha huduma ya benki. Naomba/nashauri Mheshimiwa Naibu Waziri atekelze ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mirathi, hii ni kero ambayo haijapata ufumbuzi. Mheshimiwa Omari Mzee, Naibu Waziri, aliahidi tangu mwaka 2006 kuwashughulikia warithi kutoka Jimboni Songwe. Hadi leo hii hawajasaidiwa. Nashauri Mheshimiwa Omari (Mb), Naibu Waziri, atekelze ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, majina ya wastaifu kutoingizwa kwenye Daftari la Malipo ya Pensheni. Mheshimiwa Omari Mzee, Naibu Waziri, anayo majina ya wastaifu ambao majina yao hayajaingizwa kwenye Daftari la Malipo ya Pensheni. Nashauri Mheshimiwa Omari Mzee, Naibu Waziri, atekelze ahadi yake kushughulikia kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya akaunti za wastaifu, fedha yake kuingizwa kwenye akaunti ya watu wengine. Mheshimiwa Omari Mzee, Naibu Waziri, namwomba atekelze ahadi yake kuwashughulikia wahusika.

Mheshimiwa Spika, Walimu Wilaya ya Chunya kutolipwa zaidi fedha za Bima. Hoja hii ilikwishawasilishwa Wizarani. Nashauri Wizara itekelze ahadi yake kushughulikia kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, kero kwenye Vituo vya mizani. Bado ipo kero ya kuwepo misururu ya magari kwenye vituo vya mizani (*weighing bridges*). Ni vema Wizara ikafikiria namna ya kupunguza kero hiyo kwenye mizani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya, kuweza kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri iliyolenga utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara hii, kutokana na utendaji wao mzuri wa kazi kwa kushirikiana na Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji, wataalam wa Wizara, katika kufanikisha majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sera ya “Kilimo Kwanza” katika kuongeza pato la Taifa kutokana na hali ya uchumi nchini. Nashauri Wizara:-

- Iangalie kwa makini mikakati iliyowekwa katika harakati za kuongeza pato la nchi vinginevyo lengo halitaweza kufikiwa;

- Serikali ijpange vizuri na kujitahidi kuondoa utegemezi katika bajeti ya Serikali.

- Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mkopo kwa wakulima zitolewe kwa wakati unaofaa ili ziendane na maandalizi ya Kilimo Kwanza.

- Kuisimamia Hazina kutoa fedha za maendeleo kwa wakati na ziendane na kasma ya bajeti iliyopangwa.

- Kutoa kipaumbele katika Mikoa isiyopata fedha za *SACCOS* kuwezeshwa katika msimu huu wa kilimo ili kuendana na Sera ya Kilimo Kwanza.

- Kuimarisha zaidi kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa sita ilioanishwa kwa kilimo ili kuzalisha kwa wingi na kuongeza pato la Taifa na kuangalia kasoro zetu zilizokuwa zinadhoofisha kilimo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za malipo ya pensheni kwa wastaafu kwani wastaafu wengi wamefarijika baada ya kusikia uamuzi wa Serikali kutoka kiwango cha Sh.21,000 hadi Sh.50,000/=. Naiomba Serikali kulitekeleza hili mara tu ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, suala ya MKUKUTA, mara nyingi limekuwa linasikika redioni au kupitia vyombo vingine vya habari lakini kwa wananchi wengi walio na wa kipato cha chini hawafahamu maana hiyo. Kwa kuwa azma hii kwa Serikali ni kuondoa umaskini wa kipato kwa Mtanzania, mkakati huu katika kipindi hiki uangalie sana mwananchi wa kipato cha chini zaidi na utekelezaji wake uwe na tija zaidi vijijini kwa kuwezeshwa kwa wingi wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza kiwango cha VAT cha asilimia 20% na kuweka kiwango cha 18%. Serikali iangalie uwezekano wa kuzidisha kiwango hiki katika maeneo yanayozalisha zaidi ili kuongeza wingi wa mapato ya Serikali na kupunguza katika maeneo ya biashara za wananchi walio na kipato cha chini au kuondoa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuondoa usumbufu unaojitokeza katika Shirika la Viwango *TBS* na ili kuwawezesha wafanyabiashara walio wengi wanaotoka nchini kuweza kusafirisha bidhaa zao nje na kuongeza tija za wafanyabiashara kwa haraka zaidi nashauri:-

- Kusimamia ukaguzi na kuendeleza Sera ya Uwajibikaji kwa watendaji wasiotimiza wajibu wao.

- Kusimamia wafanyabiashara wanaokiuka mipaka ya Serikali katika vituo vya mafuta, dawa na maeneo mengine ili kupunguza mzigo mkubwa wanaobeba wananchi wa kawaida na kuleta malalamiko yanayojitokeza mara kwa mara.

- Pia kuweka taaluma ya kuwawezesha Watanzania wazalendo kuwa wanawekeza katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri wote wawili, kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa na pia kwa kuandaa hotuba hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwezesha kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake kwa kutoa shilingi bilioni 2.11 ili kutunisha mtaji.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,601 hadi 50,114 kwa mwezi. Wastaafu ni wazee wetu, waliolitumikia Taifa hili kwa muda mrefu, hivyo ni vizuri kuwatambua na kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchumi kuyumba, Serikali ilitoa uamuzi mzuri wa kutoa fedha (*stimulus package*) ili kunusuru walioathirika na mtikisiko wa uchumi. Uamuzi ni mzuri lakini utekelezaji unachukua muda mrefu. Nchi ya America walivyotambua athari za mtikisiko wa uchumi, mara moja walitoa fedha zikaingia kwenye asasi zilizoathirika na sasa tunasikia uchumi kwao umeanza kuonyesha dalili za kutengemaa haraka tofauti na walivyotegemea.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera, wakulima wa kahawa, Vyama vyta Ushirika *KCU* na *KDCU* na wanunuvi wa kahawa binafsi, Kiwanda cha BUKOP wanaokoboa kahawa, wote waliathirika vibaya na mtikisoko wa uchumi. Serikali iliahidi kulipia madeni ya benki yaliyosababishwa na mtikisiko wa uchumi ili wapate kukopeshwa tena na benki, waweze kununua kahawa za wakulima. Msimu wa kahawa umeanza tangu Mei 2009, hadi leo Serikali haijatoa fedha ilizoahidi; hata kuonyesha *serious commitment*, hata mikataba kati ya Benki Kuu na Benki hizi, haijasainiwa. Ununuvi wa kahawa unasuasua, wakulima wanakosa mapato wanahangaika. Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizi?

Mheshimiwa Spika, kuna madeni ya Wazabuni yaliyotoka Wizara ya Elimu ya mwaka 2008 na 2007, yalipelekwa Hazina tangu Mei, 2009. Kwa nini hayajalipwa? Yamefungiwa Hazina na yanayolipwa ni ya mwaka huu 2009. Je, Serikali haioni huu si utaratibu mzuri wa kuficha madeni ya nyuma (2007, 2008) na kulipa ya 2009? Wazabuni wanatishia kusitisha huduma, kwani Serikali imewafilisi, kwani wengi wana mikopo ya mabenki na riba inaendelea kuongezeka, wengi hata nyumba zao zimepigwa minada. Je, ni lini basi Serikali italipa hawa Wazabuni? Kwa kuwa Serikali imevunja mkataba, kwa kuchelewesha malipo baada ya kupata huduma, kwa nini Serikali isilipe madeni na riba?

Mheshimiwa Spika, madeni ya Walimu imekuwa kero kubwa sana; kila siku tunasikia madeni ya Walimu yanaongezeka, lakini Serikali inalipa kidogo kidogo na kelele na mangung'unico ya Walimu yanaendelea. Tatizo kubwa ni kuwa hata Serikali haijui yapo madeni ya Walimu kiasi gani, wakati tunakagua Halmashauri kwenye (*LAAC*), Halmashauri nyingine hawaonyeshi madeni hayo, japokuwa yapo. Walimu ni watu muhimu sana, wanawaandaa Watanzania ki-akili na kimwili, inabidi watendewe haki ili nao wapate moyo wa kufanya kazi zao vizuri. Je, ni lini Serikali italipa deni lote la Walimu? Kwa nini Halmashauri na Wizara ambao wameshindwa kuhakiki na kuorodhesha madeni ya Walimu wasichukuliwe hatua?

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ana wajibu wa kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri zote za Wilaya na Miji, Manispaa, Ofisi za Balozi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma na miradi mbalimbali. Ili fedha zitolewazo na Serikali ziweze kukamilisha kazi/miradi iliyokusudiwa, inabidi ofisi hii, iwezeshwe ili iweze kufanya kazi yao vizuri. Kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na ofisi

hii, Kamati za Bunge *LAAC, POAC, PAC*. Wizara na Halmashauri nyingi zimeanza kufanya kazi zao vizuri na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali imeboreka, inakuwaje sasa fedha iliyotengewa ya matumizi ya kawaida ya shilingi bilioni 17.28 tu ni shilingi bilioni 3.23 zikiwa za mishahara? Zoezi la kufanya *value for money*, ni zoezi kubwa linahitaji wataalam wengi na linachukua muda mrefu. Ili ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake vizuri bajeti hii haitoshi, iongezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii. Hotuba ni nzuri sana na imegusa maeneo yote muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Wizara zenyetaa sasi mbalimbali kuagiza matumizi ya pesa kwa niaba ya Wizara bila maombi hayo kuitia Bungeni kama nyongeza kwenye bajeti zao, umekuwa ukifanywa hivyo kwa baadhi ya Wizara. Je, pesa hizo na matumizi yake huwa zinaonyeshwa kwenye vifungu gani? Lakini pia kufanya hivyo si kujiongezea bajeti bila kuitishwa na Bunge?

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*). Kwanza kama Serikali inategemea kusajili wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, ni vizuri na jina pia lingebadilishwa kwa sababu wanachama kwa hali ya maisha sasa kufikisha miaka 55/60, ni tatizo na hasa kwa wale amba wanakuwa hawana ajira tena. Je, hakuna utaratibu kwa mwanachama ambaye ameachishwa kazi na hajafikisha umri wa miaka 55 na afya yake ikawa siyo nzuri kulipwa mafao yake?

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa magawio kwenye taasisi ambazo Serikali inamilihi hisa chini ya 50%, Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha kuwa hatupotezi mapato hasa kwa wale amba hutoa taarifa ya kuzidisha matumizi na kuonyesha wanapata hasara wakati wanaendelea na biashara?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kada ya Ukaguzi wa Ndani bado kuna tatizo kubwa sana linahitaji marekebisho makubwa. Aidha, Wakaguzi wa Ndani inabidi wapewe elimu ili wajue wajibu wao badala kuwa sehemu ya “menejimenti” hali hii imekuwa ikijitokeza kwenye Mashirika ya Umma na kwenye Wizara pia.

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanywa na Wizara kwa sasa ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima ili nami niweze kutoa mchango wangu kuchangia hotuba hii.

Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mheshimiwa Omari Yusufu Mzee na wataalam wote, kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la Kilimo Kwanza. Naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa uamuzi wake katika kuitambua sekta ya kilimo na kuipatia kipaumbele kuwa kilimo kwanza. Kwa kuwa eneo hili litatengeneza ajira na kuongeza kipato kwa wananchi walio wengi, je, Serikali kupitia Wizara hii, ina mpango gani wa haraka kupeleka fedha katika Benki ya Rasilimali zitakazohudumia Dirisha la Kilimo ambapo wananchi wetu wakulima, waweze kupata mikopo kwa ajili ya kuendesha kilimo chenye tija kwa kuwa na pembejeo mbolea na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, suala la *VICOBA*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Mfuko huu kwa kuwa umeonyesha matokeo mazuri sana? Eneo hili la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na uendelezaji wa mifuko mbalimbali ya kuwawezesha wananchi wenye kipato cha chini, ni muhimu sana kutiliwa mkazo. Aidha, kuhamasisha wananchi kujiunga na *VICOBA* kwa kuwa vikundi vingi vimenufaika na kuonyesha matokeo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, Makampuni yanayochimba madini ya vito hususan kwenye eneo la *Tanzanite One Ltd*. Mererani, kwa kuwa mgodi huo huchimbwa kwa kutumia mashine za kisasa na kwa kuwa uchimbaji wao ni wa kuchimba na kuhamisha udongo wote na hivyo kuacha Bangaloo hadi trekta zinatembea chini kwa chini, baada ya kumaliza muda wao na madini yatakuwa hayapo tena. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi, kuhakikisha kuwa wanavyomaliza muda wao, watakuwa wamedhibiti mashimo hayo na kuyafukia? Je, watapata wapi udongo wa kurudishia ikiwa udongo wote wamehamisha na kusombea barabarani? Je, ikiwa kama Serikali haikufanya makubaliano yoyote ya kufukia mashimo hayo, Serikali itakuwa tayari kufanya kazi hiyo? Je, Kampuni ya *Tanzanite One* imekuwepo hapa nchini ikiendesha shughuli za uchimbaji na kuvuna utajiri wa ajabu, je, kampuni hii inawanufaishaje wananchi wanaoishi jirani na machimbo hayo?

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa utayarishaji na hatimaye uwasilishaji mzuri wa hoja ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu mfumuko wa bei nchini. Naomba kuelewa jinsi Wizara inavyojizatiti kukabiliana na tatizo hili ambalo limekuwa kilio na kero ya wananchi. Nashauri Wizara iwezeshe Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuimarisha viwanda vyatya ndani, kutumia bidhaa/malighafi zetu zaidi. Kwa kufanya hivyo, bidhaa zitazalishwa kwa wingi hapa nchini na pia katika soko zitapungua bei.

Mheshimiwa Spika, pili, maeneo ya *EPZ* na *SEZ* yaboreshwe zaidi ili tutakapozalisha bidhaa bora, zitakabili utandawazi na bidhaa zetu zitakuwa na thamani ili kupata au kuuza nje kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, niongelee mishahara ya watumishi wa Serikali. Hili limekuwa tatizo kubwa kwa muda mrefu. Mishahara ya watumishi wa Serikali kuwa midogo sana, ndiyo chanzo cha yafuatayo:-

- Kukosa Madaktari na Wahudumu wa Afya katika Hospitali zetu na Zahanati na kusababisha huduma kuzorota.
- Walimu wakihitimu wanakwenda shule za *private* na kusababisha elimu duni shule za Serikali.

- Wataalam wanaosomeshwa na Serikali kutafuta “greener pastures baada ya kuhitimu na kuacha taasisi za umma bila watumishi.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo sababu hata Hospitali za Mikoa zinakosa Madaktari na shule kukosa Walimu Wakuu wenyе taaluma bora. Naomba kujua, tatizo hili sugu hapa nchini, Wizara hii ya Fedha inasema nini na imetenga bajeti vipi katika Wizara kukabiliana na uhaba wa watumishi katika Wizara husika (Utumishi)? Nashauri Serikali, iletwe hapa Bungeni Sheria ya Mishahara ili kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Awali ya yote, nampongeza Waziri, Naibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na watendaji. Kwa leo nitazungumzia jambo moja linalonikera sana katika bajeti yetu, nalo ni uandaaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali imekaa kizamani, yaani “*Traditional Budget*” ambayo inatokana na matumizi yaliyopita mwaka uliotangulia. Ni kwa nini bajeti yetu siyo *Activity Based?* Jambo hili linajionyesha wazi ukiangalia *votes* kadhaa kwenye Idara mathalani, *Hospitality Fuel and Car Maintenance*.

Mheshimiwa Spika, mafungu niliyotaja yanakua mwaka hadi mwaka. Kwenye magari, haijalishi yamenunuliwa magari mapya au ni yale yale, ghamama zinapanda tu. Kwenye *fuel*, haijalishi magari yamepunguzwa, bado *vote* hiyo inakua tu. Wakati wa majumuisho, ninaomba kufahamishwa idadi ya magari mwaka jana na ya Hazina mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, *hospitality* imekuwa sana. Naomba tuelezwe bayana fungu hili limetengewa jumla ya shilingi ngapi mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, hizi hela zinavyotawanywa kidogo kidogo kila mahali hazituwezeshi kufikia malengo. Tuwe na dira inayoteklezeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara, Waziri, Naibu Mawaziri na wataalam wote, kwa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi iliyopangiwa fedha mwaka jana na haikutekelezeka kwa sababu Halmashauri hazikupokea fedha waliyopaswa kupokea ili kutekeleza miradi hiyo. Wizara ihakikishe kwamba *commitments* za Serikali zinatimizwa kwa kutumia fedha kwa mipango iliyoidhinishiwa ili kuwezesha shughuli za maendeleo kufanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, *Regulatory Bodies*, zijipange vizuri ili kudhibiti “*inflation*” kwani isipodhibitiwa, “*purchasing power*” ya Mtanzania itazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi, ifanye kazi na Tume ya Mipango ili iwe ni “*think tank*” itakayoandaa mikakati ya “*Policy and Economic Management*” itakayosaidia usimamizi mzuri wa “*economic growth*,” “*balance of payment*” and *government expenditure*”.

Mheshimiwa Spika, taasisi za mikopo na fedha zinapoanza ziwe *scrutinized* ili kukwepa watu/raia wasidanganywe/na kuporwa kama ilivyotokea kwa suala la 'DECI'.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba sana kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa upendo, awasaidie wote wanaokaa chini kwa udhati na kufikiria jinsi ya kuliokoa Taifa hili kutoka kwenye dibwi kubwa la umaskini

Mheshimiwa Spika, tarehe 21/7/2009, niliuliza swali hapa Bungeni kuhusu udhamini wa mikopo unaochukuliwa na Serikali yetu kupitia Benki Kuu. Serikali yetu imenijibu kwa ufasaha kabisa na kukubali kwamba, kweli huwa wanadhamini na kuniambia kwamba wamedhamini mashirika yasiyopungua tisini na tatu yakiwemo Vyama vyta Ushirika, Mashirika Binafsi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatizo sio kukopesha, tatizo ni kuweka dhamana kwa anachokopeshwa kwani akishindwa kulipa basi utalipa wewe uliyechukua dhamana na kama Serikali, itabidi kulipa sio Serikali bali ni wananchi watakoabebeshwa mzigo huo mzito. Dhamana iliyochukuliwa mpaka sasa ni shilingi bilioni 290 milioni 682 na miradi midogo ni shilingi bilioni tatu milioni 54. Hizi ni fedha nyingi sana, basi kama ni hivyo kwamba tunaweza kuwawekea dhamana, kwa nini tusiweke dhamana kwa mashirika ambayo tunahakika fedha itaingia kwa muda mfupi na deni litalipwa na Serikali itaendelea kunufaika na fedha hizo? Mfano, tuweke dhamana kwa *Air Tanzania* ili ifufuke, tuchukue *TRA* yetu wenyewe, tukopeshwe sisi Watanzania kupitia kwa wanahisa wa Tanzania, tufufue Reli yetu, muda mfupi deni litalipwa, barabara zitaacha kuharibika kwa malori mazito na kodi itakuwa kwa muda mfupi tukishamaliza deni fedha itakayoingia hapo tutanufaika, tukopeshe bandari, ili bandari zetu zipanuliwe, kuwa na utendaji wa kuridhisha ili nchi jirani zitumie bandari zetu, deni litalipwa kwa haraka na nchi itanufaika.

Mheshimiwa Spika, hivi ni baadhi tu ya vitega uchumi vyetu vinavyodorora kwa sababu hakuna fedha ya kuvifufua, kumbe tungeweza kupata dhamana ya Serikali na kuweza kufufua taratibu vitega uchumi vyetu na wananchi wetu wakafaidika na umaskini ukawa hadithi.

Mheshimiwa Spika, bado hatujatumia utajiri tulionao ambao tungeweza kuwa matajiri, ni vilio tu vinavyotoka kila siku (Sungura mdogo - hata siku moja Sungura hawi tembo).

Mheshimiwa Spika, tumekamata meli ya wageni wanaokuja nchini, wanapora utajiri wetu wanaondoka sisi tumekaa. Mwenyezi Mungu ametuletea ushahidi kamili kutuonesha utajiri anaotupa kila siku na sisi hatuutumii, meli ile imekutwa na samaki wengi wenye thamani kubwa, samaki wale sijui mpaka leo ni vipi. Tuache hayo lakini je, sisi baada ya kuona hayo kabisa, Serikali imefikiria nini na inajipangaje na sisi tupate huo utajiri wetu? Je, meli ngapi tumefikiria kukopa ili tuchote utajiri huo, tulipe hilo deni haraka na Serikali iendelee kupata fedha?

Mheshimiwa Spika, mabenki yetu tuliyonayo yanapata faida kubwa lakini Mtanzania haoni hiyo faida inakwenda wapi. Kampeni ya kuwataka wananchi watumie mabenki inafaa sana, mishahara ya wananchi wengi sasa hupitia benki, ukipita kwenye mabenki hayo misururu mirefu sana, hii inaonyesha jinsi Watanzania walivyopokea mabenki hayo, lakini cha kushangaza wananchi hao baada ya kupata faida wao hupata hasara kwa mfano, mishahara ya walio wengi (*Net salary*) ni shilingi elfu themanini (80,000) anakwenda benki anatumia shilingi sio chini ya 500/= nauli na akifika benki kuchukua mshahara wake anatumia shilingi mia nne 400 *bank charges*, hiyo ni shilingi 900 lakini yeye hapati faida kwa sababu hawezi kuacha fedha kwa mwaka mzima bila kuzichukua, kwa hiyo, hakuna faida

anayopata. Unapotaka kupata mkopo 18% ya *interest* inabidi ulipe lakini wewe kama mwanachama faida unayopata ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri wahusika wakae na wenyе mabenki haya na kuwataka kutoa faida ya kuwezesha wanachama wake waone faida ya kuzitumia benki hizo, kwa sababu wao wenyе mabenki wanapata faida ya kutosha (sio kutoa misaada ya shilingi milioni tano 5,000,000/= kwa mashule), hiyo wananchi hawaitolei shukrani, kwani huwa tunaimba siku zote uchumi umekua kwa asilimia fulani, lakini wananchi wanasesma hawajaona ukuaji huo kwani hata kula mara moja kwa siku ni kishindo kikubwa; basi waone faida inayopatikana kutoka kwenye mabenki imekuwa na inaingizwa ndani ya akauti zao.

Mheshimiwa Spika, Mabenki hayo yanapotoa mkopo kwa wanachama wake, basi wapunguze riba, riba ni kubwa sana na hiyo yote ni faida ya fedha ambazo sisi wenyewe tumeziweka, tunakopeshana basi faida tuione.

Mheshimiwa Spika, kutumia fedha za mikopo kukarabati majengo ya mashirika kwa fedha nyingi na kuyauza kwa fedha ndogo ni wizi. Naiomba Wizara ya fedha ambayo kati ya majukumu yake ni kulinda fedha ya nchi isitumike ovyo ovyo. Naiomba Wizara ya Fedha ikae na Wizara zingine zinazotumia fedha za walipa kodi, watoe adhabu kali kwa wale watakaogundulika wamefanya makosa hayo, mfano, mchango wa Mheshimiwa Ndassa, hili litiliwe maanani sana na jibu tunalishubiri kwa hamu, pamoja na mauzo na ukarabati wa nyumba za Serikali kwa waliouziwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha na viongozi wetu wanaohusika na Wizara hii muhimu. Nachangia kwenye eneo moja tu nalo ni deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tutagharamia deni la Taifa kwa kiasi cha shilingi trilion 1.5 ambayo ni karibu nusu ya mapato yetu ya ndani na kwa hiyo tunatumikia madeni. Nimefarijika kwamba malipo kwa madeni ya nje ni shilingi bilioni 106. Gharama ya deni la ndani ni kubwa sana yaani shilingi trioni 2.42. Aidha, mwaka huu limezidi mara tatu ya mwaka jana. Jambo hili ni hatari, Bunge lako lielezwe.

Mheshimiwa Spika, aidha, vitabu vyetu pamoja na hotuba ya Waziri, haionyeshi dhamana ya Serikali kuwa taasisi mbalimbali (*total disclosure of government financial commitments*), wala mpango wa muda mrefu na mfupi ili gharama ya kuhudumia madeni pia iwe wazi na itabirike. Dhamana zinazoendana na biashara na kuhusisha taasisi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kuhatarisha uhai wa Mifuko hii. Aidha, kutoonyesha *commitment* hizi, bajeti haiwi kamili kwani *sources za revenue* hazionyeshwi kwenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, haya yakielezwa, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu ambaye hana mshirika, hakuzaa wala hakuzaliwa, kwa kunijalia uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Makatibu Wakuu na watendaji wote, kwa namna wanavyofanya kazi zao, kwa ushirikiano mkubwa na kuwezesha ufanisi mzuri wa shughuli zao za kazi za kila siku.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha, ni Wizara mama, yenyewe majukumu makubwa kwa Taifa na Mataifa. Wizara hii ndiyo inayosimamia misingi ya fedha pamoja na usimamizi wa mali zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia hayo, Wizara zote zinaitegemea Wizara hiyo na yale yote tuliyopitisha hapa katika Bunge lako Tukufu, hayatekelezeki kama fedha hazitopatikana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuzipeleka fedha kwa mpango kama Wizara zilivyoomba na ule mpango wa kupeleka fedha mwisho wa mwaka, ufutwe, haufai na ndio chanzo cha upotevu wa matumizi mabaya ya fedha na kusababisha utekelezaji mbovu wa shughuli za Taifa.

Mheshimiwa Spika, malipo ya wastaafu Afrika Mashariki, bado kuna wastaafu wa Afrika Mashariki hawajapata malipo yao na kuwa wengine wameshafariki na taratibu zote za kisheria zimetekelawa na majina yametoka kwenye gazeti lakini bado hakuna kinachoendelea na wahusika wanaambiwa mafaili hayaonekani. Mfano wa hayo, ni marehemu Taswaha Juma Nasibu, vielelezo vyake vimepelekwa Wizarani, wahusika wanaambiwa faili halionekani, wafuatilie alikokuwa anafanya kazi ndugu yao. Huu si utendaji mzuri wa kazi, suala la kutafuta faili ni la nani? Naomba Waziri atakapotoa majumuisho atueleze.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata ufanuzi, nitaunga mkono hoja.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba kupewa ufanuzi juu ya uamuza wa Serikali kuondoa misamaha ya uwekezaji kupitia *TIC*, *deemed capital* kwa vifaa vya wawekezaji katika sekta ya mahoteli. Hivi sasa mishahara yote kupitia *TIC*, inasitishwa na *TRA*, je, nini msimamo na ufanuzi wa Serikali juu ya suala hili?

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hoja, anipe maelezo. Naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri wanayofanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kuwa Wizara hii ndiyo roho ya nchi, tegemeo kubwa kwa Watanzania, hivyo naomba sana Wizara hii ione umuhimu wa kupeleka fedha za maendeleo katika Wizara husika mapema ili wananchi wanufaika na bajeti hii kama Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Afya. Kama Wizara itajipanga vizuri, kwa kutumia “*Cash Budget*” ili tutumie fedha tuipatayo na matumizi yake yatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwapongeze *TRA*, kwa kazi nzuri wanayoendelea kutekeleza ukusanyaji wa mapato yetu hususani mapato ya ndani. *TRA* ni mamlaka inayoheshimika sana na Watanzania lakini mdudu ameingia ndani ya mamlaka hii na sasa mali za Watanzania zinapitishwa bandarini na *TRA* wanapitisha, ni AIBU kwa *TRA*. Hivyo basi *DG* wa *TRA* alisawazishe hili lisitokee tena (mfano nyara za Serikali kwenye kontena kwenda Hong Kong). Naendelea kuwaombea watumishi wa *TRA* waendelee kupewa motisha kwa kuzingatia kazi ngumu wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa nini *BOT* wanakataa kutoa jingo, Kitalu Na. 28, kwa *IFM*? Wewe ni Waziri, toa maamuzi ili *IFM* isomeshe watalaan wengi. Naomba Waziri anipe jibu katika majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *PPF* kwa uwekezaji wake katika Mkoa wa Mwanza, Mkoa wetu umenufaika sana na uwekezaji wao. Naomba waendelee kuwekeza zaidi katika Mkoa wa Mwanza na kama watataka viwanja vingine hata Ukerewe ikiwezekana wapeleke majengo, soko lipo kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nisisitize mambo yafuatayo:-

- (1) Fedha za “*Revolving Fund*” itolewe mapema kwa Wizara husika ili wachimbaji wadogo wanufaika.
- (2) Fedha za maendeleo zipelekwe mapema katika Wizara husika zinazowagusa wananchi wengi
- (3) Uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Serikali uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara na wasaidizi wake wote, kwa kazi nzuri na hotuba safi. Nampongeza yeye zaidi kwa kuiwasilisha hoja hii kwa ufasha.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unalenga kwenye maeneo machache tu kwani mengi tuliyaeleza kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo nawapongeza kuwa wameyazingatia.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti, nawapongeza sana kuwa katika bajeti hii, tofauti na ilivyo kwenye hotuba yako ya bajeti nzima ya Taifa, mmetilia maanani umuhimu wa bajeti ya maendeleo kwa kuyapa mafungu yote manne (*Kasma* 50,21,23 na 45) Sh.282.5 bilioni ikilinganishwa na Sh.212.6 bilioni za matumizi ya kawaada. Lakini kwenye bajeti hiyo ya maendeleo, bado tunategemea zaidi fedha za wahisani (Sh. 292.6 bilioni) kuliko za ndani Sh.25 bilioni, hii ni kasoro, kwani hizo za wahisani zisipopatikana zote au zikichelewa kuleta, kama ilivyotokea katika bajeti zilizopita, miradi yetu itaathirika. Tuanze kujitegemea jambo ambalo litawezekana tu tukidhibiti matumizi yetu ya kawaada ili tupate salio kubwa la kutumika kwenye miradi. Salio pia litaongezeka kama mapato yetu yatakuwa haraka. Mapato nayo yataongezeka haraka kama tutaweka uzito kwenye sekta zenye nafasi kubwa ya kukuza uchumi kwa mfano kilimo, miundombinu, utalii na usimamizi mzuri wa madini vinawenza kutuvusha.

Mheshimiwa Spika, kuondoa umaskini, Ibara ya 33 ya hotuba, inaorodhesha mafanikio ya ongezeko la ukuaji uchumi la asilimia 0.3 kati ya mwaka 2007 na 2008, kushuka kwa wasiojitosheleza kwa mahitaji na wanaojitosheleza kwa chakula kwa asilimia 2.2 katika kipindi cha miaka 6 (2001 – 2007). Haya sio mafanikio ya kujivunia katika kumtoa Mtanzania kwenye lindi la umaskini. Itabidi katika bajeti zijazo, tulenge ukuaji wa uchumi utakaoongezeka si chini ya asilimia tatu mwaka hadi mwaka na upunguaji wa Watanzania wasiojitosheleza kiuchumi na chakula siyo chini ya asilimia 2.5 mwaka hadi mwaka ili tufikie malengo ya milenia mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, matumizi makubwa, Serikali haina budi kuangalia kwa makini maeneo mawili (2) ambayo yanalitumbukiza Taifa katika matumizi makubwa nayo ni:-

(1) Fedha inayopelekwa kwenye Halmashauri hazidhibitiwi kikamilifu. Kuna ubadhirifu mkubwa unaotokana na baadhi ya watumishi kutokuwa waaminifu na pia uwezo mdogo wa kuchunga fedha za umma. Hili linathibitishwa na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zinaonyesha kuwa kila mwaka taarifa zao zinapata hati chafu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua kuunda chombo kingine kitakachosimamia ukaguzi wa ndani. Lakini nashauri pia sambamba na chombo hicho, Serikali iwe na mpango maalum wa mafunzo kwa Wahasibu wa Halmashauri na uvezeshaji wa Madiwani (*capacity build of Concillors*) ili wasimamie vizuri matunzo ya mali za umma.

(2) Ingawa Sheria ya Manunuzi ya 2001 ilikuwa na nia nzuri kudhibiti ubadhirifu, kwenye utekelezaji kumejitokeza mapungufu yafuatayo:-

(i) Unalazimisha manunuzi ambayo mara nyingi ni ya juu zaidi kuliko njia ya majadiliano baina ya chombo husika na baadhi ya wauzaji.

(ii) Unachelewesha manunuzi kwa kufuata mzunguko mrefu wa hatua za kupitia kabla manunuzi hayajafanyika. Matokeo yake ama kuchelewesha utekelezaji au kununua kwa bei ya juu kwa kuwa bei za vitu vingi hupanda haraka.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi hii imekuwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Kinadharia, inasemekana kuwa Msajili ana Madaraka ya Kisheria (*Statutory Powers*), kiutendaji si kweli. Mheshimiwa Waziri na mimi tuliwahi kuwa Wasajili wa Hazina tunaelewa kuwa wakati wote tulikuwa tunapokea maelekezo ya Katibu Mkuu na Manaibu wake kama walivyo Makamishna wengine matokeo yake ni kuchelewesha maamuzi. Ningekuwa na nafasi ningekueleza tukio lililonikuta mwaka 1976, ni vizuri sasa imeamriwa kuwa ofisi hii ijitegemee. Nashauri kuwa uamuzi huu utekelezwe haraka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na taasisi zake, kwa kazi muhimu na nzuri ya kusimamia maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Hivyo kwa sababu hii, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, malipo kwa Wazabuni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Waziri wa Elimu wakati wa mawasilisho ya bajeti ya Wizara yake, alilifahamisha Bunge kuwa uchambuzi wa madai ya wazabuni mbalimbali wa masuala ya elimu ulikamilishwa na kuwasilishwa Hazina ili madai haya mengine ya tangu mwaka 2003, yaweze kulipwa mara moja. Naomba Waziri atamke leo ni lini wazabuni hao wanalipwa madai yao, kwani wameendelea kuteseka sana.

Mheshimiwa Spika, kujitegemea, kwa kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za aina mbalimbali ambazo zikitumiwa vizuri, nchi inaweza kuanza kujitegemea kuliko kuendelea kuwa tegemezi mpaka kwenye bajeti ya Serikali, nauliza nini mpango wa Serikali wa kuona kuwa Tanzania inaondokana na utegemezi huu? Utegemezi unaotuondolea

uhuru wa kujiamulia mambo yetu; lakini pia utegemezi huu unatuchelewesha katika kujiletea maendeleo yetu kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, Hatifungani za Majiji na *Manispaa* (*City/Municipal Bonds*). Kwa kuwa maendeleo ya Majiji (*Cities*) na Manispaa (*Municipalities*), hayawazi kutegemea bajeti ya Serikali pekee ili kuongeza kasi, ubora na usimamizi endelevu wa ustawi wa wakazi wa maeneo hayo ambayo daima yataendelea kupanuka, nauliza lini Serikali itawezesha Majiji na Manispaa nchini kuanza kutoa Hatifungani (*City/Municipal Bonds*) ili kuongeza uwezo wao wa kuweka na kutekeleza mipango ya kisasa, bora na endelevu ya maendeleo na ustawi wa maeneo hayo? Tayari nchi ya Rwanda imekwishaanza kutekeleza mpango huu mzuri, kwa nini Tanzania tusianze sasa?

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ni wazi MKUKUTA wa pili hautakamilika na kuanza kutekelezwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11, ikiwa Serikali ina lengo thabiti la kuwa na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini unaotekelzeza. Inastahili kujipa muda kutathmini Mkukuta na kushirikisha wadau wote katika kuandaa mpango mbadala wa kukuza uchumi, kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, Wizara hii bado ina mambo mengi sana, ambayo kama yatafanyiwa kazi kama inavyostahili, basi uchumi wetu unaweza kukua kwa kasi ya ajabu.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta iongezewe mtaji ili ifike vijijini. Serikali ichukue hatua hii haraka, Benki ya Posta ni mfano mzuri wa Benki ya Wanyonge na inahitaji kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, walimu pamoja na wafanyakazi wengi ambao wanafanya kazi Tarafani, Katani na Vijijini, wanapata tabu sana kwa ajili ya mishahara yao. Serikali ichukue jukumu hilo kwa uzito.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali bado hawajapata pesa katika Benki ya CRDB na NMB, tunaomba jitihada zifanyike kwa nguvu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii, popote pale wanapotekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kusimamia vizuri mapato yanayokusanywa na TRA na mengine. Nampongeza sana kwa kubana mianya ya misamaha ya kodi na kuwabana washirika wetu wa maendeleo ili fedha zao zote wanazochangia, ziinge kwenye kapu moja badala ya kila mmoja kutoa misaada kule anakotaka na aismamie yeye.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho hakikufanyika kwa umakini ni kutotoa fedha za kutosha ili liendeshe shughuli zake kwa ufanisi. Kupunguza muda wa kujadili mapato na matumizi ya Serikali si kitendo cha maendeleo, kwa sababu mnawanyima nafasi Wabunge kuwakilisha kero za wananchi wao. Mbunge amechaguliwa kujadili kero zote toka Wizara zote, bila kuzuiwa na kuambiwa umekwishachangia mara mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati wa kugawana mapato yanayokusanywa kwa asilimia katikati ya mihimili minne; Serikali, Bunge, Mahakama na Halmashauri za Wilaya,

Miji, Manispaa na Majiji. Serikali iache kushikilia mapato na kugawia mihimili mingine kwa utashi wake.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hatua ya kuanzisha Kitengo cha Ukaruzi wa Ndani, kusimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Fedha. Naomba sana kitengo hiki kianzishwe mara moja na kupewa nyenzo za kufanya kazi ili kusimamia na kuokoa fedha nyingi zinazopelekwa kwenye Wizara zetu na Halmashauri za Wilaya. Pia nashauri Wakaruzi walioko kwenye Halmashauri, wengi wanafanya kazi kama Wahasibu chini ya Wakurugenzi, wapewe mafunzo na miongozo ya kazi zao, pia wahakikishe wanatembelea na kukagua miradi yote.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu ni vigumu sana kujiletea maendeleo, kutokana na kutopewa mikopo na mabenki yetu. Njia pekee ya kuwasaidia wananchi hawa wapate mikopo kirahisi ni kuharakisha upimaji wa mashamba yao ili wapate hati miliki za kimila. Kufanikisha zoezi hili ni lazima Wizara ya Fedha, itafute fedha za kutosha na kuipatia Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Serikali na Mashirika yake, wanalipa kodi kubwa sana kwa kukatwa kwenye mishahara yao; naomba wapunguziwe. Naomba bei za saruji, mabati na kadhalika, zipunguzwe ili kuwawezesha wananchi wetu kujenga.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, riba katika mabenki yetu ni kubwa sana kwa wateja, kiasi ambacho kinakatisha tamaa na hata wengi wakikopa wanashindwa kulipa, kutokana na riba kubwa kati ya 18% - 25%. Cha kusikitisha, wateja wakiweka fedha zao kwenye *saving account, interest* wanayopata ni ndogo sana (3%); tofauti hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Benki Kuu iingilie kati na kuhakikisha benki hizi zinatoza *interest* (riba), ambayo siyo ya juu kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali mara kwa mara inatoa tamko hapa Bungeni kuhusu matumizi ya kufanya malipo kwa kutumia dola. Nchi nyingi hata za jirani (Kenya na Uganda), wanathamini fedha zao. Huwezi kufanya malipo yoyote kwa kutumia fedha za kigeni. Kuanzia malipo ya hoteli, visa, kodi za hifadhi (*Park Fees*), lazima mgeni akabdalilishe fedha hizo katika maduka ya kubadalishia fedha na kulipa kwa kutumia *currency* yao.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu bado malipo mengi yanafanya kwa kutumia dola. Je, kama sisi wenyewe hatuithamini shillingi (*currency*) yetu; nani ataithamini?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwe ndio kiongozi wa kutoza malipo yote kwa Tanzania Shillings, mfano, *Park Fees* za Mbugani, visa za kuingia nchini na kadhalika. Hii itasaida kuinua shilingi yetu na kuithamini fedha yetu kuliko kufanya malipo kwa kutumia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni, pamekuwepo na matukio ya wizi wa fedha za wateja kutoka kwenye ATM Machine. Je, Serikali inatueleza nini au inatuhakikishia usalama gani na fedha zetu wakati tukutumia ATM Machine?

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa, Serikali kumaliza malipo ya Wastaafu ya *East African Community*. Huku ni kuwadhalilisha wazazi wetu na inaitia doa/aibu Serikali;

madai haya yataendelea mpaka lini? Hivi tatizo ni nini? Tukumbuke wazee hawa walilitumikia Taifa hili kwa moyo wao wote na tunasema wazee ni hazina ya Taifa; kwa nini wananyanyaswa?

Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri kwa Wafanyakazi wa TRA kukagua wenyewe hoteli kama wanalipa kodi ipasavyo, lakini utaratibu wanaoutumia baadhi ya wafanyakazi siyo mzuri; unakuta afisa anakwenda kwenye hoteli saa kumi na mbili asubuhi hata wageni hawajaamka tena kwa kushtukiza eti wana-*check* wageni wangapi wamelala ndani! Hii ni aibu, kuwagongea wageni na ku-*check* kama kweli wamelala!

Mheshimiwa Spika, je, ukaguzi huu wa kushtukiza huwa unafanywa kwenye hoteli kama Kempsiki na Moven Peak au ni kuwanyanyasa wazawa na kufikiri wawekezaji ndio wanafanya biashara halali? Ikumbukwe wazawa wanalipa kodi zote, hawana misamaha, wanatakiwa kupewa motisha badala ya kuwanyanyasa.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mipango ya Serikali isiiingiliwe na siasa, kuwe na dhamira ya Viongozi, Mawaziri na Wabunge. Tusigombanie sungura huyu kwa udogo wake, tukubali sungura aende sehemu kubwa, kwa mpangilio wa vipaumbele vya Kitaifa siyo Majimbo. Nawapongeza wote kwa kazi nzuri.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri wa Fedha, kwa umakini wake. Nawapongeza Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, kwa uchapakazi. Nampongeza pia Katibu Mkuu, Ndugu Khijjah, kwani mtu anayeifahamu vizuri Wizara hiyo, ni mtu mwenye maamuzi, aendelee hivyo hivyo kwa kulinda heshima yake na heshima ya Wizara na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Hazina kila mtu anaujua; Hazina ni moyo wa Serikali, siha ya Serikali inategemea utendaji mzuri wa Wafanyakazi wa Hazina. Hazina ni mapato ya Serikali, mapato ya Hazina ndiyo yanayoiwezesha Serikali kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, ili uzuri wa Hazina uonekane ni lazima kuwe na Wafanyakazi wanaothubutu na kuamua ni nini kifanyike sasa (leo) na nini kifanyike kesho. Wafanyakazi wajitume, wawe wabunifu, pamoja na kufuata maadili ya kazi, ikiwa ni pamoja na kuangalia namna ya kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, nashauri tusimamie nidhamu ya matumizi ya Fedha za Serikali na hasa upande wa manunuvi ambako ndiko kunako rushwa.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke fedha nyingi zinakwenda kwenye Halmashauri zetu; hivyo tusiwaonee aibu, tusiwaonee huruma, kwa wale watakaotumia vibaya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, najua TRA inafanya kazi nzuri sana, lakini nashauri kama ifuatavyo: Leseni za uendeshaji zibadilishwe zifanane na zile za Zanzibar; na kodi za magari nazo zibadilishwe zifanane na za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, kutasaidia sana kujua *information* za magari au za wenye leseni.

Mheshimiwa Spika, nidhamu na maadili ya Wafanyakazi ndani ya TRA bado haijaka vizuri, malalamiko ni mengi. Nashauri ikiwezekana ili kupunguza malalamiko ya wewe umeingia juzi TRA hukuwa na mali leo maisha yako mwenzetu yamebadilika, mali uliyonayo haifanani na umri wako, wawe wamejaza fomu za maadili.

Mheshimiwa Spika, je, ni utaratibu gani unaotumika kwa pikipiki na magari kutumia plate namba za *engine* badala ya namba kama utaratibu ulivyo?

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwa kuwa wadau wengi wakiwemo Walimu wa Wilaya ya Mpwapwa Bima zao za Maisha zimeiva lakini hawajalipwa hadi sasa; je ni sababu gani za msingi zinazofanya wasilipwe na je, Serikali ina maelezo gani kuhusu hali ya Shirika la Bima la Taifa (NIC) kifedha na matatizo yanayolikabili Shirika hili?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasamehe Waheshimiwa Madiwani kodi ya uingizaji wa vyombo vyaya usafiri (magari na pikipiki) ili wapate vyombo hivyo kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha za Miradi ya Maendeleo hucheleva kupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji; je ni sababu gani zinazofanya fedha hizo kucheleva kupelekwa Wilayani na kusababisha Miradi mingi kucheleva kutekelezwa na kukamilika?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliahdi kujenga Ofisi ya TRA Wilaya ya Mpwapwa; je, mpango huo umefikia wapi na utekelezaji utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa Wahasibu katika Halmashuri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji; je, Serikali ina mpango gani wa kufundisha Wahasibu wengi na kuwapeleka kwenye Halmashauri zenye upungufu wa wataalam hao wa fedha?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, matumizi ya pesa za kigeni, imekuwepo tabia suga ya matumizi ya fedha za kigeni hasa dola ya Kimarekani bila sababu maalum za kuendeleza mtindo huo. Mtindo huo unaifanya shilingi yetu idorore bila sababu. Kwa nini tusiwe kama Kenya na South Africa ambao hawaruhusu matumizi ya pesa ya kigeni zaidi ya pesa zao.

Mheshimiwa Spika, Wazimbabwe waliamua kwa makusudi kutumia pesa za kigeni kwa sababu ya *inflation* kuzidi kupita kiasi, hivyo, wakaidhinisha. Sasa Tanzania tuna sababu ipi ya kutumia pesa za kigeni bila mpangilio maalum?

Mheshimiwa Spika, Benki ni chombo muhimu sana lakini mabenki yaliyopo hayamsaidii sana Mtanzania wa kawaida, wanajali faida kupita kiasi. Riba ni kubwa sana kiasi kwamba watu wengi huogopa kukopa ili watumie mkopo huo kujiendeleza. Wizara iangalie jinsi ya kushughulikia tatizo hilo ili Watanzania waone faida ya kuwa na vyombo

hivyo kwani mabenki mengi hutoza riba kuanzia asilimia 18 – 25% hiki ni kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta iimashwe ili iweze kutumika kwani Ofisi za Posta zipo karibu kila Wilaya, ni benki yenyi mtandao mkubwa. Sasa kuna mpango wa kuanzisha Benki ya Wakulima, kwa nini benki hiyo ya Posta isitumike wakati Benki ya Wakulima ikiwa kwenye mchakato wa kuanzishwa?

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi hayajapata matawi ya benki nyingi zilizopo Dar es Salaam. Hivyo, nashauri Wizara hii ifanye jitihada za kuongea na mabenki ili Wilaya nyingi zipate huduma za benki hizo. Mfano, Bunda ipo *NMB* peke yake.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwenye migodi ya madini, sikubaliani na maamuzi ya Serikali kutofuta misamaha hiyo ya kodi kwa migodi iliyopo na badala yake wanaendelea kufaidi msamaha huo wakati huo huo, Serikali imefuta misamaha hiyo kwa wale watakaoanzisha mgodi mpya. Swali kwa Serikali, inakuwaje watu wanaofanya biashara moja wengine walipe kodi wengine wasilipe?

Mheshimiwa Spika, kama wawekezaji wa sekta ya madini wangekuwa hawapati faida, wangeendelea kuwepo? Kama Mtanzania anayefanya biashara ya mtaji mdogo analipa kodi, kwa nini wawekezaji hao wasilipe kodi? Nchi hii inahitaji sana pesa kwani *budget* yetu bado inategemea wahisani kwa zaidi ya asilimia 30%.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwa ujumla, katika *report* ya CAG (Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya 2007/2008. Misamaha ya kodi ilikuwa Shs.754,316,2000,000 sawa na 21.2% ya makusanyo yote). Hivyo, *TRA* hata wakusanye pesa kiasi gani bado hawafikii kiwango kinachotakiwa kwani misamaha hiyo inahusu pesa nyingi. Kwa maana hiyo, hamna maana kuisifia *TRA* kuvuka malengo ya makusanyo wakati bado wapo wanaosamehewa na nchi inakosa pesa nyingi. Wakati tunasamehe, tunaenda kuomba wahisani. Tuangalie upya mfumo wa kodi kwa ujumla pamoja na mfumo wa misamaha hiyo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa nini kumetokea tabia ya kutumia fedha za kigeni (hasa *USD*) katika ununuza ama malipo mbalimbali badala ya fedha za ndani (Tshs.)?

Pili, kuna usumbufu mkubwa sana wa malipo ya pensheni na fedha za mirathi kutokana na urasimu usio wa lazima. Hivi kuna tatizo ama kiini cha yote haya ni nini na ufumbuzi wake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu hasa katika kutekeleza Sera ya Kuondoa Umaskini na Uwezesaji Wananchi Kiuchumi, bado hatujawekeza kwenye kuwawezesha Watanzania wazalendo (yaani wananchi), mikopo na pesa za kuwawezesha wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo. Nashauri pesa nyingi zielekezwe kwa wananchi hao wanyonge.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Fedha zingoje maridhiano ya Bunge kabla ya kutumia.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Pili, nimshukuru Waziri, Manaibu Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana, ni Wizara inayoongoza Wizara zote kwa kuziwezesha kifedha ili ziweze kutekeleza mipango ya maendeleo katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kusimamia makusanyo ya kodi kikamilifu na kubuni kodi mbalimbali ambazo hazina kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania, ina rasilimali nyingi sana kiasi kwamba kama Serikali italisimamia vema, nchi yetu itakuwa moja ya nchi tajiri hapa Afrika. Tukijipanga vizuri katika sekta ya madini ambayo inakua sana tutapata pato la kutosha. Umuhimu wa mikataba ya madini chini ya Tume ya Bomani, ukitumiwa vizuri italeta tija kubwa kwa uchumi wa Tanzania. Serikali iwe na ubia kati ya mwekezaji ili Taifa liweze kupata na kunufaika na mapato ya madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi, ni vema Serikali iangalie upya misamaha hiyo, kuna baadhi ya misamaha ambayo huwa inanuifaisha watu binafasi. Kuna mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo hupata msamaha wa kodi lakini huwa ni msamaha wa viongozi au kiongozi wala sio wa taasisi. Naishauri Serikali kusimamia misamaha kwenye *NGO*'s na taasisi za dini.

Mheshimiwa Spika, makusanyo katika Bandari ya Dar es Salaam, Tanga yasimamiwe vizuri, pasiwepo uchelewaji wa wateja pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watumishi wa *TRA* ambao si waaminifu, huwa wanakusanya fedha nyingi hasa sehemu za mipakani lakini fedha zinazopelekwa Serikalini huwa kidogo. Pawepo na tathmini ya uhakiki ili kinachokusanya, kilingane na tathmini halisi, kama tathmini itakuwa chini, watumishi watakusanya na utasema umevuka lengo zaidi ya asimilia mia.

Mheshimiwa Spika, mara makusanyo yanapokuwa tayari ni vema yapelekwe mara moja kwenye miradi husika ili iweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Benki ya *NMB* kujitokeza kufungua Tawi lake pale Itigi, maandalizi hayo na uamuzi wa Meneja wa Kanda ya Kati yamepokelewa kwa shangwe na wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi. Kutokana na uchumi wa eneo hilo la Itigi na Mgandu, bado kuna haja ya kuwa na tawi lingine la *NMB* au *CRDB*, Mgandu, mji mdogo wa Mitundu. Naiomba Wizara isimamie kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Matawi haya mapema ili kuwapunguzia wananchi adha ya kufuata huduma za Benki Manyoni na Singida.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Waziri na Manaibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nampongeza sana Waziri, Manaibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ya usimamizi wa uchumi wa nchi yetu, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nilizungumzia matatizo ya huduma iliyokuwa inatolewa na *NMB*, Wilayani Misungwi haikuwa ya kuridhisha kwa sababu ya mahala pa kufanya kazi palikuwa padogo. Ombi langu limesikilizwa, *NMB* imejenga nyumba nzuri na huduma kwa sasa ni nzuri. Naiomba ofisi yako hasa wewe Waziri, uje uizindue, karibu sana Misungwi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuhamisha watumishi, Walimu wa Sekondari kwenda *TAMISEMI*, lipo tatizo limejitokeza, jana nimepokea malalamiko hadi 29/07/2009, Walimu zaidi ya 14 walikuwa hawajui cha kufanya baada ya kwenda katika akaunti zao na kujikuta hakuna chochote. Naomba nipate majibu ili Walimu wa Sekondari Wilayani Misungwi wapate haki yao.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vimekuwa na matatizo ya upataji wa mikopo toka mabenki. Naiomba sana Serikali itumie Benki ya *TIB* kukopesha Vyama vya Ushirika kuanzia mwaka 2010/2011, hii ni kwa sababu za makusudi kuinua ushirika na wakulima kwa ujumla wake.

Mhehsimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, ipo haja kwa *PPRA* kufanyiwa marekebisho kwa sababu inachelewesha shughuli za umma kutokana na mchakato wake kuwa mrefu mno, iletwe ifanyiwe marekebisho haraka.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inavyo vyuo vingi vilivyochni yake hivyo ni wazi kabisa vijana wanaomaliza vyuo hivyo walioandaliwa wapewe ajira waitumikie nchi. Mfano *IFM* inatoa kozi ya kodi, ni vyema vijana wanaohitimu chuoni hapo wakaajiriwa ili wasimamie ukusanyaji wa mapato ya nchi kuliko kuwaacha wajitafutie badala yake atapata kazi tofauti na kozi aliyosomea.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya watumishi wa Hazina, nao wanahitaji mishahara mizuri, hivyo ni muhimu kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji hao maana ndiyo wanaosimamia pesa na kazi zote za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sana Waziri anijibu juu ya mishahara ya Walimu wa Sekondari Wilayani Misungwi wana hali mbaya. Si vyema nikasimama kwenye vifungu kwa jambo ambalo liko ndani ya uwezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Gavana wa Benki na watendaji wakuu wa taasisi pamoja na *TRA* katika Wizara na kwa ujumla wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa jitihada wanazofanya ili kutimiza majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unahu zaidi wananchi wa Jimbo la Mbinga Mashariki na nitashukuru sana kama watasaidiwa:-

(1) Wizara itupe ratiba ya utekelezaji wa miradi ya *MCA* kwa mfano barabara ya Peramiho (Songea) - Mbinga inaanza kujengwa lini?

(2) Mwaka 2007, Idara ya Kuondoa Umaskini ilifanya semina kuhusu MKUKUTA na *VICOBA* Wilayani Mbinga. Serikali kupitia Mkurugenzi wa Idara hii, aliahidi kurudi baada ya muda mfupi kutoa semina kwa kina juu ya *VICOBA* ikiwa ni pamoja na kuanzisha, mpaka sasa ahadi hii haijatekelezwa na wananchi wanasubiri. Kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi kwa hiyo naomba Wizara itekeleze ahadi hiyo kama sehemu ya mapambano dhidi ya umaskini.

(3) Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Chuo cha Mipango kimesemwa ni chuo kinachotoa mafunzo mbalimbali. Naomba Wizara itusaidie wataalamu hawa waje Mbinga kufanya mafunzo kwa Watendaji wote wa Vijiji, Watendaji wote wa Kata na Makatibu Tarafa wote, hasa wakati huu tunaopeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri pamoja na dhana ya kuibua miradi, wananchi wanapaswa kuongozwa. Mpango wa *DADPS* haufanikiwi kadri ya matarajio kwa sababu uelewa ni mdogo lakini pia miradi mingi haitekelezwi vyema. Tatizo pamoja na sababu nyingine ni uelewa. Pengine tukifanya '*pilot training*' pale Mbinga, tutaona tofauti na hivyo tunaweza kupeleka mafunzo hayo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, madeni/malimbikizo ya mishahara hasa Walimu. Hili ni tatizo kubwa lakini ni tatizo ambalo halipaswi kuwepo. Nani anayelisababisha na kwa nini? Ni muhimu kupata majibu. Ziko taasisi zipo mpaka Wilayani/Tarafa kama *NMB* mbona hakuna mtu anakosa mshahara? Hata taaluma nyingine ndani ya Serikali zina matatizo makubwa. Naamini Wizara ya Fedha na Uchumi, inaweza kabisa kubaini njia itakayohakikisha tunaondokana na tatizo hili. Dhana kwamba hawa wako Halmashauri/TAMISEMI, haiwezi kutumika katika mazingira haya. *Central Government and Precisely* Wizara ya Fedha na Uchumi lazima iinglie jambo hili si tu ni gharama kuteswa vijana wetu lakini pia ni aibu.

Mheshimiwa Spika, *Mwananchi Fund*, nimepata bahati ya kutembelea viwanda vidogo na taasisi kama *TEMDO*, *Carmatec*, lakini pia *UDSM*, Shule ya Biashara. Hawa wote wameanzisha Viatamizi. Wajasiriamali hawa wanahitaji mtaji ili wazalishe zaidi. Wanahusisha pia vijana wanaomaliza vyuo vikuu. Mfuko huu ungeweza kuwasaidia sana watu/wananchi wa namna hii na hii ingesaidia sana ukuaji wa viwanda na hasa *Agro processing*.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri na wafanyakazi wote mafanikio katika mwaka wa 2009/2010.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Mkulo (Mb), kwa hotuba yake nzuri na inayoleta matumaini kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 20/07/2009, wakati nikiwakilisha bajeti ya Wizara yangu (*MST*), suala la fedha za utafiti kufikia asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa kama ilivyaoagizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilijitokeza. Katika kulitolea maelezo suala hili, ulilieleza Bunge kwamba Serikali imetenga kiasi cha asilimia 0.4 cha pato ghafi la Taifa na kwamba maelezo ya kina ungeyatoa siku ya kusoma bajeti ya Wizara yako (29.07.2009, Nukuu ya *Hansard*).

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba yako na kukusikiliza kwa makini bila kusikia lolote kuhusu fedha za utafiti? Kama fedha hizo kweli zipo, nitashukuru kufahamu ziko wapi na ni kiasi gani?

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ni faraja kubwa na furaha kusikia ya kuwa kiwango cha pensheni kwa wastaafu kitaongezeka kwa mwaka huu wa fedha wa

2009/2010. Haya yalitangazwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi katika hotuba yake katika kikao hiki kinachoendelea cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, nasema kuwa hii ni faraja kwa sababu baada ya kulitumikia Taifa kwa uadilifu katika maisha yake yote, mstaafu anatazamia kupata kiinua mgongo na stahili zake wakati wa uzee akiwa na nguvu na uwezo wa kufanya kazi umepungua.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kuwa sio wastaafu wote wanapata haki yao hii stahili. Hapa ni-*declare interest* kwanza. Wahadhiri (Walimu) wastaafu wa kilichokuwa Chuo Kishiriki cha Afya Muhimbili (*Muhimbili University College of Health Sciences*) ambacho sasa ni Chuo cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili (*Muhimbili University of Health and Applied Sciences*) mpaka hivi leo hawajapata pensheni zao kikamilifu. Wengine mpaka hivi leo hawajapata hata senti moja ya pensheni zao, ingawa ni miaka minge. Sasa wamekuwa wakigonga milango tofauti ya ofisi za Wizara ya Fedha na Uchumi. Waswahili wanasema “mstahamilivu hula mbivu” lakini kwa kuogopa ya kuwa wastaafu hawa wasije wakala mbovu, tunaomba Waziri wa Fedha atoe tamko rasmi kuhusu lini wastaafu hao watapata haki zao. Kuna msemo wa Kiingereza usemao ‘*Right delayed is right denied*’.

Mheshimiwa Spika, hapa pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na watendaji wa Wizara, kwa kuyachunguza kwa kina masuala yetu na baada ya kuridhika na uhalali wa madai yetu, wameiandalia Wizara ya Fedha na Uchumi, ili kuwakumbusha juu ya stahili za wastaafu hawa. Inasikitisha kuwa mpaka leo hii Wizara ya Fedha na Uchumi haijibu barua kutoka Wizara ya TAMISEMI.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpungeza Waziri, Naibu Mawaziri, Naibu Katibu Wakuu, Wataalamu na watumishi wote wa Wizara hii walioshiriki katika uandaaji wa bajeti hii na kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, pesa (asilimia moja) za utafiti, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Azimio la Addis Ababa mwaka 2007, aliahidi (pamoja na wakuu wengi wa nchi zinazounda AU) kwamba Serikali yake itatenga asilimia moja (1%) ya pato la Taifa kwa ajili ya shughuli za utafiti. Jambo hili halikutekelezwa kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009. Sasa naomba kujua, je, pesa hizi zipo kama Waziri wa Fedha aliyoliarifu Bunge hivi karibuni na kama zipo zimebekwa wapi? Maana vitabu vyta bajeti havionyeshi zilipo pesa hizo!

Mheshimiwa Spika, aidha, Waziri wa Fedha alikaririwa na Gazeti la *The Guardian* la tarehe 01/06/2009, akisema pesa hizo zitaratibiwa na Baraza la Taifa la Uvezeshaji Kiuchumi (*National Economic Empowerment Council (NEEC)*). Je, taarifa hii ni sahihi? Kama ni sawa, Waziri amepata wapi madaraka ya kuhamisha uratibu wa shughuli za utafiti kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ambayo ilianzishwa kwa Sheria Na.7 ya mwaka 1986 na Ibara ya 5 ya Sheria hiyo ikibainisha kabisa kwamba kazi ya uratibu wa masuala ya utafiti ni ya *COSTECH*.

Mheshimiwa Spika, pili, malipo ya pensheni kwa wastaafu, kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kuongeza kiwango cha malipo kwa wastaafu kutoka Tshs.21,000/= hadi T.shs.51,000/=. Hata hivyo, naiomba sana Wizara ya Fedha iharakishe/iwe inawalipa pesa

zao mapema kwani kwa sasa ucheleweshaji ni mkubwa sana. Ucheleweshaji huo husababisha malalamiko makubwa sana na wananchi kuona kama Serikali haiwajali.

Mheshimiwa Spika, tatu, malipo ya Bima zilizoiva, hili ni eneo ambalo wananchi hulilalamikia sana. Bima nyingi, zile za maisha, elimu na kadhalika, ambazo zimeiva tangu miaka ya 2005/2006 na kuendelea nyingi, hazijalipwa hadi leo. Naomba Serikali ilisaidie Shirika hili ambalo hutumia kuliko linavyozalisha, ili wadai wake waweze kulipwa haki zao. Haipendezi kuona karibu kila eneo Serikali inalalamikiwa na wananchi, aidha, naomba kujua mpango wa Serikali kuitia Shirika la Bima, ni lini sasa litamaliza kulipa madeni ya wale wote wanaidai Bima.

Mheshimiwa Spika, nne, Taasisi (*NGO's*), zinazojihusisha na ukopeshaji pesa wananchi. Zipo taasisi nyingi sana zinazojihusisha na biashara ya aina hiyo. Taasisi hizo ni kama vile "*Bay Port Financial Services, Pride Tanzania, Blue Financial Services*" na kadhalika. Taasisi hizo hutoza riba kubwa sana na wakopaji wengi wamejikuta wanajitumbukiza kwenye mikopo ya aina hiyo kwa sababu wenye taasisi hutumia lugha ya udanganyifu kuwapata wakopaji. Hali hii imesababisha malalamiko makubwa sana toka kwa wananchi na kundi kubwa lililoathirika ni Walimu na watumishi wa afya. Naiomba na kuishauri Serikali iache kuwaingiza watumishi wake wenye mikopo ambayo badala ya kuinua uchumi wao, huadidimiza. Pili, Benki Kuu idhibiti taasisi hizo ili zisiwanyonye wananchi.

Mheshimiwa Spika, tano, riba na amana za mabenki. Pamoja na mpango mzuri wa Wizara hii kudhibiti riba kubwa zinazotokana na mabenki kwa wakopaji wao ukilinganisha na faida inayotolewa kwa amana za wateja, bado naiomba Serikali kuitia Wizara hii na Benki Kuu walifanyie kazi suala hili kwa haraka sana ili wananchi wengi wafaidike na mikopo ya Benki kuliko sasa ambapo benki zinawanyonya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara, kuanzia Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kazi nzuri na kuandaa hotuba inayoeleweka. Mchango wangu ni kama ifuaatavyo:-

(a) Ni muhimu kwa Wizara kuona uwezekano wa kutumia shilingi ya nchi badala ya matumizi ya dola kwenye malipo ya hotelini na kadhalika hasa zile hoteli kubwa kubwa za kitalii kama nchi zingine zinavyothamini sarafu zao.

(b) Malipo kwa wastaifu na warithi, pungezi kwa Serikali kwa kuboresha utaratibu wa kuwalipa wastaifu pensheni zao kuitia benki lakini bado wanahangaika na gharama za usafiri kufikia benki hizo toka vijijini. Serikali itafute njia ya kutatta changamoto hii labda malipo yapitie kwenye taasisi za fedha ambazo ziko mpaka vijijini.

(c) Ni ukweli kwamba warithi bado wanahangaika sana katika kupata mirathi yao kutokana na urasimu mkubwa uliopo na hali ya nenda rudi kesho, nenda rudi inayoendelezwa na wataendaji husika. Nashauri kitengo husika kiangaliwe kwani warithi wanassumbuliwa sana, kiasi cha wengine wanakata tamaa na kuacha haki yao kupotea.

(d) Suala la uwezeshaji wananchi. Nashukuru Serikali ina dhamira ya kuwezesha kiuchumi yale makundi maalumu ya kijamii wakiwemo wenye ulemavu, wazee na kadhalika. Hata hivyo, naiomba Wizara itoe mwongozo mahsuswa wa jinsi ya kuwapatia mkopo watu hawa kwa vile kwa kiasi kikubwa hawawezeshwi kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na watendaji wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti hiyo vizuri lakini pia kwa kuendesha shughuli za Wizara vizuri.

Mheshimiwa Spika, uwazi kwenye vituo vya forodha mipakani. Napendekeza na kuomba kuwa ili kuweka mambo wazi na kwa kuwa uelewa wa wananchi wanaopitia kwenye mpaka wa Murongo – Karagwe kuelekea Uganda sio mkubwa sana, kwenye Kuta za Ofisi za Forodha ziwekwe jarida/tangazo za rate au viwango vya ushuru unaopaswa kutozwa na vile vya asilimia “ 0% ” vitajwe. Hapa ninamaanisha zile bidhaa tu zinazoingizwa sana na wananchi; kama sukari, chumvi, mafuta ya kula, sabuni, maji ya chupa na kadhalika. Utaona kwamba wananchi wa maeneo hayo wanategemea sana bidhaa toka Uganda kwa sababu ya location yao. Hili likifanyika, litawasaidia sana wananchi. Wengi wanatafuta njia za panya ili kuitisha bidhaa ambazo kumbe hazina hata ushuru.

Mheshimiwa Spika, *NBAA*, napendekeza na kushauri kwamba *NBAA* isaidiwe kuendeleza mradi inaouendesha wa ujenzi wa Kituo cha Utaalamu wa Uhasibu kilichopo Bunju kwa kuwa kitakuwa cha manufaa sana.

Mheshimiwa Spika, msimamo, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Prof. Mustafa Haidi Mkulo, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omary Yusufu Mzee, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi yenye mwelekeo wa kuboresha huduma katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa, kutamka rasmi kuwa, ninaunga mkono hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa asilimia mia kwa mia kwani na nina imani kubwa na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo pamoja na Manaibu Mawaziri wake wote wawili bila kumsahau Katibu Mkuu. Ninawaombea Mwenyezi Mungu awape afya, nguvu, busara na mshikamano, ili waweze kutekeleza vema mipango yao.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kusaidia wajasiriamali, ninaipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kusaidia wajasiriamali ili waweze kuondokana na umaskini kwa kuwakopesha fedha kuitia taasisi mbalimbali pamoja na fedha za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bado elimu kwa wajasiriamali haijafika vizuri hasa vijijini hususani wanawake, hivyo, elimu itolewe hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa wajasiriamali ina masharti magumu na iko mbali na wananchi. Mfano mikopo kuitia mfuko wa JK inayopitia *CRDB* na *NMB* riba kubwa na mabenki yako mbali na wajasiriamali walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa wastaifu na warithi. Ni ukweli usiofichika, huduma kwa wastaifu na warithi, bado ina ukiritimba mkubwa na iko mbali sana na wastaifu na warithi. Pamoja na Serikali kueleza Bunge kuwa, huduma imesogezwa Mikoani lakini malipo ya wastaifu na warithi hayafiki kwa wakati, hivyo, walengwa hulazimika kufuata Dar

es Salaam. Ninaionba Serikali kulisimamia suala hili kwa karibu sana ili walengwa waweze kupata haki zao mapema na bila gherama kubwa. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA na MKURABITA. Napenda kuieleza Serikali kuwa, inayo mipango mingi sana na yenye nia njema kwa wananchi bali elimu haifiki kwa wananchi, hivyo, wanaonufaika na mifuko hii yenye malengo mazuri kwa wananchi mfano sasa kuna MKUKUTA Na.II wakati MKUKUTA wa mwanzo huduma yake haikufika kwa Watanzania wengi hata kuuelewa vizuri. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, dhamana kwa wawekezaji wanaokopa Serikalini. Ninatambua kuwa, Serikali hutoa dhamana kwa wawekezaji wakubwa wanapotaka kukopeshwa na taasisi za Serikali mfano *BOT*, *NSSF* na kadhalika. Hii huwa ni nia njema ya kukuza uchumi wa nchi yetu. Tatizo ni pale baadhi ya wawekezaji wanaposhindwa kulipa mikopo yao. Ninaishauri Serikali kuiangalia upya mikataba ili kuepuka hasara inayoweza kutokea pale mwekezaji anaposhindwa kulipa mkopo na mzigo huo kuwa wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuweka mipango mizuri ya kuwalinda wawekezaji ili wasikwame kuendesha miradi yao na kusababisha hasara kubwa mfano viwanda vyetu bidhaa zao kukosa soko kwa sababu ya kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mishahara na madai mbalimbali ya watumishi wa Serikali. Bado kuna tatizo la mishahara ya watumishi kufika kwa kuchelewa, vituo vya kuchukulia mishahara kuwa mbali mfano benki ya *NMB*. Pia madai mbalimbali mfano ya Walimu kuchelewa kulipwa na kusababisha migogoro ya Serikali na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya maendeleo kucheleweshwa. Ni dhahiri mifuko mbalimbali ya maendeleo inayopitia kwenye Halmashauri zetu nchini, inaongeza kasi ya maendeleo sana vijijini na mijini. Tatizo, usimamizi wake hauko makini, Serikali ifuatilie kwa karibu na pia fedha hutumwa kwa kuchelewa sana.

**MHE. ARCH. FUYA. G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, pamoja na watendaji wengine wote hapo Wizarani na taasisi zake kwa kazi mnayoifanya pamoja na hotuba hii. Nawapongeza pia kwa kuunga mkono uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa ninayoiona ni pale Serikali/Wizara hii inaposhindwa kudhibiti kabisa matumizi ya fedha za kigeni katika manunuza ya ndani ya nchi, jambo linalozidi kuididimiza shilingi yetu na kuzidi kuonekana haina nguvu na hivyo thamani yake kuendelea kudharaulika. Hili ni jambo ambalo tumekuwa tulipigie kelele miaka mingi sana lakini cha kustajabisha, bado tunaendelea na dola ndio imeshika kasi kubwa mfano ni kwenye ada za shule za binafsi, huduma za mahoteli, hata baadhi ya kodi za Serikali na kadhalika. Hii ni aibu! Ninapendekeza Serikali itoe tamko kwenye hili la kutumia pesa za kigeni nchini!

Mheshimiwa Spika, ninashauri sera zetu za fedha/kibenki, ziangaliwe ili benki za biashara zishauriwe kupunguza riba wanazowatoza wananchi.

Mheshimiwa Spika, hongereni kwa kuwakumbuka wastaa fu wetu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri pesa kwenye Wizara mbalimbali zipelekwe kwa wakati ili kuepuka matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia Halmashauri zetu Mawilayani zina-operate *accounts* nyingi sana kiasi kwamba ni mkanganyiko sana kwa Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara idhibiti mfumuko wa bei kwani dalili siyo nzuri yaani mwenendo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo (Mb), Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na taasisi na wataalamu wote wa Wizara na taasisi zake, kwa hotuba nzuri na utendaji bora.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kuhusu jitihada za kuboresha uvezeshaji wa wananchi kiuchumi. Ni muhimu sana kuchukua hatua thabiti za kuboresha uvezeshaji wananchi kiuchumi ili wananchi wanyonge waweze kufaidika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta mafanikio yanayotarajiwa katika kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, jitihada maalum ifanyike katika kuharakisha ufunguzi wa Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) na hatimaye ufunguzi wa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda viwanda vya ndani, ipo haja ya kurekebisha kodi kwa viwanda vichanga na hasa vile ambavyo vinapata ushindani usio wa haki kwa bidhaa zinazotoka nchi za nje. Aidha, kuna umuhimu mkubwa wa kutazama upya na kuhuisha mlolongo mkubwa wa kodi kwa bidhaa zetu mbalimbali za ndani ili ziweze kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nzuri ya kuanzisha Kitengo cha Sera ya Ununuzi wa Umma, ipo haja ya kuwa na sera ya kutoa kipaumbele kwa bidhaa zinazozosalishwa nchini kama vile samani za ofisini, mavazi kwa vikundi maalum na vifaa vya shulenii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuongeza pensheni na kuboresha taratibu zake za malipo. Hata hivyo, hili bado ni eneo la kero kubwa na ipo haja ya kuongeza kasi ya maboresho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kilio cha muda mrefu bado wafanyabiashara na wenye mahoteli wengi wanatoza malipo ya huduma au mauzo yao kwa Dola ya Kimarekani (USD). Hatua za dhati zichukuliwe kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. PROF. RAPHAEL R. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ludewa tumeahidiwa kupewa Tawi la Benki *NMB* Mlangali. Mwakilishi wa *NMB* alishakagua eneo na kwamba tumewekwa kwenye orodha ya kupata Tawi la Benki Mlangali lakini tumeshauriwa kupata msukumo wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mlangali ndiyo inayochangia zaidi ya 75% ya uchumi na mapato ya Wilaya na ina zaidi ya wakazi 15,000, licha ya kuzungukwa na Kata zenye watu

wengi sana kama Lugarawa na Mawengi. Ina Shule ya Sekondari (Form I – VI); madhehebu ya dini na biashara kadhaa. Kuna mradi wa umeme (*Mini-Hydro*) ulianza na ni karibu na eneo la machimbo na viwanda (*Liganga*) pamoja na Chuo cha Ufundı (*VETA*) kitakachojengwa Shaurimoyo, kuna biashara kubwa ya mahindi (*SGR*) pamoja na kahawa na pareto vyote vikilimwa Mlangali na maeneo yanayozunguka. Tunaomba ushawishi wa Wizara ya Fedha na Uchumi tupatiwe Tawi la Benki Mlangali (Ludewa).

Mheshimiwa Spika, ofisi inayohusika na ulipaji wa pensheni za wastaafu katika Wizara hii lazima iwe na matatizo sana. Mwenyewe napata matatizo na usumbufu mwingi kufuatilia pensheni za wastaafu wa Ludewa bila mafanikio , kulikoni?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais, bado kazi za Tume hiyo hazionekani ni kama haipo. Hii ni kasoro kubwa sana katika nchi yetu kwani nchi karibu zote zilizoendelea zina “*Think tanks*” ili kuelekeza maendeleo ya nchi. Hiyo Tume inafanya kazi gani?

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi ya kwanza kumpongeza sana Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya. Aidha, nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ninaomba nichangie machache:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima ya Taifa (*NIC*), liliwahi kufanya kazi nzuri ya kuwashudumia Watanzania na kuwa kati ya mashirika yenyе ufanisi mkubwa sana nchini. Ninasikitika kusema kuwa Shirika hili la Umma, hivi sasa lina hali mbaya sana, limekabiliwa na ukata mkubwa, matokeo yake ni kushindwa kumudu majukumu yake. Majukumu hayo ni pamoja na kulipa bima zilizoiva, kulipa madai ya ajali, moto na kadhalika. Hivi sasa kuna mrundikano mkubwa sana ya madai Mikoani hadi Makao Makuu ya Shirika ambapo hadi Desemba, 2008 yamefikia shilingi 28.03bin/=.

Mheshimiwa Spika, bima ni mkataba kati ya mteja na chombo cha bima. Wateja wa Shirika la Bima la Taifa wamekuwa mstari wa mbele kuchangia bima zao mbalimbali, zikiwemo za Maisha, Ajali, Magari, Elimu na kadhalika. Kinachosikitisha ni kuwa inapofika upande wa Shirika la Bima ya Taifa kutekeleza wajibu wake wa kulipa madai ya wateja wake, shirika halitekelezi wajibu wake kwa visingizio mbalimbali na kuleta usumbufu mkubwa kwa wateja wake.

Mheshimiwa Spika, mfano, katika Wilaya ya Kondoa karibu Walimu wote wa Shule za Misingi na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya Kondoa, ni wateja wa Shirika la Bima ya Taifa. Wengi wao ni wateja wa Bima za Maisha na Elimu. Bima zao nyingi zimeiva tangu miaka mitano iliyopita, kila siku ni njoo kesho, huu ni wizi. Kwa kuwa Shirika la Bima ya Taifa ni Shirika la Umma, Serikali ina wajibu wa kulikwamua na kusaidia wateja kulipwa madai yao haraka wakiwemo watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, ninaambiwa kuwa Serikali inachukua hatua ya kuuza baadhi ya mali za Shirika ili kulipa madai ya wateja. Ninaomba Serikali iharakishe mchakato huu ili wadai, wateja walipwe na kwa kuwa wamecheleweshewa malipo walipwe pamoja na riba.

Mheshimiwa Spika, kucheleta kutoa fedha mapema kutoka Hazina, utekelezaji wa miradi ya maendeleo inacheleta kutohana na Hazina kucheleta kutoa fedha kwa wakati. Kwa kuwa Serikali inatumia “*Cash Budget*” ninaomba fedha za maendeleo zitolewe kila robo mwaka.

Mheshimiwa Spika, agizo la Rais la kutenga asilimia moja (1%) ya pato la Taifa kwa ajili ya utafiti nchini litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hotuba ya Waziri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutapokea michango ya Naibu Mawaziri wawili kila mmoja asizidi dakika 15 halafu mtoa hoja kwa muda usiozidi dakika 30. Sasa nitamwita kwanza Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja ambayo imetolewa, imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi leo hii. Lakini kabla sijaenda na michango yangu nataka niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili napenda niwashukuru viongozi wangu wa juu wote ndani ya Serikali na ndani ya Chama cha Mapinduzi ikiwa pamoja na Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo kwa kunisiaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. Lakini vile vile napenda niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiembe Samaki kwa kuelewa kwamba majukumu niliyonayo ni makubwa nikiwa Jimboni Mbunge wao nawawakilisha lakini vile vile ni Naibu Waziri nawawakilisha Watanzania wote. Kwa hivyo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile na mimi nataka nisije nikakosa usingizi leo hii nataka nimshukuru sana mke wangu. Nimshukuru sana mke wangu, niwashukuru sana mabinti zangu wote watatu, Salma, Amne na Safia pamoja na mama yao Nariman. Kwa kweli wamenisiaidia sana katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Vile vile wamenisiaidia kufahamu nina majukumu mazito, muda mwangi ninawaacha peke yao. Nawashukuru sana nawaomba waendelee na jitihada hizo katika kunisiaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo naomba sasa nielekeze hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu na mimi napenda nisaidie kutoa ufanuzi katika hoja mbalimbali. (*Makofi*)

Kwanza naomba nitoe ufanuzi katika hoja ambayo imetolewa ya wastaifu. Kulikuwa kuna hoja tano ndani ya hoja ya wastaifu. Naomba nieleze moja baada ya moja kuzitolea ufanuzi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliotupongeza kwa kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,000 hadi kufika shilingi 50,000, ingawa wengine wamesema kidogo. Lakini nataka niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge haba na haba hujaza kibaba na chururu si ndondo. Sisi kama Serikali tutajitahidi kila hali ya uchumi inapokuwa tuzidi kuongeza pensheni za wastaifu na hilo ndiyo litakuwa jukumu kubwa la Serikali na tutafanya hivyo kwa sababu wastaifu ni Watanzania wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile lilitoka wazo hapa kwamba baada ya mstaifu kufariki basi ni vyema pensheni yake ile ikaendelezwa kwa mkewe kama ni mume au kwa

mumewe kama ni mke. Nataka niseme kwamba pensheni zinalipwa kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu za nchi. Kilichopo pale hivi sasa mstaafu anapofariki na kama amewaacha watoto chini ya miaka 21 pensheni itaendelea kwa kipindi cha miaka mitatu. Lakini kama hakuacha mtoto akifariki pensheni ile ina-*cease* ni wajibu wetu sisi Wabunge, sheria tumeitunga sisi kama kunahitajika mabadiliko yoyote basi Wabunge mtatushauri kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile imetolewa hoja nyingine kwamba kwa nini wastaaafu kwa nini hatuwalipi *slip* ili kuweza kuelewa malipo yao. Nataka niseme tu kwamba kabla ya mwaka 2004 wastaaafu tulikuwa tunawalipa pensheni zao kupitia cheki. Cheki ile ilikuwa inakwenda na *slip* kuweza kutambua mapato yake. Lakini baada tulipoamua kupeleka mifuko mbalimbali kupitia katika *account* zao zile *slip* nazo zilioneekana kwamba sasa hakuna uwiano mkubwa baina kupitisha kwenye *account* zile *slip*. Lakini kwa sababu ya haja hii ya wastaaafu wenyewe wameiona kwamba ni muhimu suala hili tunalitafakari na huenda tukarejesha ile hatua ya kuwapatia *slip* wastaaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine lililokuja na limeelezewa kwa nguvu zaidi. Hoja hizi nataka niseme zimeelezewa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Godfrey Zambi, sasa hivi amezungumza na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Lakini lililoelezewa kwa nguvu zaidi ni lile ambalo Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, amelionyesha hapa *GN* 89. Nataka niseme yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, *GN* 89 ya Juni 29, 2004 ninayo hapa na tumejaribu kuipitia kwa kina. Nataka niseme yafuatayo kwenye *GN* hii. Kwanza *GN* hii ilitolewa tarehe 29 Juni, 2004, wakati huo ilikuwa bado hatujapitisha *Finance Bill*. Kwa hiyo, hiki ni kitegezo kimoja kinachotuashiria kwamba hii siyo *GN* sahihi, siyo *GN* ya kweli. Lakini kama hilo halitoshi *GN* hii inazungumzia kwamba malipo hayo yatarudi nyuma miaka miwili yaani yataanza mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kumbukumbu zake haijawahi kutoa pensheni kwa kuirudisha nyuma miaka miwili zaidi. Kwa hivyo, hicho ni kigezo kingine kinatuonyesha kwamba *GN* hii si halali. Lakini kama haitoshi hiyo, kima cha pensheni kinatolewa, *it is a policy issue*. Inatolewa kupitia hotuba ya Waziri ambayo mwaka ule amesoma. Waziri amesoma hotuba mwaka 2006 nimeipitia hotuba ya Waziri haina kipengele alichoongeza pensheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge aliyeleta hoja hii, sasa hivi kuna utaalam mwingi sana wa kuchenza na *document* kama hatukuwa na tahadhari na kuzingalia *document* hizi kabla hatujaziwasilisha Bungeni, tunaweza tukagombanisha viongozi na wananchi wetu. Nakuombeni sana tuzingalie *document* hizi kabla hatujaziwasilisha katika Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo nataka nilielezee ni suala la MKUKUTA. Ilikuwa hoja hapa kwamba MKUKUTA ulikuwa una gharama na hautekelezeki. Hoja hii imewasilishwa na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji. Nataka niseme tu kwamba MKUKUTA kweli ulikuwa na gharama. Lakini uliweza kutekelezeka kwa *resource* hizo hizo tulizokwa nazo na vigezo muhimu ambavyo MKUKUTA umeviweka ni vingi. Lakini kila siku tukizungumza MKUKUTA hautekelezeki tunazungumza kwa misingi ya mapato ambayo mtu mmoja mmoja anatia mfukoni, si kweli. Mapato peke yake hayakuwa ndiyo vigezo vya MKUKUTA kutekeleza kwake.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA ulikuwa una sekta ya afya, tumetekeleza vya kutosha. MKUKUTA ulikuwa una elimu, tumetekeleza vya kutosha, MKUKUTA ulikuwa una maji, tumetekeleza vya kutosha, hatusemi kwamba tumetekeleza asilimia mia moja. Lakini tumetekeleza, lakini kwa misingi hii ya kwamba kipengele cha mapato hakijaonekana kwamba kimejaza mifuko ya wananchi, ndicho tunachokiona siku zote. Nataka niseme tu, Serikali inaweka njia ya mapato ya mtu mmoja mmoja kuweza kuongezeka. Lakini mtu mwenyewe aliyezungumza hapa ni Mheshimiwa Job Ndugai, mtu mwenyewe anatakiwa kuongeza juhudi asilimia 80 au zaidi ili kipato chake kiweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezuka katika eneo hili ni kwamba hatujafanya tathmini kwa lengo la kwenda katika MKUKUTA namba II, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, tathmini imeshaanza kufanywa. Hivi sasa kuna *workshop* zinaendelea katika Halmashauri zetu, Mwanza, Tabora, jana tu ya Morogoro imefungwa imemalizika. Lengo ni kukusanya maoni juu ya MKUKUTA. Lakini vile vige nataka niseme kwamba warsha hizi zitawashirikisha vige vige *NGO's, CBO's* zitawashirikisha Wabunge, zitawashirikisha vige vige vyama vya siasa ili waweze kutupa maoni katika kutekeleza MKUKUTA namba II. Namwomba Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji ashiriki kikamilifu wakati utakapofika atusaidie maoni yale aliyonayo katika kutekeleza MKUKUTA namba II. Lengo letu tufanikishe kwa sababu nchi ni yetu sote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumziwa ni suala la kuwasaidia sana wakulima hasa katika kuwapatia bei ya mazao. Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim amezungumzia kwa nguvu kidogo, akasema kwamba nje bei za mazao ni kubwa lakini ndani hapa tunawalipa wakulima bei ndogo na akatoa mfano wa karafuu. Nataka niseme kwamba huo ndio uchumi. Kwa nini nasema huo ndio uchumi, kwa sababu tunapozalisha bidhaa zetu hapa ndani na tukazipeleka nje kuna gharama za *packing*, gharama za usafiri na usafirishaji, nani atazifidia. Wanazifidia wale ambao tunawauzia kule nje. (*Makofi*)

Kwa hiyo, zile gharama ndizo zinazofanya kuwe kuna tofauti baina ya bei anayolipwa mkulima na bei tunayouzia kutoka nje na nadhani huo ndio uchumi hasa. Ungeniambia kwamba sisi tunawapa wakulima bei kubwa halafu nje tunauza kwa bei ndogo, pale ungenipa mashaka makubwa sana. Huo sio uchumi, lakini kwa hivi tunavyokwenda nadhani huo ndio uchumi, la msingi hapa ni nini, ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda vyetu vya ndani ambapo vinatengeneza *packing material*. Tulizungumza kwa nguvu kubwa wakati tunazungumzia Wizara ya Viwanda haki ya kuwa na magunia yetu wenyewe ndani yatazalisha na tutawasaidia wakulima wetu kuyanunua magunia yale kwa bei nafuu. Hiyo ndio itakayosaidia. (*Makofi*)

Lakini vige vige badala ya kuuza *raw material* tuuze *semi-finished goods* zitawenza kusaidia katika kutoa pato zuri kwa wakulima wetu. Mimi ninakubali kama ni Serikali, nakubali kama ni Mtanzania, nakubali kama ni mtoto wa mkulima, mkulima aweze kupata bei nzuri. Lakini vige vige sio *at the expense of the Government*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ambayo imezungumziwa kwa nguvu leo asubuhi na mdogo wangu Mheshimiwa Lucy Mayenga na mimi nataka nieleze tu, ndugu yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga, ameeleza hapa kwamba tokea tumeingia madarakani miaka minne sasa...

(*Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, tulichokifanya na kukimaliza angalau asilimia 90 ni nini? Nataka nimwambie tu kwamba ndugu yangu, mdogo wangu Mheshimiwa Lucy, Serikali siku zote ni endelevu. Huwezi ukasema kwamba Serikali ya Benjamin Mkapa imeondoka na mambo yake yote msitekeleze, mje na ya kwenu. *It can't be.* Lazima myaendeleze na resources mnazozitumia ni hizo hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nataka nimuambie sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, ukizungumzia sekta nzima haiwezekani, ukizungumzia sekta ya barabara *it is true*, sisi tutaondoka hatutamaliza kujenga barabara, watakuja wengine, hawatamaliza kujenga barabara, lakini ukizungumza barabara moja moja, zipo tulizozikamilisha. Lakini vile vile nataka nimwambie tu, katika jitihada hizo, ndugu yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga, afungue macho kidogo, Chuo Kikuu Cha Dodoma, tumekianzisha na sasa hivi 90% kinamalizika na mwezi Januari, kesho kutwa, chuo kile kitakuwa kimeshamalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba muendelezo wa shughuli za Serikali, hauwezi ukaishia katika Serikali moja, huo utakuwa si muendelezo wa shughuli za Serikali. Serikali ni lazima inabeba mambo ambayo yameachwa na mwenzake anakwenda nayo na ye ye anaacha yake mwenzake anakwenda nayo, hata kama Serikali inachukuliwa na wapinzani, basi mnapeana vijiti, wanaendeleza. Nazungumzia kwa Serikali ya Marekani, sizungumzii kwa Serikali ya Tanzania. Namuona ndugu yangu Mheshimiwa ibrahim Sanya, amefurahia sana, mfano wa Serikali ya Marekani, sio Serikali ya Tanzania, kwa Tanzania bado kidogo, wapinzani bado kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Job Ndugai, amezungumzia kitu kizuri sana, amezungumzia jinsi ya kuoanisha sekta mbalimbali kwa lengo la kuinua uchumi wetu na kuinua hali za Watanzania. Mimi nataka nikubaliane naye kwa 100%, kwa sababu kama kuna sekta pale ya hoteli, sekta ya utalii, ni lazima sekta ya kilimo cha ndani kiweze kulisha sekta ile, sio suala tena la kwenda kuagiza. Tumezungumza kwa hasira sana, kwa nguvu sana kipindi kilichopita, kuagiza kuku kutoka Afrika ya Kusini, kuagiza kuku kutoka Brazil, lakini sekta ya kilimo ya ndani, lakini juhudhi hizo ili ziweze kufanyika, sisi wenyewe watanzania ni lazima tuongeze jitihada katika uzalishaji. Sekta ya barabara vile vile nayo ina mchangano mkubwa sana katika kumuwezesha mkulima kuweza kufikisha mazao yake katika soko, vile vile sekta nydingine zinaoana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninakubaliana sana na Mheshimiwa Job Ndugai, kwamba tuweze kuoanisha sekta zetu ili tuweze kwenda na nataka nitoe ushauri hapa kwa sekta mbalimbali, waangalie ndani zaidi kuliko kuangalia nje; leo baadhi ya mahoteli yanaagiza vifaranga kutoka nje, waangalie ndani zaidi, wakisha *ku-exhaust* ndani ndio watafute nje. Mimi ninataka tu niseme kwamba maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tumeyapokea, na ninataka niahidi kwamba yametusaidia sana na ninataka niungane mkono na Mheshimiwa Waziri wangu katika kuyatekeleza maoni haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hoja hizo, naomba tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa ya kujiunga na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, katika kupokea ushauri na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, ambavvyo vimekuwa kwa maandishi na vile vile kwa kuzungumza hapa Bungeni. (*Makofi*)

Naanza kwa kuunga hoja mkono, lakini kwa niaba ya wananchi wa Meru, ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa imani yao, kwa mapenzi yao kwangu, na kwa ushirikiano wao mkubwa sana. Kata ya Leguruki, Ngarenanyuki, King'ori, Kikatiti, Maji ya Chai, Mji mdogo wa Usa, Makiba, Maroroni, Mbuguni, ninawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi ikiongozwa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa ushauri wao, kwa mchanganuo wao, kwa mawazo yao, naishukuru Kambi ya Upinzani kwa taarifa yao iliyowasilishwa na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, wamesema mambo mazuri japo moja lilinipa kizunguzungu lile la MKUKUTA, lakini si hoja. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushauri na mawazo makubwa na mazuri ambayo yametolewa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na sasa nomba nianze kujibu baadhi ya hoja hizo, zitakuwa sio nyingi lakini nianze na Kambi ya Upinzani, kuhusu lile la *Special EPA Stock* kwamba tunakumbuka chanzo cha *External Payments Areas Account (EPA)*, kwamba chanzo chake, chimbuko lake ni miaka ya 1980 ya kwenye uchumi wetu kwamba miaka ile uchumi wetu ulikuwa dhaifu, hatukuwa na fedha za kigeni na kwa hiyo, wenye viwanda, wafanyakishara, kwa dhamana ya Serikali wakaendelea kuagiza mali na dhamana ya Serikali ilikuwa ni kwamba Serikali ingewalipa wale ambao wangeleta vifaa nchini ili mradi wale ambao wangekuwa wameagiza wamelipa kwa pesa za Tanzania kwenye *account* maalum kwenye iliyokuwa Benki ya Biashara (*National Bank of Commerce*).

Mheshimiwa Spika, ilipofika Septemba 1997, Benki ile ilirekebishwa, ilivunjwa na akaunti ile ikahamishiwa Benki Kuu na Benki Kuu akawa ndio wakala kwa niaba ya Serikali kwa kulipa yale madeni pale ambapo wale ambao wangedai wangetokea. Lakini jinsi miaka ilivyopita, fedha zile ambazo ni za kigeni, ukilinganisha na sarafu ya Tanzania ambayo ilikuwa inapoteza thamani, ziliikuwa zinaanza kuzalisha thamani kubwa ya vitabuni kuliko ya awali na kwa hiyo, zile hati fungani zilizotolewa mwaka 2005/2006, zinatokana na tofauti kati ya thamani ya awali na thamani ya 2005; kingereza ni *difference in exchange*. Kwa mfano, miaka ya 1980, dola kwa shilingi ilikuwa ni shilingi mathalani tisa, na kwa hiyo dola 1,000 maana yake ni kwamba kwa shilingi za Tanzania ni shilingi 9,000/= tu. Kufikia mwaka 2005/2006, dola zile zile 1,000 kwenye vitabu vya Benki Kuu sio tena shilingi 9,000/= ni shilingi 900,000/= na kwa sababu yale madeni yalikuwa makubwa, kwa hiyo, ile akaunti ikawa na yenye imekuwa kubwa kwa fedha za Tanzania, lakini ni deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ikakubali Benki Kuu, itoe Hati Fungani ambazo hazina riba za miaka 45, ambazo zingeiva mwaka 2050. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, alipokagua vitabu vya Benki Kuu, kwenye ripoti yake akatoa taarifa kwamba kufanya hivyo hakuendani na *International Financial Reporting Standards*, kwa hiyo, ni lazima irekebishwe. Serikali ikakubali, kwa hiyo, mwaka jana Serikali imekubali Hati Fungani nyengine ya miaka 15 ambayo itakuwa na riba ya 6% na kwa hiyo, thamani ile ambayo ilikuwa kwenye Hati Fungani za nyuma, sasa italipwa ndani ya miaka 15. Sasa cha kusisitiza hapa, ni kwamba hapa hatuzungumzii fedha taslim, tunazungumzia thamani ambayo imetokana na kupungua kwa thamani ya shilingi yetu ukilinganisha na fedha za kigeni ambazo ziliikuwa kwenye ile akaunti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hasara ambayo inaonekana kwenye vitabu vya Benki Kuu. Hesabu za Benki Kuu zina sarafu za aina mbili, kwanza shilingi ya Tanzania lakini vile vile fedha za kigeni ambazo ndizo tunatunzia fedha za akiba za nchi na kila miezi mitatu, miezi sita, baada ya mwaka mmoja, kunakuwa na kuthaminisha zile fedha zetu za kigeni. Kwa hiyo,

ikiwa fedha ya Tanzania imepoteza thamani, kwenye vitabu vyetu vya Benki Kuu, kwa sababu vinaandikwa kwa shilingi yetu ya Tanzania, itaonesha kwamba kuna hasara. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mnachosema kwamba kuna hasara, ni kweli inaoneshwa kwamba ni hasara, lakini sio hasara ya fedha taslimu; ni thamani ya fedha inayotokana na tofauti ya hizi sarafu za kigeni na fedha yetu ya Tanzania. Ikiwa hali inabadilika kwamba sasa fedha yetu thamani yake ukilinganisha na fedha za kigeni imeboreka, basi kwenye akaunti hiyo hiyo badala ya kuonesha kwamba ni hasara, unaona kwamba inakuwa ni faida na niseme nimalizie katika hili kwamba hakuna fedha taslimu ambazo zimeshalipwa kutoka kwenye hii akaunti ya *EPA*, toka agizo hili lilipotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili inahusu hoja ambayo imetolewa na Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, inahusu kuweko na akaunti nyingi kwenye Halmashauri zetu. Ni kweli, ni nyingi tunakiri na hali hiyo sio hali nzuri, imezungumziwa pia na Mheshimiwa Athumani Janguo, na naomba niseme na nitaarifu kwamba tayari Serikali Kuu, imeshaanza kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo. La kwanza ni kuanzisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani, ambayo itatusaidia katika kusimamia matumizi na uandikaji wa vitabu vya hesabu vya Halmashauri zetu, ambalo ni tatizo kubwa. Lakini la pili ni kuondoka kwenye jinsi ambavyo vitabu vya Halmashauri na Serikali Kuu vile vile, zinatengeneza vitabu vya mahesabu sasa hivi na kuingia kwenye viwango vya Kimataifa na nilijibu swali hapa wiki hii kuhusu *International Public Sector Accounting Standard* na kwa namna hiyo, tunaamini hapo tutakapokuwa tumekamilisha mazoezi haya mawili pamoja na lile la kuongezea wataalamu wetu wa taaluma ya kihasibu uwezo zaidi wa kumudu usimamizi wa fedha, sisi tunaamini kwamba tutakuwa tumepiga hatua. Lakini kama Kamati ilivyosema, ni kwele akaunti 10,000 zilifungwa lakini bado ni kweli Halmashauri zetu karibu zote zina idadi ya akaunti nyingi za Benki kuliko ambavyo inashauriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu Benki ya Posta na inahusu umuhimu wa kuiimarisha ile Benki; Rai hii imetolewa na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana naye na ndio sababu mwaka huu wa 2009/2010 Benki ya Posta, imetengewa shilingi bilioni moja. Lakini niseme kwamba sio mwaka huu ndio mwanzo wa kuirekebisha hii Benki, kumekuwa na hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa. Kwa mfano, moja ni kuwasafishia mizania yao kwa Serikali kuwalipia madeni yao, lakini la pili vile vile ni kuwaachia gawio ambalo kwa kawaida wangelipa Serikali Kuu, Mfuko Mkuu wa Hazina na kukubaliana nao kutumia zile fedha kuiimarisha Benki ile. Lakini niseme kwamba Benki hii haiko kwenye Wilaya zote za nchi yetu, hiyo sio sahihi; kwa sababu, pamoja na yale matawi 27 yaliyotajwa ambayo sasa moja limeongezeka na kuwa 28, Benki hii ya Posta ina vituo vya kutoa huduma za fedha kwenye Posta zetu na ziko 115. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa kweli unaweza kusema kwa usahihi kabisa kwamba Benki ya Posta, ina matawi 28 jumlisha na 115, kwa hiyo, ina matawi 143. Nitakachokiri hapa ni kweli, ukiingia mle, hayako kwenye kiwango ambacho ungetegemea lile tawi liwe, lakini mimi ninaweza kusema hapa kwamba juhudzi za kuboresha matawi haya na kuiimarisha benki hii zinaendelea, maana Serikali inajua kwamba Benki hii, zaidi kuliko labda Benki nyingine nyingi, ndio benki ambayo imefika zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, anaulizia ni kwa nini Serikali haijaruhusu matumizi ya Hati Fungani za Majiji na Miji kwa ajili ya kujiongezea kipato kwa njia ya mikopo, yani *Municipal Bonds*?

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba hii ni njia nzuri ambayo inaweza kutumika na najua kwamba kuna juhudhi ambazo zimefanyika kutazama kama mazingira yetu yanaturuhusu, mazingira ya miji yetu, maana tunazo aina mbili za Hati Fungani za *Municipal Bonds*. Unaweza kutoa Hati Fungani ambazo zinategemea ule mradi wenyewe au ambazo ni *Revenue Bonds* au vile vile ukakopa kwa kutumia uwezo wa Serikali kukopa, *General Obligation Bonds*. Lakini kwa vyovoyote vile, hatimaye Benki Kuu, inatoa dhamana kwa ukopaji ule. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaposema kwamba turuhusu Manispaa zetu zikope kupitia Hati Fungani, tunachosema ni kwamba na Serikali Kuu iwe tayari kudhamini hiyo mikopo. Sasa hilo ni moja ya mambo ambayo sasa hivi yanatazamwa na pale tutakaporidhika kwamba ndiyo, tumeshamaliza njia nyingine ambazo zinaweza kuwapatia vipato Manispaa zetu, basi nina hakika kwamba na njia hii itatumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mengine mengi ambayo yangehitaji kuyazungumzia, lakini ninaomba nimalizie kwa mara nyingine kukushukuru kwa muda ulionipa na nimalize kwa kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana michango ilikuwa mingi, licha ya kwamba muda ulikuwa kidogo lakini michango ya maandishi ilikuwa ni mingi sana. (*Makofi*)

Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge wa Viti Maalum, alichangia kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mohamed Amour Chamboh, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wangu na Mheshimiwa Jeremia Sumari, Naibu Waziri pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia Bajeti hii kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Hadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Guido Sigonda, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Benedict Ole-Nyangoro, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mhonga Ruhanya, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Kama kuna mtu nimemsahau, anaweza akaleta tukatangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujibu, ningeomba kwamba asubuhi wakati nataja nchi na mashirika yanayoisaidia Tanzania kwa bahati mbaya sana nililisahau shirika ambalo ni muhimu sana kwetu, *International Monetary Fund (IMF)*. Kwa hiyo, katika ile orodha kwenye *Hansard*, ningeomba *International Monetary Fund* iwe mwanzo mwanzo, baada ya *World Bank* ije *IMF*. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyechangia, nilisema Chambo, ni Mohammed Chomboh. Samahani, kwa hiyo *hansard* irekodi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, michango ilikuwa mingi sana, waliozungumza sio wengi lakini waliochangia kwa maandishi ni wengi sana na michango ni mingi sana. Kwa hiyo, itakuwa ni vigumu sana kumtaja kila mtu alichangia nini, ila nitajitahidi tu kujibu yale ambayo ni ya kiujumla. La kwanza kabisa ni hili la 1% ya utafiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haikudharau maagizo ya Marais wa Afrika wala agizo la Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Baada ya agizo la Mheshimiwa Rais, Serikali ililifanyia kazi, lakini tatizo tulilolipata ni kwamba mpaka hivi ninayozungumza hakuna chombo kimoja ambacho kinashughulikia utafiti hapa Tanzania, pamoja na kwamba kuna *COSTECH*, lakini sio *COSTECH* peke yake; viko vyombo vimetapakaa, Mawizara, Mavyuo Makuu na wengine. Sasa tatizo linakuja kwamba kama mavyombo haya yote haya yanafanya utafiti, tutakapopanga 1%, tuipeleke wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako niseme tu, kwa mfano Wizara ya Fedha, tuna aina fulani ya utafiti ambayo kwa mwaka inagharimu karibu bilioni 7.6 na hii iko ndani ya Bajeti. Wizara ya Kilimo na Chakula, jumla ya maeneo yote ya *research* ukichukua *research* za mazao, *research* za mbegu, *research* za nini, kwa jumla yake ndani ya Bajeti ya kilimo kuna jumla ya shilingi bilioni 27.66, Wizara ya Viwanda na Biashara, kuna jumla ya shilingi bilioni 4.9, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, wana jumla ya shilingi bilioni 156, hii ukijumlisha na *University* na vitu vingine. (*Makofii*)

Wizara ya Ardhi, ina shilingi milioni 738.7, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Wizara ya Madini, Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia ndio kuna *COSTECH* huko, ambako wenyewe wana shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, ukiiangalia Bajeti hii nzima ni kwamba pesa nyingi hasa za utafiti ambazo ziko ndani ya Bajeti, haziko *COSTECH*, ziko katika Wizara nyingine na maeneo mengine. Sasa tulichofanya Serikali ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa bahati nzuri ameniagiza tutafute kwa kina Wizara zote za Serikali, ni kiasi gani cha pesa katika Wizara zao kimepangwa kwa ajili ya utafiti. Sasa tukishapata ile, ndio tutaweza kujua kwamba je, zile zote *tizi-pull* pamoja ili tuwe na eneo moja ambako ndio utafiti unafanyika na kwa hiyo, ili tuweze kupata kiasi kile ambacho tunapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hizi nilizozitaja zinakuja jumla ya shilingi 305,727,271,037/=, pesa ambazo ziko ndani ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 katika maeneo tofauti, katika akaunti tofauti, katika Wizara tofauti. Ukichukua *GDP* kwa mwaka 2008/2009, ya trilioni 31.1 unapata 0.98%. Kwa hiyo, hata kabla hatujasema kwamba chombo fulani ndio kiwe kinafanya utafiti, tayari tuna 1%, maana hizi pesa zote ambazo tumezitenga tayari ni 0.98% ambayo ni karibu 1%. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba ukienda kwenye Bajeti yetu, huwezi kukuta mahali maalum ambapo tumeweka 1% kwa ajili ya utafiti, 1% unaipata katika Mawizara kadhaa. Kwa hiyo, baada ya zoezi ambalo limeagizwa na Mheshimiwa Waziri

Mkuu, nataka kukuhakikishia kwamba tutakuja na mfumo wa kwamba 1% itakaa kwenye Idara gani, lakini hiyo ni Serikali tutakaa chini na kukubaliana. Ni matumaini yangu kwamba wale ambao walikuwa na wasiwasi kwamba hakuna pesa za *research* sasa mtakuwa mmeputa jibu na kwamba hatukukaidi agizo la Mheshimiwa Rais. Tumelifanya kazi kwa kina sana na tutaendelea kulifanya kazi mpaka tuje tupate pesa hizi zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba mimi ambaye ninazungumza nao, *COSTECH* wanasema ni wao ndio wanafanya *research*, lakini ukizungumza na Chuo Kikuu, wanasema hapana, sisi tuna *line* yetu ya *research*. Kwa hiyo, ni Wizara ya Elimu na tutafika mahala kwa sababu ni Serikali tutakubaliana kwamba *okey*, kama *research* ni 1%, basi hizi pesa sasa ziwekwe wapi. Lakini kwa sasa hivi siwezi kusema kwamba pesa hizi 1% zote ziko katika Wizara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala na kwa sababu pia limechangiwa na wengi, wengi ambao wamezungumza hapa mmeyasikia yale waliyochangia. Lakini wengine ambao wamechangia kwa maandishi hamkuyasikia yale ambayo wamechangia. Kuna suala la *TIB*, mtaji wa *TIB*, dirisha la kilimo na kuanzisha Benki ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninataka kukuhakikishia kwamba hili limeshughulikiwa kikamilifu. Mtaji unaotakiwa ku-*capitalise TIB* kwa taarifa ya wataalam, ni shilingi bilioni 140. Kwa sasa hivi tumefikisha bilioni 50 tutaendelea na utaratibu tuliuopanga mpaka baadaye tuje tufikishe bilioni 140. Hii haiwezi kuchukua mwaka mmoja itabidi ichukue muda mpaka tuje tufikie hapo tutapotaka kufika.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi. Kwanza nataka kuwahakikishia kwamba tuna ushirikiano mzuri kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi na hasa kati ya Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Muungano na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Tunashirikiana kupeana taarifa, tunashirikiana kupeana mbinu za kisasa, tunashirikiana kufundishana mambo ya *information technology* na Bajeti ya mwaka huu Waziri mwenyewe Mheshimiwa Dr. Mwinyi Haji Makame, alikuja Dar es Salaam tutakaa siku nzima na wataalam wake wa Bajeti waliyopanga Zanzibar na bajeti yetu vinashabihiana na bajeti yetu kwa namna kubwa sana baada ya ushirikiano ule. (*Makofi*)

Tunataka kuwahakikishia kwamba tumeanza ushirikiana ambao ni mzuri na nina hakika kwamba katika muda mfupi ujao pengine wenzetu nao bajeti yao inawezekana ikatayarishwa kwa namna sisi tunaitayarisha.

Katika hili nizungumzie hili pia la *Joint Finance Commission*. Ni kweli kwamba taarifa ya *Commission* au Tume ilikuja Serikalini 2006, taarifa ile ililetwa kwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Muungano ikapeleka nakala kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni kweli pia kwamba tumekuwa tukieleza kwa miaka kadhaa, lakini nataka kukuhakikishia kwamba kikao cha mwisho ambacho Mwenyekiti wake alikuwa Makamu wa Rais tulijadili suala hili kwa kina kama Mawaziri wa pande zote mbili na Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa maelekezo kwa pande zote mbili na akatupa muda maalum. Muda maalum tuwe tumemaliza suala hili ili maamuzi yaweze kufanyika.

Kwa hiyo, Shemeji yangu Mheshimiwa Maulidah, nataka nikuhakikishie kwamba na kwa sababu hutaki kutoa shilingi, kwa hiyo sina matatizo sana nataka kukuhakikishia kwamba

tulipo sasa ni pazuri. Mkutano ulifanyika mwezi wa Tano, nadhani hakuitisha kikao kwa sababu ya kikao hiki cha Bunge nina hakika baada tu ya Bunge, inawezekana Mheshimiwa Makamu wa Rais akaitisha kikao cha pande zote mbili. Pande zote mbili tumeshawapa wataalam wetu kufanya kazi. Nadhani kikao hicho kwa upande wa Tanzania Bara au kwa upande wa Serikali ya Muungano tunaongozwa na Waziri Mkuu na kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi inaongozwa na Waziri Kiongozi. Lakini sasa kuna Makamu wa Rais ambaye yuko juu ya wote hao, yeye ndiyo Mwenyekiti na hiyo imesaidia sana kuweza kusukuma maamuzi fulani ambayo pengine yalikuwa yakichelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba hili litafika hatima yake mapema iwezekanavyo sitaki niji-*commit* kwa sababu Mwenyekiti wa kikao hiki ni bosí wangu. Sitaki niji-*commit* kwamba ifikapo tarehe fulani tutakuwa tumemaliza, nitakuwa naenda njé kidogo ya utaratibu. Lakini naweza nikasema kwamba haitachukua muda mrefu kama huu muda ambao tumechukua miaka mitatu kushughulikia suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie kwa kina ni hili la Mkulo, kutoroka vikao na Mawaziri wa Zanzibar. Vikao baina ya Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Muungano vina utaratibu wake.

Kuna Kamati za wataalam, kuna Kamati za Makatibu Wakuu, kuna Kamati za Mawaziri, kuna Kamati zile za Mawaziri kumpa *briefing* kwa sisi huku Serikali ya Muungano kumpa *briefing* Waziri Mkuu, kuna vikao vya kumpa *briefing* Makamu wa Rais. Hakuna mtu mmoja ambaye anaweza kusema kwa sababu hayuko kwenye kikao basi maamuzi hayawesi yakafanyika. Mbaya zaidi kwamba kikao kile ni cha Makamu wa Rais, kikao kile kina Waziri Mkuu, kikao kile kina Waziri Kiongozi wa Zanzibar, haiwezekani Waziri wa Tanzania mmoja akwamishe maamuzi ya kikao kile. (*Makofi*)

Kama kuna kitu kinakwama hakikukwamishwa na mie kinakuwa kimekwamishwa na mambo mengine. Katika kipindi cha takriban mwaka mmoja na nusu ambacho mimi nimekuwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kumekuwepo na vikao vingi vya wataalam, lakini kumekuwepo na vikao vitatu tu, vilivyoendeshwa na Makamu wa Rais, akiwepo Waziri Mkuu na akiwepo Waziri Kiongozi.

Vikao viwili, niliwakilishwa na Naibu Mawaziri na kwa sababu Naibu Waziri kateuliwa na Rais, mimi nimempa maagizo katika kikao hiki wataalam wamesema hivi, kaseme haya na haya, huwezi kusema kwamba mimi sikuhudhuria kikao. Kwa hiyo hata vile viwili ambavyo niliwakilishwa na Manaibu Waziri wangu *unless* mtu aseme kwamba Manaibu Waziri hawa sasa hawana kazi. Kwa hiyo, katika vikao vile viwili pia niliwakilishwa sawasawa na Naibu Waziri Sumari, ambaye alihudhuria vikao vyote viwili alikuja akanipa *briefing* na katika ile *briefing* hakuna kilichozungumzwa pale kwamba kilitaka *specific decision* ya Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba kwa sababu Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Muungano hakuwepo basi maamuzi hayakufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka kidogo kwenda ndani kidogo, mazingira ya tuhuma kumhusu Mkulo, yalitokea baada ya Waziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuzungumza ndani ya Baraza la Wawakilishi kuhusu *petrol* na gesi asilia kwamba hivi si vitu vya Muungano. Sasa Waziri wa Fedha na Uchumi sio mjumbe wa Kamati ya Mawaziri ya Nishati, kuna Mawaziri wa Nishati Zanzibar, kuna Mawaziri wa Nishati Serikali ya Muungano wa Tanzania na hawa wamekuwa wakifanya vikao na tunazo kumbukumbu

hakuna kumbukumbu hata moja inayozungumzia kwamba kwa sababu Mkulo hakuwepo basi hawakufanya maamuzi. Kwa hiyo, nataka kukanusha kwa nguvu zangu zote kwamba si kweli kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania alitoroka vikao.

Nilihudhuria vikao vyote vinavyotakiwa kuhudhuriwa na kimoja nilihudhuria mimi mwenyewe na kile ambacho nilihudhuria mimi mwenyewe ndiyo hiki ambacho nimetoa taarifa kwamba Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa *specific instructions* kwa Mawaziri si Waziri wa Fedha pekee yake kile kikao kina Mawaziri wengi, kwa Mawaziri wote wanaounda ile Kamati. Kwamba wawe wametekeleza masuala fulani fulani ifikapo tarehe fulani. (*Makofi*)

Sasa kwa hiyo kwanza nakanusha, kwamba mimi sikuhusika kukwamisha mafuta na gesi asilia kwamba isiwe ya muungano sio husika kwa sababu sikukaa hicho kikao na sikuhusika pia kukwamisha maamuzi fulani eti aliye kwenda kwenye kile kikao ni Naibu Waziri wangu kateuliwa na Rais, kapewa majukumu, mimi ninapokuwa sipo, Manaibu Waziri wangu wakienda kuhudhuria kikao ni halali kabisa kama vile mimi mwenyewe nimehudhuria kikao hicho. (*Makofi*)

Kuna suala la kunusuru uchumi, na kwamba kuna trillion 1.7 kwamba hazionekani kwenye Bajeti. Ni kweli ile trilioni 1.7 sio zote ziko kwenye bajeti nyingi ya zile pesa kwanza ni *rescue package* ambayo tumeipata kutoka mashirika ya kifedha.

- (i) *IMF* wametupa dola milioni 328 kwa ajili ya ku-support kwenye *balance of payments*.
- (ii) *World Bank* wametupa pesa nyingi nyingi tu kwa ajili ya kilimo na masuala mengine.

Upungufu wa mapato ya Serikali ambao ni sawa na IMF walituruhusu kwamba tungeweza tukapata 1.2 ya GDP kwa mwaka 2008/2009, ambayo ni sawa sawa ni shilingi bilioni 323 na kwa mwaka 2009/2010 kuna shilingi 505 bilioni ambayo ni sawasawa na asilimia 1.6. Pesa tasilimu ambazo tumeziweka katika ule mpango ambao Mheshimiwa Rais aliusoma, kwa wazee wa Dodoma wa tarehe 10 ni shilingi bilioni 21.6 hizo ndizo pesa tasilimu ambazo zitatolewa na Hazina na hizo ziko kwenye bajeti. Hizi nyingine zote hizi ni ama una *guarantee*, sasa uki-*guarantee*, jamani najua kuna *guarantee*, ambazo zimetolewa na najua kwamba kuna malalamiko ya hapa na pale kwamba hamna *guarantee* inawezekana wasilipe.

Mheshimiwea Spika, lakini dhamana hizi tunazozitoa sio pesa tasilimu, mabenki yale yaliyotoa pesa kwa ajili ya mazao na hasa pamba, kahawa, maua Arusha kule na korosh. Wale waliochukua pesa kwenda kununua mazao yale walinunua kwa bei ya juu, walipotaka kuuza bei imeshuka. Kwa hiyo, wakiuza wanauzu kwa hasara wakashindwa kulipa zile fedha walizokopa.

Yale mabenki yanasema sisi *unless Serikali mnatu-guarantee* kwamba hawa watakuja kulipa, sisi hatuwezi kutoa mikopo mingine. Sasa Serikali isipojiingiza kufanya hiyo, maana yake ni kwamba pamba haitanunuliwa, kahawa haitanunuliwa na mazao mengine hayatanunuliwa. Kwa hiyo dhamana sio pesa ambazo unazo mfukoni ni *contingent liability* tunatoa guarantee kwa benki leo kumhakikishia kwamba kama katika muda wa miaka miwili huyu atakuwa amelipa basi asilimia 50 ya deni hili Serikali italilipa asilimia 50 itakuwa hasara kwa ile benki. Kwa hiyo, *cash flow* ya pesa kutoka itakuwa ni baada ya miaka miwili.

Kati ya leo na 24 *month to come*, huwezi kuziona hizo pesa ndani ya bajeti ya Mkulo, au ndani ya bajeti ya kilimo. natumaini kwamba limeelewaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa sababu Manaibu wangu walisaidia kujibu hoja fulani fulani nilifikiri kwamba hizo za ujumla nizijibu mimi mwenyewe lakini kama kuna mengine ambayo yatajitokeza wakati wa kupitia vifungu, naweza nikatoa *clarifications* hapa na pale. Nashukuru sana kwa michango mingi tulioipata. Nashukuru kwamba mimi ndiyo niliyeanzisha *debate* hii tarehe 11 nashukuru kwamba leo nahitimisha *debate*, ni matumaini yangu kwamba kwa sababu wengine wote wamepewa basi yule muandaaji naye mtampa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Uchumi, Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi amekwishaaitoa na imeungwa mkono na sasa Katibu atatuongoza kwenye utaratibu wa Kanuni ya 100.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 34 - HAZINA**

Kifungu 2001 - <i>Government Budget Division</i> .....Sh. 440,084,860,000
Kifungu 2002 - <i>Policy and Research</i> .....Sh. 148,476,396,000
Kifungu 2003 - <i>Treasury Registrar</i> .....Sh. 0
Kifungu 4001 - <i>External Finance</i> .....Sh. 6,399,821,000
Kifungu 7001 - <i>Poverty Eradication and Empowerment</i> .....Sh. 2,651,417,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 23 - MHASIBU MKUU**

Kifungu 3001 - <i>Public Debt Management</i> .....Sh. 2,284,271,200
Kifungu 3002 - <i>Expenditure Management</i> .....Sh. 2,471,840,000
Kifungu 3003 - <i>Financial Management</i> .....Sh. 82,001,152,300
Kifungu 3004 - <i>Systems and Internal Audit</i> .....Sh. 5,391,618,750
Kifungu 3005 - <i>Sub Treasury Arusha</i> .....Sh. 247,325,000
Kifungu 3006 - <i>Sub Treasury Coast</i> .....Sh. 209,457,200
Kifungu 3007 - <i>Sub Treasury Dodoma</i> .....Sh. 265,766,400

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3008 - *Sub Treasury Iringa*.....Sh.217,400,000

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wakati Kambi ya Upinzani inatoa maoni yake tulihoji juu ya kasima namba 22 9900 ambayo inasomeka kama ni ushauri wa kitaalam ambayo itatumia karibu bilioni 1.9 tuliona matumizi hayo ni makubwa na tuliomba...

**MWENYEKITI:** Unazungumzia wapi hapo sasa kwa sababu tuko kwenye mikao hii *sub treasury*. Labda hiyo unayozungumzia ni *sub treasury* ya Iringa ambayo sidhani kama ni suala la kitaifa sijui.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya  
Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3009 - <i>Sub Treasury</i> Kagera.....	Sh. 217,807,000
Kifungu 3010- <i>Sub Treasury</i> Kigoma.....	Sh. 216,444,100
Kifungu 3011 - <i>Sub Treasury</i> Kilimanjaro.....	Sh. 229,616,000
Kifungu 3012 - <i>Sub Treasury</i> Lindi.....	Sh. 234,635,200
Kifungu 3013 - <i>Sub Treasury</i> Mara.....	Sh. 226,532,000
Kifungu 3014 - <i>Sub Treasury</i> Mbeya.....	Sh. 230,129,000
Kifungu 3015- <i>Sub Treasury</i> Morogoro.....	Sh. 271,572,000
Kifungu 3016 - <i>Sub Treasury</i> Mtwara.....	Sh. 223,726,000
Kifungu 3017 - <i>Sub Treasury</i> Mwanza.....	Sh. 235,847,000
Kifungu 3018 - <i>Sub Treasury</i> Rukwa.....	Sh. 240,717,500
Kifungu 3019 - <i>Sub Treasury</i> Ruvuma.....	Sh. 225,444,400
Kifungu 3020 - <i>Sub Treasury</i> Shinyanga.....	Sh. 222,744,000
Kifungu 3021 - <i>Sub Treasury</i> Singida.....	Sh. 224,644,750
Kifungu 3022 - <i>Sub Treasury</i> Tabora.....	Sh. 238,880,400
Kifungu 3023 - <i>Sub Treasury</i> Tanga.....	Sh. 220,718,400
Kifungu 3024 - <i>Sub Treasury</i> Manyara.....	Sh. 223,889,400
Kifungu 7001 - <i>Pension and Gratuity</i> .....	Sh. 841,503,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote*)

#### FUNGU 45 - OFISI YA UKAGUZI

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Sh.12,166,023,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.858,430,000
Kifungu 1003 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.139,590,000
Kifungu 1004 - <i>Ministerial Audit Division</i> .....	Sh.875,570,000
Kifungu 1005 - <i>Regional and Local Government Audit Division</i> .....	Sh.1,343,005,000
Kifungu 1006 - <i>Value For Money Audit Division</i> .....	Sh.505,970,000
Kifungu 1007 - <i>Treasury Audit Division</i> .....	Sh.807,900,000
Kifungu 1008 - <i>Technical Support Research and Consultant</i> .....	Sh. 584,150,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya mabadiliko yoyote*)

*Bunge Zima Bila*

## **FUNGU 50 - WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**

Kifungu 1001 - *Administration and General.....Sh. 9,128,338,600*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mshahara wa Waziri. Wakati nachangia kwa maandishi asubuhi nililuzia juu ya hiyo *stimulus package* Serikali ilikuwa imeahidi kwamba italipia mashirika yaliyokuwa yamenunua kahawa madeni hayo kwenye benki sasa nimesikia Waziri amesema watatoa dhamana lakini kwa mkao wa Kagera msimu wa kahawa ulianza tangu mwezi wa tano.

Kwa hiyo, mashirika ya kununua kahawa yanasuasua kwa sababu mabenki wamewanyima hela, kwa sababu inaelekea hata benki kuu hawajasaini mkataba wowote ule na mabenki yaliyokuwa yanatoa fedha kwa makampuni yanayonunua kahawa kama *KCU, KDCU* na wao wanaokobo na kama *BUKOP*, nataka kujuwa sasa msimu unakaribia naomba ufanuzi ni lini sasa hizo hela zitatolewa kusudi hizo kahawa ziweze kununuliwa na Watanzania wakazi wa mkao wa Kagera waweze kufaidika na mpango huu?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mshashu, ni kweli ametuandikia na ningependa kumpa majibu kwamba nilitaja shilingi bilioni 21.9 ambazo ndizo zitatumika kama cash kwa ajili ya hizo pamba na kahawa korosho na maua. Wakati anazungumza tarehe 10 Juni, maombi tuliyokuwa tumeyapata yalikuwa hiyo 21.9 bilioni. Sasa baada ya kujuwa kwamba sasa Serikali imekubali, Benki Kuu sasa imepokea maombi zaidi kuliko yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa wakati ule.

Sasa kwa vyotevye vile usingeweza kulipa madeni mara mbili kuliko tuliyokuwa tumeabajeti, sasa benki kuu wamekamilisha mchakato. Na nataka kukuhakikishia kwamba wakati wowote sasa na mimi nimeletewa taarifa leo ya mchakato ulikofikia wakati wowote Benki Kuu wataruhusu mabenki kupata zile pesa. Kwa hiyo, zoezi hilo litaanza wakati wowote kuanzia sasa. (*Makofi*)

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilichangia kwa maandishi na nilizungumzia kuhusu wastaafu wa Afrika Mashariki na nilimtaja Mzee wangu Fahaki Faswaha Juma Nasibu ambaye alikuwa mfanyakazi wa Afrika Mashariki, jina lake lilitoka kwenye magazeti, watusika wakaitwa na wakachukua hatua zote lakini hadi leo hajalipwa.

Wamehangai sana mpaka mwisho wakanitumia mimi Mbunge wao kufuatilia suala hilo. Walinipa nyaraka nimezileta Wizarani lakini hadi leo hawajapata malipo hayo wala sijapata maelezo yoyote. Mheshimiwa waziri naomba anipe ufanuzi kuhusu malipo hayo.

**MWENYEKITI:** Nadhani hili ni la Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee ndiye huwa anazama sana kwenye mambo haya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumesoma mchango wa Mheshimiwa Ameir Ali Ameir na tumeona hayo maelezo ambayo ametuelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme tu kwamba kuchapishwa katika gazeti ni jambo lingine na malipo ni jambo lingine. Nasema ni jambo lingine kwa sababu gani? Ni kwa sababu lazima faili la mhusika liweze kupatikana, tumejaribu sana kuhangainika kutafuta faili la mhusika na bado hatujachoka tunaendelea kulitafuta.

Nataka niseme tu kwamba siyo kesi ya Mheshimiwa Ameir tu peke yake, kesi kama hizi tunazo mbili au tatu lakini bado hatujachoka tunazifanya kazi na tukishakamilisha tu tutaweza kumlipa mafao yake kama mwenyewe alivyosema. Hivyo vielelezo alivyonavyo mkononi nataka nieleze tu kwamba sasa hivi utaalamu umekuwa mkubwa sana unaweza, ukapewa nyaraka ukazifanya kazi zikaja zikagundulika baadaye na *Auditors* kwamba zile nyaraka ziliwa ni feki. Tutakapolipata faili lake tutajaribu kutafuta kila njia ili tuweze kumpa mafao yake kama kweli alikuwa ni mfanyakazi wa Afrika Mashariki.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sihitaji mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini ninataka ufanuzi kidogo.

Sisi Ludewa tuna tawi moja tu la Benki ya *NMB* Ludewa Mjini, haitoshi, huko nyuma tulikuwa na tawi lingine Malangali ambalo lilifungwa lakini kuanzia mwaka juzi tumeanza kuomba *NMB* wafungue tawi Malangali kwa sababu nyingi sana ambazo ni pamoja na kuanzishwa kwa Soko la Kimataifa pale Malangali. Lakini vile vile kuna kituo kikubwa cha ununuzi wa Mahindi kwa watu wa *SGR*. Lakini vilevile si mbali kutoka Liganga kwa hiyo kuna ukuaji mkubwa wa huduma.

Kwa hiyo, tuliomba tupewe tawi pale, *NMB* walikubali wakasema *no problem* tumeingizwa kwenye orodha tunakuja kama watatu hivi. Lakini nikaambishiwa kwamba uwasiliane na *Treasury* hususani Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa sababu ndiyo wana *regulate* wapi matawi ya benki yapelekwe. Sasa nimeona labda niulize hapa kama hilo ni kweli Mheshimiwa Mkulo unawenza ukatufikiria kwani tunahitaji sana tawi la Benki Malangali.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swalii la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi.

Kwanza nakiri kwamba tulizungumza naye na nilimsaidia, *Managing Director* wa *NMB* alimtuma *Branch Manager* wa Iringa kwenda kufanya huo utafiti na ni kweli kwamba wameorodheshwa kuanzishishiwa tawi pale. Sasa hii taarifa ya kwamba kwa sababu mabenki yana *regulations* zinazofanyiwa na Benki Kuu Hazina ni *shareholder* tu pale. Sasa kama wamekupa majibu hayo kwamba mimi nahusika kusaidia tawi lianze mapema pale, nafikiri tukimaliza Bunge karibu ofisini nita *exercise influence* ili uweze kupata hilo tawi mapema iwezekanavyo.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nilipokuwa nikichangia nilielezea haki za mafao ya wastaifu yanapokosewa wakati wa kukokotoa.

*Report ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia June 30, 2007 ilibainisha kwamba majalada 714,000 yaligundulika, majadala 514 yangelipwa pungufu shilingi milioni 816. Pia report ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia June 30,2008 iligundua kwamba kutakuwa na mapunjo kama hayo ya milioni 288.*

Je, Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa kuweza kukabiliana na matatizo hayo ili wastaafu wetu wasipunjwe wakati wanapostaaifu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo mafupi ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane na *report* ya *Auditor General* na ninataka nikubaliane naye kwa sababu mafao ya wastaafu kuna vigezo viwili muhimu sana lazima viwe vya uhakika ili mafao yaweze kuwa ya uhakika.

Vigezo hivyo kwanza ni barua ya kuajiriwa, yaani ambayo itaweba kuonyesha muda amba o uliweza kufanya kazi katika ile Taasisi kama umefanya kazi miaka kumi au kumi na tano hicho ni kigezo kimoja muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mshahara wako wa mwisho, sasa kwa nini mafao yanakosewa? Mafao yanakosewa kwa sababu hizi taarifa zinakuwa zinatofautiana katika faili la Mwajiriwa, mara nyine unaweza ukapata katika faili la mwajiriwa kuna mshahara amba o yeye mwenyewe ameshaupita. Sasa sisi tunapopata faili lake ni lazima tukokotoe kulingana na barua au kulingana na taarifa zilizopo katika faili lake.

Lakini tunapopata taarifa sahihi kutoka kwa waajiri wake kwamba mshahara wake haukuwa ule tuliokokotoa sisi huwa tunafanya masahihisho yale ili tuweze kumlipa kile ambacho anastahili kulipwa na tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo pale ambapo mafao ya wastaafu yatakuwa pungufu. Lengo letu ni kwamba kila mstaafu alipwe mafao yake kwa ukamilifu.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, Kambi ya Upinzani ilihoji ni kwa nini hadi leo wafanyakazi waliokuwa katika kiwanda cha Sukari cha Kilombero amba o walistaafishwa mwaka 2000 hawajalipwa mafao yao, ni wachache sana hadi leo wamelipwa mafao yao lakini wengi wamebaki na kilio wakisubiri mafao yao hadi leo. Tunaomba ufanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilisikia kwenye mchango na nimesikia tena akizungumza.

Masuala ya aina hii yanashughulikiwa na Wizara tofauti, ni Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Lakini kwa sababu tumelisikia tutalifuatilia na tutalifanyia kazi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilioutoa pamoja na mambo mengine nilielezea suala la Chuo cha Uhasibu Tanzania tawi la Mtware kuwa lina mazingira magumu kutokana na kutumia majengo ya Saba Saba ambayo hayakulengwa kuwa chuo.

Lakini chuo hiki kina kiwanja cha siku nyingi ambacho Wizara haijawahi kutenga pesa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Naomba kupata maelezo ni lini Chuo hicho kitakuwa na majengo yake yenye na kwenye kiwanja chake.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjulische Mheshimiwa Juma Njwayo kwamba Jumamosi iliyopita nilifungua tawi la chuo hiki Singida na kinachofuata katika mpango wao ni hicho cha Mtware. Kwa hiyo, nina hakika katika mwaka ujao kutakuwa na pesa za kuanza ujenzi wa chuo cha Mtware.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati wa kampeni mwaka 2005 kwenye Chama Cha Mapinduzi tulihimiza sana kwamba Wanawake na vijana watawezesewa, na katika mchango wangu wa maandishi katika hotuba ya Waziri leo ninazo taarifa kwamba kule Mbinga ilifanyika semina ya MKUKUTA na suala la Vikoba iliongelewa na wananchi walilipenda sana na wakati ule Serikali iliahidi kwamba ile semina ya Vikoba ingefanyika kwa namna ya pekee ili kuwawezesha wananchi.

Sasa natambua kwamba Mheshimiwa Waziri haukuwa na nafasi ya kufafanua katika muda uliopewa, pengine ungetupa matumaini watu wa Mbinga na hasa kwa sababu wanasubiri sana na wanavyofahamu ni kwamba Serikali haidanganyi wa Mbinga Mbinguni.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeupitia mchango wa Mheshimiwa Mbunge, nataka nimwambie tu kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanawezeshwa ili waweze kujinasua na umaskini walionao. Nataka nimuhakikishie kwamba kwa sababu tumeshaanza semina katika hilo eneo alilosema la Mbinge, nataka nimuhakikishie kwamba stage ya pili ni kuwawezesha Watanzania waliopo maeneo ya Mbinga.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilichangia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu *export levy* kwa zao la Korosho. Sheria hii ilipitishwa mwaka 2006/2007, nashukuru kwamba kwa mwaka 2008/2009 kuna matumaini ya fedha hizo kulipwa kwa Halmashauri zinazolima Korosho. Lakini hakuna maelezo yoyote tunayoyapata kuhusu *export levy* ya mwaka 2006/2007 na 2007/2008, maelezo ya Serikali yanahitajika ili kutueleza fedha hizi ziko wapi mpaka sasa hivi hazijatolewa na kama zilitumika tuelezwe basi zimetumika kwa shughuli gani? kwa madhumuni ya Korosho au kwa madhumuni gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo na ufanuzi juu ya hasa ile miaka miwili ya mwanzo baada ya kuitisha Sheria hii ya *export levy*.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nalifahamu sana hilo, ni kweli kwamba mwaka jana tuliamua kwamba pesa hizi kama Sheria inavyosema, 65% ipelekwe kwenye Halmashauri na inayobaki inakwenda Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati uamuzi ule unafanyika kuna maamuzi mengine yalikuwa yameshafanyika kwamba Bodi ya Korosho ilikuwa imeshanunua pembejeo zote zilizohitajika kwa hiyo tungesema kwamba zile pesa tuzipeleke kwenye Halmashauri Bodi ingeshindwa kufanya ile kazi na ingeshindwa kabisa kusambaza madawa na vitu vingine.

Kwa hiyo, ndani ya Serikali tulifanya *consultations* Waziri wa Kilimo, Mimi na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli busara ikatupa kwamba hatungeweza kuacha yale madawa na pembejeo nyingine ambazo zimeshanunuliwa tungepata hasara.

Kwa hiyo, iliamuliwa kwamba pesa za miaka ya nyuma basi zipelekwe kwa Bodi kwenda kufidia hayo na bahati nzuri mimi Mheshimiwa Waziri Mkuu alinituma Mtwara, Mkuu wa Mkoa alitueleza hilo pia. Lakini baada ya kumweleza kilichotokea aliridhika na ninafikiri kwamba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa sababu aliahidi atawezu kuwajulisha Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na ile Mikoa mingine ambayo inalima Korosho kwamba pesa zile kwa kweli hazikutumiwa vibaya, zilitumika sawasawa kabisa kwa sababu wakati huo Bodi ilikuwa na madaraka ya kuagiza pembejeo waka-*assume* kwamba kwa sababu wanayo madaraka basi zile pesa zingepelekwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo lakini kuanzia mwaka huu tumeshaamua kwamba sasa ile 6.5% ya pesa zitapelekwa kwa Halmashauri husika na tuliamiwi pale kwamba wameridhika na mfumo huo. Lakini kama kuna tatizo lolote lile nadhani Mheshimiwa Anna Abdallah tunaweza tukakutana na kukupatia *details* ili angala uridhike kwamba kila kitu kwa kweli kilifanyika sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate ufanuzi.

Nilipokuwa nikichangia kwa kuongea na kwa maandishi nilisema kwamba Wizara ndiyo inayotoa Wataalamu wa uhasibu wanaohitajika kwa wingi hata kwenye Halmashauri zetu lakini katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha kuna tatizo la kuwaweka vijana katika *hostel*, na niliomba kwamba katika *Plot* Namba 28/11 ni jengo ambalo lilikuwalinatumwa na Benki Kuu lakini sasa hivi hawalitumii.

Naomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wote wako katika Wizara yake, haoni sasa kuna haja ya kuwapa hawa *IFM* jengo hilo?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na tumepeata maombi ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha kulitaka hilo jengo, lakini lile jengo lilipewa Benki Kuu. Kwa hiyo, busara inatutuma kwamba ni lazima tuzungumze na Benki Kuu kama wataona kwamba ni sahihi basi tunaweza tukafanikiwa kulipata jengo hilo. Sisi kama Serikali hatuna matatizo lakini ukweli ni kwamba jengo siyo la Serikali kwa sasa ni la Benki Kuu lakini ninavyomfahamu Prof. Ndulu tutazungumza naye ili tuone kama anawenza akatusaidia katika hilo.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sina tatizo na mshahara wa waziri isipokuwa katika mchango wangu wa maandishi niliulizia suala la malipo kwa wazabuni wa Wizara ya Elimu.

Wakati wa mawasilisho ya hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Waziri wa Elimu alisema mchakato wa kuwatambua wazabuni na madai yao ulishakamilika na madai hayo kupelekwa Hazina ili yalipwe. Sasa mimi naomba ufanuzi ni lini wazabuni hawa watalipwa nchi nzima?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulieleza kwamba uhakiki wa madai hayo ulikuwa umekamilika na kwamba madai hayo yalipelekwa Hazina kwa ajili ya malipo na kama Waheshimiwa Wabunge mnavyoona kwenye hotuba ya Bajeti fedha zimetengwa kwa ajili ya deni la taifa na ni kwa ajili ya madeni ya ndani na nje na ni matumaini yetu kwamba malipo hayo yatafanywa mapema. (*Makofî*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimestushwa kidogo na majibu ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja ambayo nime *raise* pengine na wenzangu walii *raise* kuhusu pesa za utafiti na katika majibu yake akasema kwamba wamelazimika hizo pesa sijui sasa kuzipeleka kwenye Taasisi gani kwa sababu nilimwuliza kama zinakwenda kwenye *National Economic Empowerment Council* kama alivyokaririwa mapema au namna gani. Lakini sasa hapa pia akatuambia kwamba hakuna Taasisi yoyote ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria inayo *Coordinate shughuli* za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi ninayo Sheria na bahati nzuri sana kwenye mchango wangu wa maandishi niliwaambia Sheria Namba 7 ya mwaka 1986 inayoanzisha *COSTECH* imainisha kabisa katika Ibara ya 5 kwamba shughuli za utafiti katika nchi zitakuwa *coordinated* au zitaratibiwa na *COSTECH*. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri anasema hakuna chombo cha namna hiyo.

Naomba maelezo ya Waziri kama Sheria hii imezikwa au namna gani?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilichoeleza mimi ni kwamba kama Serikali kwanza ni kwamba tunataka 1% huo ni uamuzi ambao umeshafanyika kwa sababu kwanza aliyesema ni Mkuu wa Nchi, Mwenyekiti wa *Cabinet* ndiye mwenye nchi yake akishasema kasema.

Tatizo tulilolipata sisi ni kwamba ukichukua hii karatasi ambayo nimkuonyesha tuna bilioni 305 ambazo ni karibu 1% ya *GDP* ya 2008/2009 lakini pesa hizi zime *spread* kwenye kila Wizara na *the biggest* katika hii yaani *the biggest* Wizara ambayo ina hizi pesa ni Wizara ya Kilimo ambazo ni 27 billion. Hii Wizara ya Elimu ya Juu na hasa *COSTECH* yenye we ina *only* 13 billion.

Kwa hiyo, ni ukweli kwamba hata hivi tulivyo sasa hivi inawezekana hiyo Sheria ipo lakini na hawa nao wana Sheria zao, maana *TBC* wanafanya *research* wana Sheria yao, Chuo Kikuu wanafanya *research* wana Sheria yao, Chuo Kikuu *SUA* imepeleka vijana na wenyewe Maprofesa pale wanafanya *research* wana Sheria yao. Kwa hiyo, kila mmoja ana Sheria yake ya kufanya *research*, kinachotakiwa sasa ni *ku-pull* pamoja hawa wote wanaojilusisha na *research* ili kuwe na tija katika ile *research* itakayokuja huko mbele ya safari. Sasa kwa mfano tukisema tuamue bilioni 305 tuzipeleke *COSTECH* wakati *absorption capacity* yao mpaka sasa hivi ni 13 billion hapa mwingine atasema kwamba pesa zinatumika vibaya hiyo ndiyo mwanzo tu wa kuwapa pesa wazitumie vibaya kwamba hawajawahi kupata zaidi ya 15 billion kwa mwaka mmoja tangu *COSTECH* iundwe na Serikali sasa huwezi leo ukachukua 1% ya *GDG equivalent to 305 billion shillings* ukawape *COSTECH* ambao *they have never had even 15 billion* kwa mwaka.

Sasa nasema kinachofanyika kwa Serikali ni kwamba sasa hivi Mheshimiwa Mbunge nataka nimhakikishie kwamba hakuna *institution* moja hapa nchini inayofanya *research*, kila

mmoja anafanya *research*. Ukizungumza na Prof. Mkandara atakuambia sisi haswa ndiyo *researchers* hapa, *COSTECH* wale wote wanatoka hapa kwetu. Kwa hiyo, hizo tuletee sisi na sisi tutazifanyika kazi vizuri, sasa kama Serikali hatuwezi. Sasa hili la *National Economic Empower Council* magazeti yanaweza kuandika kama wanavyoweza kuandika wewe mwenyewe umesema hapa leo. Nilichozungumza hapa ni kwamba Sheria ya *National Economic Empowerment Council Responsibility* yao ya pili katika *Charter* yao ni kufanya research ya uwezeshaji, kutafuta watu maskini na wana umaskini wa aina, *what level* ya umaskini ili waweze ku determine jinsi gani ya ku-set mfumo wa kuwawezesha.

Sasa ile *research* yao ndiyo niliyozungumza mimi na hiyo ndiyo niliyowasetia pesa kwa sababu kwanza iko chini yangu kwa hiyo nime *set* kweli pesa za kuwapa, lakini hizo pesa siyo hizi 305 billion. Kwa hiyo, yote mawili, hizo pesa ambazo tume-*set* kwa ajili ya *National Economic Empowerment Council* wanastahili kuzipata kwa Sheria waliyounda wao na hizi nydingine ambazo wame *spread* kwene hizi Wizara chungu nzima na vyombo chungu nzima kama chuo kikuu na kadhalika na wao pia wanastahili kupata kwa Sheria zilizowaondoa wao. Ukienda kusoma ile *charter* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam la kwanza wanasema *Education, Research, Consultant* na hiyo ni Sheria kama unataka Mheshimwa Zambi kaisome hiyo Sheria ya Chuo Kikuu, ukienda ya *SUA* ni hivyo hivyo *Education, Research* na *Consultants*. Kwa hiyo, kwa Sheria yao wanaruhusiwa kufanya *research* na ndiyo hiyo wamekuwa wakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu na kingine hizi *research institutions* ambazo tunazo *over 60%* siyo pesa ya Serikali ni misaada. Vyuo vikuu hivi wana vyuo vikuu vya nje ambavyo vinawasaidia pesa, wana *institutions* kama *Technical Institutions* kama *Bill Gates* na kadhalika ambao wanawasaidia pesa. Kwa hiyo, hata hizi 305 billion kwa Bahati nzuri 60% ni pesa ambazo zinatolewa na wafadhili kwa ajili hiyo. (*Makofi*)

Sasa ningewomba tu Mheshimiwa kwamba asubiri hizi za *National Empowerment Council* wala asizimezee mate, hizo ni za kwao na wanastahili kuzipata kwa Sheria waliyounuda. Sasa hii ya 1% tumeshagundua kwamba zipo pesa za *research* lakini zime *spread all the place* ni vizuri tuka *pull together*. Lakini itakuwa ni uamuvi wa Serikali sasa kwamba tukisha *pull hizi together* kama uwezo wa *COSTECH* ni just 13 billion inawezekana kweli tukawapa 305 billion huo utakuwa ni uamuvi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa maelezo hayo, hatimaye tunafikia mwisho, Mheshimiwa George M. Lubeleje karibu!

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka maelezo kwamba Serikali iliahidi kujenga Ofisi ya *TRA* Wilaya ya Mpwapwa sasa ni miaka mitatu nafuutilia jambo hili bila mafanikio. Je, Serikali ina maelezo gani? Ni lini ujenzi wa ofisi hiyo utaanza?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini lazima nikiri kwamba sikujitayarisha kwa swali hilo, lakini tutazungumza na wenzetu wa *TRA*, kwa sababu ni ofisi yetu na makusanyo kule ni mazuri lakini tutazungumza na *TRA* tuone itakuwaje. Siwezi kuahidi kwamba mwakani tutafanya lakini nakuhakikishia Mheshimiwa George M. Lubeleje jirani yangu kwenye jimbo kwamba tutasaidia hilo. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi sina sababu sana na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, isipokuwa tatizo langu nilikuwa nimechangia juu ya mishahara ya Walimu wa Sekondari Wilayani Misungwi. Nilipoongea na Mkurugenzi wa Halmashauri akasema wengine wote wameshapata mishahara yao isipokuwa Walimu wa shule za Sekondari. Sasa nilitaka nielewe tatizo liko wapi hasa?

**MWENYEKITI:** Walimu wa Sekondari, Walimu wote wengine wa msingi na wengine wa juu wamelipwa ila wa Sekondari bado nadhani ni kwenye Wilaya yake ya Misungwi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo! Nitalifuatilia hili mara moja ili niweze kupata jawabu hilo. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh.10,860,764,700
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Sh.8,104,167,300
Kifungu 1004 - <i>Legal Services</i> .....	Sh.610,409,700
Kifungu 1005 - <i>Information Education and Communication</i> .....	Sh.847,412,200
Kifungu 1006 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.303,706,100
Kifungu 1007- MCC Tanzania.....	Sh. 619,213,000
Kifungu 1008 - <i>Procurement Management Unit</i> ....	Sh.659,262,300
Kifungu 1009 - <i>Public Procurement Policy Unit (PPU)</i> .....	Sh.5,018,571,400
Kifungu 2001 - <i>Government Budget Division</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2002 - <i>Policy and Research</i> .....	Sh. 0

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2003 - *Treasury Registrar*.....Sh.48,671,386,800

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kwenye kifungu 2003 item 229900 (*Other Operating Expenses*) figure inaonesha kwamba ni shilingi Bilioni 42 kutoka shilingi milioni 837 ni *jump* kubwa sana lakini swali langu la msingi jingine hapa ni kwamba, hii ndiyo ofisi ya *Treasury Registrar* anayeshika mitaji yote ya Serikali. Hivi karibuni kuna tatizo kubwa sana la reli, na huenda Serikali ikatakiwa kuwekeza kiasi kingine cha fedha kwenye reli. *Figure* hii sioni kama inafanana fanana sana na wajibu wa Serikali kwenye suala la reli, nilikuwa naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali, pesa hizi ni za madeni ya Mashirika. Kuna madeni ya Mashirika kama *TTCL, ATCL* wanadaiwa na *South African Airways* na Mashirika mengine ambayo yamepata matatizo lakini ni mashirika ya Serikali, sasa kama *Air Tanzania* tusipoilipia madeni yake ndege zake zinaweza zikakamatwa. Kwa hiyo, hii shilingi bilioni 42, ni pesa za madeni hayo. *TRL* haipo hapa, hii ina mpango tofauti kabisa tunaitafutia pesa kutoka mahali pengine kuna *World Bank*, kuna India na mahali pengine. Kwa hiyo, hizi ni *specifically* kwa Mashirika ambayo tayari tumeishathabitisha kwamba wana madeni fulani na Serikali inawajibika kulipa ili kuyanusuru Mashirika yale.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 – External Finance .....	Shs.	0.00
Kifungu 5001 – Stock Verification.....	Shs.	7,952,642,200
Kifungu 6001 – Computer Services.....	Shs.	1,995,674,700
Kifungu 6002 – Tax Revenue Appeals Board	Shs.	870,135,900
Kifungu 6003 – Technical Audit Unit ...	Shs.	879,825,300
Kifungu 6004 – Tax Revenue Appeals Tribunal .....	Shs.	575,712,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko  
yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba nimshurkuru sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu alitukumbusha kwamba, tumeruka kifungu hiki. Kwa hiyo, ni vizuri ni kutoa sifa pale zinapostahili.

## FUNGU 22 – DENI LA TAIFA

Kifungu 1001 – Administration and General - Shs.1,515,794,540,000

*(Hapa Wabunge Kadhaa walismama ikiwa ni pamoja na  
Mhe. Bernadeta K. Mushashu)*

**MWENYEKITI:** Oh, kumbe wewe ulikuwa na nia nacho! Huyu Mama hatari kabisa!  
Basi tuanze na wewe! (*Kicheko*)

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi na Wabunge wengi waliochangia. Nazungumzaia Vote 22, Programme 10, Sub-Vote 1001, kipengele 810400, (*Short Term Domestic Loans*). Tulichangia na wengi wameulizia juu ya madeni ya wazabuni ya Wizara ya Elimu ya mwaka 2007/2008 ambapo Naibu Waziri wa Elimu mwezi Aprili alituambia hapa yote yamepelekwa Hazina kusudi Hazina iyalipe. Ningependa kujuu kwenye kipengele hiki ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kuwalipa wazabuni hao kutoka Hazina na ni kiasi gani kimetengwa kulipa madeni ya walimu ambayo yameishahakikiwa na yakapelekwa Hazina kwa ajili ya kulipa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kukamilisha kazi kwa mujibu wa Kanuni ya 100 nitaongeza muda usiozidi dakika thelathini (30) kuanzia saa Mbili Kasorobo (1:45). Mheshimiwa Waziri..

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Maghemba nafikiri aliishajibu hilo swali kwamba tumetenga pesa za kufanya hayo. Lakini kwamba, ni kiasi gani specifically kwa hilo naomba kwamba mpaka nitakapofika Dar es Salaam, Wataalam wanipe. Lakini tumetenga pesa za ku-clean haya madeni yote ambayo yanatupa taabu ili at least kwenye mambo ya Walimu na wengine tuwe hatuna kitu tuanze mambo mengine. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nimemwuliza Mheshimiwa Waziri, au labda niende kwanza kwenye *specific aspect* hapa. Ukiangalia kwa mfano *Short Term Domestic Loans* ambayo ni kifungu 810400 na *Long term Domestic Loans* ambayo ni kifungu 810500, hata ukichukua moja tu utaona kwamba , kuna ongezeko kubwa la madeni na ndiyo maana ukiangalia unaona kwamba, ghamama ya kulipia madeni ni kubwa mno ambapo ukichukua mwaka 2007/2008 ilikuwa shilingi Bilioni 561 na leo tunapaswa kulipia mara tatu ya mwaka 2007/2008. Kwa hiyo, nina hakika Bunge hili linahitaji kujua ni vipi mwenendo wa kukopa zaidi ndani unathibitibwa kweli au kuna matatizo gani ambayo yanatuweka kwenye sehemu ya namna hii? (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo tumelipata ni kwamba, kwa miaka kadhaa tulikuwa hatulipi. Kwa hiyo riba ndiyo imesababisha sana ongezeko hilo. Ukiangalia pale *Principal* unaona ni shilingi bilioni 53 lakini ile riba ndiyo imetufanya tuwe katika nafasi hiyo. Sasa ndiyo tumeamua mwaka huu kwamba, *Let us clean the balance sheet* ili ku-*avoid* riba kuendelea ku-*accumulate*.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi nina tatizo la ufanuzi kuhusu wapi hela za *TRL* zitakuwa kwa sababu Mheshimiwa Waziri kasema bado wanaongea na *World Bank* na watu wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kifungu gani?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Ni kifungu hichohicho cha *Public Debt!*

**MWENYEKITI:** Ndiyo tafuta *sub-item* hapo!

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Kwenye *Interest Payments to Foreign Non-Resident Institutions* ambacho ni kifungu 250100.

**MWENYEKITI:** *TRL is not a non-resident Institution!*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Ni *World Bank!* *World Bank is a non-resident Institution* Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unaulizia mkopo wa *World Bank*?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Eh! Kwa sababu huko ndiko zitakakotoka hizo pesa alizosema Mheshimiwa Waziri, sasa hali ikoje maanake wasiwasi wangu mimi inaelekeaa tutapitisha Bajeti hapa na yeye ndiye atakayekwenda tena kukopa halafu haijaingia kwenye Bajeti yake, naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Kama mkopo haujaiva sijui.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umeanza kunisaidia. Hizi pesa tulizoziweka hapa ni kwamba zimeishaiva hizi na hasa pale ninaposema riba kwamba, kwa miaka karibu mitatu, minne hatukuwa tunalipa hii mikopo kwa hiyo *principal* inabaki palepale lakini riba ina-*acumulate* kila mwaka. *TRL* wamesaini mkataba na *International Finance Corporation (IFC)* ambayo ni *Subsidiary* ya *World bank* zile pesa hazijatolewa kwa hiyo hatuwezi kuzi-book hapa kwamba tutazilipa na hata kupata kwenyewe hatujazipata. Ninavyofahamu Mheshimiwa Juma Kaboyonga ni mchumi mahiri unalipa baada ya kuzitumia, hata kuzipata hatujazipata na hazikutolewa kwa sababu *World*

*Bank walisita kuzitoa baada ya kutoridhika na mambo fulani fulani sasa yale kuna mazungumzo tunayafanya. Kuna timu imeundwa na Mheshimiwa Juma unafahamu, kushughulikia matatizo ya TRL ili Finacing Parckage iweze kukamilishwa na tuone shirika hili linawenza likaenda namna gani.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pesa ambazo ni Dola million 44, hizo tumeishakubaliana na *World Bank* tunachotakiwa kufanya sasa hivi ni kukubaliana kwamba je, *TRL is it now manageable?* Kwamba wakipewa hizi pesa hazitaingia kwenye *dish*. Sasa Serikali ikiweza kuwahakikishia *IFC* hilo, *World Bank* watawaambia watoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi hata kutoka hazijatoka kwa hiyo hatuwezi kuzi-book kuzilipa maana hata kupata hatujazipata. (*Makofi*)

(*Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

### **MPANGO WA MAENDELEO**

#### **FUNGU 21 – HAZINA**

Kifungu 2001 – <i>Governt Budget Division</i> .....	Shs. 5,890,000,000
Kifungu 2002 – <i>Policy and Research</i> .....	Shs.60,553,530,000
Kifungu 2003 – <i>Treasury Registrar</i> .....	Shs. 0
Kifungu 4001 – <i>External Finance</i> .....	Shs. 1,845,520,000
Kifungu 7001 – <i>Poverty Eradication and Empowerment</i> .....	Shs. 6, 240,000,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI**

Kifungu 3003 – *Financial Management* .....Shs.12,050,765,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Kifungu 1001 – <i>Administration and General</i> .	Shs.2,971,220,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> ..	Shs.5,319,412,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**

Kifungu 1001 – <i>Admnistration and General</i> ..	Shs.1,698,410,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i> Shs.	3,702,500,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i> ..... ..	Shs.1,210,400,000

Kifungu 1004 – <i>Legal Services</i> .....Shs.	0
Kifungu 1005 – <i>Information Education and Communication</i> .....	Shs.390,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1007 – *MCC Tanzania*.....Shs.176,571,992,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Iterm 4108*, Tunduma – Sumbawanga *Road Construction*. Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, kwa maelezo ya Waziri anayehusika, wa Miundombinu ni kwamba itaanza kujengwa mwezi Desemba, 2009.

Lakini pesa hizi kama tunavyoona zote ni za *MCC*. Tunataka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo au ufanuzi kama wananchi wa Mikoa ya Mbeya na Rukwa wawe na matumaini kwamba barabara hiyo itaanza kujengwa mwezi Desemba kama ambavyo iliahidiwa na Wizara. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni moja. Kwa hiyo, nataka kumhakikisha kwamba maelezo aliyojatoa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ni sahihi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – <i>Government Budget Division</i> .....Shs.	0
Kifungu 2002 – <i>Policy and Research</i> .....Shs.	0
Kifungu 2003 – <i>Treasury Registrar</i> .....Shs.2, 250,900,000	
Kifungu 4001 – <i>External Finance</i> .....Shs.	0
Kifungu 5001 – <i>Stock Verification</i> .....Shs.	0
Kifungu 6001 – <i>Computer Services</i> .....Shs. 2,342,200,000	
Kifungu 6002 – <i>Tax Revenue Appeals Board</i> .....Shs.	0
Kifungu 6003 – <i>Technical Audit Unit</i> .....Shs.	0
Kifungu 6004 – <i>Tax Revenue Appeals Tribunal</i> ....Shs.	0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirejea)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka 2009/2010 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadiro haya. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa  
Mwaka 2009/2010 yalipitishwa rasmi na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna kikao kifupi sana hivi sasa kinaitishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Kifupi sana kwa sababu inabidi wenzetu tena waungane nasi kwenye *briefing* ya *CDCF*. Kwa hiyo, wajumbe wote wa *PAC* (Kamati ya Hesabu za Serikali) wanaweza kutoka hivi sasa ili waweze wakakutane.

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha tena tuna pia kikao nacho siyo kirefu cha kuwekana sawa kuhusu *CDCF* kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Nawaomba sana, ni kweli tumefanya kazi kubwa. Bahati mbaya hatukuweza kupitisha Muswada wa *Appropriation*, lakini si mrefu. Kwa hiyo tutaanza nao kesho.

Kwa hiyo, naomba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge jioni hii, basi tuweze kuelekea Ukumbi wa Msekwa ili tumalize kazi hiyo nayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,  
tarehe 31 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*